Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

---

## Kikao cha Nane – Tarehe 22 Juni, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Randama za Makadirio ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka 2012/2013.

**SPIKA:** Ahsante sana, umeomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na atakaye uliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya.

Na. 58

## Utengenezaji wa Barabara Kwenye Mitaa Mbalimbali Dar es Salaam

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Jiji la Dar es Salaam linaendelea kujengwa majengo mapya mazuri, marefu yenye kuleta sura mpya ya jiji hilo, ujenzi unaofanywa na Mashirika na watu binafsi mbalimbali kwa matumizi ya aina mbalimbali lakini barabara nyingi zipitazao kwenye maeneo hayo na mitaa yake ni mbovu sana na hazilingani na hadhi ya majengo hayo mapya na kuwa kero na usumbufu kwa watu wanaoishi karibu na maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali itajenga upya au kuzitengeneza barabara hizo ili zifae kupitika nyakati zote na kuliweka jiji katika hali safi ya kuvutia kama nchi nyingine wanavyofanya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lina barabara zenye urefu wa kilomita 2459 kati ya barabara hizo kilomita 598 asilimia 24.3 ni za lami na kilomita 1352 ambazo ni sawasawa na asilimia 55 ni za changarawe na kiliomita 509 ambazo ni sawa sawa na asilimia 20.7 ni za udongo.

Kati ya barabara hizi kilomita 560 sawa na asilimia 22.8 zinasimamiwa na Wizara ya Ujenzi zinasimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia wakala wa barabara na kiasi kinachobaki kinasimamiwa na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Temeke.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilomita 1899, zinazosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kupitia Halmashauri ya Kinondoni, Ilala na Temeke, Serikali imekuwa ikiboresha kwa kuzifanyia matengenezo barabara hizi kwa kutumia fedha za ndani, hususan mfuko wa barabara ambapo kwa mwaka 2010/2011 zilitumika bilioni 4.9, mwaka 2011/2012 zimetumika shilingi biioni 5.96 na mwaka 2012/2013 inatazamia kutumia bilioni 7.34.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali Serikali imekuwa ikifanya matengenezo mbalimbali katika barabara hizo. Baadhi ya wahisani hao ni Serikai za watu wa Japan pamoja na Benki ya Dunia. Serikali kwa kushirikiana na wahisani hao inajenga barabara ya Bagamoyo kuanzia Morocco hadi kibaoni. Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia Serikali inatekeleza mradi wa Dar es Salaam *Metropolitan Development Project* ambao umetengewa dola milioni 75 sawa sawa na shilingi bilioni 112.5 kwa kuanzia ambapo kwa kiasi hiki inategemewa kuongezeka. Mradi huo upo hatua ya kumtafuta mshauri ya kufanya wa kufanya usanifu. Kazi ya matengenezo ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam kupitia mradi huu inatarajiwa kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokuwa ikifanyia matengenezao barabara zake kadri fedha zinavyopatikana. Ni matazamio yetu mradi huu wa DMDP utakamilika barabara nyingi za jiji la Dar es Salaam zitakuwa zimeboreshwa. *(Makofi)*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili, Jiji la Dar es Salaam linapanuka kwa kiasi ambacho hatukutarajia na kwa fedha zinazotengwa ni kidogo mno ukilinganisha na gharama za utengenezaji wa barabara. *(Makofi)*

Je, ingawaje *gradually* tunakwenda kidogo kidogo kutokana na hizi taarifa za fedha zilitumika kuanzia 2010/2011, 2011/2012 na mwaka huu inatarajiwa kutumika kiasi gani? Serikali iko tayari sasa walau kwa kipindi cha Bajeti ya mwakani zikatengwa kila mwaka siyo chini ya bilioni 30 tukaondosha tatizo la barabara katika Jiji la Dar es Salaam?

Katika mipango miji barabara ni tatizo lakini wakati huo huo majengo yanayojengwa katika Jiji la Dar es Salaam yanahitajia *parking* ambalo limekuwa tatizo kubwa ukilinganisha na idadi ya watu wanaoishi katika jiji la Dar es Salaam. Halmashauri husika pamoja na Serikali zinamipango gani kuhakikisha kabla ya kutoa vibali kukatengwa maeneo maalum ili wanapojenga hayo majumba kwenda juu kwa gorofa kumi na zaidi watu waweze kuwa na parking za uhakika ili kupunguza upungufu katika Jiji la Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**:

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Sanya najua yeye ni Mbunge wetu wa Mji Mkongwe kule lakini anaonyesha *concern* kubwa kwa sababu anaangalia mambo kitaifa. Kwa hiyo sisi tunakupongeza sana kwa hili unalolizungumza hapa. *(Makofi)*

Umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam na mambo yote yanayokwenda pale sidhani kama kuna mtu yeyote hapa anaweza akabisha kuhusu jambo hili, ni jambo la msingi sana. Ule mradi ambao tunazungumza sasa hivi ambao nimesema kwamba uta-*operate* mradi ule mkubwa ambao umekwenda Mbeya, Tanga na maeneo mengine mengi mpaka hapa Dodoma mnaona unafanyika, ulihitaji shilingi bilioni 165 kama tungeiingiza Dar es Salaam katika mpango ule, mpango wa Dar es Salaam unahitaji shilingi bilioni 365. Kwa hiyo unaweza ukaona kwamba ukisema uzichukue zile ambazo *World Bank* wanatusaidia zote zile Dar es Salaam ingechota zote zingeondoka. Kwa hiyo kilichofanyika hapa ni kwamba tumeona kwamba tuombe sasa msaada huu na ndiyo maana nimeeleza hapa kwamba kuna mpango maalum ambao unatumika.

Mheshimiwa Sanya anachosema hapa anasema hivi kwanini usingeweka katika Bajeti yako kila mwaka bilioni 30, bilioni 30 *which makes a lot of sense* mimi navyoona katika kipindi cha miaka mitano utakuwa umekusanya nini. Watu wanaohusika katika jambo hili kama nilivyosema siyo sisi tu TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi na wahusika wako hapa wanasikia wako wadau mbalimbali ambao wanajiingiza katika mpango. Mimi

nachosema ni kwamba concern hii tunaiona na ni muhimu kwamba tuifanyie kazi ili tuone jinsi tunavyoenda. Lakini pia itategemeana na uwezo wetu wa kiuchumi ndicho ninachokiona pale. Lakini la pili analolizungumza ni muhimu zaidi kuliko tunavyofikiri. Majengo yanajengwa pale yanajengwa halafu baadaye huna *parking* huna mahali pa kufanya kesho unaamka unataka kupitisha barabara kule na nini na vitu vingine vya namna hiyo. Kwa sasa hivi utaratibu na amesema yeye mwenyewe alipokuwa anauliza swali Mheshimiwa Spika, huwezi ukamruhusu mtu kujenga jengo lolote mahali popote mpaka apate kitu kinachoitwa *building permit*.

Wadau mbali mbali wataangalia ili kuhakikisha kwamba inakidhi yote haya ambayo unayazungumza hapa. Kwa hiyo tunasema kwamba Mheshimiwa Sanya anatoa mawazo mazuri na tutayachukua haya ni jambo ambalo tutalifanyia kazi lakini ndivyo tunavyofanya sasa hivi hapa na ndiyo maana unaona sasa tumeanza *satellite* zinaanza mji wa Kigamboni ule unawekewa mamlaka yake sasa ili uweze kujengwa pale kuondoa haya matatizo tusije tukasema kwamba tumeshavurugika ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana hivi karibuni Serikali ilitangaza kwamba watapandisha baadhi ya barabara katika mkoa wa Dar es Salaam ili barabara hizi zitoke katika mamlaka ya Manispaa kwenda Serikali kuu. Je, Wizara itakuwa tayari kutupatia majina ya hizo barabara ambazo zimepandishwa hadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ooh! Mheshimiwa Naibu Waziri mwingine wa ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge anazungumzia tutatoa taarifa katika kipindi kijacho.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa msongamano mkubwa ulioko katika Jiji la Dar es Salaam unasababishwa kwa kiasi kikubwa na miundombinu ambayo ni ya hafifu hasa ya barabara. Kwa kuwa hili ni janga, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kutumia chombo kama jeshi letu la wananchi wa Tanzania ili waweze kufanya kwa haraka sana tuweze kutumia reli itokayo Ubungo mpaka katikati ya Jiji? Pamoja na kutumia reli kutoka Pugu mpaka katikati ya Jiji hasa wakati wa *peak hours* na pia kutumia usafiri wa majini kutoka Bagamoyo mpaka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwa kuweka *gats* na jeshi uwezo huo linalo na likawa ni jambo la haraka?

**SPIKA:** Haya Waziri wa Ujenzi kaingia sijui alisikia swali hilo kama hakusikia...

**WAZIRI WA UJENZI:** Arudie kidogo swali Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ni kutumia usafiri wa reli katikati mji pale, siku moja si nilikusikia unasema.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbatia kama ifuatavyo. Kwanza ni kweli kabisa kwamba Serikali ina mipango mingi ya

kuhakikisha kwamba inapunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Katika hatua mbalimbali ambazo zimeanza zimechukuliwa ambazo bahari nzuri amezieleza Naibu Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri wa Ujenzi ni pamoja na kuanza ujenzi wa barabara nyingi tu katika jiji la Dar es Salaam. Kwa taarifa tu ya Bunge hili kwa sasa hivi kuna mradi wa zaidi wa shilingi bilioni 300 unahusisha ujenzi wa barabara ya kutoka Kimara kwenda Kivukoni, kutoka Fire kwenda Kariakoo, kutoka Magomeni, kwenda Morocco, na katika upana wa barabara ambao unapanuliwa pale, kuna sehemu nyingine kwa mfano kama ile ya fire itakuwa na njia nane, na sehemu zingine zitakuwa na sehemu sita. *(Makofi)*

Lakini pia kuna upanuzi wa barabara ya kutoka Mwenge kwenda Tegeta wa njia nne zaidi ya bilioni 88 zinatumika. Na katika awamu ya pili itaanzia Mwenge Morocco kilomita 4.1 lakini pia kuna ujenzi wa daraja la Kigamboni zaidi ya bilioni 244 lakini pia kuna barabara nyingine ambayo itaanza kujengwa katika bajeti ya mwaka huu kuanzia rangi tatu kuja Kariakoo ambayo itakuwa njia sita. *(Makofi)*

Lakini mbali ya hivyo kuna barabara ambazo tumezichukua baada ya kuombwa na Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam, zililetwa barabara za mapendekezo katika Wizara yetu karibu barabara 25 tumezi-*adopt* ambazo katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha maalum kwa ajili ya ya kuanza kuzitengeneza barabara hizo katika jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Lakini mbali ya hivyo tutaanza pia kutumia usafiri wa maji kwa sababu ndani ya bahari hakuna msongamano kwa hiyo patakuwa na feri ambazo zitakuwa zinatoka mjini zinaenda mpaka Bagamoyo na kuna vituo saba ambavyo tumevianisha katika bajeti ya mwaka huu tutapanga. *(Makofi)*

Na kupitia Wizara ya Mawasiliano na uchukuzi Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi amekwishazungumza kwenye mkutano wa Jangwani kwamba ataanza kuangalia uwezekano wa kuanza kutumia reli katika maeneo ya kutoka Pugu kwenda mjini na maeneo mengi. Kwa hiyo hili suala linashughulikiwa kwa kikamilifu katika kuhakikisha kwamba msongamano katika jiji la Dar es Salaam unapungua. Lakini mbali ya hivyo katika bajeti ya mwaka huu tuna mpango pia wa kuanza kujenga Dar es Salaam express way kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kwa njia ambayo tuta-involve kwa njia ya PPP. Kwa hiyo nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbatia kwamba juhudi kubwa zinafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha zinapunguza barabara za Dar es Salaam. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo suala hili limekula muda wa maswali mengine, mkiona naruka mwingine hivyo ndivyo hivyo. Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola swali linalofuata.

Na. 59

## Chanzo cha Maji cha Mto Nzivi

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Miundombinu ya maji ya mto Nzivi ili kuwawezesha wananchi wa vijiji vya Nzivi, Malangali, Mbalamaziwa, Maguvuni, Iramba, Ukemele, Idunda na Idumilavanu wanaotegemea chanzo hicho?

(b) Je, ni kwanini Serikali haifanyi ukarabati wa matanki ya maji ya vijiji vya Swala, Nyololo, Maduma, Nyigo, Kibao na Igowole ili yaweze kutumika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya miundombinu ya maji katika vijiji vya jimbo la Mufindi Kusini vina matatizo ya upatikanaji wa maji. Kijiji cha Nzivi kina vyanzo vya maji vya Kingege na Nyaupele ambavyo kwa sasa havifanyi kazi. Halmashauri hivi sasa inaendelea na na usanifu wa mradi huo kwa lengo la kubaini gharama zinazohitajika kukarabati vitegamaji pamoja na miundombinu ya mabomba ili uanze kufanya kazi na kuhudumia vijiji vya Mbalamaziwa, Maguvani, Iramba, Ukemele, Nyambembe, Kitelewasi, Mkangwe, Kinegembasi na Idetero.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kutumia bwawa la Nzivi kama chanzo cha maji Halmashauri imekamilisha usanifu wa mradi wa maji

kutoka bwawa hilo ili kupeleka maji katika kijiji cha Nyololo-Njiapanda ambacho kina uhaba mkubwa wa maji. Gharama zinakadiriwa kufikia shilingi milioni 500 mpaka utakapokuwa umekamilika. Kutokana na ukomo wa bajeti ya miradi ya maji ya mwaka 2012/2013. Halmashauri inakusudia kuweka mradi huu katika mpango wa bajeti wa mwaka 2013/2014.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba matanki ya maji katika vijiji vya Sawala, Nyololo, Maduma, Nyigo, Kibao na Igowole hayafanyi kazi kwa kiasi cha kuhitaji ukarabati. Halmashauri imekamilisha usanifu wa mradi wa maji Sawala na Kibao na kubaini kwamba zinahitajika shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ukarabati. Katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 Halmashauri imetengewa shilingi milioni 804.1 kwa ajili ya kazi hiyo.

Kazi zitakazofanyika ni ukarabati wa banio kuweka mabomba mapya na kuimarisha mifumo yote ya maji. Mradi huu ukikamilika utanufaisha vijiji vya Sawala, Mtwango, Lufuna na Kibaoni. Ukarabati wa Matanki katika vijiji vilivyobaki utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha kila mwaka. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri na pia nashukuru kwamba Serikali inakubaliana kwamba vijiji nilivyovitaja hapa havina maji kabisa. *(Makofi)*

Sasa je, Serikali inachukua hatua gani za haraka, kuhakikisha kwamba wananchi wale wanaweza kupewa maji na ndiyo maana katika swali langu hili nimesema ni lini. Kwa sababu nilikuwa najua kabisa Serikali inafahamu matatizo makubwa ya pale. Sasa

nimesema ni lini matokeo yake nimepewa maelezo mengine, sasa naomba Serikali inihakikishie ni lini wananchi wale wanaweza kupewa maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, mimi nataka nikuthibitishie kwamba mimi nimekwenda Mheshimiwa Lugola anafahamu kwamba nimekwenda kwake kule na hili tatizo tumekiri hapa kwa sababu tumeona kwa macho yetu kwamba kuna tatizo pale.

Mwaka uliopita wa fedha walikuwa na shilingi milioni 804.1 kama inavyotamkwa kwa mwaka huu unaofuata tena milioni 804.1. Mimi namwomba sana Mheshimiwa aendelee na jitihada hizi tutashirikiana naye kwa sababu hawa wananchi ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge wana matatizo ya maji kwa hiyo hatuwezi kubishana hapa.

Tunachosema hapa ni kwamba sasa hivi tunapitisha hii katika Bajeti lakini nimwombe wiki ijayo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuja hapa na Bajetina Waziri wa Nchi katika Wizara yetu atapita hapa, ataomba kibali cha Bunge hili ili tuweze kutumia hizo fedha.

Harakaharaka Mheshimiwa Kigola na wenzako naomba mpitishe zile fedha ili tuweze kwenda kushughulikia huo mradi kama unavyozungumzia hapa. (*Makofi*)

Na. 60

**Wazee Kusamehewa Kulipa Kodi za Nyumba**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Wazee wengi wana kipato duni na wengine hawana kabisa kipato. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasamehe Wazee kulipa kodi za nyumba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi za majengo kwa wazee unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya nyumba kifungu Na. 7(i) na kifungu Na. 19(3) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982. Sheria hizi kwa pamoja zinatoa utaratibu unaotumika kukusanya kodi ya majengo na msamaha wa kodi h iyo kwa Wazee wasio na uwezo. Vigezo vifuatavyo vinatumika kuwatambua wazee wanaostahili kusamehewa kodi ya majengo ambavyo ni umri usiopungua miaka 60, nyumba inayostahili kusamehewa ni ile inayotumika na huyo mzee kwa makazi pekee na hana kipato kwa sababu mbalimbali ikiwemo uzee na malazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotakiwa kufuatwa na Wazee wanaoomba msamaha wa kodi ni kuandika barua ya kuomba msamaha kwa Mwenyekiti au Mtendaji wa Mtaa mahali anapoishi. Serikali ya Mtaa itaandika barua ya mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Manispaa kupitia kwa Afisa Mtendaji

wa Kata ikiambatanisha na muhtasari wa kikao. Baada ya mchakato huo, Mkurugenzi ataetembelea nyumba husika na kutoa mapendekezo kwenye kamati ya Kudumu ya Fedha na Uongozi kwa maamuzi. Hadi sasa, maombi 24 yamewasilishwa na yanaendelea kufanyiwa kazi katika Manispaa ya Ilala.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi na ninashukuru kwa kupata majibu mazuri lakini sasa naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Waziri ameelezea vizuri kwamba kuna sheria inayowalinda Waziri na kwa kuwa mpaka sasa hivi katika Jimbo la Ukonga na sehemu nyingine Wazee wananyanyasika sana na wananyanyaswa na *TRA* kwa kuhitajika kulipa kodi. Je, sasa Serikali iko tayari kwa kutumia vyombo mbalimbali au njia yoyote ile kutoa elimu kwa wazee na watendaji ili sheria hiyo iweze kueleweka kwa upana kwa wazee wote kwa ujumla wao na waweze kuendelea kuifaidi sheria hiyo?

Swali la pili, kwa kuwa tumekuwa tunazungumzia suala la wazee wasiokuwa na kipato au waliokuwa na kipato duni kulipwa *pension* na kwa kuwa Serikali ilikwisha kuonyesha nia nzuri ya kuwalipa wazee hawa *pension.*

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza jambo hili ili wazee hawa waweze kutumia vizuri maisha yao yaliyobaki hapa duniani na watakapoondoka waweze kuacha baraka kwa nchi yetu badala ya laana?

**SPIKA:** Hili la pili, jana Waziri alijaribu kueleza na nafikiri ataeleza tena kwenye hotuba yake. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali moja la kwanza, kwa maelekezo yako, kama ifuatavyo na ninakushukuru pia kwa maelekezo uliyotoa.

Mheshimiwa Spika, labda nisaidie kidogo hapa, sheria hii tunayoizungumzia hapa inaambatana na ile sheria ya *Property Tax,* kama unakumbuka vizuri katika Bunge lako wakati uliopita tulikuwa tumepitisha sheria miaka mitano iliyopita wakati tukiwa kwenye jengo la Pius Msekwa. Iliyokuwa inaanzisha *pilot study* kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam yaani kwamba tutakuwa na utaratibu ambao *TRA* itasaidia Halmashauri hizi za jiji kuokota hizi kodina hii anayosema ya elimu ndiyo maana unaiona kwamba inaleta maana kwa sababu kwa kweli wamekuwa wanakutana na wanafanya utaratibu na kuona kwamba ni kwa namna gani tunaweza kufanikiwa.

*TRA* inaokota mapato yale kwa niaba ya Halmashauri, sasa hawa wazee wanaoishi katika zile nyumba wakati mwingine wanapata msukosuko, si sheria tu kwamba imesema hivyo. Tarehe 5/10/2005 Rais wa Awamu wa Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliagiza kwamba wazee wasamehewa kulipa kodi ya majengo yaani *property tax* kwa nyumba zao wanazozitumia kuishi yaani *residential houses only* na ambazo hazitumiki kwa biashara au kupangisha.

Kwa hiyo, hapa hakuna maswali yaani kusema kwamba hii mnafanya au hamfanyi *there is no question about that,* ni lazima itekelezwe hiyo na sheria tunayoisema ipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuthitibishie kwamba yeye anaomba tutoe elimu kwa wananchi wetu ili waelewe. Lakini tatizo kubwa tunalolipata katika *operationalisation* ya hii *idea* ni kupambanua kwa sababu mzee huyu anaweza akakaa mwaka mmoja au miwili amefariki dunia wengine wanabana mle ndani lakini ambao wana uwezo wa kuweza kulipa hii *property tax.*

Tutafanya hivyo kama ilivyoelekezwa hapa na Mheshimiwa Mbunge. Tutashirikiana naye na Halmashauri hizi zinazohusika zimezungumzwa na Wakurugenzi wote tuone njia nzuri ya kuwasaidia hawa wazee ambao imebainika kwamba ni kweli hawa wazee hawana uwezo wa aina yoyote. (*Makofi*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Suala hili la huduma hizi za wazee limekuwa ni tatizo mpaka leo karibu nchi nzima Serikali ilitoa tamko kwamba wazee wasilipe gharama yoyote katika huduma za afya. Waziri wa TAMISEMI anatoa kauli gani kupeleka waraka huu katika maeneo ya Vijijini ambapo mpaka leo wazee wananyanyasika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu

ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu kama ifuatavyo:-

Mimi nataka nieleze pia hili kwa sababu ni jambo ambalo linatusumbua pia. Ni hivi ni kweli kwamba tumetamka kwamba wazee hawa wawe wanapata huduma kama vile unavyozungumza watoto wenye umri wa miaka mitano, akina mama wajawazito na wengine wote.

Sasa tatizo ambalo tunalo sasa hivi ni kubaini hawa watu, maelekezo ambayo tumeyatoa nawaomba Waheshimiwa Wabunge wanisikilize vizuri. Tumezitaka Halmashauri zetu zitoe vitambulisho, unajua yuko mtu mwingine unaweza ukamuangalia anaonekana mzee kumbe ni kijana tu, anapiga maji yake vizuri na kadhalika.

Mimi ninachosema hapa na maelekezo ya Serikali ni kwamba Halmashauri zetu zote ziorodheshe hawa wazee wote wanaofahamika wajue kwamba hawa ni wazee wenye umri huo unaozungumzwa hapa. Akimaliza na wakishapatikana maelekezo ya Serikali ni kwamba hao wazee wapate hizo huduma bure kama inavyosemwa hapa. Nasema ni kweli kabisa Mheshimiwa Mangungu anavyozungumza hapa tatizo kubwa limekuwa ni kupambanua na kuweza kuwabaini na kuweza kujua ni nani wanahusika.

Naomba tushirikiane wote kwa pamoja ili tuweze kujua kwamba hawa wazee gani, wakishapata vitambulisho maelekezo ya Serikali ni kwamba waweze kusaidiwa na vitambulisho vinavyovizungumza hapa simaanishi hivi vitambulisho vya kitaifa namaanisha vile

vya Halmashauri tu kwa ajili ya kuweza kufanya hilo analolisema Mheshimiwa Mangungu.

**SPIKA:** Hilo zoezi alilosema Waziri wa Kazi likifanikiwa nadhani litajibu matatizo haya yote. Muda umekwisha tupo nusu ya safari yetu kwa hiyo, tunakwenda Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar atauliza swali hilo.

Na. 61

**Wito wa Vijana Kujiunga Kwenye Vikundi ili Waweze Kutambuliwa na Kupewa Mikopo**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR** aliuliza:-

Serikali imetoa wito kwa vijana kujipanga katika vikundi maalum vya Ujasiriamali ili waweze kutambuliwa na kupewa Mikopo kwa urashisi:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kutoa elimu kwa vijana hao ili waweze kuitikia wito huo?

(b) Je, tangu Serikali itoe wito huo, imefanya tathmini gani kujua kama kauli yake hiyo imefanikiwa kwa kiwango gani?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa na kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Kati ya mwaka 2009 na 2011, Wizara imetoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha kwa vijana 75,026 ili kuwawezesha vijana hao kuwa na ari na nia ya kujiunga pamoja kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Mafunzo haya yamewahusisha pia viongozi wa vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali ambao nao walienda kuwafundisha vijana wengine.

(ii) Wizara imeendelea kuzihimiza Sekretarieti za Mikoa na Halmshauri za Wilaya ambazo hazijaajiri Maafisa Maendeleo ya Vijana zifanye hivyo. Mpaka sasa tayari Mikoa 14 na Wilaya 30 wameshaajiri Maafisa Vijana. Maafisa hawa, pamoja na mambo mengine watasimamia uundwaji wa vikundi vya vijana na kuwapatia mafunzo ya usimamizi wa uendeshwaji wa vikundi hivyo.

(iii) Ili kuharakisha usomaji na uelewa wa makundi yote ya vijana, sera ya maendeleo ya vijana ya mwaka 2007 imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka vyama kwa vijana na wadau wengine. Sera hii imesambazwa kwenye mikoa na Wilaya zote kupitia Makatibu Tawala za Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri ili kutimiza azma ya kutoa mafunzo.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini zimefanyika katika nyakati tofauti kwa kutumia mikakati mbalimbali. Mikakati hii ni kama ifuatayo:-

Kupata taarifa yakinifu juu ya vikundi vya vijana na shughuli wanazozifanya *(Youth Mapping).* Taarifa tulizonazo zinaonyesha kwamba kuna vikundi vya vijana vya uzalishaji mali 3,884 katika mikoa 20 kwa jumla ya Wilaya 76. Kwa ujumla vikundi hivi vina wanachama 28,607 na kati ya hao wasichana ni 9,994 na wavulana 18,613. Tunatarajia pia kuboresha taarifa za vikundi vya vijana wakati wa wiki ya vijana ambayo hufanyika kila mwaka wakati wa kuazimisha kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru (Mwaka huu ni tarehe 8-14 Oktoba, 2012, Shinyanga) tutaendelea pia kutathmini ufanisi wa vikundi vya uzalishaji mali vya vijana pamoja na kuvishindanisha.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa vijana ndiyo nguvukazi ya taifa, nina maswali mawil ya nyongeza.

Je, Serikali inafanya kazi ya ziada ili kuona mikoa yote ya Tanzania inaondosha kero hii?

Je, Wizara kwa nini haikuweza kutumia vyombo vya habari na vijarida ili kuweza kuwafikia vijana wote wa Tanzania kwa kuondoa kero hiyo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, kama ifuatavyo:-

Kwanza, suala la Serikali itachukua juhudi gani za ziada ili kuondoa kero za vijana hapa nchini. Nadhani nimelijibu kwa kirefu katika jibu langu la msingi. Kwanza napenda tu niseme kwamba Serikali itaendelea

kuhimiza mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini ambazo hazijaajiri Maafisa vijana kuendelea kuajiri maafisa hao na kutilia nguvu za makusudi kabisa. Lakini pia Wizara yangu ikishirikiana na TAMISEMI itaendelea kuhimiza Halmashauri za Wilaya zote hapa nchini kutenga ile 5% ya mapato kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya vijana.

Lakini pia Serikali itaendelea kuboresha mfuko wa vijana na kuendelea kutoa mikopo ya vijana kupitia *SACCOS* zao mbalimbali na kama tunavyofahamu Serikali imetoa wito wa makusudi kabisa kwa halmashauri mbalimbali kuhakikisha vikundi vya vijana ambavyo vipo katila Halmashauri zao wanapewa mafunzo ya namna ya kuendesha *SACCOS* na kadhalika.

Wizara itashirikiana pia na TAMISEMI kuendeleza kutambua na kuhimiza vijana kuanzisha vikundi mbalimbali ili viweze kuwapatia kipato na sisi tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwapatia mafunzo mbalimbali. Sasa katika suala la pili la kuhusu kutumia vyombo ili kuweza kuwafikia vijana mbalimbali. Mimi nadhani kwa kikubwa ni swali zuri na angalizo zuri lakini hilo pia ndiyo angalizo ambalo Wizara yangu inalitumia hasa ukipelekea kuwa Wizara yangu pia inasimamia masuala hayo hayo.

Masuala ya vijarida yanatekelezeka ukipelekea kwamba Wizara yangu pia inasimamia masuala hayohayo. Masuala ya vijarida yanatekelezeka kama nilivyosema, tuna sera yetu ambayo imesambazwa nchi nzima na vijarida mbalimbali na katika

makongamano mbalimbali ambayo yanahusisha vijana vijarida vinatumika kwa hali ya juu.

Lakini kubwa nilizungumze hapa kwamba ni muhimu kwamba tunapokimbia kushughulikia masuala ya majarida tuwajengee pia vijana wetu pamoja na wananchi kwa ujumla utamaduni wa kusoma kwa sababu unaweza ukatengeneza vijarida wakaviangalia na wakavitupa. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ambayo Wizara yangu inataka kusimamia kwa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba tunajenga vijana wenye kupenda kujitolea, wenye kupenda kujitolea, wenye kupenda kujitegemea na wenye kupenda kufanya kazi lakini pia wenye utamaduni chanya wa kujituma kujisomea na kujitegemea. Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mbali na elimu ya ujasiriamali vijana wanapata matatizo sana katika upatikanaji wa mitaji na siku hizi katika Halmashauri zetu ile asilimia 5 iliyokuwa ikitengwa inaonekana haipo kwa sababu kulikuwa na matatizo ya urejeshaji ambapo mikopo hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wanawake na vijana. Vilevile mabilioni ya JK inaonekana imeshindana kwa vijana kupata kutokana na kwamba hawana dhamana ya kupata mikopo hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba pamoja na elimu ya ujasiriamali vijana wanapata mitaji?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la

nyongeza la kutoka kwa Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, kuhusu umuhimu wa vijana kupata mitaji na Serikali ina mpango gani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, lakini pia hata lile la nyongeza wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia kwamba Serikali imejipanga na katika kujipanga huko tumehakikisha kwamba vikundi mbalimbali ambavyo tunavihimiza kupatikana katika Halmashauri mbalimbali zinapewa mafunzo na pia agizo la kuhakikisha kwamba 5% ya mapato ya Halmashauri ni agizo ambalo mpaka sasa hivi Serikali inalifuatilia kwa karibu.

Sasa uwezekano wa vijana mbalimbali kuweza kupata mitaji inategemea na uuwezekano wao wa kuweza kukopesheka ndiyo maana nimesema mafunzo ni muhimu waweze kuelekezwa vizuri ili watakapopata nafasi ya kuweza kukopa ambalo ndiyo suala kubwa ambalo Serikali inalifanyia kazi kwa kupitia mfuko wetu wa vijana, waweze kutumia hizo fedha vizuri.

Lakini pia katika kupitia ule mfuko wa vijana utawafikia wale tu ambao tayari wameshajipanga vizuri na watakaokuwa *identified* kuweza kupata huo mfuko ni wale ambao tayari wanaweza kukopesheka lakini pia tayari pia wataweza kutoa matunda kutokana na kile watakachokipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 62

**Mradi wa Maji wa Kutegwa Katika Mto Mpeng'o**

**MHE. MODESTUS K. KILUFI** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Ipwani na Mawindi waliomba mradi wa maji ya kutegwa kutoka Mto Mpeng'o Wilayani Njombe na wameshaandaa njia utakakopita mtaro na maandalizi mengine muhimu.

(a)Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha madi huo?

(b) Kwa kuwa, upembuzi uliofanyika umeonyesha gharama za mradi zitakuwa shilingi bilioni nane (8,000,000,000/=) fedha ambazo Halmashauri haina. Je, Serikali itauchukua mradi huo kuwa wa kitaifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja na kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa awamu za vipindi vya miaka mitano katika Halmashauri zote kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2025. kwa kuanzia Halmashauri zimechagua vijiji 10 vya kipaumbele ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika awamu ya kwanza kati ya vijiji 10 ilivyochagua imeanza kutekeleza miradi ya maij katika vijiji vya Ubaruku na Chimala.

Tarehe 12 Juni, 2012 Halmashauri hiyo imesaini mikataba na Mtaalamu Mshauri wa kusimaima ujenzi na Mkandarasi wa ujenzi. Kwa sasa mkandarasi

anafanya maandalizi ya kuanza kazi (*Mobilisation*). Jumla ya shilingi bilioni 743 zimetengwa kutekeleza miradi ya maji Ubaruku na Chimala.

Mheshimwa Spika, mradi wa maji wa Luduga – Mawindi ambao chanzo chake ni mto Mpeng'o ulioko Wilayani Njombe umepangwa kutekelezwa katika awamu ya pili ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

Mradi huo unahusisha Vijiji vya Luduga, Hanjawanu, Iyayi, Igando, Malangali na Mpanga katika Wialaya Njombe na vijiji vya Namienga, Itipingi, Kangaga, Mkandami, Matemela na Ipwani vilivyoko katika Kata za Ipwani na Mawindi Wilayani Mbarali. Vijiji vya Mbarali vimo katika mpango wa vijiji 10 vilivyopendekezwa na Halmashauri. Kinachotakiwa ni Halmashauri za Mbarali na Njombe kuuweka mradi huo kwenye mipango yake na fedha zake zinatengewa kupitia programu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji ya kitaifa ni ile tu inayohusisha maeneo makubwa ambayo hutumia nishati ya umeme kwenye mitambo ya kusukuma maji ambapo gharama zake ni kubwa katika uendeshaji na matengenezo na hivyo si rahisi kwa watumiaji wa mradi kuugharamia. Mradi wa Luduga-Mawindi ni wa maji ya mtiririko hivyo gharama zake hazitakuwa kubwa kiasi cha wananchi kushindwa kugharamia uendeshaji na matengenezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge utulivu, maana yake naona kuna mazungumzo kila

mahali. Kwa hiyo, siyo vizuri. Mheshimiwa Kilufi swali la nyongeza.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza**.**

(i) Kwa vile ametaja Kata za Ubaruku na Chimala kwamba ndizo zinatekelezwa kwa kupangiwa milioni 743, kumbukumbu zangu zinaonesha Kata hizo zilikuwa kwenye Bajeti ya mwaka uliopita. Sasa kama ndiyo hivyo mwaka huu zinaelekea kupewa fedha hizo tena. Nataka nijue. Je, fedha zilizokuwa zimetengwa na Bajeti ya mwaka uliopita zilifanya kazi gani na zilikuwa kiasi gani? (*Makofi*)

(ii) Kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, niliomba mradi huo uwe wa kitaifa kulingana na gharama ya shilingi bilioni nane (8) ambazo zimeanishwa na Wataalam. Kwa maelezo yake amesema kwamba Serikali huwa inachukua miradi ambayo wananchi watashindwa kuigharamia.

Naomba nimwombe kwa heshima na taadhima kwamba, bilioni nane (8) kwa vijiji hivyo vilivyotajwa havina uwezo wa kugharamia. Naomba Serikali iuchukue mradi huu ili wale wananchi ambao toka nchi hii ipate uhuru hawajawahi kupata maji ya bomba na majirani zao wa Njombe tu pale wana maji ya bomba.

**SPIKA:** Mnawaonea wivu sasa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Kilufi kwa namna ya pekee kwa jinsi anavyofuatilia matatizo ya maji katika jimbo lake la Mbarali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kwamba fedha zilizotamkwa shilingi milioni 743 zimetekeleza kazi katika awamu iliyopita. Suala ni kwamba katika awamu iliyopita miradi hii ya maji imeanza kutekelezwa kutoka mwaka 2007 na Wilaya ya Mbarali ilitengewa shilingi milioni 671 ambazo mpaka sasa hivi ndiyo zimefika kule Wilayani. Sasa shughuli ambazo zimefanywa kutoka muda huo mpaka sasa hivi ni kwamba ulifanyika utafiti kwenye visima katika vijiji vinne vya Ubaruku, Yala, Simike na Udindila.

Baada ya kufanya ule utafiti ikagundulika kuwa ni vijiji vitatu ambavyo vina maji ambavyo ni Ubaruku, Simike na Udindila.

Sasa shilingi milioni 83 zimelipwa kwa ajili ya kuchimba visima kwenye maeneo haya ambayo nimeyataja. Shilingi milioni 310 zimelipwa kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu kwenye maeneo yote ya vijiji vinne (4). Kwa hiyo, utaona kwamba shilingi milioni 743 ilikuwa ni Bajeti ya mpango na kwa maana hiyo sasa ili kukamilisha mradi wa Ubaruku ambao ndiyo uko kwenye kipaumbele zinahitajika shilingi milioni 346 ili kuanza sasa ujenzi wa miundombinu.

Kwa hiyo, kwa maana ya kazi zilizofanyika kwa fedha zilizopita ni hiyo ya uchimbaji wa visima kwenye maeneo ya vijiji vitatu, kujihakikishia kama maji yapo na

kulipa mshauri ambaye amefanya kazi katika maeneo hayo manne yote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ambalo anaomba kwamba, kwa sababu ya gharama za mradi, mradi huo uingizwe kwenye miradi ya kitaifa. Kama nilivyoeleza ni kwamba miradi inachukuliwa kuwa ni ya kitaifa pale tu inapoonekana kwamba gharama za uendeshaji na matengenezo ni kubwa. Sasa ninachoweza kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ni kwamba, wakae pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ili waweke mradi huu kwenye kipaumbele. Wakiishauweka kwenye kipaumbele maana yake ni kwamba fedha ambazo zinatoka kwenye *WSDP* kwa maana ya Serikalini basi zote zitaelekezwa kwenye mradi huu mkubwa unaoanzia Njombe kwenda Mbarali.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea kwa sababu majibu yalikuwa marefu na mazuri, sasa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Na. 63

**Kusaidia Sekta ya Uvuvi**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisaidia wakulima wa kipato cha chini kwa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo na hata kwa dawa za mifugo, lakini kwa upande wa uvuvi miradi mingi imekuwa ikielekezwa zaidi sehemu za

mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi kuliko sehemu zingine.

(a) Je, Serikali sasa haioni ipo haja ya kuendeleza nguvu zake pia kusaidia wavuvi wadogo kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika na maziwa mengine nchini?

(b) Vikundi vya wakulima wakishirikiana na halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga wamejenga soko la Kimataifa la Samaki lakini hawana chumba cha baridi *(cold room)* cha kutunzia mazao hayo ya uvuvi. Je, Serikali ipo tayari kusaidia kumalizia ujenzi wa chumba hicho cha baridi ili kukidhi haja ya soko liliyokusudiwa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati ya kuendeleza raslimali za uvuvi nchini zikiwemo zile zilizopo katika Kanda ya Ziwa Tanganyika. Moja ya mikakati hiyo ni utekelezaji wa programu ya uwiano na usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika ambapo wavuvi wadogo wadogo kwenye mwambao wa Ziwa hilo wanajengewa uwezo ili waweze kunufaika na raslimali za uvuvi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya Wachakataji *(fish processors)* wa mazao ya uvuvi 260

kutoka mikoa ya Rukwa na Katavi tayari wameishapatiwa mafunzo ya kuongeza thamani. Vilevile Serikali itajenga mialo minne ya kupokelea samaki katika Manispaa ya Ujiji Kigoma (Kibirizi), Halmashauri za Kigoma (Muyobozi), Nkasi (Kirando) na Mpanda (Ikola).

Hadi sasa maeneo ya kujenga mialo hiyo tayari yameishabainishwa na uchoraji wa miundombinu ya mialo hiyo unaendelea ambapo kibali cha kupata mtaalam mwelekezi wa kusanifu michoro ya mialo hiyo kimeishatolewa. Kukamilika kwa mialo hii kutasaidia wavuvi kuongeza ubora wa mazao yao na kuongeza kipato. Pia Halmashauri zimeelekezwa kuwasaidia wavuvi na wafugaji wa viumbe kwenye maji kupitia mpango wa *DADPs* kuwapatia nyenzo na zana.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuwapongeza Halmashauri ya Sumbawanga ikiwemo na itakayoundwa ya Wilaya mpya ya Kalambo na mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) kwa juhudi zao za makusudi za kujenga soko la Kimataifa la Samaki Kasanga.

Ili kukamilisha mradi huu vizuri ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kutumia sehemu ya fedha za ndani ikiwa ni pamoja na fedha za mapato yatokanayo na shughuli za Uvuvi na kupitia mpango wa *DADPs* kwa ajili ya kujenga chumba cha kuhifadhia samaki na mazao ya uvuvi *(cold room)* kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge. Wizara yangu ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa sababu mchango unaoingia kwenye pato la Taifa kutokana na sekta ya uvuvi umekuwa mdogo sana na sisi tumekuwa mashahidi. Je, ni lini Wizara itatoa uamuzi wa kuwakopesha wavuvi ambao wanatumia zana duni ili waongeze uzalishaji wao? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa, katika ziara ya Mheshimiwa Makamu wa Rais alipotembelea soko la samaki la Kasanga baada ya kujionea mwenyewe alikiri ukubwa wa lile soko. Je, Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bajeti yake kupita twende naye akathibitishe juu ya ukubwa wa mradi ule ili awe tayari kusaidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tena kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakiri kwamba mchango wa sekta ya uvuvi kwenye pato la Taifa ni mdogo. Lakini katika Wizara tayari sera ipo na sheria zinazohusika, na kama Wizara tayari tuna rasimu ya kuendeleza sekta ya uvuvi. Katika rasimu hiyo ambayo programu ipo tayari maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo. Kwa hivyo, nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge kwamba

ninaomba tujaribu kuwahamasisha wavuvi wadogo wadogo ili wajiunge katika vikundi vya kuwawezesha kupata mikopo mara programu hiyo itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Makamu wa Rais alitembelea mkoa wa Rukwa mwezi wa pili mwaka huu na tarehe 23, Februari, mwaka huu 2012 alifungua soko hilo. Katika risala iliyosomwa kwake wananchi walimwomba asaidie katika kujenga *cold room* lakini pia kuhakikisha kwamba nishati ya kuendesha mitambo hapo imepatikana. Yeye alitoa ahadi kwamba atasaidia katika ujenzi wa *cold room*, lakini pili ameishaomba maandalizi yafanyike ili kuwepo na jenereta, na pia utaratibu wa *solar system* kuhakikisha soko hilo litaendeshwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, niko radhi baada ya Bunge hili tuandamane pamoja tukatazame hayo aliyopendekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuna muda mfupi kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi.

Na. 64

**Barabara ya Kwa Sadala – Masama – Mula**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE** aliuliza:-

Barabara ya Kwa Sadala – Masama- Mula wilayani Hai inayojengwa kwa kiwango cha lami ilistahili kuwa imekamilika katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwaka 2010 kwa mujibu wa Mkataba.

((a) Je, ni lini barabara hiyo itakamilika na je, Mkandarasi ameishalipwa kiasi gani hadi sasa?

(b) Je, ni nini gharama ya ujenzi wa barabara hiyo kwa mujibu wa Mkataba na ni kiasi gani cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara hiyo na ni wangapi tayari wameishafidiwa?

(c) Ni kiasi gani cha fedha za ziada kitakacholipwa kutokana na kucheleweshwa kwa ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c ) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Mula yenye urefu wa km. 12.5 ulianza mwezi Mei 2010 na ulitarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja. Mradi huu haukukamilika kama ilivyopangwa kutokana Mkandarasi kuchelewa kufanya *mobilazation* pamoja na kuchelewa kwa uhamishwaji wa miundombinu ya huduma za kijamii za

umeme na maji katika eneo la ujenzi. Aidha, tatizo jingine lilikuwa ukosefu changarawe kwenye eneo la Mradi na kuchelewa kukamilika kwa tathmini ya fidia. Mpaka sasa utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2012. Mkandarasi hadi sasa amekwishalipwa kiasi cha shilingi milioni 1,397.313.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba, mradi huu unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 5,343.455. kiasi hiki hakijumuishi gharama za uhamishaji wa miundombinu ya umeme na maji na fidia. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 101.222 zimetumika kulipia uhamishaji wa miundombinu ya huduma za kijamii na fidia za mali zilizoondolewa kupisha ujenzi. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 90.268 zimetumika kufidia mali za wananchi 23 na shilingi milioni 10.954 zimetumika kugharamia uhamishaji wa miundombinu ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, ongezeko au punguzo la gharama kutokana na mradi kuchelewa endapo litakuwepo, litajulikana baada ya kukamilika kwa mradi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuwliza Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza.

(i)Kwa vile barabara hii inagusa vijiji vya Kwa Sadala, Roo, Sono, Mgwela na Mboreni na inapita katikati ya makazi na mashamba ya watu ambayo ni *densily populated* na kwa maana hiyo barabara hii kukosa *diversions* za kutosha na hivyo kulazimisha

Mkandarasi, mashine zake, wananchi na magari yao kupita barabara hiyo hiyo moja inayojengwa.

Kwa kuwa barabara hii ilipangwa kukamilika katika kipindi cha mwaka mmoja na hadi sasa imekamilika kwa asilimia 40 tu na fedha iliyolipwa ni shilingi bilioni 1.3 na bado tuna bilioni nne (4), na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi kwamba barabara hii itakamilika Desemba 2012 ikiwa ni miezi sita (6) kutoka sasa hivi.

Mheshimiwa Waziri utapenda kuwahakikishia wananchi wa jimbo langu kwamba mwaka huu utakuwa umetenga fedha za kutosha kiasi cha bilioni nne (4) ili kukamilisha azma ya Serikali yetu ambayo ni azma nzuri sana ya kukamilisha barabara hii kabla ya Desemba mwaka huu kama ulivyoahidi kwenye jibu lako?

(ii)Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana yanayohusiana na fidia ya wale ambao wamedhurika na ujenzi huu ikiwemo ukweli kwamba barabara hii itapita katikati ya soko la kihistoria la Masama Mula.

Je, Mheshimiwa Waziri kutokana na wingi wa malalamiko ambayo yananifikia utakuwa tayari tukafanye ukaguzi katika eneo hili ili kuweza kupata ufumbuzi wa kudumu kuhusiana na malalamiko ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme kama nilivyojibu kwamba

barabara hii itakamilika Desemba, 2012, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia kuhakikisha hiyo kazi inakamilika.

Swali la pili kama fedha zitatengwa. Naomba Ndugu yangu Mheshimiwa Mbowe pamoja na Wabunge wengine muunge mkono Bajeti hii ipitishwe ili kusudi fedha hizi ziweze kupatikana. *(Makofi/Kicheko)*

Katika swali la pili kuhusiana na kutembelea mradi naomba nikuhakikishie kwamba tutakwenda kuangalia na kusikiliza malalamiko ya wananchi kuhusiana na hizo fidia ili tuweze kuyafanyia kazi.

Na. 65

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne/Sita Kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha**

**MHE. SILVESTERY F. KOKA** alijiuliza:-

Barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa mbalimbali nchini *(Morogoro Road)* inayounganisha zaidi ya asilimia themanini na tano (85%) ya mikoa na Wilaya za Tanzania Bara pamoja na Nchi jirani inakuwa na msongamano mkubwa wa magari hususan eneo la kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha, hali inayosababisha uharibifu wa Barabara, ajali na muda mwingi kupoteza.

Je, Serikali ina mpango gani kabambe wa kupanua barabara hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha kwa njia nne (*four lanes*) au hata sita ili kuondoa tatizo hilo kabisa.

**NAIBU W AZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestery F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga, "*Express way'* kuanzia Dar es Salaam hadi Chalinze (km 100) ya njia sita (njia tatu kila upande).

Katika taarifa ya tathmini (*preliminary study*) iliyofanyika mwezi Septemba, 2011 imethibitika kuwa kutokana na wingi wa magari yaliyopo katika barabara hii, inawezekana kutekeleza mradi huu kwa njia ya *Public Private Partneship (PPP)* na kuendeshwa kama *toll road* (barabara ya kulipia).

Serikali kwa sasa inatafuta wawekezaji wa ndani au nje ili wawekeze katika mradi huu kwa kujenga *express way* ya njia sita kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kupata mkopo wa muda mrefu kwa ajili hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata fedha kwa ajili ya mpango huu kabambe kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na hatimaye ujenzi wa

barabara ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100) utaanza na baadaye kuendelea hadi Morogoro.

Wito wangu ni kwa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi ya barabara kati ya Dar es Salaam – Morogoro waanze kuondoka wenyewe kwani wanavunja Sheria ya Barabara na hawatalipwa fidia wakati upanuzi utakapoanza.

**MHE. SILVESTER F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa sasa tatizo la msongamano katika barabara hii ni kubwa, msongamano unaoingiliana na watembea kwa miguu, baiskeli pamoja na pikipiki, ambao husababisha ajali za mara kwa mara. Serikali ina mpango gani wa dharura kusaidia kuokoa janga hili ambalo pia linatudididimiza kiuchumi?

(ii) Kwa kuwa, sasa maeneo ya Kibaha, Tumbi, Picha ya Ndege, Kongowe, Misugusugu hadi Visiga kuna barabara ya zamani ya lami, ambayo imetelekezwa na inaendelea kuchakaa?

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo ni mkombozi mkubwa hasa wakati wa ajali na kuondoa msongamano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niseme kwamba, watu wafuate sheria kwa sababu kwenye barabara hizi zipo

njia za watembea kwa miguu, lakini unakuta wengine wanapita na magari. Sasa ni vizuri tukafuata sheria kama tutataka tupunguze ajali. Pia katika upanuzi kama nilivyosema, tutazingatia kuwe na barabara za magari na za watembea kwa miguu na bodaboda au baiskeli.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili, barabara anayoizungumzia ni ya zamani, baada ya kujenga barabara mpya kutokana na Sheria ya Barabara ilishushwa daraja, kwa hiyo, barabara hii inatakiwa itengenezwe na Halmashauri.

Na. 66

## Fidia kwa Mali za Watu Zilizoathiriwa na Ujenzi wa Barabara

**MHE. ABIA M. NYABAKARI** aliuliza:-

Katika ujenzi wa barabara za lami Mkoani Rukwa, kuna nyumba, miti ya matunda, vibao vya shule, miti na mashamba ya watu vinaendelea kuondolewa wakati ujenzi wa barabara unaendelea na wahusika hawajafidiwa kitu chochote:-

Je, ni vigezo gani vinavyotumika ili mtu apewe haki yake au mtu huyu apewe fidia na mwingine asipewe fidia na wote wako kwenye eneo moja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika ili watu walipwe fidia ya mali zao zilizoathirika kwa upanuzi wa barabara ni vile vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Barabara *(Highway Ordinance Cap. 167)* ya Mwaka 1967. Kwa misingi ya Sheria hii, mtu anayestahili kulipwa fidia ni yule ambaye mali zake zipo nje ya eneo la hifadhi ya barabara la mita 22.5 kutoka katikati ya barabara ya zamani na wale ambao wamefuatwa na ongezeko la mita 7.5 kwa kila upande wa Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za Mwaka 2009. Kwa wale waliofuatwa na ongezeko la upana wa hifadhi ya barabara, mali zitakazofidiwa ni zile ambazo zimekuwepo kabla ya Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, watu wote ambao mali zao zilikuwa ndani ya mita 22.5 kila upande wa barabara hawastahili kulipwa fidia kwani wamevunja Sheria ya Barabara ya Mwaka 1967.

**MHE. ABIA M. NYAKABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Katika zoezi la ujenzi wa barabara Mkoani Rukwa kuna nyumba ya mwalimu ilipasuka katika Kijiji cha Mpui, Shule ya Msingi Mpui. Je, Serikali itakuwa

tayari kufidia nyumba hiyo pamoja na wanavijiji wa Matanga, Kisumba, Chala na sehemu nyingine?

(ii) Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kufuatana na mimi kwenda kujionea wewe mwenyewe madhara yaliyopo na ulipwaji ulivyofanyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sheria imetamka mali ambazo zinatakiwa zifidiwe kulingana na hifadhi ya barabara. Sasa kama kuna nyumba ambayo anasema imepasuka, hili ni suala ambalo linatakiwa lifanyiwe utafiti kuonesha kwamba limepasuka kwa sababu ya ujenzi wa barabara au lipo ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo inabidi tuliangalie tuone limepasuka kwa sababu gani, inawezekana nyumba yenyewe ilijengwa kwa tope, sasa ikitikisika lazima itapasuka. Kwa hiyo ni suala la kufanyia tathmini.

Katika sehemu ya pili, nipo tayari kwenda kukagua Mradi huo na nitamwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitakwenda kuangalia hizo athari ambazo anazisema. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umeisha na maswali yameisha, kwa hiyo, nawashukuru sana.

Leo wataalamu wangu wa kuleta orodha ya wageni wamechelewa kuleta, kwa hiyo, wageni nitakaotakiwa kuwatambulisha tutawatambulisha baadaye kidogo kwa sasa hivi orodha haipo. Tuna matangazo mawili tu ya kazi.

Kwanza kabisa, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba, leo tarehe 22 kutakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 219, Jengo la Utawala. Kikao hicho kitafanyika, mnaweza kuruhusiwa hata mapema zaidi kwa sababu nadhani mnaangalia kazi inayohusika. Mtafanya kikao chenu saa 5.00 asubuhi, kwa hiyo, Kamati ya Uchumi na Fedha kwa sababu leo ni siku yetu ya mwisho, tunawaruhusu wafanye kikao saa 5.00, mambo wanayotaka kushauriana na Waziri yawe bayana.

Kuna tangazo la Ofisi linasema kwamba; ninaomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa wanaombwa kurejesha Fomu za Vitambulisho vya Taifa walizopewa kuzijaza. Maafisa wa NIDA wapo Mapokezi, Jengo la Utawala kwa ajili ya kupokea fomu hizi kuanzia tarehe 22 Juni, 2012. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wale waliopokea fomu za kujaza kuhusu vitambulisho ni vizuri mkafanya hivyo na wamefanya vizuri kwa kuwa ninyi mko hapa pamoja mnaweza kufanya hivyo mkarahisisha kazi ya *NIDA* kwa kurudisha zile fomu.

Kwa hiyo, kama nilivyosema, wageni nitawatangaza baadaye sijapata orodha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Unajua mwongozo utaniongoza nini maana mpaka sasa ni mimi niliyefanya kazi mnaniongoza nini? Mheshimiwa Kiwia, tafadhali hebu sema tunakusikiliza.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, ni kwa mujibu wa Kanuni ya 47 ambayo nitaisoma hapa: "Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi na la dharura na muhimu kwa umma."

**SPIKA:** Hebu eleza jambo gani la dharura tuliloliona sisi hatujasikia.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, ninaposimama hapa leo ni siku ya tatu kuna mgomo wa wavuvi na wafanyabiashara wa samaki wa Kanda ya Ziwa. Mgomo huu unatokana na wamiliki wa viwanda kushusha bei ya samaki kwa makusudi kabisa kwa asilimia zaidi ya 50. Bei ya samaki ya awali viwandani walikuwa wananunua minofu ya samaki kwa zaidi ya shilingi 5,000, lakini sasa hivi wananunua kwa shilingi 2,150.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linagusa zaidi ya Watanzania 5,000,000 na zaidi wanaotoka Kanda ya Ziwa; si tu kwamba lina athari katika uchumi, lakini pia linapunguza Pato la Taifa. Kwa ujumla, jambo hili lina-*paralyse* kabisa uchumi wa Wananchi wa Kanda ya Ziwa wanaotegemea biashara ya uvuvi. Kwa hiyo, naliomba Bunge lako Tukufu, nitoe Hoja ya Kuahirisha

Shughuli za Bunge ili kuweza kujadili jambo hili la muhimu linalogusa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiwia, haiungwi mkono na sitatoa ruhusa kwa sababu wanaohusika wanalifanyia kazi na wala hakuna maelezo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Mgomo wa Madaktari

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Sita wa Bunge lako Tukufu, tarehe 3 Februari, 2012, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, alitoa Kauli ya Serikali kuhusu mgomo wa Madaktari uliokuwa umeikumba nchi yetu kwa muda wa takriban wiki mbili. Katika kauli hiyo ya Serikali, ilielezwa kuwa chimbuko la mgomo huu lilikuwa ni madai ambayo yalikuwa yakitolewa na wataalam mbalimbali waliokuwa kwenye mazoezi kwa vitendo *(Interns),* kwa kucheleweshewa posho zao na kwamba wangeitisha mgomo kwa ajili hiyo. Baada ya hali hiyo kujitokeza, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa

Jamii, ilifanya juhudi na kuwalipa walimu hao fedha walizokuwa wakidai. Baada ya malipo hayo kufanyika tarehe 5 Januari, 2012 mgogoro huo ukahama kutoka kwa *Interns* na kuwahusisha wataalamu wa kada nyingine za afya wakiwemo Madaktari. Hivyo basi, mnamo tarehe 14 Januari, 2012 mgogoro ulibadili sura na kuwahusisha Madaktari walio chini ya Chama cha Madaktari Tanzania *(Medical Association of Tanzania - MAT).*

Mheshimiwa Spika, madai yaliyoainishwa na Madaktari ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Mshahara wa Madaktari wanaoanza kazi wa shilingi 350,000;
(ii) Posho ya kuitwa kazini *(On Call Allowance)* ya asilimia kumi ya mshahara;

(iii) Posho ya Mazingira Hatarishi *(Risk Allowances)* asilimia 30 ya mshahara;

(iv) Madaktari kupewa nyumba au posho ya nyumba ya asilimia 30 ya mshahara;

(v) Posho ya Mazingira Magumu *(Hardship Allowance)* asilimia 40 ya mshahara;

(vi) Posho ya Usafiri ya asilimia kumi ya mshahara au wakopeshwe gari;

(vii) Madaktari wapewe *green card* za Bima ya Afya;

(viii) Malipo ya posho ya kuchunguza maiti yaongezwe;

(ix) Kuchukua hatua dhidi ya Watendaji Wakuu wa Wizara; na

(x) Wapatiwe Chanjo ya *Appetites B.*

Jumla ya posho zinazodaiwa ni asilimia 120 ya mshahara huo unaodaiwa wa shilingi 350,000.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Katika kushughulikia mgogoro huo, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati ya Serikali ili kufanya mazungumzo na Wawakilishi wa Madaktari kuhusu madai yaliyowasilishwa Serikalini. Kamati hii imefanya kazi chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na tayari baadhi ya madai yamepatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kufanyika kwa mabadiliko ya Watendaji Wakuu wa Wizara ya Afya;

(ii) Posho ya *Interns* ambayo imeanza kulipwa kuanzia mwezi Februari, 2012 na kupewa kipaumbele na Serikali kupitia Hazina kwa kutolewa mapema kama mishahara inavyotolewa kabla ya *OC;*

(iii) *On Call allowance* imeanza kulipwa kwa viwango vipya kuanzia Februari, 2012. Viwango vipya ni shilingi 15,000 kwa *Interns,* shilingi 20,000 kwa

*Registrars* na shilingi 25,000 kwa Madaktari Bingwa. Tangu malipo haya yalipoanza kufanyika mwezi Februari, 2012 hadi Juni, 2012, Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 7.9. Aidha, malipo hayo yameingizwa katika bajeti mpya ya mwaka 2012/13 na kiasi cha shilingi bilioni 18.9 kimetengwa kwa ajili ya Watumishi wa Sekta ya Afya. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5.4 ni za Wafanyakazi wa Fungu 52 la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, linalohudumia Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali Maalum. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 13.5 ni kwa ajili ya Watumishi wa Sekta ya Afya ngazi za Mikoa na Halmashauri;

(iv) Posho ya uchunguzi wa maiti *(Posterm Allowance),* imeongezwa kufikia shilingi 100,000 kwa Daktari na shilingi 50,000 kwa Wasaidizi kutoka shilingi 10,000 ya awali;

(v) Imekubalika Madaktari wapewe *Green Card* za Bima ya Afya;

(vi) Katika bajeti ya mwaka 2012/13 fedha zimetengwa kwa ajili ya kununua Chanjo ya *Appetites B* kwa ajili ya kuwakinga Wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya;

(vii) Wizara imewasilisha Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) mapendekezo ya muundo kutoka kwa Wauguzi, Wafamasia na Wataalamu wa Teknolojia ya Maabara kwa ajili ya kupitia na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Muundo wa Wizara ya

Afya na Ustawi wa Jamii hususan uanzishwaji wa Idara za maeneo hayo;

(viii) Madaktari watakopeshwa magari kwa utaratibu wa watumishi wa kukopeshwa magari ambapo Watumishi wa Sekta ya Afya watapewa kipaumbele;

(ix) Katika kuboresha mazingira ya kazi, Wizara katika bajeti ya mwaka 2012/13 imeongeza fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa na vifaatiba. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TAMISEMI watasimamia vyanzo vya mapato kutoka Bima ya Afya, Mfuko wa Afya ya Jamii na malipo ya papo kwa papo ya uchangiaji wa huduma za afya ili asilimia inayotengwa kwa ajili ya kununua dawa itumike ipasavyo; na

(x) Wizara imepokea na kuidhinisha fedha za mafunzo ya Shahada ya Uzamili kwa wanafunzi 63 wa *MUHAS* ambao hawakuwa na ufadhili awali.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo hayakuweza kufikiwa mwafaka kwa sasa kutokana na hali halisi ya uwezo wa Serikali ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Nyongeza ya mishahara kwa Madaktari kufikia shilingi 3,500,000, nyongeza iliyowekwa katika bajeti ya mwaka 2012/13 ni asilimia 15;

(ii) Nyongeza ya Posho ya Mazingira Hatarishi *(Risk Allowance)* ya asilimia 30;

(iii) Posho ya Mazingira Magumu *(Hardship Allowance)* asilimia 40;

(iv) Suala la Madaktari wote kupewa nyumba au posho ya nyumba ya asilimia 30; na

(v) Posho ya usafiri ya asilimia kumi.

Hata hivyo, maeneo haya yanazungumzika na Serikali ipo tayari kuyashughulikia kwa awamu kadiri uwezo utakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali imefanya jitihada zifuatazo:-

Baada ya mazungumzo kati ya Kamati ya Serikali na Wawakilishi wa Madaktari, iliyoundwa kushughulikia suala hili, Wawakilishi wa Madaktari waliamua kwenda kutoa taarifa *(feedback)* kwa wenzao katika kikao kilichofanyika tarehe 9 Juni, 2012. Kupitia vyombo vya habari, baada ya mkutano huo walitangaza kuwa Madaktari Wanachama wa *MAT* hawajakubaliana na taarifa hiyo na kwamba wanatangaza mgogoro na Serikali na endapo ufumbuzi wa madai yao hautopatikana baada ya wiki mbili kuanzia tarehe 9 Juni, 2012 walipokutana, watatoa uamuzi wa hatua watakayochukua. Baada ya taarifa hiyo kutokea katika vyombo vya habari tarehe 12 Juni, 2012, nilimwandikia Rais wa *MAT,* Ndugu Namala Mkopi, kumsihi na kumtaka yeye na Uongozi wa Chama chake wakutane nami ili kuzungumzia maeneo

ambayo hawakukubaliana na Kamati ya Serikali ili kuyatafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Rais wa *MAT* alitoa jibu kwamba, wamekuwa na mazungumzo na Kamati ya Serikali kwa takriban miezi mitatu bila kuona mafanikio waliyotarajia na kwamba kwa kuwa Bajeti ya Serikali imeshapangwa, hawana imani kwamba mazungumzo zaidi yataleta tija. Matarajio yangu yalikuwa kwamba, baada ya Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya Viongozi wa Wizara ya Afya, Madaktari wenzangu wangenipa nafasi ya kujadiliana nao ili kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huu. Wizara ya Afya ina timu mpya ya Uongozi kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Kaimu Katibu Mkuu na Kaimu Mganga Mkuu Kiongozi na sote tulikuwa na dhamira njema ya kufanya majadiliano na Madaktari kwa madhumuni ya kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huu.  Kwa bahati mbaya sana, hawakuwa tayari kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea taarifa kutoka Mikoani kwa Viongozi Wawakilishi wa Madaktari wa Chama cha Madaktari Tanzania *(MAT)*, wanatembelea mikoani kuwashawishi Madaktari na watumishi wa kada nyingine za Sekta ya Afya kuunga mkono nia yao kutokubaliana na hatua zinazochukuliwa na Serikali na kujiunga na mgomo pale watakapopeana taarifa rasmi. Mikoa waliyotembelea ni pamoja na Dodoma, Mwanza, Shinyanga, Mara, Kilimanjaro na Mtwara.  Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa alikataza vikao hivyo visifanyike.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa; kwa kuwa suala hili lipo chini ya Mahakama kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, yaani *The Commision for Mediation and Arbitration*, Serikali pamoja na Madaktari tunatakiwa kufuata taratibu na kurudisha suala hili kwenye Tume hiyo kwa hatua zaidi. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 19 Juni, 2012, pande zote mbili ikiwa ni Serikali kwa upande mmoja na Chama cha Madaktari kwa upande mwingine, walipeleka taarifa ya mgogoro uliokuwepo na kuelezea hatua zilizokuwa zimefikiwa hadi wakati huo mbele ya msuluhishi kama ilivyotakiwa. Baada ya msuluhishi kusikiliza maeneo hayo, alitoa maoni yafuatayo na naomba kunukuu: “Kuwa mgogoro umekosa suluhu, pande mbili kwa pamoja wamekubaliana kwamba, mgogoro huo umekosa suluhu katika hatua iliyopo ya usuluhishi na kuwa wamekubaliana kupeleka mgogoro huo Mahakama Kuu.”

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hiyo, hivi sasa hatua iliyopo ni mgogoro huu kupelekwa Mahakama Kuu, Kitengo cha Kazi, ili Mahakama iweze kutoa uamuzi wake. Serikali itakuwa tayari kutekeleza maamuzi yoyote yatakayotolewa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti ambao umekuwa ukiikabili Serikali yetu, Serikali kwa muda wote imekuwa ikithamini taaluma ya Madaktari na taaluma nyingine. Kwa kudhihirisha hili, ningependa kuelezea mambo yafuatayo:-

(i) Wanafunzi wote wanaosomea Udaktari nchini wamekuwa wakipata udhamini wa Serikali kwa

masomo yao kwa asilimia mia moja bila ya kukopeshwa na Bodi ya Mikopo, tofauti na fani nyingine ambazo hukopeshwa na baadaye kutakiwa kurejeshwa mkopo huo wa masomo kwa Serikali;

(ii) Udaktari ni taaluma pekee katika Utumishi wa Umma ambapo wakiwa wameajiriwa bado Serikali imewaruhusu kufanya kazi katika sekta binafsi kwa muda ambao hawapo kazini, yaani *Private Practise* tofauti na kada nyingine za watumishi wa taaluma zingine kama vile Wanasheria na kadhalika; na

(iii) Mwaka 2005 Serikali ilifanya uamuzi wa kuweka muundo mzuri wa mishahara ya Watumishi wa Sekta za Afya ambao kwa sasa mshahara wa kuanzia wa Daktari aliyemaliza mafunzo ni shilingi 957,700, ikilinganishwa na kada nyingine kama Wahandisi ambao wamemaliza digrii kama Madaktari, wao wanaanza na mshahara wa shilingi 600,000 na Wahasibu wanaanza na shilingi 300,000 mpaka shilingi 400,000. Juhudi hizi zilifanywa kwa makusudi, Serikali ikitambua kwamba wote ni watumishi muhimu, lakini kwa Madaktari ambao wanashughulikia maisha ya watu ilionekana kuwa kuna umuhimu wa kuwaongezea kufidia ugumu wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande mwingine imejitahidi kwa kiasi kikubwa, kuboresha huduma za afya nchini kwa hatua mbalimbali kama vile kununua vitendea kazi na vifaa tiba, kufanyia ukarabati hospitali mbalimbali zikiwemo za Rufaa na kadhalika. Kutokana na jitihada zote hizi za Serikali, ninawasihi Madaktari wote nchini, waone kuwa Serikali ina nia njema katika

suala hili na wakubaliane na mapendekezo yanayotolewa na Serikali kwa kuwa bado ina nia ya kuboresha mazingira ya kazi zao na kuyapatia ufumbuzi wa madai yao ili kuwepo na ufanisi katika utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kadiri ya uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosikia katika vyombo vya habari kwamba, Madaktari kupitia chama chao, wanatarajia kuitisha mgomo mwingine kuanzia tarehe 23 Juni, 2012; ninatoa wito kwa Madkatari nchi nzima kuacha mpango huo kwa sababu madhara yatokanayo na mgomo wa Madaktari ni makubwa na yanagharimu maisha ya watu moja kwa moja, tofauti na migomo inayofanywa na kada nyingine za wafanyakazi. Hivyo, hawana budi kufikiria kwa kina ili kuepuka madhara ambayo yatagharimu maisha ya Watanzania wasio na hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 76(1) cha Sheria ya Mahusiano Kazini (Namba 6) ya Mwaka 2004, kinabainisha makundi ya wafanyakazi ambao hawaruhusiwi kugoma. Moja kati ya kundi hilo ni wafanyakazi ambao wameajiriwa katika huduma muhimu, yaani *essential services.* Kifungu cha 77(2) cha Sheria hii kimeainisha huduma ambazo ni muhimu kama ifuatavyo: Mji na usafi; umeme; afya na maabara; zimamoto na udhibiti wa safari za anga na mawasiliano ya ndege.

Mheshimiwa Spika, Serikali muda wote imeonesha nia njema ya kujadiliana na Uongozi wa Madaktari ili kutafuta ufumbuzi wa masuala waliyoyawasilisha kwa

kuzingatia uwezo wa Serikali. Hivyo, kwa mara nyingine ninawasihi sana wasichukue hatua za kugoma na wawe na subira hadi mwafaka utakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Matumizi ya Mwongozo siyo sahihi, kila wakati mnaomba mwongozo. Hapa nina kauli ya Waziri wala sijasema kitu, ninyi mnaanza na Mwongozo wa Spika. Sivyo hivyo, hii ni Taarifa ya Serikali na suala lenyewe sasa linaenda Mahakamani. Naomba liende huko.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nina Wabunge wale niliosema nitawatambua. Naomba Ofisi yangu muwe mnawahi kwa sababu kila kitu kinakwenda kwa utaratibu wake. Pale kwenye *Speaker's Gallery* kuna Viongozi kutoka Kanisa la Pentekoste, nafikiri Jimbo Kukuu hapa Dodoma. Yupo Mhashamu Askofu Dkt. Damas Mkasa, amefuatana na Mchungaji Bathoromayo Chegetela na Mchungaji Nestory Zakaria. Nadhani kuna mgeni mwingine ambaye sijaona jina lake.

Wapo wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Wanafunzi 85 na Walimu wao kutoka Chuo cha Diplomasia cha Dar es Salaam, wakiongozwa na *Dean of Student* ambaye ni Dkt. Hatib Kilagiza na Nemela Mangula, Rais wa Wanafunzi

na Wanafunzi wote. Karibuni sana, tunaamini kabisa mnafanya wajibu wenu wa kusoma vizuri na kama tunavyosema wakati wote maisha ni matatizo siyo starehe. Kwa hiyo, matatizo mnayoyapata pale shuleni ni sehemu ya mafunzo ya maisha muyavumilie msome vizuri.

Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga ni mwanafunzi mwenzao waliyesomea naye pale. Kwa hiyo, karibuni sana. Mheshimiwa Said Mtanda, amewahi kusomea pale kwa hiyo amewaalika wenzie.

Kuna wageni 20 kutoka Jimbo la Hanang, Mkoa wa Manyara; naomba wasimame. Ahsanteni sana na karibuni sana.

Kuna wanafunzi 45 wanaofanya mafunzo ya vitendo hapa Bungeni. Hawa ni wanafunzi wanaofanya *practical* hapa Bungeni; wako wapi? Nadhani wametoka, karibuni sana na mtakutana na Wabunge wakati wowote ule, kwa hiyo, mnatakiwa kuwa na tabia njema wajue ninyi ni wanafunzi ambao mko kwenye *practical.*

Tuna wanafunzi 22 kutoka Chuo cha Ardhi kilichopo Tabora. Ahsanteni sana na nadhani mtapata nafasi ya kuongea na Waziri wenu wa Ardhi na Naibu Waziri yupo hapa.

Kuna Walimu 17 na Wanafunzi 30 wa Shule ya Msingi ya Jimbo la Chilonwa, Kata ya Machali

Dodoma; hawa wako wapi? Karibuni wengine wako hapa juu; ahsante sana Walimu na Wanafunzi.

Tunao wanafunzi wanaosoma mwaka wa tatu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM);* naomba wasimame walipo kama hawapo watakuwa wamekosa nafasi kwa asubuhi hii na nadhani watapata nafasi baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, lile swali ambalo Mheshimiwa Kiwia aliliuliza, naomba Serikali itoe kauli Jumatatu kwa sababu suala lenyewe ni ubishani kati ya wavuvi na wale wanaonunua mazao. Sasa fikiria sisi hapa ni jambo la dharura tutasemaje. Jambo la dharura ni lile ambalo sisi tukifanya tutachukua hatua lakini lile ni mabishano yaliyopo kati ya wanunuzi na wavuvi. Kwa hiyo, naomba Serikali itupe kauli kuhusu suala alilosema Mheshimiwa Kiwia.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SULEIMAN MASOUD NCHAMBI SULEIMAN:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika kuhusu nini?

**MHE. SULEIMAN MASOUD NCHAMBI SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 47. Kwa kuwa tatizo la wavuvi linafanana na wakulima wa pamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nasema hivi, naomba ukae; Kanuni zinasema jambo fulani likikataliwa huwezi kuuliza tena. Sasa tumelikataa lile

wewe tutakupaje nafasi? Tunaendelea. Katibu, hatua inayofuata.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hapana, mwongozo unatumika vibaya. Katibu tunaendelea na kazi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, napongeza serikali kwa kuandaa Bajeti nzuri ambayo itaendeleza programu mbalimbali za mwaka uliopita. Hata hivyo nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, ingawa serikali imefuta kodi kwa bodaboda jambo ambalo ni zuri lakini nachelea kuamini kuwa vijana wote hao hizo pikipiki ni zao. Wao vijana ni wafanyakazi tu wengi wao sio wamiliki. Hivyo basi tunaweza kufikiri tunawasaidia vijana kumbe

tunawasaidia wamiliki kukwepa kodi. Naomba suala hili serikali litafakari upya hata kwa Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaanza sasa kuwa mazoea kwamba fedha tunazopitisha Bungeni hazitolewi ipasavyo kwenye Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali, nashauri serikali ihakikishe kuwa fedha zinazopitishwa zitolewe vilivyo na zisitumike kwa matumizi yasiyopangiwa au yasiyokusudiwa. Kwa kutosimamia matumizi vizuri, nchi itakosa mtiririko mzuri wa kukamilisha programu mbalimbali zinazopangwa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 47 wa Bajeti (hotuba) nimefarijika kusoma kwamba mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam utaanza kutekelezwa ukiwa unasimamiwa na *TPDC.* Naamini shida ya umeme itakwisha kabisa au kupungua wakati gesi hiyo itakapotengeneza umeme ambao utakuwa wa bei rahisi ukilinganishwa na huu unaotokana na mitambo ya mafuta tena ya kukodisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nahitaji ufafanuzi ni kwa jinsi gani maeneo litakamopita hilo bomba watafaidika na umeme utakaotokana na gesi hiyo. Nahitaji ufafanuzi huo ili isije ikajitokeza changamoto kama ilivyokuwa kwa maeneo/vijiji vilivyopita bomba toka Songosongo mpaka Dar es Salaam ukurasa wa 48 wa hotuba serikali imedhamiria kuimarisha mawasiliano kwa TEHAMA ili kuboresha upatikanaji wa taarifa za makisio ya ndani na nje ya nchi. Napongeza sana dhamira hii lakini kwa upande mwingine nadhani lengo

hili halitafanikiwa kwa sababu gharama kwa watumiaji simu za viganjani *(airtime)* zimeongezwa toka asilimia 10 hadi 12. Nashauri kodi/tozo iongezwe kwa watoa huduma i.e. mitandao ya simu iliyopo nchini kuliko kumwumiza mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali ione uwezekano wa kupunguza *PAYE* kwa waajiriwa hapa nchini kwa sababu hata kama wafanyakazi wataongezewa mshahara bado hali yao itakuwa duni tu kwa vile jinsi mshahara unavyopanda ndivyo *PAYE* inavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, wastaafu kwenye Bajeti hii wamesahauliwa na ni wazi maisha yao ni magumu sana na familia zina maisha magumu ya ombaomba na njaa kali.

Mheshimiwa Spika, hata mafao yao wastaafu wanayopata wakati wa kustaafu si sahihi, kwani imeonekana wanapunjwa na imedhihirika wakati wa kukokotoa hesabu sahihi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 kati ya majalada 4960 yaliyokaguliwa majalada 137 yangelipwa pungufu shilingi milioni 167.

Mheshimiwa Spika, mtindo huu umebainika tena mwaka 2010/11 katika majalada 4788 yaliyokaguliwa majalada 282 yangelipwa pungufu milioni 539.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hizi toka *CAG* imedhihirisha hata wale wanaolipwa ziada kuna mchezo mchafu unaofanywa katika miongoni mwa walio na dhamana ya kuwapatia wastaafu haki zao.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi unapomlipa mtaafu pensheni ya kila mwezi Sh. 50,144/= wastani wa Shilingi 1700 ni aibu kubwa kwa serikali kutowajali wastaafu wake.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri serikali kuandaa mazingira ya kuboresha mazingira ya mafao ya wastaafu angalau pensheni ya kima cha chini angalau Shilingi 300,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya serikali imegusia ajira, Mkukuta II, na kuendeleza viwanda lakini inasikitisha kwamba Bajeti imeshindwa kutenga fedha za kufufua viwanda, vingi vimekufa. Viwanda vya korosho Kusini mikoa ya Lindi na Mtwara. Kiwanda cha magunia moshi kimekufa. Kiwanda cha Urafiki Ubungo cha Kanga na vitenge na vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, serikali ni vyema ikaandaa mazingira ya kufufua viwanda vilivyokufa na kuongeza ajira kwa vijana na hapa dhana ya Mkukuta II utaweza kutekelezeka kwa uhalisia na kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii ya Bajeti. Nina maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *SAGCOT* imemegewa pesa nyingi sana za Bajeti hii na miradi mingine ya *ASDP* na *DASIP* zimepunguzwa pesa. Naomba mwaka kesho msirudi na *SAGCOT II.*

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme vijijini, mji wa Hungumarwa umeshafanyiwa usanifu wa kupata umeme lakini mwaka umeisha umeme bado na Bajeti hii iweze kuleta umeme hapo Hungumarwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji vijijini naomba pia iliyotengwa ipelekwe kama ilivyopangwa. Sisi tarafa ya Mwamashimba, wilaya ya Kwimba maji ya visima virefu hayapatikani tunategemea marambo na maji ya bomba ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *CDF,* naomba huo mfuko uongezewe pesa kwa sababu huo mfuko huwa unasaidia wananchi kwa miradi midogo midogo. Tunazipelekea fedha kutoka mfuko huu wa *CDF,* wakati tukisubiri miradi mikubwa ya serikali.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya huduma za simu. Naomba kushauri serikali iangalie huduma ya M-pesa inayotolewa na haya makampuni kama ifuatavyo:-

(i) Wana masharti yanayofanana na mabenki;

(ii) Wanaweka akiba *BOT* kama mabenki;

(iii) Wanatoza kodi kwenye huduma hiyo;

iv)Kwa siku ni bilioni 4 inazunguka; na

(v) Watu wanaajiriwa, hivi huduma inaweza kutumika na fedha chafu mbaya inahatarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege – Mwanza umepangiwa pesa mwaka huu 2012-2013 naomba hiyo pesa ifike kwa muda uliopangwa tumesubiri miaka mingi wana Mwanza kupata uwanja wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, reli naomba kama ilivyopangwa kwamba Desemba mwaka huu itafika Mwanza kupitia Kwimba mimi naomba hili litekelezwe kwa kikamilifu hii ndiyo njia pekee ya kupunguza hali ya wananchi kwa sababu ya gharama ndogo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo na mbegu, mimi naomba serikali ituongezee mbegu za pamba na mahindi kwa wilaya ya Kwimba mbegu zinazoletwa hazitoshi tunaomba ziongozwe.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais, aliahidi barabara ya lami kutoka Magu – Ngudu – Hungumarwa. Naomba hiyo barabara iwekwe kwenye Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika naunga mkono Bajeti. Ahsante sana.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya wizara ya nchi ya Ofisi ya Rais. Vijana wengi wanatoka vijijini wanakimbilia mjini yaani hawa vijana hawajawezeshwa na serikali haijawa *serious* kwa kuwezesha vijana katika sekta ya kilimo. Imekuwa ni mipango isiyotekelezeka kwa muda mrefu nakupekea vijana wengi kukata tamaa na kukimbilia mjini na hili suala la kilimo kwanza limekuwa kama wimbo wa Taifa. Na ukiangalia wanaonufaika ni watu wa chache walengwa wakuu hawanufaiki na hilo suala la kilimo kwanza mpaka sasa. Ukiangalia mpaka sasa benki za wakulima bado hazijawafikia walengwa ni lini benki hizo zitatawanya matawi ili kuwafikia walengwa vijijini? Serikali ihakikishe wakulima wanapata pembejeo kwa wakati muafaka asilimia kubwa ya wanawake wa vijijini wanatumia jembe la mkono ni lini serikali itawapatia wanawake hao kilimo cha kisasa kama matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, swala zima la miundombinu, nchi yoyote yenye maendeleo lazima tuwe na reli ya kusafirishia mizigo, barabara na kadhalika. Lakini leo hii Tanzania hatuna reli ya kusafirishia mizigo ukiangalia wakulima wengi wanashindwa kusafirisha mizigo kama mazao na wafanyabiashara nao wanashindwa kusafirisha bidhaa zao ni lini serikali itaonyesha kwa vitendo kushughulikia suala zima la miundombinu hususan reli? Ili kuingizia serikali pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la uchumi kumekuwa na ubadhirifu yaani baadhi ya viongozi wamekuwa wakijilimbikizia mali yaani kuchukua mali za Umma na kuingia mikataba mibovu na kuisababishia serikali hasara ya madeni na wananchi kubaki maskini na kutoipenda serikali yao. Je, ni kwanini watu ambao wanahujumu uchumi wa taifa letu hawafilisiwi mali zao na kufungwa? Ni kwanini mikataba ya wawekezaji haiwekwi wazi kwa wananchi wakaifahamu na mikataba hiyo kufanywa na watu wachache? Ukiangalia kama sekta ya madini hainufaishi wananchi waliozungukwa na migodi hiyo hawanufaki na madini hayo wanaonufaika ni watu wachache ukiangalia hawa huduma za jamii kama shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ukusanyaji wa mapato ya serikali, wawekezaji wengi wamekuwa wakikwepa kulipa kodi serikalini na kuisababishia serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenye maendeleo itategemea ulipaji kodi lakini Watanzania wengi hawalipi kodi. Kwa mfano Kariakoo baadhi ya wafanyabiashara hawalipi kodi hata maghorofa ambayo yanajengwa Kariakoo yana pesa chafu (haramu) na wafanyabiashara wengi wa magorofa hayo ukianza kuwachunguza hawalipi kodi na kuisababishia Serikali hasara kubwa ya pato la taifa. Nashauri serikali iangalie kwa makini vyanzo vya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwani vyanzo hivi kuna baadhi ya viongozi si waadilifu wanajilimbikizia mali kupitia mapato ya serikali.

Mheshimiwa Spika, suala zima la Afya, serikali haijawa *serious* kuhusu suala zima la afya na Bajeti hii naona haikidhi katika suala zima la afya na kila siku tumekuwa tukiwapoteza baadhi ya akinamama wanapokuwa wanaenda kujifungua kutokana na hospitali kukosa madawa ya kutosha na vitendea kazi na majengo kuwa chakavu, kukosa madaktari bingwa na kumekuwa na upungufu wa wauguzi na baadhi ya Watanzania kupoteza maisha. Kwa hiyo, Bajeti hii haijakidhi katika suala zima la afya.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nianze na kutounga mkono Bajeti hii kwa kuungana na wachangiaji wengine kuwa Waziri wa Fedha airudishe na kuifanyia marekebisho kwa baadhi ya maeneo kama kilimo na ufugaji, afya, miundombimu, elimu, misamaha ya kodi, kwa nini mfumko wa bei uko juu sana ambao unazidi kumkandamiza Mtanzania. Bajeti ya 2011/2012 ilikuwa asilimia 35 Bajeti ya 2012/2013 itakuwa asilimia 30 kwa nini ishuke badala ya kupanda? Nami siungi mkono Bajeti ilirudishwe na kurekebishwa upya.

**MHE. GRACE SINDATO KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu huu kwa maandishi, kuhusu mapendekezo ya Makadirio ya Bajeti ya serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe msimamo wangu kwamba siungi mkono Bajeti hii iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Imekuwa ni kawaida ya serikali

hii ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kutuletea Bajeti ambazo hazitekelezeki, sitakuwa tayari kupitisha tarakimu kubwa za mabilioni ya fedha ambazo mwisho wa siku hazifiki kwenye wizara kama tulivyozipitisha katika Bunge letu hili lazima ifike wakati serikali hii ambayo ndiyo yenye jukumu la kukusanya kodi kutimiza yale ambayo waliwaahidi Watanzania yaani maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa Bajeti zetu hazieleweki tunataka nini kila mwaka vipaumbele kila siku vinabadilika. Kutangatanga huku ndiko kunakosababisha kutokuelewa vipaumbele tulivyopitisha mwaka jana vinaweza kufanikiwa kwa kiasi gani ili tujue tulikwama wapi ili tuongeze fedha eneo hilo ili mwisho wa siku kuwe na kitu cha kuonyesha. Kwa utaratibu huu tunaokwenda nao wa kila mwaka kutoa vipaumbele vipya tunaendelea kuzalisha madeni ya miradi iliyoko kwenye hivyo vipaumbele ambavyo havikamiliki. Suala la kilimo limekuwa likisemwa kila siku lakini hakuna mabadiliko yoyote ukizingatia asilimia 80 katika nchi yetu ni wakulima tena wengi wako vijijini ambako hakuna msaada wanaopata kutoka serikalini mpaka sasa hilo suala la kilimo kwanza, kwao ni kama ndoto bado wanatumia jembe la mkono pembejeo hawazipati bado wakivuna hawana soko la kuuza bidhaa zao.

Wafanyabiasahara wachache ndiyo wanaonufaika kwa kwenda huko vijijini kununua mazao hayo kwa bei rahisi na kumwacha mkulima huyu kuendelea kuwa maskini. Nafikiri umefika wakati wa kujua kuwa wakulima wako wangapi na tujue

mahitaji yao pia tuzungumze nao, kwani itawezekana yale mazingira mazuri wanayopewa wawekezaji kwenye mashamba makubwa na watu wetu wapewe ili kuwawezesha wananchi wetu kumiliki mashamba madogo na kuwatengenezea miundombinu ambayo itawawezesha kuitumia. Kwa kufanya hivyo kutaweza kuajiri watu wengi katika eneo hili la kilimo badala ya mtu mmoja kuwa na mashamba makubwa na kuacha wananchi wetu kuwa vibarua katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, huduma muhimu kama simu serikali inaongeza kodi kwa mwananchi ambaye amekuwa akilipa gharama kwa makampuni haya hii haiingii akilini kabisa kama serikali imeshindwa kutafuta njia nyingine ya kuongeza mapato yake ikaona irudi kwa mwananchi yule yule akilipia kodi kupitia simu. Niunge mkono mapendekezo ya msemaji wa kambi ya upinzani kwamba kodi hiyo ilipwe na kampuni za simu kupitia kodi ya mapato na kwa wananchi kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa *TRA* imevuka malengo kwa kukusanya zaidi (asilimia 104). Ningetaka kujua kama tulivuka malengo ni kwanini fedha tulizopitisha kwenye wizara, Mikoa na Halmashauri zetu hazikupelekwa na kusababisha miradi mingi kushindwa kutekelezwa kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limekuwa linajitokeza kila Bajeti ni kuongeza kodi kwenye sigara, soda, pombe, hivi ni nchi gani duniani inayotegemea vitu hivyo tu kila mara kuongeza pato la nchi? Hii imesababisha wananchi wetu wengi kuishia kunywa

pombe ambazo hazina ubora wa kutosha na kuwasababishia madhara katika miili yao. Hivi ikitokea Watanzania wakiacha kuvuta sigara na kunywa pombe nchi yetu itakuwa kwenye hali gani? Tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana kwenye misamaha ya kodi hasa kwenye eneo la madini. Ni kwa nini hatutaki kuachana na mikataba hiyo ambayo inawanufaisha wawekezaji toka nje na kuwaacha Watanzania wakiumia kwa kutozwa kodi ambazo hazina msingi zinawaumiza tu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ila siungi mkono Bajeti hii.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imetofautiana na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ulitoa mapendekezo yake katika matumizi ya miradi ya maendeleo kwa kutenga asilimia 35 lakini Bajeti imeshuka na kuwa si zaidi ya asilimia 30 ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imezingatia matumizi holela yasiyokuwa ni ya kutatua matatizo ya wananchi wa Tanzania. Bajeti imelenga katika makongamano, semina, warsha, safari za viongozi, pango na kuanzisha Mikoa na Kata za kisiasa. Mwaka 2011/2012 Bajeti ya jumla ilikuwa trilioni 13 na matumizi katika miradi ya Maendeleo trilioni 15 wakati matumizi ya miradi ni 4.5. Hivyo utaona ni kwa jinsi gani Bajeti hii haiwezi kukwamua matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuzingatia mgawanyo mzuri wa kutoa vipaumbele ukiangalia Bajeti ya mikoa ya Kusini haimo kabisa katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji wakati Kusini ina hazina ya mito mikubwa mingi kama Rufiji, Matandu, Mavuji, Mbwemkuru, Lukuledi, Lumesule, Ruvuma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikutaja mpango wa kuongeza nguvu ya umeme kwa wananchi wa mikoa ya Kusini. Bali imezingatia kuhamisha gesi ya *Mnazibay* na kwenda kuongeza nguvu maeneo ambayo tayari umeme upo tena umeme wa gridi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikutaja mapato ya serikali yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru kupitia stakabadhi ya mazao ghalani. Ni kiasi gani kimekusanywa tokea mpango huo uanzishwe na ni yapi manufaa waliyopata wazalishaji wa korosho wa mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti imetaja mfumuko wa bei na hasa katika bei za vyakula ambapo kuna ongezeko la kutoka asilimia 12 - 26 mwaka 2011 na sasa kuwa wastani wa asilimia 24 lakini ukiangalia mahitaji ya Mtanzania nusu ya gharama inatumika kwa mahitaji ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imeendelea kufuata utaratibu wa *Cash Budget.* Hili ni tatizo si tu la kitaifa bali hata katika Wilaya na mikoa. Mradi mingi ya Maendeleo imekwama kutokana na kukosa fedha, mikopo ya fedha na fedha za wahisani. Leo mpaka tunamaliza Bajeti ya 2011/2012 si zaidi ya asilimia 30 ya

Bajeti katika Halmashauri ya Lindi ilifika kwa miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawakopesheki kutokana na vikwazo na vigezo vinavyotumiwa na wakopeshaji. Mfano SUMA JKT ambao wanahitaji kupata dhamana ya mali isiyohamishika kama nyumba au shamba. Hivi mkulima gani au wakulima wangapi wenye uwezo wa kumiliki mali hizo.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawazingatiwi katika kupanga Bajeti ya pembejeo kwa wakati, wakati serikali ikipanga mipango yake ya matumizi hapa Dodoma. Mkulima wa Lindi na Mtwara ana haha kutafuta sulphur kwa ajili ya mikorosho yake mpaka *sulphur* inapofika msimu wa upuliziaji umeisha na hivyo kumkosesha mkulima mazao.

Mheshimiwa Bajeti hii haikueleza kinagaubaga mpangilio wa utoaji ajira na hasa katika sekta isiyo rasmi. Lakini kilichopo hata kwa wale wanaotakiwa kuajiriwa ukiritimba umekuwa mkubwa, ukiangalia katika maeneo ya utoaji leseni upatikanaji viwanja na mashamba, pembejeo, madawa na vifaa vya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuzingatia malengo ya milenia kwa kutozingatia kumsaidia mtoto katika sekta ya Afya. Utafiti unaonyesha matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa bado ni hafifu na hasa vijijini. Matumizi ya dawa za kuongeza maji na kupunguza magonjwa ya matumbo (*oral dehydration*) na kadhalika umekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imethubutu, imeweza na inasonga mbele katika kuona maisha ya Mtanzania yanazidi kudidimia. Ni wakati pekee kwa serikali kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya kwa:-

(i) kuhakikisha jamii, taasisi katika kupanga mipango yake ya mandeleo;

(ii) iondoe misamaha holela kwa wawekezaji;

(iii) idhibiti wanaokwepa kulipa kodi; na

(iv) iwekeze katika miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho siungi mkono hoja.

**MHE. LAMECK OKAMBO AIRO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Bajeti hii kama ifuatavyo. Bajeti hii kwa kweli haijengi kwenye miradi ya maendeleo ikilinganishwa na ahadi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliyowaahidi wananchi wakati wa uchaguzi uliopita. Kwa maana hiyo mimi ninashauri miradi ya maendeleo isogezwe hadi asilimia 35 au 40.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ingeelekezwa sana kwenye Kilimo hasa kwenye kilimo cha kumwagilia hasa sehemu ambazo hazipati mvua mara kwa mara kanda ya Ziwa na kanda ya kati.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa pamba bei katika soko la dunia imeshuka. Bodi ya pamba

imepanga bei kati ya Sh. 510 mwaka jana bei ilikuwa Sh. 100 na 1200 nashauri serikali itoe ruzuku ya Shilingi Kati ya 300 au Shilingi 400

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda viwanda vya ndani. Pamekuwepo na tatizo la ajira katika nchi yetu lakini kwa makusudi serikali ikiamua kulinda viwanda vyetu vya ndani na kuviwezesha kuongeza mazao yatokanayo hapa nchini yatafanyika hapa Tanzania na thamani hizi zifanyikie kule kule mazao yanakolimwa ili kuzuia vijana kukimbilia mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri: Mfumo wa bidhaa zinazotokana na pamba zipewe msamaha wa ongezeko la kodi *(VAT) – zero rate* kwa bidhaa za nguo na mavazi hii itaongeza mapato na ajira kwa wafanyakazi kulipa *(PAYE).*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Bajeti Bungeni.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi la kulizingatia na kudhibiti mfumko wa bei za vyakula ili kutunza mapato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii haikuzingatia punguzo hasa katika vifaa vya ujenzi kama vile bati na saruji, hii ingesaidia sana wananchi kuweza kumudu kununua vifaa hivyo, na hivyo kuweza kupata kuishi

katika nyumba iliyo bora kiafya. Kwa maana hiyo haya mambo mawili niliyoyataja – kupunguza bei za vyakula na kupunguza bei za bati na saruji itawafanya wananchi walio wengi kumudu kwa kuanza kutadhimini maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii kwa kiasi kikubwa haioneshi umakini wa ukusanyaji wa mapato/kodi.

Mheshimiwa Spika, kama walivyoshauri wengine kuelekeza nguvu zake zote kwa makampuni yote ya simu makampuni yote ya madini nishati kukusanya kodi kwa ajili ya Maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa kuwa makini kuweka mkazo mkubwa juu ya miundombinu ya kibiashara zaidi kama vile reli, viwanda na bandari. Mambo haya matatu kama tunakuwa makini sana kwa kuzingatia (1) Reli, (2) Bandari (3) viwanda maendeleo ya Tanzania yatakuwa kwa kiwango kikubwa kodi kufikia asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka maendeleo katika mpango wa maendeleo lazima uweke vipaumbele hivi katika angalau asilimia 50 ya Bajeti yote ili kuona hatua hii inasaidia hata nchi jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mgimwa kuteuliwa na

Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara ya Fedha, ambayo ni kitovu cha serikali. Pia niwapongeze wanawake wenzangu walioiweka historia na kuwa manaibu Waziri wa Fedha kwa pamoja. Mheshimiwa Rais kuna uhakika ameunda "*the winning team*" kumteua Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, kama Manaibu Mawaziri, Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pili nitoe pongezi kwa umahili wao Mheshimwa Waziri Mgimwa, kwa Bajeti ambayo ameiandaa kwa ufasaha na kwa muda mfupi tangu aanze kazi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nieleze kabisa kuunga mkono hoja. Ninataka hata hivyo yafuatayo yafafanuliwe vyema zaidi ili wananchi waelewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono uamuzi katika ibara ya 97 (i) Kufanya marekebisho ya sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kuweka kiwango cha chini cha mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo cha sh. Milioni 3 kisichotozwa kodi. Hatua hii ni muhimu na itasaidia kuwawezesha vijana wetu wanaojiajiri kufanya biashara zao ndogo ndogo bila kubugudhiwa hadi mtaji wao utakapoongezeka. Hata hivyo kuna umuhimu kwa Mheshimiwa Waziri kufafanua kwamba kundi hili la wafanyabiashara wadogo wadogo pia linajumisha wakulima wanauza mazao yao sokoni. Ni jambo la kusikitisha kwamba Halmashauri nyingine zimekuwa kero kwa wananchi. Badala ya kuweka utaratibu kuunda vyama vya ushirika ili kukusanya mapato kwa utaratibu wa *CESS* wameibuka na *barriers*

barabarani na wanawaharass wakulima wanaokwenda sokoni kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Muleba wanateswa sana na utaratibu huu. Utakuta mkulima anatozwa sh. 200 kwa mkungu wa ndizi. Kama atafanikiwa kuuza Sh. 5000 atakuwa ametozwa asilimia nne ya mapato yake, kiwango ambacho kiko juu sana. Mbaya zaidi anazuiwa na kulipishwa kodi hiyo njiani kwa hiyo mkulima huyo asipompata mnunuzi wa ndizi yake basi anakuwa amelipa kodi hiyo kutoka mfukoni mwake kwa hiyo kumwongezea umaskini. Mheshimiwa Spika, ninaomba na kushauri jambo hili litafafanuliwe lieleweke. Kwa mantiki hiyo utaratibu wa ushuru unaowekwa na Halmashauri haufai maana unakuwa ni kisingizio cha kutoza kodi wakulima wadogo wadogo wakati bidhaa za viwandani vimesamehewa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika ibara 94 (i) imependekezwa kufanya marekebisho ya ada na tozo mbalimbali za wizara, mikoa na idara zinazojitegemea. Aidha, kumekuwa na malalamiko kwamba tozo za ardhi *(land rent)* ziko chini sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha kuliona hili na kupendekeza kurekebisha viwango hivyo. Ninashauri hata hivyo viwango hivyo vya tozo za ardhi ambavyo vimekuwa chini sana viongozwe zaidi katika Bajeti ijayo ili thamani ya ardhi inayopanda kila siku isaidie kuongeza mapato ya serikali. Wale watakaoibuka kupinga viwango vipya vya tozo za ardhi ni wale

wanaomiliki ardhi kubwa lakini hawatumii kulima bali *land speculation*. Mheshimiwa Spika, itambuliwe kwamba ni aibu na fedheha kuwa na ardhi kuikodisha kwa wakulima wadogo wadogo kwa bei kubwa wakati wanapotakiwa kulipa *land rent* wanalalamika eti tunazuia uwekezaji. Ni mwekezaji gani huyu ambaye hawezi kulipa *land rent.* Ninakupongeza kuliona hili. Aidha atakayeshindwa kulipia ardhi airejeshe serikalini apewe mtumiaji mwingine.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sina budi kuipongeza serikali kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Maendeleo ya wizara yangu kutoka bilioni 22 hadi bilioni 71 ongezeko la asilimia 322 isitoshe Bajeti ya Maendeleo inazidi Bajeti ya kawaida kwa kiasi kikubwa. Bajeti ya Maendeleo Wizara ya Ardhi ni asilimia 61. Ninampongeza Waziri wa Fedha kuliona hili na kutenga Bajeti itakayotuwezesha kuboresha miji yetu hasa kutengwa pesa kwa mradi wa mji mpya wa Kigamboni. Kwa kuwa asilimia 100 ya makusanyo itabaki wizarani, moja kwa moja, asilimia 30 itabaki kwenye Halmashauri. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha asaidie kuhakikisha basi hata katika ngazi hii, Bajeti ya Maendeleo ya ardhi inakuwa kubwa kuliko matumizi. Miji yetu ikipangwa na ardhi ikapimwa, Hati zikitolewa hakika mapato ya serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa dhati ya nafsi yangu napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu

Waziri kwa uteuzi. Natumaini watatumia fursa hii ya kutumikia nchi na wananchi kwa uadilifu na uzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wengine waliochangia pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni juu ya umuhimu wa kupunguza fedha kutoka kwenye matumizi ya kawaida *(OC)* na kuzihamishia kwenye matumizi ya maendeleo hususan kwenye maeneo ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwa Serikali kuongeza fedha kwenye reli haihitaji kueleza. Kwa kuwa umuhimu wa reli katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati umuhimu wake umeshazungumzwa sana. Ni aibu kuongeza matumizi ya kawaida (*OC)* kwa zaidi ya bilioni 800 wakati matumizi ya maendeleo katika maeneo ya msingi ni finyu.

Mheshimiwa Spika, ni aibu mahitaji halisi ya reli (mfano, Kilosa–Gulwe – Kidete – Gulwe) ni bilioni 38,850 (ili kukamilisha kazi ya matengenezo na uimarishaji wa maeneo yote yaliyoathiriwa na mvua) kilichopatikana ni bilioni 4.9 tu, pungufu bilioni 33,900.

Mheshimiwa Spika, reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali ili kuongeza uwezo wa reli ya kati wakati mahitaji ni shilingi bilioni tisa zilizopangwa katika bajeti ni shilingi milioni 350!

Mheshimiwa Spika, reli ya Itigi na Tabora ambayo ni muhimu sana nayo imejikuta katika mkumbo huo huo.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kuangalia ni kwa namna gani mafungu yasiyo na tija yatapunguzwa ili kuokoa reli yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kilimo, hakuna ubishi juu ya mchango wa kilimo katika pato la Taifa. Lakini kama ilivyo katika maeneo mengine yenye umuhimu wa kukuza uchumi na pato la Taifa, kilimo kimepuuzwa na Serikali yetu inategemea wawekezaji na si nguvu za ndani katika kufufua kilimo. Huku ikifahamu kwamba kati ya sekta ambazo zitasaidia katika kupunguza ajira na umaskini wa kipato ni kilimo. Hapa si kwa Watanzania kuwa vibarua, manamba na vijakazi kama ambavyo wawekezaji wataigeuza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inahitaji wakulima wenye mafanikio, mafanikio hayo hayawezi kupatikana kwa kuwa tegemezi. Tukiweza kuwatengenezea mazingira mazuri wakulima wetu kwa kugawa ardhi kwa Watanzania wazalendo na kuhakikisha kunakuwa na miundombinu ya kutosha, pamoja na mbegu kama nchi tutafanikiwa sana. Hii itatuhakikishia uhakika wa chakula, lakini zaidi amani na utulivu ndani ya nchi. Hili wimbi kubwa la vijana linalozagaa mtaani, pasi kuwa na ajira litaligharimu Taifa katika muda mfupi ujao. Serikali lazima ihakikishe kwamba vijana wanajumuishwa katika mipango yote mikubwa ya kiuchumi ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya kodi Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, Kifungu cha (vii)(d) nashauri, kama ambavyo Serikali imepunguza viwango vya ushuru wa bidhaa kwa mvinyo na zabibu inayozalishwa hapa nchini, Kifungu cha vii (c) pamoja na bia kuna haja pia ya Serikali kupunguza viwango vya ushuru kwa vinywaji vikali vinavyozalishwa na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya watumishi, mwisho lakini sio kwa umuhimu ningependa pia kupata taarifa ya kiasi cha pesa ambacho wanadaiwa watumishi wa kada mbalimbali.

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, katika hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kupunguza makali ya maisha ni hatua ambazo zimeongezea gharama Serikali bila ya kufikia malengo yaliyotarajiwa na Serikali. Matokeo ya hatua hii yalikuwa ni hafifu tofauti na matarajio. Aidha, gharama zimekuwa kubwa kulinganisha na matokeo yaliyopatikana. Hatua zilizochukuliwa za kuzalisha umeme wa dharura kwa kutumia mafuta ni umeme ghali sana na ambapo umepelekea Shirika la Umeme *(TANESCO)* kupandisha bei ya umeme na hatimaye kuwapandishia bei watumiaji na matokeo yake kuwazidishia ukali wa maisha. Kutokana na matokeo haya ni dhahiri kwamba umeme unaotokana na makaa ya mawe na gesi utiliwe mkazo zaidi badala ya kutegemea umeme wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua iliyochukuliwa ya kugharamia ununuzi wa usambazaji wa mahindi

pamoja na kutoa vibali vya kuagiza sukari bila ya kutoza ushuru ilikuwa ni hatua nzuri yenye lengo la kudhibiti upandaji bei na kuwaondolea ukali wa maisha na wakulima kuweza kuuza mazao yao. Hata hivyo, malengo hayo hayakufikiwa. Malengo haya yangefikiwa pindi Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ingewezeshwa na kutumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba Bodi hii pamoja na kuwa imeanzishwa tangu mwaka 2009 hadi sasa haijapatiwa mtaji *(working Capital)* na kuiwezesha kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba Bodi hii ikipatiwa mtaji huo itafanya kazi nzuri sana, sio tu ya kudhibiti mfumko wa bei, lakini pia kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa vibali umepelekea wafanyabiashara kupandisha bei ya sukari kwa kutoagiza sukari kwa wakati na hatimaye kujiongezea faida kama ilivyo kawaida ya wafanyabiashara wote duniani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ipewe mtaji haraka ili iweze siyo tu kununua mazao, lakini pia kuagiza na kusambaza nafaka aina zote katika kipindi ambacho kuna upungufu ili kuondoa upungufu na kudhibiti mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuongeza mapato moja kati ya maeneo ambayo nchi yetu

inaweza kuongeza mapato ni kuimarisha utalii. Kuimarisha utalii kunahitaji nguvu kubwa kutoka kwa wawekezaji wa nje. Ni suala la kuweka vizuri miundombinu mizuri na yenye kuondoa usumbufu kwa watalii. Nchi yetu inazo fukwe nzuri za kuvutia, inazo mbuga zenye wanyama wa kupendeza, tunayo maeneo ya kihistoria yenye kuvutia watalii. Serikali ingefaa sasa kuwekeza katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kupata maelezo juu ya ahadi ya Serikali (Hazina) ya 2008 kuhusu kuingiza Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida kwa jumla katika Mpango au Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015 ambapo awali mkoa huo haukuwekwa kabisa licha ya kuwa unaorodheshwa kama ndiyo mkoa maskini zaidi kuliko mikoa yote. Tulitakiwa kuleta Hazina mipango yetu ya Wilaya ya Manyoni kwa Majimbo yote mawili Mashariki na Magharibi, kitu ambacho tulifanya tukawasilisha Hazina mwaka huo huo kutimiza maagizo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, tafadhali nipatiwe maelezo na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Mheshimiwa Waziri mpya na Manaibu wake wawili wanaanza kazi wakiwa watu safi na mipango mizuri. Rai yangu ni kwamba, wakatae aina yoyote ya vishawishi vitakavyopelekea walegee katika kukazia utekelezaji wa mipango ya bajeti hii muhimu. Wakilegea au kulazimishwa

kutazama nyuma, basi, nchi yetu itaendelea kuwa nchi ya majaribiro tu, nchi ya mipango isiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, tuna imani na Mawaziri hao ambao wanaweza kutegua kitendawili cha umaskini wa nchi yetu *it can be done play your part*.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, tukitaka kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ni lazima tukuze uchumi wetu, tukitaka kuendelea kutawala nchi hii ni lazima tukuze ajira kwa kukuza uchumi kupitia uzalishaji. Nchi zote zilizoendelea zilianza kukuza uchumi wake kwa kuwekeza kwenye viwanda vyenye *backward linkage* na kilimo hususan viwanda vya pamba, kusindika mafuta na *textile* na *garment manufacturing*. Viwanda hivi vitaongeza thamani ya mazao yetu, vitazalisha ajira na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kwenye viwanda vya pamba ulishafanyika na vilivyopo vinatosha, sasa tuelekeze nguvu kwenye uwekezaji kwenye *spinning mills, knitting and dying factories and garment manufacturing factories*. Sasa hivi pamba inayozalishwa Tanzania inayoongezewa thamani hapa nchini ni asilimia 29 tu, zaidi ya 70% inapelekwa nje bila *processing*.

Siyo tu tunapeleka nje pamba, bali tuna-*export* ajira pia. Nashauri Serikali ifanye yafuatayo ili kuvutia uwekezaji kwenye eneo hili:-

(i) Iondoe kodi ya *VAT* kwenye viwanda vyote vya nyuzi na nguo ili bidhaa zake zishuke thamani na viwanda hivi vishindane na vile vya nje (China, India, Bangladesh, Thaiwan na kadhalika);

(ii) Serikali iongeze kodi kwenye bidhaa zote za nguo kutoka nje ya nchi;

(iii) Iondoe kodi ya *VAT* kwenye mafuta ya pamba ili yashuke bei yashindane na yale yatokayo nje ya nchi;

(iv) Itenge fungu la fedha pale Tanzania *Investment bank Limited* ili ziwekwe *special scheme* ya kukopa kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda vyenye *backward linkage* kwenye kilimo (mafuta, *textile and garment manufacturing*). Mikopo hii iwekewe *special interest rate* (kati ya asilimia 4 – 6) kwa kuwa *investment* kwenye aina hii ya viwanda ni *capital intensive* na *payback period* ni kati ya miaka mitano hadi saba kama uchumi uko imara na hauyumbi; na

(v) Serikali iweke bei maalum ya umeme kwenye viwanda hivi. Hayo

yakitekelezwa nchi yetu itashuhudia mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kelele za ajira kukosekana zitapungua. Ukifanya uwekezaji wa Tanzania Shilingi Bilioni 150 tu utakuwa umewezesha viwanda *(intergrated)* takriban vitano ambavyo vitaweza ku-*consume* zaidi ya asilimia 60 ya pamba ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu ukifanyika kwa miaka miwili na wakakopeshwa vijana, tutaweza kuleta mapinduzi makubwa ndani ya miaka ishirini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili kwanza kuteuliwa na Mheshimiwa Rais pamoja na matayarisho ya bajeti ambayo inajibu changamoto nyingi zinazoikabili nchi yetu. Kimsingi, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, ni lazima Serikali idhibiti matumizi yake kwani hata tukipanga mabilioni mengi kama hakutakuwa na usimamizi mzuri na kudhibiti matumizi kikamilifu, bajeti haitakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zilizo nyingi hazifanyi jitihada ya kutafuta mapato ya ndani na kutegemea wapate ruzuku kutoka Serikalini. Naomba Serikali izibane Halmashauri kujizatiti kutafuta mapato ya ndani. Halmashauri zisizotimiza hili

zikaripiwe na ikibidi wakatwe asilimia fulani katika ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua thabiti kufufua viwanda vyetu hasa Viwanda vya Nguo. Jambo hili litaongeza ajira na kupunguza bei ya mavazi nchini. Vile vile tutaweza kutumia pamba yetu na hivyo wakulima watafaidika na kuongeza kipato. Hivyo ili kufufua viwanda vyetu vya nguo ni muhimu viwanda vipewe msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani *VAT* kwenye bidhaa za nguo na mavazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato ni vyema Serikali ikabuni vyanzo vingine vya mapato na tusiendelee kutegemea mapato kutoka katika vinywaji kama bia, soda na mvinyo. Makampuni ya Simu yaangaliwe vizuri ili yatoe kodi inayostahili. Naomba pia ile Tume ya *TCRA* ya kuchunguza suala hili isimamiwe vizuri na wakamilishe kazi hiyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tuhuma ya kwamba katika madini Serikali haipati kodi ni vizuri likafanyiwa kazi na kufanya marekebisho yanayostahili na kuondokana na tuhuma hii ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya bajeti kupitishwa, naomba Serikali ipeleke mafungu kama yalivyopitishwa, hasa mafungu ya Serikali za Mitaa na tusirudie makosa ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti ya Serikali. Lakini nashauri kwa dhati Serikali ibane matumizi zaidi na iwe makini sana. Wizara moja inakuwaje na fungu la kukirimu wageni la shilingi 298,000,000 kwa mwaka mmoja? Tazama Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Watendaji Wakuu wa Serikali katika Wizara na Idara wanaosafiri nchini kila mmoja anasafiri na gari lake. Hata kama wote wanakwenda sehemu moja, kwa mfan,o kuja hapa Bungeni kwa nini maafisa watatu au hata wanne wasipande gari moja?

Mheshimiwa Spika, pili, futa ushuru na tozo ndogo ndogo kwa wakulima ambazo ni kero kubwa. Mkulima anapelekea ndizi mkungu mmoja sokoni anatozwa ushuru njiani katika kizuizi *(barrier)* na pale gulioni. Bei ya ndizi ni Sh. 1500 hadi 3000, ushuru unaweza kufikia sh. 500 hadi 1000. Hii ni kero kubwa sana. Mkulima ananyonywa na kunyanyaswa. Kodi gani hii, kama ni sheria ni haramu. Sera na sheria mama za kodi inasema kiwango cha chini kutozwa kodi ni Sh. 140,000 kwa mwezi. Ndizi inauzwa Sh. 2000 inatozwaje kodi? Tulifuta kodi ya kichwa, tulifuta kodi ya maendeleo na zingine. Je, kwa nini hatufuti kodi hizi kandamizi na za kinyonyaji kwa wakulima maskini sana wa nchi yetu?

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali ya CCM kwa kuendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto za kiuchumi zinazopelekea ugumu wa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, duniani kote pamekuwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi ikiwemo mfumko wa bei, uzalishaji mdogo, madeni, ukosefu wa ajira na mzunguko mdogo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ya Marekani zaidi ya miaka 30 ilipita (tangu baada ya Vita vya Pili vya Dunia, 1939) wamekuwa wakikabiliana na changamoto za uzalishaji, mfumko wa bei, upungufu wa ajira kwa uchache wake. Hata hivyo, Marekani kama ilivyo Tanzania iliamua kuanzisha sera ya fedha ili wataalam mbalimbali wa uchumi waweze kufanya utafiti mbalimbali utakaopelekea njia sahihi za kuimarisha uchumi wa Mataifa yao. Wataalam wa uchumi walibaini kwamba njia sahihi ya kuweza kuimarisha uchumi kwa kutatua matatizo yanayohusiana na ugumu wa maisha ikiwemo upatikanaji wa ajira, uzalishaji, mzunguko wa fedha ulio imara ni kuimarisha udhibiti wa mfumko wa bei na kuimarisha mifumo ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, ndani ya nchi yetu ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika Mashariki imedhibiti kwa kiwango kikubwa mfumko wa bei hadi kufikia wastani wa asilimia 17.8 kwa mwaka 2011/2012. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba, hali ya ugumu wa maisha kwa Mtanzania bado imeendelea kuwepo. Kwa miaka kadhaa sasa, nchi yetu imekabiliwa na changamoto ya ukosefu au upungufu wa ajira, tatizo la ukosefu wa ajira linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kitaalam kama ambavyo wataalam wa uchumi wameweze kueleza vizuri kitaalam madhumuni ya

kuimarisha bei, nidhamu ya matumizi ya fedha ikiwa na mtazamo wa kukuza na kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi ambalo bado wataalam wetu wa uchumi hawajalitatua ni namna ambavyo tunaweza kutumia fursa mbalimbali za kupata ajira. Kama mfumko wa bei utadhibitiwa, hapawezi kuwa na wanunuzi wa bidhaa kama hakuna ajira zinazoweza kutupatia Watanzania kipato (fedha).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti ya Wizara ya Fedha kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, ningependa kusisitiza kwamba pamoja na juhudi mbalimbali, ningependa wachumi wetu watoe suluhisho la ukosefu wa ajira ni moja ya *elements* za *macroeconomy* tuige mifano ya nchi zilizoendelea kama Marekani. Katika nchi ya Marekani sera yao ya fedha iliyowekwa kwa mujibu wa *Federal Reserve Act* imeainisha malengo ambayo Serikali inakusudia kuyafikia na malengo hayo yapo kwenye sheria yao ya *Federal Reserve*. Katika malengo yake makuu mawili ni pamoja na kuimarisha bei na *to promote maximum sustainable output and employment* yaani kuongeza uzalishaji na ajira.

Mheshimiwa Spika, zipo ajira zisizo rasmi ambazo vijana wengi wamekimbilia. Waendesha bodaboda ni vijana walio na ajira zisizo rasmi. Vijana hawa kwanza nashauri wawe na mfumo mzuri wa kufanya ajira zao ziwe na tija endelevu. Waingizwe kwenye mfumo ulio rasmi wa hifadhi za jamii ili waweze kunufaika na huduma za mifuko hiyo kama mwajiriwa aliye kwenye mfumo rasmi. Kwa kuwaingiza kwenye Mfuko wa

Hifadhi za Jamii wataweza kuwa na uchumi endelevu kwani kazi za bodaboda mara nyingi zimekuwa zikileta ajali na kupelekea kuvunjika baadhi ya viungo kama vile miguu. Hivyo ni dhahiri kwamba, kama watajiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii watanufaika na mafao ya ajali kazini.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua nzuri na sahihi ya kukabiliana na ugumu wa maisha ni kuondoa ama kupunguza kodi kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotokana na malighafi za hapa hapa nchini wetu. Serikali yetu ikiondoa kodi au ikipunguza kodi kwenye bidhaa hizo maana yake uzalishaji utaongezeka na ajira pia itaongezeka. Ukuaji wa ajira utaongeza kodi ya *PAYE* ambayo ukusanyaji wake kutoka katika sekta ya ajira umekuwa ndiyo eneo lenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika hili ningependa kutolea mfano viwanda vya nguo na mavazi ambavyo uzalishaji wake unatokana na zao la pamba, zao ambalo linazalishwa kwa wingi na hutoa ajira kwa wakulima wadogo wadogo zaidi ya laki tano nchini. Hayo ni manufaa makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono bajeti hii.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wangu ni kwamba, mfumo wa utafutaji na ubunifu katika vyanzo

vya mapato ufanyiwe kazi zaidi ili kuongeza vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, suala la miradi ni kubwa, ni *strategic,* iende sambamba na suala ya kuzalisha ajira mfano, kuwepo na *data centre* ya kutambua idadi kamili ya vijana wasomi ambao miradi hiyo mikubwa ambayo ni *strategic* itakapoanza, sharti la uwekezaji katika miradi hiyo liwe ni kuajiri vijana wetu. Hivyo, tutakuwa tumetatua tatizo la ajira na mengine kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, suala la kufufua viwanda vya ndani ni la msingi sana hatutakiwi kukwepa ni lazima sasa bila kigugumizi kuondoa kodi katika mazao ghafi ya biashara ili kusaidia kuongeza ajira na kuinua mapato ya wakulima. Mfano, zao la mahindi, korosho, mpunga, kahawa, tumbaku na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la *pension* kwa wazee ni suala la msingi sana. Huu ni utekelezaji wa matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei ni tatizo kubwa, Serikali ipate njia mwafaka ya kushughulikia mfumko wa bei. Kwa kuongeza uzalishaji chakula, kuboresha miundombinu, kilimo cha umwagiliaji na *Rural roads* zifanyiwe kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la kubana matumizi lakini pia suala la kupandisha mishahara ya wafanyakazi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza Serikali kwa kazi nzuri anayofanya Waziri na Manaibu Waziri wa Fedha kwa mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Ugandan List*, kwa kuwa mapato ya nchi yetu hutokana na uwekezaji na hasa wa viwanda. Inaeleweka wazi kuwa nia njema ya ushirikiano wa *EAC Exemption* ya *Ugandan List* imewekwa, lakini inaonekana Uganda hawako tayari kuiondoa *list* hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa imeathiri viwanda vyetu na vingine vimehamia Uganda.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, Waziri asiwakubalie *list* hii kuendelea kuwepo, sababu hata hivyo kodi inayotozwa *EAC* baada ya malumbano makubwa haina madhara kwa Uganda maana wanauza nchi nje ya *EAC* na kutudhulumu sisi vinginevyo na sisi tupeleke *list* yetu kiushindani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Simu *EAC*, kuongezeka kwa kodi ya simu si jambo baya ndani ya *EAC*. Tunaomba hivi sasa karibu makampuni yote yaliyopo Tanzania yanafungua biashara *EAC* hata nje, kwa hiyo wanapata mapato na faida kubwa sana, nyingi zinapunguza hata bei zao kwa ajili ya kupata wateja.

Mheshimiwa Spika, angalizo, tusiwakamue wananchi wetu kwa kunufaisha uwekezaji wa makapuni haya. Sawa tuoanishe kodi za Afrika Mashariki lakini zitolewe na makampuni hayo na wala

sio kutoka wa wateja ambao hutoa *VAT* na hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Deep Sea Fishing and Agriculture,* uwekezaji katika kilimo kwa ujumla ni mdogo, napendekeza uwekezaji na ruhusa ya kuruhusu meli za uvuvi mdogo mdogo na hata mkubwa majosho na uwekezaji juu ya viwanda vya kusindika samaki na nyama. Ili kunyanyua ajira na uchumi wa kundi hili.

Mheshimiwa Spika, *double taxation*, Zanzibar na Tanzania Bara, napongeza jitihada zilizoanza kwa kuoanisha kodi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hii ni kero ishughulikiwe haraka sana. Itaimarisha biashara baina ya Tanzania Zanzibar na *EAC* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, *Revision* ya mgao wa Zanzibar, napendekeza katika ongezeko la uwekezaji na rasilimali zinazopatikana Tanzania napendekeza *revision* ya mgao kwa Zanzibar, vigezo viwe wazi na *implementation* ianze haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo wa wananchi, naunga mkono jitihada za Serikali kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi, wakulima, wafanyakazi na wajasiriamali wadogo wadogo. Kubwa zaidi itabidi Serikali iruhusu uwekezaji katika viwanda ili tuwe na mwelekeo wa kuongeza thamani. Hili litasaidia kuongeza mauzo ndani ya Afrika Mashariki na Kanda nyingine za Afrika na nje ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Serikali kuweka msimamo juu ya kuwafikiria wana bodaboda. Lakini wale wengine je, tunawafikiria vipi? Mama lishe, kondakta, wauza mkaa na mchicha, nao wataanza kulalamika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, tumeona jinsi maisha ya wananchi yalivyozidi kudidimia katika lindi la umaskini, tumeona jinsi mchakato na mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani ulivyozidi kuzorota kwa kukumbwa na uvujaji wa mapato, udanganyifu katika ulipaji kodi, utovu wa utashi wa kizalendo wa kutafuta au kuibua vyanzo vipya vya mapato, kushindwa kupunguza misamaha ya kodi kwa makampuni mbalimbali na kutoza kodi stahiki kwa makampuni katika sekta ya mawasiliano. Suala gumu ambalo limeukabili uchumi wa Tanzania na ambalo wachumi wanapaswa kulijibu, ni kwa nini katika miaka ya hivi karibuni uchumi umekuwa bila kupunguza umaskini? Hili swali ambalo Wabunge wengi wamelizungumzia.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza ni je, bajeti ya mwaka huu imetoa jibu sahihi kwa suala la uchumi wetu unaokuwa bila kupunguza umaskini? Kwa kiasi kikubwa jibu ni hapana, kwani mambo mengi yanayopendekezwa yanawasaidia watu wa tabaka la kati na la juu. Bajeti imeelemea zaidi kwenye matumizi kuliko maendeleo na matumizi ya posho, gharama za

magari ya Serikali na kadhalika ni makubwa mno na hayaashirii kwamba Serikali ina utashi wa kubana matumizi. Wabunge wengi wamekuwa wakishauri kuwa Serikali iachane na utaratibu wa sasa wa magari ya Serikali na kuanzisha utaratibu mpya ambapo watumishi wanaostahili wapewe mkopo wa magari na kupewa fedha ya mafuta, lakini mpaka sasa Serikali haijasikia na kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ulivyo, katika vipaumbele vyake na katika matengeo ya fedha ya maendeleo huwezi kupunguza umaskini kwa wananchi wa hali ya chini kwa vijijini na hata mijini. Ili lengo hili lifikiwe, lazima vipaumbele vibadilishwe na kuelekeza rasilimali zetu kwenye mambo ambayo yanawagusa maskini vijijini na mijini moja kwa moja, kama ilivyopendekezwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo kama yakipewa kipaumbele, yanaweza kuleta mapinduzi katika maisha ya watu wa chini na kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa umaskini vijijini na mijini. Mambo hayo ni pamoja na kilimo cha kisasa, elimu, afya, mishahara inayofaa na pensheni kwa wazee. Haya yanawagusa moja kwa moja watu wa hali ya chini vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndicho kiwe kipaumbele namba moja. Tuwekeze katika pembejeo bora, tuwape mafunzo wakulima walime kisasa, tuanzishe miradi ya umwagiliaji katika maeneo yenye vyanzo vya maji vinavyofaa, tuhakikishe wakulima wanapata zana za kilimo za kisasa (plau, trekta na kadhalika); njia nzuri

ni kuanzisha viwanda vya zana hizi kwa namna yoyote inayowezekana hapa nchini na kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu. Kilimo kiendelee kuwa kipaumbele namba moja kila mwaka na kila mwaka shughuli za kilimo zitaendelea kuwapunguzia umaskini wananchi.

Mheshimiwa Spika, elimu ndiyo ingekuwa kipaumbele namba mbili. Nchi zote zilizoendelea na zinazoendelea huipa msisitizo elimu. Hapa nchini kwetu, mfumo wa elimu umekumbwa na matatizo lukuki. Matatizo ya mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi, shule za sekondari, vyuo mbalimbali, vyuo vikuu yamesababisha viwango vya elimu kushuka. Jambo hili limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu bila hatua za dhati kuchukuliwa kubadili hali hii. Hadi sasa hatua ambazo zimeshachukuliwa hazijabadilisha hali kwa kiasi cha kuridhisha. Serikali sasa iamue kuwekeza katika sekta hii ili hatimaye tuwe na shule za msingi za kisasa, shule za sekondari za kisasa na vyuo vikuu vya kisasa. Elimu ni sekta inayowagusa watu wa hali ya chini moja kwa moja. Serikali ikiboresha miundombinu ya elimu watoto wengi sana wa wakulima na wafanyakazi watapata elimu bora na kwa hiyo watakuwa wamejikomboa. Kadhalika, elimu ikiwa ni kipaumbele namba mbili na ikatengewa fedha ya kutosha mradi wa vyuo vya ufundi, ambao upo lakini haujaanza kutekelezwa; utatekelezwa na kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, kama hotuba ya Kambi ya Upinzani inavyopendekeza, afya pia ingekuwa kipaumbele cha tatu, kwa mtiririko wetu. Afya inagusa

moja kwa moja wananchi maskini. Sekta ya afya ikiimarishwa kwa kuwa na mpango kabambe wa kuleta mageuzi ya kiafya vijijini na mijini, bila shaka hali za maisha ya watu wa kawaida zitakuwa afadhali. Kama wakiwa na afya bora basi watashiriki kikamilifu katika uzalishaji na furaha yao katika maisha itaongezeka.

Mheshimwa Spika, jambo lingine ambalo kambi ya upinzani imelizingatia ni kupandisha kiwango cha chini cha maisha, hivi sasa ni magumu mno. Mwaka jana Kambi ya Upinzani ilipendekeza Sh. 315,000 kuwa kima cha chini, mwaka huu pendekezo hili limerudiwa. Kama Serikali ingetekeleza jambo hili, lingewapunguzia umaskini watu wengi.

Mheshimwa Spika, kipaumbele kingine ni pensheni ya wazee ambayo Serikali katika vikao au mikutano mbalimbali ilisharidhia. Tunashangaa kuona kuwa halikuzungumziwa; labda litaletwa katika bajeti ya Wizara husika. La kusisitiza ni kwamba, wazee ni watu wanaohangaika sana vijijini na mijini kwa kuwa hawana nguvu tena za kufanya kazi. Serikali itakuwa imesaidia kama ikipitisha pensheni ya wazee hata kama ni shilingi 30,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya Kitaifa kama reli, bandari, ndege, viwanja vya ndege, barabara, nishati ipangiwe ratiba ya utekelezaji. Mathalani mwaka huu 2012/2013 Reli ya Kati na Tazara vikamilishwe. Mwaka huu bomba la gesi la Mtwara – Dar es Salaam likamilishwe. Miradi ya viwanja vya ndege ipunguzwe ibaki mitatu tu. Dar es Salaam,

Songwe, Mwanza. Fedha itengwe ili tununue ndege mbili mwaka 2012/2013, mbili mwaka utakaofuata na kadhalika. Miradi ya barabara iliyopo ndiyo ikamilishwe kwanza kabla ya kuanza miradi mingine. Badala ya kutapanya fedha iliyopo kwenye miradi lukuki, Serikali ijikite kwenye miradi inayoweza kutekelezwa kwa fedha iliyopo.

Mheshimiwa Spika, swali linaweza kuulizwa, je, fedha ya kuwekeza katika kilimo, elimu, afya kwa lengo la kuleta mapinduzi katika sekta hizi itatoka wapi? Kambi ya Upinzani imeonesha wazi njia za kutumia mfano, kupunguza misamaha ya kodi; kuhakikisha kuwa wote wanaopaswa kulipa kodi wanalipa kupanua wigo wa kodi na kadhalika. Kinachohitajika ni utashi wa kisiasa na kupambana na ubadhirifu uliokithiri na kufanya maamuzi magumu ya kurejea mikataba mibovu ya madini na gesi yanayoendelea kulikosesha Taifa mapato ambayo yangesaidia katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba, Serikali ijipange vizuri ili ishughulikie tatizo la uzembe kazini na utamaduni ulianza kujengeka kwa watu kutofanya kazi kwa bidii na maarifa. Ikumbukwe kuwa nchi zote zilizoendelea watu walifanya kazi kwa bidii na maarifa. Jambo hili lishughulikiwe kwa haraka.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, bajeti haimsaidii kabwela wa Tanzania na hasa wananchi wa Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara). Uongozi wa Awamu ya Nne umeonekana siyo makini katika kusimamia shughuli za maendeleo na kudhibiti

matumizi ya fedha kama ilivyodhihirishwa kwenye taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi wa Fedha za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2012/2013 imeendelea na utamaduni (utaratibu) ule ule wa kutaja kuzingatia Mkukuta – II na kadhalika bila kufafanua mahusiano halisi ya sera na mipango hiyo na inavyotekelezwa na bajeti. Ahadi za bajeti ya 2011/2012 hazikutimizwa. Hali hiyo imesababisha maisha kupanda na shilingi kuendelea kushuka. Mfumuko wa bei na vyakula ni wa juu (asilimia 24.5), bajeti ya maendeleo haitekelezwi, tatizo kubwa la bajeti yetu ni kuwa matumizi ya Serikali hayatekelezi bajeti ya maendeleo kwa kutenga kiasi kidogo cha fedha za maendeleo.

Mheshimwa Spika, Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara kutengewa kiasi kidogo cha fedha za bajeti, pamoja na wingi wa rasilimali kama madini na gesi asilia. Kukosekana kwa miundombinu ya kiuchumi wananchi wa maeneo hayo hukimbilia miji yenye ustawi na kusababisha maeneo hayo kuwa na watu wachache Lindi ina watu 14 kwa kila kilomita moja na makisio ya watu laki tisa kwa mkoa wote, hii ni dhuluma inayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya siwezi kuunga mkono hoja ya bajeti na wala sitakubaliana na wazo la Serikali la kusafirisha gesi kutoka Mtwara kuipeleka Tanga, sisi wenyewe vijana wetu wakihama kwenye miji yao.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya miradi ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2011/2012 yatakuwa chini kwa Shilingi bilioni 600 ukilinganisha na bajeti iliyopitishwa na Bunge. Baadhi ya sekta, matumizi halisi ya maendeleo ni chini ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo ya 2012/2013 ni ndogo. Matumizi yote ya Serikali yameongezeka toka trilioni 13.1 na kufikia Shilingi Trilioni 15.1; bajeti ya maendeleo imepunguzwa toka Shilingi trilioni 4.9 mwaka 2011/2012 na kufikia trilioni 4.5 mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya namna hii huwezi kuinua uchumi wa wananchi wako. Lakini pia inazidi kuwaumiza wananchi wa Kusini; Lindi na Mtwara kiuchumi pamoja na rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu imekuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa jambo ambalo husababisha shughuli za kimaendeleo kukwama. Mapato ya Serikali yanashuka kutokana na misamaha holela na kuporomoka kwa maadili ya watumishi ambao hatimaye hudai rushwa kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kusini ina ardhi ya kutosha kwa kilimo, lakini siyo bajeti 2011/2012 wala 2012/2013 ambayo inazungumzia kuinua sekta ya kilimo wala kuonesha njia ni jinsi gani itaboresha Viwanda vya Korosho na zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kusini inalima mbegu za mafuta kama ufuta, karanga, mahindi pia ni maeneo yanayozalisha nazi kwa wingi. Bajeti haisemi chochote kuhusu hatua za kuchukua kuboresha uzalishaji na kuwatafuta wawekezaji kwenye sekta ya viwanda vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kusini ni maarufu kwa uvuvi, bajeti haijaeleza chochote kwenye sekta hii ya uvuvi na jinsi ya kutafuta wawekezaji ambao wangeweza kujenga Viwanda vya Kusindika Minofu ya Samaki.

Mheshimiwa Spika, watu wa Mikoa ya Kusini wanajulikana kuwa wapo sasa kupitia gesi asilia na ni kwa lengo la kuihamisha na siyo kuendeleza mikoa hiyo. Hilo halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kama wazalishaji wa saruji wanaonesha angalau juhudi za kuwekeza kwa kusudio la kujenga Viwanda vya Sementi kwa kutumia malighafi inayopatikana huko kwa nini gesi nayo isionekane kuwanufaisha watu wa Mikoa hiyo ya Kusini ambayo robo tatu ya vijiji havina umeme kabisa na baadhi ya Wilaya kukosa umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchini na baadhi ya nchi jirani zinahitaji kubwa la matumizi ya mbolea, kwa nini Serikali isioneshe nia kupitia bajeti kupata wawekezaji wa Kiwanda cha Mbolea na badala yake inakazania kuhamisha na kupeleka maeneo mbali ili ikaboreshe viwanda vya huko na

kuwaacha wakazi wa Mikoa ya Kusini wakiendelea kuukumbatia umaskini?

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza kuwa siungi mkono bajeti wala siungi mkono nia ya Serikali ya kuitoa gesi asilia Mnazibay – Mtwara na kuipeleka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa tayari kuunga mkono usafirishaji wa gesi na kuwa mmoja wa wahamasishaji ili kurahisisha upitishwaji wa bomba endapo kupitia bajeti hii nitahakikishiwa mambo yafuatayo:-

(i) Vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba vipatiwe umeme;

(ii) Shule ziboreshwe kwa majengo na vitendea kazi, pia zipatiwe waalimu wa kutosha;

(iii) Malipo ya mrahaba wa gesi asilimia nne Mtwara na Kilwa;

(iv) Kiwanda cha Mbolea kijengwe Mtwara ili kuongeza ajira;

(v) Serikali iboreshe kilimo kwa maeneo ya Kusini; na

(vi) Zahanati kwa vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya kiuchumi kwa Mikoa ya Kusini na mingine yenye rasilimali na iko

nyuma, bajeti iboreshwe kwenye eneo la maendeleo ili maisha yawe nafuu.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, napongeza serikali kwa kuandaa Bajeti nzuri ambayo itaendeleza programu mbalimbali za mwaka uliopita. Hata hivyo nina ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Spika, ingawa serikali imefuta kodi kwa bodaboda jambo ambalo ni zuri lakini nachelea kuamini kuwa vijana wote hao hizo pikipiki ni zao. Wao vijana ni wafanyakazi tu wengi wao sio wamiliki. Hivyo basi tunaweza kufikiri tunawasaidia vijana kumbe tunawasaidia wamiliki kukwepa kodi. Naomba suala hili serikali litafakari upya hata kwa Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaanza sasa kuwa mazoea kwamba fedha tunazopitisha Bungeni hazitolewi ipasavyo kwenye Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali, nashauri serikali ihakikishe kuwa fedha zinazopitishwa zitolewe vilivyo na zisitumike kwa matumizi yasiyopangiwa au yasiyokusudiwa. Kwa kutosimamia matumizi vizuri, nchi itakosa mtiririko mzuri wa kukamilisha programu mbalimbali zinazopangwa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 47 wa Bajeti (hotuba) nimefarijika kusoma kwamba mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam utaanza kutekelezwa ukiwa unasimamiwa na *TPDC.* Naamini shida ya umeme itakwisha kabisa au kupungua wakati gesi hiyo itakapotengeneza umeme ambao utakuwa wa bei rahisi ukilinganishwa na huu

unaotokana na mitambo ya mafuta tena ya kukodisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nahitaji ufafanuzi ni kwa jinsi gani maeneo litakamopita hilo bomba watafaidika na umeme utakaotokana na gesi hiyo. Nahitaji ufafanuzi huo ili isije ikajitokeza changamoto kama ilivyokuwa kwa maeneo/vijiji vilivyopita bomba toka Songosongo mpaka Dar es Salaam ukurasa wa 48 wa hotuba serikali imedhamiria kuimarisha mawasiliano kwa TEHAMA ili kuboresha upatikanaji wa taarifa za makisio ya ndani na nje ya nchi. Napongeza sana dhamira hii lakini kwa upande mwingine nadhani lengo hili halitafanikiwa kwa sababu gharama kwa watumiaji simu za viganjani *(airtime)* zimeongezwa toka asilimia 10 hadi 12. Nashauri kodi/tozo iongezwe kwa watoa huduma i.e. mitandao ya simu iliyopo nchini kuliko kumwumiza mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali ione uwezekano wa kupunguza *PAYE* kwa waajiriwa hapa nchini kwa sababu hata kama wafanyakazi wataongezewa mshahara bado hali yao itakuwa duni tu kwa vile jinsi mshahara unavyopanda ndivyo *PAYE* inavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, wastaafu kwenye Bajeti hii wamesahauliwa na ni wazi maisha yao ni magumu sana na familia zina maisha magumu ya ombaomba na njaa kali.

Mheshimiwa Spika, hata mafao yao wastaafu wanayopata wakati wa kustaafu si sahihi, kwani imeonekana wanapunjwa na imedhihirika wakati wa kukokotoa hesabu sahihi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 kati ya majalada 4960 yaliyokaguliwa majalada 137 yangelipwa pungufu shilingi milioni 167.

Mheshimiwa Spika, mtindo huu umebainika tena mwaka 2010/11 katika majalada 4788 yaliyokaguliwa majalada 282 yangelipwa pungufu milioni 539.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hizi toka *CAG* imedhihirisha hata wale wanaolipwa ziada kuna mchezo mchafu unaofanywa katika miongoni mwa walio na dhamana ya kuwapatia wastaafu haki zao.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi unapomlipa mtaafu pensheni ya kila mwezi Sh. 50,144/= wastani wa Shilingi 1700 ni aibu kubwa kwa serikali kutowajali wastaafu wake.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali kuandaa mazingira ya kuboresha mazingira ya mafao ya wastaafu angalau pensheni ya kima cha chini angalau Shilingi 300,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya serikali imegusia ajira, Mkukuta II, na kuendeleza viwanda lakini inasikitisha kwamba Bajeti imeshindwa kutenga fedha za kufufua viwanda, vingi vimekufa. Viwanda vya korosho Kusini

mikoa ya Lindi na Mtwara. Kiwanda cha magunia moshi kimekufa. Kiwanda cha Urafiki Ubungo cha Kanga na vitenge na vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, serikali ni vyema ikaandaa mazingira ya kufufua viwanda vilivyokufa na kuongeza ajira kwa vijana na hapa dhana ya Mkukuta II utaweza kutekelezeka kwa uhalisia na kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii ya Bajeti. Nina maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *SAGCOT* imemegewa pesa nyingi sana za Bajeti hii na miradi mingine ya *ASDP* na *DASIP* zimepunguzwa pesa. Naomba mwaka kesho msirudi na *SAGCOT II.*

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme vijijini, mji wa Hungumarwa umeshafanyiwa usanifu wa kupata umeme lakini mwaka umeisha umeme bado na Bajeti hii iweze kuleta umeme hapo Hungumarwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji vijijini naomba pia iliyotengwa ipelekwe kama ilivyopangwa. Sisi tarafa ya Mwamashimba, wilaya ya Kwimba maji ya visima virefu hayapatikani tunategemea marambo na maji ya bomba ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *CDF,* naomba huo mfuko uongezewe pesa kwa

sababu huo mfuko huwa unasaidia wananchi kwa miradi midogo midogo. Tunazipelekea fedha kutoka mfuko huu wa *CDF,* wakati tukisubiri miradi mikubwa ya serikali.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya huduma za simu. Naomba kushauri serikali iangalie huduma ya M-pesa inayotolewa na haya makampuni kama ifuatavyo:-

(i) Wana masharti yanayofanana na mabenki;

(ii) Wanaweka akiba *BOT* kama mabenki;

(iii) Wanatoza kodi kwenye huduma hiyo;

(iv) Kwa siku ni bilioni 4 inazunguka; na

(v) Watu wanaajiriwa, hivi huduma inaweza kutumika na fedha chafu mbaya inahatarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege – Mwanza umepangiwa pesa mwaka huu 2012/2013, naomba hiyo pesa ifike kwa muda uliopangwa tumesubiri miaka mingi wana Mwanza kupata uwanja wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, reli naomba kama ilivyopangwa kwamba Desemba mwaka huu itafika Mwanza kupitia Kwimba mimi naomba hili litekelezwe kwa kikamilifu hii ndiyo njia pekee ya kupunguza hali ya wananchi kwa sababu ya gharama ndogo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo na mbegu, mimi naomba serikali ituongezee mbegu za pamba na mahindi kwa wilaya ya Kwimba mbegu zinazoletwa hazitoshi tunaomba ziongozwe.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais, aliahidi barabara ya lami kutoka Magu – Ngudu – Hungumarwa. Naomba hiyo barabara iwekwe kwenye Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika naunga mkono Bajeti. Ahsante sana.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya wizara ya nchi ya Ofisi ya Rais. Vijana wengi wanatoka vijijini wanakimbilia mjini yaani hawa vijana hawajawezeshwa na serikali haijawa *serious* kwa kuwezesha vijana katika sekta ya kilimo. Imekuwa ni mipango isiyotekelezeka kwa muda mrefu nakupekea vijana wengi kukata tamaa na kukimbilia mjini na hili suala la kilimo kwanza limekuwa kama wimbo wa Taifa. Na ukiangalia wanaonufaika ni watu wa chache walengwa wakuu hawanufaiki na hilo suala la kilimo kwanza mpaka sasa. Ukiangalia mpaka sasa benki za wakulima bado hazijawafikia walengwa ni lini benki hizo zitatawanya matawi ili kuwafikia walengwa vijijini? Serikali ihakikishe wakulima wanapata pembejeo kwa wakati mwafaka asilimia kubwa ya wanawake wa vijijini wanatumia jembe la mkono ni lini serikali

itawapatia wanawake hao kilimo cha kisasa kama matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, swala zima la miundombinu, nchi yoyote yenye maendeleo lazima tuwe na reli ya kusafirishia mizigo, barabara na kadhalika. Lakini leo hii Tanzania hatuna reli ya kusafirishia mizigo ukiangalia wakulima wengi wanashindwa kusafirisha mizigo kama mazao na wafanyabiashara nao wanashindwa kusafirisha bidhaa zao ni lini serikali itaonyesha kwa vitendo kushughulikia suala zima la miundombinu hususan reli? Ili kuingizia serikali pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la uchumi kumekuwa na ubadhirifu yaani baadhi ya viongozi wamekuwa wakijilimbikizia mali yaani kuchukua mali za Umma na kuingia mikataba mibovu na kuisababishia serikali hasara ya madeni na wananchi kubaki maskini na kutoipenda serikali yao. Je, ni kwanini watu ambao wanahujumu uchumi wa taifa letu hawafilisiwi mali zao na kufungwa? Ni kwa nini mikataba ya wawekezaji haiwekwi wazi kwa wananchi wakaifahamu na mikataba hiyo kufanywa na watu wachache? Ukiangalia kama sekta ya madini hainufaishi wananchi waliozungukwa na migodi hiyo hawanufaki na madini hayo wanaonufaika ni watu wachache ukiangalia hawa huduma za jamii kama shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ukusanyaji wa mapato ya serikali, wawekezaji wengi wamekuwa wakikwepa kulipa kodi serikalini na kuisababishia serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenye maendeleo itategemea ulipaji kodi lakini Watanzania wengi hawalipi kodi. Kwa mfano Kariakoo baadhi ya wafanyabiashara hawalipi kodi hata maghorofa ambayo yanajengwa Kariakoo yana pesa chafu (haramu) na wafanyabiashara wengi wa maghorofa hayo ukianza kuwachunguza hawalipi kodi na kuisababishia Serikali hasara kubwa ya pato la taifa. Nashauri serikali iangalie kwa makini vyanzo vya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwani vyanzo hivi kuna baadhi ya viongozi si waadilifu wanajilimbikizia mali kupitia mapato ya serikali.

Mheshimiwa Spika, suala zima la Afya, serikali haijawa *serious* kuhusu suala zima la afya na Bajeti hii naona haikidhi katika suala zima la afya na kila siku tumekuwa tukiwapoteza baadhi ya akinamama wanapokuwa wanaenda kujifungua kutokana na hospitali kukosa madawa ya kutosha na vitendea kazi na majengo kuwa chakavu, kukosa madaktari bingwa na kumekuwa na upungufu wa wauguzi na baadhi ya Watanzania kupoteza maisha. Kwa hiyo, Bajeti hii haijakidhi katika suala zima la afya.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nianze na kutounga mkono Bajeti hii kwa kuungana na wachangiaji wengine kuwa Waziri wa Fedha airudishe na kuifanyia marekebisho kwa baadhi ya maeneo kama kilimo na ufugaji, afya, miundombimu, elimu, misamaha ya kodi, kwa nini mfumko wa bei uko juu sana ambao unazidi kumkandamiza Mtanzania. Bajeti ya 2011/2012 ilikuwa

asilimia 35 Bajeti ya 2012/2013 itakuwa asilimia 30 kwa nini ishuke badala ya kupanda? Nami siungi mkono Bajeti ilirudishwe na kurekebishwa upya.

**MHE. GRACE SINDATO KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu huu kwa maandishi, kuhusu mapendekezo ya Makadirio ya Bajeti ya serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe msimamo wangu kwamba siungi mkono Bajeti hii iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Imekuwa ni kawaida ya serikali hii ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kutuletea Bajeti ambazo hazitekelezeki, sitakuwa tayari kupitisha tarakimu kubwa za mabilioni ya fedha ambazo mwisho wa siku hazifiki kwenye wizara kama tulivyozipitisha katika Bunge letu hili lazima ifike wakati serikali hii ambayo ndiyo yenye jukumu la kukusanya kodi kutimiza yale ambayo waliwaahidi Watanzania yaani maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa Bajeti zetu hazieleweki tunataka nini kila mwaka vipaumbele kila siku vinabadilika. Kutangatanga huku ndiko kunakosababisha kutokuelewa vipaumbele tulivyopitisha mwaka jana vinaweza kufanikiwa kwa kiasi gani ili tujue tulikwama wapi ili tuongeze fedha eneo hilo ili mwisho wa siku kuwe na kitu cha kuonyesha. Kwa utaratibu huu tunaokwenda nao wa kila mwaka kutoa vipaumbele vipya tunaendelea kuzalisha madeni ya miradi iliyoko kwenye hivyo vipaumbele ambavyo havikamiliki. Suala la kilimo

limekuwa likisemwa kila siku lakini hakuna mabadiliko yoyote ukizingatia asilimia 80 katika nchi yetu ni wakulima tena wengi wako vijijini ambako hakuna msaada wanaopata kutoka serikalini mpaka sasa hilo suala la kilimo kwanza, kwao ni kama ndoto bado wanatumia jembe la mkono pembejeo hawazipati bado wakivuna hawana soko la kuuza bidhaa zao. Wafanyabiasahara wachache ndiyo wanaonufaika kwa kwenda huko vijijini kununua mazao hayo kwa bei rahisi na kumwacha mkulima huyu kuendelea kuwa maskini.

Nafikiri umefika wakati wa kujua kuwa wakulima wako wangapi na tujue mahitaji yao pia tuzungumze nao, kwani itawezekana yale mazingira mazuri wanayopewa wawekezaji kwenye mashamba makubwa na watu wetu wapewe ili kuwawezesha wananchi wetu kumiliki mashamba madogo na kuwatengenezea miundombinu ambayo itawawezesha kuitumia. Kwa kufanya hivyo kutaweza kuajiri watu wengi katika eneo hili la kilimo badala ya mtu mmoja kuwa na mashamba makubwa na kuacha wananchi wetu kuwa vibarua katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, huduma muhimu kama simu serikali inaongeza kodi kwa mwananchi ambaye amekuwa akilipa gharama kwa makampuni haya hii haiingii akilini kabisa kama serikali imeshindwa kutafuta njia nyingine ya kuongeza mapato yake ikaona irudi kwa mwananchi yule yule akilipia kodi kupitia simu. Niunge mkono mapendekezo ya msemaji wa kambi ya upinzani kwamba kodi hiyo ilipwe na kampuni za simu

kupitia kodi ya mapato na kwa wananchi kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa *TRA* imevuka malengo kwa kukusanya zaidi (asilimia 104). Ningetaka kujua kama tulivuka malengo ni kwanini fedha tulizopitisha kwenye wizara, Mikoa na Halmashauri zetu hazikupelekwa na kusababisha miradi mingi kushindwa kutekelezwa kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limekuwa linajitokeza kila Bajeti ni kuongeza kodi kwenye sigara, soda, pombe, hivi ni nchi gani duniani inayotegemea vitu hivyo tu kila mara kuongeza pato la nchi? Hii imesababisha wananchi wetu wengi kuishia kunywa pombe ambazo hazina ubora wa kutosha na kuwasababishia madhara katika miili yao. Hivi ikitokea Watanzania wakiacha kuvuta sigara na kunywa pombe nchi yetu itakuwa kwenye hali gani? Tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana kwenye misamaha ya kodi hasa kwenye eneo la madini. Ni kwa nini hatutaki kuachana na mikataba hiyo ambayo inawanufaisha wawekezaji toka nje na kuwaacha Watanzania wakiumia kwa kutozwa kodi ambazo hazina msingi zinawaumiza tu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ila siungi mkono Bajeti hii.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imetofautiana na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ulitoa mapendekezo

yake katika matumizi ya miradi ya maendeleo kwa kutenga asilimia 35 lakini Bajeti imeshuka na kuwa si zaidi ya asilimia 30 ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imezingatia matumizi holela yasiyokuwa ni ya kutatua matatizo ya wananchi wa Tanzania. Bajeti imelenga katika makongamano, semina, warsha, safari za viongozi, pango na kuanzisha Mikoa na Kata za kisiasa. Mwaka 2011/2012 Bajeti ya jumla ilikuwa trilioni 13 na matumizi katika miradi ya Maendeleo trilioni 15 wakati matumizi ya miradi ni 4.5. Hivyo, utaona ni kwa jinsi gani Bajeti hii haiwezi kukwamua matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuzingatia mgawanyo mzuri wa kutoa vipaumbele ukiangalia Bajeti ya Mikoa ya Kusini haimo kabisa katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji wakati Kusini ina hazina ya mito mikubwa mingi kama Rufiji, Matandu, Mavuji, Mbwemkuru, Lukuledi, Lumesule, Ruvuma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikutaja mpango wa kuongeza nguvu ya umeme kwa wananchi wa mikoa ya Kusini. Bali imezingatia kuhamisha gesi ya *Mnazibay* na kwenda kuongeza nguvu maeneo ambayo tayari umeme upo tena umeme wa gridi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikutaja mapato ya serikali yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru kupitia stakabadhi ya mazao ghalani. Ni kiasi gani kimekusanywa tokea mpango huo uanzishwe na ni yapi manufaa waliyopata wazalishaji wa korosho wa mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti imetaja mfumuko wa bei na hasa katika bei za vyakula ambapo kuna ongezeko la kutoka 12% - 26% mwaka 2011 na sasa kuwa wastani wa asilimia 24% lakini ukiangalia mahitaji ya Mtanzania nusu ya gharama inatumika kwa mahitaji ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imeendelea kufuata utaratibu wa *Cash Budget.* Hili ni tatizo si tu la kitaifa bali hata katika Wilaya na mikoa. Mradi mingi ya Maendeleo imekwama kutokana na kukosa fedha, mikopo ya fedha na fedha za wahisani. Leo mpaka tunamaliza Bajeti ya 2011/2012 si zaidi ya asilimia 30 ya Bajeti katika Halmashauri ya Lindi ilifika kwa miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawakopesheki kutokana na vikwazo na vigezo vinavyotumiwa na wakopeshaji. Mfano, SUMA JKT ambao wanahitaji kupata dhamana ya mali isiyohamishika kama nyumba au shamba. Hivi mkulima gani au wakulima wangapi wenye uwezo wa kumiliki mali hizo.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawazingatiwi katika kupanga Bajeti ya pembejeo kwa wakati, wakati serikali ikipanga mipango yake ya matumizi hapa Dodoma. Mkulima wa Lindi na Mtwara ana haha kutafuta sulphur kwa ajili ya mikorosho yake mpaka *sulphur* inapofika msimu wa upuliziaji umeisha na hivyo kumkosesha mkulima mazao.

Mheshimiwa Bajeti hii haikueleza kinagaubaga mpangilio wa utoaji ajira na hasa katika sekta isiyo

rasmi. Kilichopo hata kwa wale wanaotakiwa kuajiriwa ukiritimba umekuwa mkubwa, ukiangalia katika maeneo ya utoaji leseni upatikanaji viwanja na mashamba, pembejeo, madawa na vifaa vya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuzingatia malengo ya milenia kwa kutozingatia kumsaidia mtoto katika sekta ya Afya. Utafiti unaonyesha matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa bado ni hafifu na hasa vijijini. Matumizi ya dawa za kuongeza maji na kupunguza magonjwa ya matumbo (*oral dehydration*) na kadhalika umekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imethubutu, imeweza na inasonga mbele katika kuona maisha ya Mtanzania yanazidi kudidimia. Ni wakati pekee kwa serikali kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya kwa:-

(i) kuhakikisha jamii, taasisi katika kupanga mipango yake ya mandeleo;

(ii) iondoe misamaha holela kwa wawekezaji;

(iii) idhibiti wanaokwepa kulipa kodi; na

(ivi) iwekeze katika miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho siungi mkono hoja.

**MHE. LAMECK OKAMBO AIRO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Bajeti hii kama ifuatavyo. Bajeti hii

kwa kweli haijengi kwenye miradi ya maendeleo ikilinganishwa na ahadi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliyowaahidi wananchi wakati wa uchaguzi uliopita. Kwa maana hiyo mimi ninashauri miradi ya maendeleo isogezwe hadi asilimia 35 au 40.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ingeelekezwa sana kwenye Kilimo hasa kwenye kilimo cha kumwagilia hasa sehemu ambazo hazipati mvua mara kwa mara kanda ya Ziwa na kanda ya kati.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa pamba bei katika soko la dunia imeshuka. Bodi ya pamba imepanga bei kati ya Sh. 510 mwaka jana bei ilikuwa Sh. 100 na 1200 nashauri serikali itoe ruzuku ya Shilingi Kati ya 300 au Shilingi 400.

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda viwanda vya ndani. Pamekuwepo na tatizo la ajira katika nchi yetu lakini kwa makusudi serikali ikiamua kulinda viwanda vyetu vya ndani na kuviwezesha kuongeza mazao yatokanayo hapa nchini yatafanyika hapa Tanzania na thamani hizi zifanyikie kule kule mazao yanakolimwa ili kuzuia vijana kukimbilia mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri: Mfumo wa bidhaa zinazotokana na pamba zipewe msamaha wa ongezeko la kodi *(VAT) – zero rate* kwa bidhaa za nguo na mavazi hii itaongeza mapato na ajira kwa wafanyakazi kulipa *(PAYE).*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Bajeti Bungeni.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi la kulizingatia na kudhibiti mfumko wa bei za vyakula ili kutunza mapato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii haikuzingatia punguzo hasa katika vifaa vya ujenzi kama vile bati na saruji, hii ingesaidia sana wananchi kuweza kumudu kununua vifaa hivyo, na hivyo kuweza kupata kuishi katika nyumba iliyo bora kiafya. Kwa maana hiyo haya mambo mawili niliyoyataja – kupunguza bei za vyakula na kupunguza bei za bati na saruji itawafanya wananchi walio wengi kumudu kwa kuanza kutadhimini maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii kwa kiasi kikubwa haionyeshi umakini wa ukusanyaji wa mapato/kodi.

Mheshimiwa Spika, kama walivyoshauri wengine kuelekeza nguvu zake zote kwa makampuni yote ya simu makampuni yote ya madini nishati kukusanya kodi kwa ajili ya Maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa kuwa makini kuweka mkazo mkubwa juu ya miundombinu ya kibiashara zaidi kama vile reli, viwanda na bandari. Mambo haya matatu kama tunakuwa makini sana kwa kuzingatia (1) Reli, (2) Bandari (3) viwanda maendeleo ya Tanzania yatakuwa kwa kiwango kikubwa kodi kufikia asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka maendeleo katika mpango wa maendeleo lazima uweke vipaumbele hivi katika angalau asilimia 50 ya Bajeti yote ili kuona hatua hii inasaidia hata nchi jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mgimwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara ya Fedha, ambayo ni kitovu cha serikali. Pia niwapongeze wanawake wenzangu walioiweka historia na kuwa manaibu Waziri wa Fedha kwa pamoja. Mheshimiwa Rais kuna uhakika ameunda "*the winning team*" kumteua Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, kama Manaibu Mawaziri, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pili, nitoe pongezi kwa umahili wao Mheshimwa Waziri Mgimwa, kwa Bajeti ambayo ameiandaa kwa ufasaha na kwa muda mfupi tangu aanze kazi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nieleze kabisa kuunga mkono hoja. Ninataka hata hivyo yafuatayo yafafanuliwe vyema zaidi ili wananchi waelewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono uamuzi katika ibara ya 97 (i) Kufanya marekebisho ya sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kuweka kiwango cha chini cha

mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo cha sh. milioni tatu kisichotozwa kodi. Hatua hii ni muhimu na itasaidia kuwawezesha vijana wetu wanaojiajiri kufanya biashara zao ndogo ndogo bila kubugudhiwa hadi mtaji wao utakapoongezeka. Hata hivyo kuna umuhimu kwa Mheshimiwa Waziri kufafanua kwamba kundi hili la wafanyabiashara wadogo wadogo pia linajumisha wakulima wanauza mazao yao sokoni. Ni jambo la kusikitisha kwamba Halmashauri nyingine zimekuwa kero kwa wananchi. Badala ya kuweka utaratibu kuunda vyama vya ushirika ili kukusanya mapato kwa utaratibu wa *CESS* wameibuka na *barriers* barabarani na wanawaharass wakulima wanaokwenda sokoni kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Muleba wanateswa sana na utaratibu huu. Utakuta mkulima anatozwa sh. 200 kwa mkungu wa ndizi. Kama atafanikiwa kuuza Sh. 5000 atakuwa ametozwa asilimia nne ya mapato yake, kiwango ambacho kiko juu sana. Mbaya zaidi anazuiwa na kulipishwa kodi hiyo njiani kwa hiyo mkulima huyo asipompata mnunuzi wa ndizi yake basi anakuwa amelipa kodi hiyo kutoka mfukoni mwake kwa hiyo kumwongezea umaskini. Mheshimiwa Spika, ninaomba na kushauri jambo hili litafafanuliwe lieleweke. Kwa mantiki hiyo utaratibu wa ushuru unaowekwa na Halmashauri haufai maana unakuwa ni kisingizio cha kutoza kodi wakulima wadogo wadogo wakati bidhaa za viwandani vimesamehewa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika ibara 94 (i) imependekezwa kufanya marekebisho ya ada na tozo

mbalimbali za wizara, mikoa na idara zinazojitegemea. Aidha kumekuwa na malalamkiko kwamba tozo za ardhi *(land rent)* ziko chini sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha kuliona hili na kupendekeza kurekebisha viwango hivyo. Ninashauri hata hivyo viwango hivyo vya tozo za ardhi ambavyo vimekuwa chini sana viongozwe zaidi katika Bajeti ijayo ili thamani ya ardhi inayopanda kila siku isaidie kuongeza mapato ya serikali. Wale watakaoibuka kupinga viwango vipya vya tozo za ardhi ni wale wanaomiliki ardhi kubwa lakini hawatumii kulima bali *land speculation*. Mheshimiwa Spika, itambuliwe kwamba ni aibu na fedheha kuwa na ardhi kuikodisha kwa wakulima wadogo wadogo kwa bei kubwa wakati wanapotakiwa kulipa *land rent* wanalalamika eti tunazuia uwekezaji. Ni mwekezaji gani huyu ambaye hawezi kulipa *land rent.* Ninakupongeza kuliona hili. Aidha atakayeshindwa kulipia ardhi airejeshe serikalini apewe mtumiaji mwingine.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sina budi kuipongeza serikali kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Maendeleo ya wizara yangu kutoka bilioni 22 hadi bilioni 71 ongezeko la asilimia 322 isitoshe Bajeti ya Maendeleo inazidi Bajeti ya kawaida kwa kiasi kikubwa. Bajeti ya Maendeleo Wizara ya Ardhi ni asilimia 61. Ninampongeza Waziri wa Fedha kuliona hili na kutenga Bajeti itakayotuwezesha kuboresha miji yetu hasa kutengwa pesa kwa mradi wa mji mpya wa Kigamboni. Kwa

kuwa asilimia 100 ya makusanyo itabaki wizarani, moja kwa moja, asilimia 30 itabaki kwenye Halmashauri. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha asaidie kuhakikisha basi hata katika ngazi hii, Bajeti ya Maendeleo ya ardhi inakuwa kubwa kuliko matumizi. Miji yetu ikipangwa na ardhi ikapimwa, Hati zikitolewa hakika mapato ya serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naanza hoja yangu moja kwa moja kuchangia Bajeti hii ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka huu 2012/2013 imeweka vipaumbele saba ambavyo vitasaidia kuimarisha na kudumisha ustawi wa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji katika sekta ya kilimo ambayo inaajiri takriban asilimia 75 ya nguvu kazi nchini ilipungua kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 hadi asilimia 3.6 mwaka 2011, wakati kasi ya ongezeko la watu limeendelea kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya umeme gesi, mafuta ya kupikia, mchele, sukari, upungufu wa nishati na umeme, kuporomoka kwa thamani ya shilingi na upungufu wa chakula katika Kanda ya Afrika Mashariki hali inayotokana na ukame. Mahitaji ya chakula katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Somalia, Sudan na Sudani Kusini,

Mheshimiwa Spika, haya yote yameongeza kasi ya upandaji wa bei za chakula na sukari na hadi Aprili, 2012, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 18.7% ukilinganisha na asilimia 8.6 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Spika, mfumko huo, haujumuishi chakula na nishati mwaka ulioishia Aprili, 2012, uliongezeka hadi asilimia 9,0 kutoka asilimia 5.7 Aprili, 2011. Hii ilitokana na kuongezeka mfumko wa bei za mafuta katika nchi zinazofanya biashara na Tanzania hususan China na India.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei ya chakula, umeongezeka na kufikia asilimia 24.7 Aprili, 2013, kutoka asilimia 9.2 Aprili 2012. Mfumko wa bei ya nishati umeongezeka hadi kufikia asilimia 24.9 Aprili, 2012 kutoka asilimia 22.1, kwa mwaka ulioishia Aprili, 2011.

Mheshimiwa Spika, fedha zote za maendeleo mwaka huu ni asilimia 30 tu na asilimia 70 ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hii inatoa wasi wasi kwamba Serikali bado haijajipanga vizuri katika kukwamua maishi ya Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, tofauti ya bajeti ya mwaka jana, mwaka huu fedha za maendeleo zimepunguzwa kutoka trilioni 4.9 mwaka jana hadi kufikia trilioni 4.5 mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hii ndilo jambo ambalo linatoa wasi wasi mkubwa kwa Watanzania walio wengi ambao walitegemea kuwa mwaka wa fedha wa

2012/2013 Bajeti ya Maendeleo itapanda hadi kufikia angalau asilimia 45 toka zile za mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali ijistahidi katika kusimamia matumizi ya Serikali ili iweze kuendana na kukabiliana na hali ya maisha ya Mtanzania wa kawaida. TANZANIA BILA YA UMASKINI 2016/2017 INAWEZEKANA baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM NASSORO KISANGI**: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja ya bajeti ya Serikali asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuandaa Bajeti nzuri yenye maslahi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti nzuri zipo changamoto na ushauri unaotokana na muonekano wa Bajeti nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingi ambazo zitaongelewa na Waheshimiwa Wabunge walio wengi na haja ya kupunguza matumizi ya Serikali na tusiondoe kabisa safari za nje kwa kuwa kuona ni kujifunza ni lazima tuone maendeleo na tujichanganye na wenzetu ku-*share* ujuzi kwa mslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tupunguze tu safari za nje kwa ujumla isipokuwa zile zenye umuhimu wa kipekee kama vile za kielimu, matibabu na mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ni vyema tuliangalie ni kutumia vyanzo vya mapato kwa kupandisha kodi katika soda, bia na sigara. Vyanzo hivi vimepitwa na wakati katika miaka 50 ya uhuru sasa tubadilike.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyanzo vingi vya mapato. Serikali sasa iwe na ubunifu wa kutafuta vyanzo kama vile utoaji wa vilemba katika migodi yetu na kuchunguza *warehousing bonded* zetu kujua mali na kodi zinazolipwa na wafanyabiashara ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kupandishwa kwa bei ya soda ni kuwaua njaa watoto wetu wanaosoma mashuleni na vyuoni kwani wao wanatumia soda kama kinywaji na chakula cha kuwatia nguvu (*energy*) waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa vyuo, wanaofanya kazi jijini, watoto wa sekondari chakula cha mchana kwao ni soda na *chips,* soda na *biscuit,* soda na mihogo na wale wafanyakazi wa ofisini, chakula chao kikuu ni soda na vitafunwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali yetu ifanye mabadiliko na kuhusisha wajasiliamali wa vyuo vikuu na haswa ukizingatia sasa tuna kozi ya Enterpreneurship katika vyuo vikuu na wataalam wapo ni vyema tuwashirikishe katika kubuni mitindo ya kupata vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine utakuwa katika ukusanyaji wa kodi za majengo nikiwa kama mjumbe wa kamati ya mkoa wa Dar es Salaam ya kufuatilia ulipwaji wa kodi za maendeleo. Napenda kuipongeza TRA kwa kazi nzuri ya kukusanya kodi za majengo pamoja na changamoto nyingi zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ishsirikiane na Halmashauri katika kufanikisha zoezi hilo bila ushirikiano itakuwa ngumu. Kutokana na maendeleo ya uwekezaji katika majengo na baada ya tathmini zilizofanyika ni matumaini yangu kuwa chanzo hiki kinaweza kikatusaidia katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kukua kwa pato la Taifa kumekuwa kwa kusuasua kama ifuatavyo: 2010 pato la Taifa yaani *GDP* likikuwa kwa asilimia 7.0 mwaka 2011 pato la Taifa lilishuka kwa asilimia 0.6. Serikali inatarajia kuwa na ongezeko la asilimia 6.8 jambo ambalo haliwezekani ukizingatia historia ya Bajeti zetu nchini. Ukienda nyuma miaka kumi, ukuaji wa Pato la Taifa umekuwa hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali sasa ielekeze nguvu kutatua matatizo ambayo yamekuwa ni kikwazo cha maendeleo yetu likiwemo tatizo la umeme na ukame.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuondokana na tatizo la umeme ni lazima Serikali iwekeze zaidi kwenye nishati mbadala kama *solar energy* na *wind power*.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itawekeza kwenye nishati ya jua ambayo ni "*renewable*" hakika tatizo la umeme litakuwa limepungua kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na tatizo la umeme, endapo tutuepuka kuwekeza kwenye umeme unaopatikana kwa gharama kubwa hasa ule utokanao na mafuta ambayo tunayanunua kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, ili tuondokane na changamoto ya ukame ni lazima Serikali iwekeze kwenye *irrigation system.* Ni vyema serikali ikawekeza zaidi kwenye *irrigation system* kama ifuatavyo:-

- *Drip micro spray* na *sprinkler irrigation system.* Ushauri Serikali iwekeze zaidi kwenye aina hizo mbili za *irrigation* ukizingatia faida za aina hii ya kilimo cha umwagiliaji. Faida kubwa ya kutumia *drip micro spray* na *sprinkler* ni kwa sababu aina hizi za umwagiliaji hazitumii maji mengi na hutoa mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itajikita kutatua matatizo yetu kwa kutumia njia za kudumu katika kutatua matatizo ya nchi yetu, hakika *GDP* ya Taifa itapanda.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa neema na rehema zake nyingi alizonineemesha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya kila mwaka ya Serikali ni muhimu sana kwa maendeleo ya mustakabali mwema wa nchi yetu. Hivyo, hapana budi bajeti iandaliwe vizuri na kwa umakini mkubwa ulio na ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa na uwezo, nia nzuri na uzalendo wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wasaidizi wake (Naibu Mawaziri) wote wawili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo wa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, bajeti hii ina mapungufu labda kwa sababu hakupata muda wa kutosha wa kufanya uchambuzi wa kina kwa mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni tegemeo la uchumi wa nchi yetu kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula, kupata ziada ya kuuza nje ili kupata fedha za kigeni, lakini pia ni sekta inayoajiri zaidi ya asilimia sabini ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo hapana budi sekta ya kilimo inahitaji kuongezewa fedha ili kuiboresha. Kima kilichotengwa katika Bajeti hii bilioni 192.2 ni kidogo na hakikidhi haja na Kaulimbiu ya "KILIMO KWANZA."

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji hasa wa barabara na reli. Uchukuzi na usafirishaji ni lazima uende sambamba na uboreshaji wa kilimo ili mazao yatakayolimwa yaweze kusafirishwa kwa reli kwa masafa marefu na barabara kwa masafa marefu, na barabara kwa masafa mafupi ili kuweza kupunguza kwa mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei kwa kiasi kikubwa unachangiwa na ukosefu wa miundombinu imara ya uchukuzi. Kuna baadhi ya mikoa ina ziada kubwa ya uzalishaji wa chakula, sekta ya uchukuzi ikiboreshwa itapunguza sana kasi ya mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa katika sekta ya uchukuzi hazikidhi haja ya kuimarisha reli, hasa reli ya kati ambayo safari za garimoshi zinasuasua! Usafirishaji kwa reli unasaidia sana kupunguza mfumko wa bei kwani bidhaa zinasafirishwa kwa bei nafuu. Huu ni kwa sababu safari moja ya treni ina uwezo wa kusafirisha mizigo mingi kwa pamoja. Kukosekana usafirishaji wa treni ndiyo maana mfumko wa bei umeshuka kwa asilimia 1.1 tu kwa kipindi cha miezi mtano kutoka asilimia 19.8 *December,* 2011 hadi asilimia 18.7 mwezi Aprili 2012! Hii ni aibu kwa nchi! Nchi ambayo ina ziada ya uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuongeza Bajeti ya kilimo ya mwaka huu angalau kwa asilimia 25 ifikie bilioni 250.7.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia fedha zilizotengwa kwa Wizara ya Uchukuzi zigawanywe katika vipaumbele vichache ili ziweze kufanya kazi inayoonekana. Msukumo mkubwa uwekwe katika kuiwezesha reli ya kati kufanya kazi kwa angalau safari saba kwa wiki.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia uwanja wa ndege wa Songwe umaliziwe na ufunguliwe ili uanze kazi mara moja na uweze kuingiza mapato yatakayosaidia kujaza mfuko wa hazina na kufungua zaidi sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia makampuni ya madini yalipe kodi! Tufanye *review* ya mikataba. Madini yetu yanamalizwa bila ya nchi kupata chochote! Kusubiri mikataba mipya ya madini ndiyo tutoze kodi ni kufanya mzaha! Maeneo yote yenye madini, yameshaingiwa mikataba, hiyo mikataba mipya tutaifunga kwa madini yepi?!

Mheshimiwa Spika, tuwe imara kuivuna *Gas* yetu kwa maslahi ya nchi.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi ngumu na nzito inazozifanya zikiwemo changamoto mbali mbali kwa kuandaa mipango na mikakati mbali mbali ya kutaka nchi yetu iondokane na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka kwamba serikali yetu iliandaa mpango wa maendeleo wa miaka

mitano ambao ni moja ya harakati za kukuza uchumi nchini. Jukumu la Serikali pamoja na mambo mengine lazima Serikali ihakikishe na kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba mpango huo unafanikiwa na unatekelezeka na kuona kwamba wananchi wa Taifa hili wanafaidika na mpango huo.

Mheshimiwa Spika, ikiwemo kubuni vyanzo vya mapato na kubadili visivyotekelezeka ili kuhakikisha kwamba mapato ya nchi yanaongezeka kwa kiasi kikubwa ili itakapafikia mwisho wa tathmini kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kubuni vyanzo vya mapato ni pamoja na kuelekeza fedha za maendeleo vijijini ili vyanzo vilivyobunmiwa viweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia pamoja na uchache wa Bajeti unaolikumba Taifa letu ingeelekeza fedha za miradi ya maendeleo katika vipaumbele vichache kwanza ni kuhakikisha vimekuwa kama tunavyohitaji na mwaka unaofuata kuelekeza fedha hiyo katika vipaumbele vingine. Hatua hii ingetusaidia sana kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mipango iliyoandaliwa na Taifa letu ni mizuri sana na inawezekana sisi kama Tanzania tukashindwa kutokana na uchache wa Bajeti na mpango huo huo ukakopiwa na mataifa mengine makubwa kwa kuendeleza uchumi wao siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya sisi, fedha haitoshi, inapelekwa kwa baadhi ya wakati

unaporuhusu na hivyo haikidhi haja kulingana na ukubwa wa miradi yenyewe tunayotaka kuizalisha, matokeo yake katikati ya utekelezaji miradi mingi inakwama kutokana na uchache wa fedha na mwisho kuleta malalamiko kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ihakishe kwamba inaeleekeza na kutenga fedha zinazoweza kukamilisha miradi michache kwanza ili maendeleo tunayohitaji yaweze kufikiwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikishwaji wa wananchi, wadau mbali mbali katika maandalizi ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali ikaangalia namna ya kubadilisha utaratibu wake wa uandaaji wa Bajeti uliozoeleka na sasa kuwashirikisha wadau mbali mbali, taasisi na mashirika mbali mbali ili kuweza kutoa mawazo yao kuhusu Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kila mara tumekuwa tukiishauri Serikali kuhusiana na ushrikishwaji mapema na mawazo yatakayopatikana kufanyiwa kazi na kuwekwa ndani ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua kama hiyo itakapofuatwa itaweza kuondoa malalamiko kwa kiasi kikubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, utegemezi. Sasa hivi kumekuwa na mkakati kwa mataifa makubwa kuzitaka nchi rafiki kufuata msimamo wa ndoa za jinsia moja na

tukiangalia kwamba Tanzania ni nchi moja inayoendelea kupokea misaada mbali mbali kutika mataifa hayo, pia kama Tanzania kibajeti tumekuwa tukiendelea kutenga fedha nyingi za wafadhili kwa miradi ya maendeleo ya Taifa letu ambazo hatuna uhakika wa kusitishwa misaada hiyo sasa au baadaye.

Mheshimiwa Spika. Ni vyema sasa Serikali ikaweka mkakati wa muda mrefu kuhakikisha kwamba tuimeondoa utegemezi siku hadi siku kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kupanga mipango mizuri ikiwa ni mtiririko wa utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika utekelezaji wa mipango hiyo lazima Serikali ijipange vizuri kwa sasa kuelekeza nguvu zake kule vijijini hatua kwa hatua ili tuweze kukuza vyanzo vya mapato vilivyopo vijijini kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mawazo ya wadau, taasisi, wananchi mbalimbali wabunge wakiwemo viongozi mbalimbali, mashirika yetu mbalimbali ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu na maandalizi ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia usimamizi wa fedha za umma ni muhimu katika kukuza maendeleo ya Taifa letu. Tunafahamu kwamba fedha zinazoelekezwa katika miradi ya maendeleo zinapelekwa nusu nusu na kusababisha kusita kwa baadhi ya miradi kumalizika

kwa wakati mwafaka. Hii ni moja ya mambo yanayosababisha kukwama kwa miradi mbali mbali kwani fedha zilizokusudiwa kwa kutokamilika kufikia hatua ya kufanyiwa ubadhirifu au kupotea kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi hewa. Likomeshwe kabisa na kuchukuliwa hatua zinazofaa kwa waliohusika na upotevu huo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwa makampuni yanayoingia nchini iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu ni kuhusu fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Bajeti hii bado ni kidogo. Serikali iangalie namna ya kuziongeza kwani kutapelekea kudhoofisha juhudi za Serikali kwa kupeleka fedha kidogo kule miradi ilipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hutoba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2012 imelenga kukabiliana na changamoto zinazokabiliana na Watanzania hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu imezingatia vipaumbele vya mpango wa kwanza wa maendeleo kwa wananchi wake. Tunashukuru Serikali kwa shabaha yake ya kukuza ukusanyaji wa mapato kwa

lengo la kukuza Bajeti ya Serikali pia nishukuru Serikali kwa mpango mzima wa kukuza sekta binafsi ili kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Serikali kwa mipango mizuri ya Bajeti yake hii.

Mheshimiwa Spika, imani yangu kwa Serikali mwenendo wa ukusanyaji mapato 2011/2012 Serikali kama itakuwa makini juu ya swala zima la ukusanyaji na usimamizi mzuri wa mapato imani yangu mapato yatapanda na tutaweza kutimiza lengo la Bajeti yetu kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya makusanyo ya kodi itokanayo na vijana wa boda boda pamoja na machinga kodi iondoshwe badala yake kodi ipandishwe baadhi ya maeneo mengine. Mfano, vinywaji vikali na sigara ziendelee kupandishwa kwa vinywaji vya ndani pamoja na vya nje kwani hivi si vya lazima bali ni vya starehe tu.

Mheshimiwa Spika, vitu vya kuangalia vya msingi kwa wananchi wetu wa Tanzania na kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kati ya vitu vya kupewa kipaumbele hasa pamoja na bei ya sukari, mchele, mafuta ya taa. Vitu hivi vinawatenga wananchi wa vijijini hasa, naomba kwa ukubwa wa Serikali na usikivu wake uangalie maeneo hayo kwa ukubwa wake wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa viwanda nchini ni kichocheo kikubwa cha ongezeko la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kuboresha na kuanzishwa viwanda kwa sababu tunayo malighafi za kutosha, tuna pamba, ngozi, matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kwa namna ya kipekee kabisa usambazaji wa maji, umeme na barabara.

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kuangalia kwa makini suala zima la mahitaji ya msingi kwa Wilaya husika kwa jitihada za Serikali zinapelekea baadhi ya maeneo kutofanana kwa matatizo. Mfano kuna wilaya sasa hazihitaji barabara bali zinahitaji maji na chakula. Kuna maeneo mengine hayana mahitaji/shida ya maji bali yana shida ya barabara.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kabla ya matumizi ya Bajeti hii lazima tufanye tadhmini ya mahitaji kwa mpango mahitaji ya wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa umuhimu mkubwa kwa maslahi ya vijana wa Tanzania pamoja na Watanzania kwa jumla.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwai Dkt. Mgimwa (Mb), Manaibu Mawaziri wake wote wawili; Mheshimiwa Saada Mkuya na

Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (Mb), Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kuweza kufanikisha kuwasilisha Bajeti katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma katika kitabu cha Bajeti ukurasa wa tano utaona lengo la Serikali limezingatia kukabiliana na changamoto zinazozokabiliwa na chakula nchini, kupambana na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa sita tunaona Serikali inalenga kuimarisha ukusasnyaji wa mapato na kusimamia matumizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu bado haijakuwa na mpango mzuri sana wa kusimamia mapato yake na kuwa vyanzo vipya vya mapato hasa katika halmashauri zetu zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika halmashauri zetu kumekuwepo na mianya mingi sana ya wizi inayosababisha upotevu wa mapato yanayotokana na uzembe na ufujaji wa mali za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa nini isitungwe sheria ya kulazimisha halmashauri zote zitumie mfumo wa TEHAMA ili kuweza kuthibiti wizi na baadhi ya watendaji wanaoweka mitandao yao kwa ajili ya kutafuna pesa za halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kamati yetu ilipotembelea kitengo cha *TCRA* walituonesha mfumo waliougundua

wa ukusanyaji mapato katika halmashauri na wakatupatia mfano wa Halmashauri iliyofanikiwa kwa sababu ya kufunga mfumo huo, ambayo ni Halmashauri ya Temeke. Walisema kabla ya kutumia mfumo huo halmashauri ilikuwa inakusanya shilingi bilioni sita na baada ya kutumia mfumo huo wakaweza kukusanya shilingi bilioni 26.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yao wakatueleza kuwa mfumo huo umetungwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam. Halmashauri za Ilala na Kinandoni wanasuasua kutumia mifumo hiyo na ndiyo maana nasema iwe ni lazima ili Serikali yetu iwe na wigo mkubwa wa ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo vyetu wenyewe badala ya kutegemea pesa za wahisani ambazo tunazipata kwa masharti magumu.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba Serikali ijaribu kubana matumizi yake. Inatenga pesa nyingi sana kwa ajili ya matengenezo ya magari wakati kipo kitengo cha Serikali kinachohusika na Wizara ya Ujenzi *(TEMESA)* na utaona pesa imetengwa kwa ajili ya kitengo hicho ni kwa nini Serikali isilazimishe magari yote ya Serikali kutengnezwa katika kitengo hicho? Ili kupunguza matumizi mabovu ya magari na wizi mkubwa unatumika katika *garage* za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kama hilo haliwezekani ni bora kitengo hicho kingefungwa ili kupunguza gharama za wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilikuwa naombi ufafanuzi kuhusu faini zinazotozwa kwa ajili ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, tulipofanya ziara Kamati yetu ya miundo mbinu kukaa na ujenzi wa barabara nchini tulikuta makandarasi wengi hawajalipwa malipo yao na wamehama kutokana na ucheleweshaji huo makampuni yameanza kutoza *(interest)* sasa ningependa kujua nini tatizo la ucheleweshaji huo ni nini? Ucheleweshaji huo haukidhi hiyo *interest* inayotozwa? Hiyo *interest* inajumuishwa katika Bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, ni vyema miradi hii ya barabara ingeangaliwa ili inayoweza kutekelezeka kwa kuliko kuwa na miradi mingi inayoendelea kuongeza gharama na isiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, mwisho niulize kuhusu ucheleweshaji wa kibali cha Serikali kuzipatia halmashauri zetu kibali kutoza kodi ya leseni tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi. Naomba kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, riba ya kukopea inapokuwa kubwa kiasi huathiri dhana nzima ya mwananchi kupata mkopo. Angalizo; mfumko wa bei uliopo kwa

sasa umesababishwa na upungufu wa uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali. Mfano sukari, unga, umeme na upandaji wa bei za mafuta. Mkakati wa kupunguza mfumko wa bei lazima ilenge chanzo halisi cha mfumko wa bei. Ieleweke kuwa mfumko wa bei unatokana na upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula na kupanda kwa bei ya mafuta duniani na sababu zingine zinazofanana na hizi. Ushauri; ni vyema Serikali ijipange vyema kukabiliana na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato 2011/2012. Serikali iliendelea kukopa na kulipa madeni – kitendo hiki cha Serikali kuendelea kukopa na kulipa madeni kinapelekea kuonesha kuwa Serikali mapato yake sio stahimilivu.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni vyema Serikali iboreshe mifumo ya ukusanyaji mapato ya ndani ili yatumike kulipia madeni na si mikakati inayotumika ya kukopa na kulipa madeni.

**MHE. DKT. MILTON MAKONGORO MAHANGA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii lakini nina mambo matatu ya kusisitiza: Kama serikali haitakuwa makini katika kufuatiliaji wa fedha na mipango ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, basi ahadi ya serikali kwamba kufikia mwishoni mwa 2014, tatizo la maji Dar es salaam litamalizika, inaweza kushindikana na litakuwa jambo baya kwa serikali yetu na chama tawala.

Msongamano katika jiji la Dar es Salaam ni tatizo na ni janga la Taifa. Mpango wa mabasi yaendayo

kasi pekee hautaweza kumaliza tatizo hili bila barabara unganishi kujengwa na ziwe imara. Barabara hizi unganishi zimeainishwa vizuri na mpango umewekwa kuonyesha namna zitakavyojengwa na kukarabatiwa ili kusaidia kuondoa msongamano. Lakini kwa kweli serikali haijaainisha vizuri na kuweka mkakati wa uhakika wa kupata au kuweka fedha za miradi hiyo ndani ya miaka mitatu hii ijayo, kama ilivyoahidiwa. Serikali ijielekeze sasa kuweka fedha za barabara hizi.

Serikali katika mwaka 2012/2013 kwa mara nyingine, haijatenga Shilingi bilioni 18 za kuwahamisha wananchi wa Kipunguni ili kupisha upanuzi wa JNIA. Baada ya miaka 15 wananchi wa Kipawa na Kigilagila walilipwa fidia na wakaondoka. Sasa tumewaacha wananchi wa Kipunguni wakiwa hawajui hatima yao na hawawezi kujiendeleza kimakazi kwa muda wote huo.

Mheshimiwa Spika, tafadhali serikali ifanye hima kulipa fidia hii.

Mheshimwa Spika, kumekuwa na dhana (isiyo sahihi kiuhalisia) kwamba Bajeti ya maendeleo ya 2012/2013 ni asilimia 30 tu na hao wananchi wakiwemo Wabunge wametaka Bajeti ya Maendeleo ipandishwe ifikie asilimia 40 ya Bajeti nzima.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba si kweli kwamba Bajeti ya Maendeleo ni asilimia 30 tu. Hata kama haifikii asilimia 40, Bajeti ya maendeleo ni zaidi ya asilimia 35. Tatizo ambalo liko ni kwamba mfumo wa mahesabu *(accounting)* ya uandaaji wa

Bajeti una mapungufu kidogo na hautoi hali halisi ya Bajeti ya Maendeleo na nitaeleza.

Mheshimiwa Spika, ruzuku inayotolewa na serikali kuu ya shilingi 1,706,418,064,527 kwa mamlaka, wakala, vyuo vya umma, bodi mbalimbali, kamisheni na taasisi zingine zinazojitegemea ambazo zote zinaoneshwa kama matumizi mengineyo. Wakati ukweli ni kwamba taasisi zote hizi zinatumia sehemu kubwa tu ya ruzuku hii kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya taasisi husika. Taasisi zingine hizi kama *Road Board* inayopokea zaidi ya shilingi bilioni 300 inatumia karibu ruzuku yote hii kwa ajili ya maendeleo kwa maana ya kujenga na kukarabati barabara kwenye halmashauri zote nchini. Aidha, ruzuku yote ya mikopo kwa wanafunzi kwa kweli ni suala la uwekezaji kwenye elimu ambayo ni suala la Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukiachia ruzuku ya bilioni 2,031 za mishahara kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, ruzuku nyingine inayokwenda kwenye halmashauri hizi pamoja na *own source* sehemu kubwa tu ya ruzuku na mapato haya inatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini kwenye Bajeti ya Serikali fedha zote hizi zinaonyeshwa kama matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hata kama *Government Accounting* inaonyesha hivyo mimi naamini kwamba fedha za kununulia mitambo, magari, samani za nyumbani, samani za ofisi na vifaa, matengenezo na ukarabati wa majengo na ujenzi wake (vitu ambavyo uhai wake ni miaka 5 kuendelea, siyo sahihi kuitwa *OC.*

Hivi kwa kweli ni vitu vya maendeleo. Ukiacha Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Bajeti ya mwaka 2012/2013 inaonyesha kwamba kiasi cha bililoni 85.499 kitatumika kwa ajili ya manunuzi ya vifaa hivyo, ujenzi na ukarabati mkubwa wa majengo. Kiasi hiki kimahesabu kinatakiwa kiwekwe kwenye Bajeti ya deni la Taifa la bilioni 2,745 kuna gharama kubwa tu zenye *nature* ya *development.*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia mfumo wa uandaaji wa bajeti siku zijazo ili kuonyesha usahihi kwenye Bajeti ya Maendeleo ya *OC.*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Fedha. Kwanza nipongeze hotuba hii ya Waziri wa Fedha. Ni Bajeti safi sana ila inataka utekelezaji na nidhamu ya hali ya juu ili fedha hizo zitumike kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana wa Bodaboda itakuwa ni vyema ili waondolewe kodi waweze kujikimu na maisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fungu la maendeleo lizidishwe kwa sababu maendeleo ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Kama vile umeme barabara mashule zahanati na maji vijijini na mjini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuziboresha treni, jambo muhimu sana kwa sababu treni ndiyo mkombozi wa wanyonge. Kwa hivyo serikali isimamie kikamilifu treni ili ziwe imara na zifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu naunga mkono hoja hii, Ahsante sana.

**MHE. JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE**: Mhe.Spika, naunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu, aidha baada ya kuunga mkono hoja naomba nichagie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Usafiri Ziwa Tanganyika, kama kuna hatari ambayo tunatarajia muda si mrefu ni kwa usafiri wa meli iliyo kongwe kuliko zote kwenye uso wa Ziwa, Meli ya M.V. Liembe.

Mheshimiwa Spika, meli hii inayosafiri ndani ya ziwa hili kwa kuanzia nchi ya Zambia, kuelekea Kigoma ikiwa na ratiba isiyokuwa na uhakika kutokana na uchakavu mkubwa hivyo mara kwa mara kulazimika kufanyiwa matengenezo. Ni vizuri Serikali ikaepusha ajali kama ile ya M.V. Bokuba. Kwa kuzingatia ni muda mrefu kwa maana ya umri wa meli hii na ikawa kama kivutio cha watalii kwa meli iliyo na umri mrefu duniani iliyojengwa na Wajerumani.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha ushirika, zaidi ya Watanzania asilimia sabini wako vijijini na maisha ya yanaendeshwa kwa kutegemea kilimo. Naishauri Serikali kuhakikisha kwamba pembejeo zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa bei ambayo wataweza kumudu.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii ninapoandika wapo Mawakala ambao walifanya kazi ya kusambaza pembejeo kwa wakulima Mkoani Rukwa na baadhi ya

mikoa mingine na kazi hii imefanyika kwa ufanisi mkubwa lakini cha kusikitisha hadi leo Mawakala hao hawajalipwa pesa zao na hivyo kuingia hasara kubwa kwa wale waliokopa pesa kwani riba imekuwa kubwa sana kutokana na muda kuwa mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana pamoja na pembejeo kufika ni kwa kuchelewa hata viwango vyake havikuwa bora na hivyo kutokutoa matokeo yaliyotarajiwa hivyo naiomba Serikali ihakikishe kwamba pembejeo zinazowafikia wakulima zinakuwa ni zile zenye ubora.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa pamoja wa mafuta, lengo zuri la kuanzisha mpango wa kuagiza mafuta *(Bulk Procurement)* limekuwa na dosari kutokana na kipengele cha kwenye mkataba *(clause)* inayoruhusu kuongeza kiasi fulani cha *ethanol* kwenye mafuta ya petroli kimetumika vibaya kwa kuingiza mafuta ya petroli yasiyokidhi kiwango kwa shehena iliyoingizwa mwezi Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ni hali ya kusikitisha kwa shirika la taifa la viwango *(TBS)* kuweka kipengele cha kuruhusu kuchanganya *ethanol* kwenye mafuta ya *petrol* kabla kuwa na kipimo cha kuweza kubaini kiasi cha *ethanol* na kipengele hiki kiliwekwa kwa maslahi ya nani na hasa ukilinganisha bei ya *petrol* na ile ya *ethnol* kuna tofauti kubwa mbona hivyo kuwa kichocheo kikubwa cha kuchakachua mafuta ya *petrol.*

Mheshimiwa Spika, kwa tabia ya *ethanol* jinsi inavyokuwa inapokaribiana na maji ni wazi kwamba *petrol* inayoingizwa nchini kwa kupitia Bahari ya Hindi na matenki tuliyonayo si rahisi udhibiti maji kutoingia kwenye *petrol* hivyo naishauri Serikali ihakikishe kipengele hiki kinaondolewa kwenye mkataba na kama ni lazima kiwepo basi *ethanol* hii ichanganyiwe hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maduka ya fedha yasiyo rasmi, tulipitisha sheria yetu kuhusu udhibiti wa pesa haramu kwa bahati mbaya sana kumekuwa na ubadhirifu wa pesa katika maduka yaliyozagaa Kariakoo hasa kwa wa Watanzania wenye asili ya Kiasia na wenye asili ya Kisomali ambayo yanatumika kwa kutorosha pesa kwa kupokea pesa Tanzania na kuruhusu *withdraw* kufanyika nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa kuteulliwa kushika nafasi ya Uwaziri wa Fedha na Unaibu Waziri. Napongeza Katibu Mkuu na Watumishi wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo, serikali idhibiti matumizi. Serikali itoe aina maalum ya magari na iachane na V8, Safari za nje ziadhibitiwe,

makongamano, semina na warsha ambazo siyo za lazima zidhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, usumbufu wa bandarini Dar es Salaam kwa wananchi wanaotoka Zanzibar, Serikali iondoshe utaratibu uliopo sasa wa kulipa kodi mara mbili (wananchi kulipa kodi Zanzibar na akifika Dar es salaam kulazimika kulipa kodi tena). Serikali iondoshe kero kwa wajasiriamali wanaotoka Zanzibar na bidhaa ndogondogo kulipishwa kodi tena na wepesi (ni kero).

Mheshimiwa Spika, Kilimo, Serikali iangalie uwezekano maalum wa kuweka ruzuku katika vifaa vya kilimo kama matrekta, majembe, madawa na pembejeo. Serikali ichukue hatua kuweka mkakati wa kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kujitegemea kwa chakula. Kuwepo na mpango maalum wa kujengwa mabwawa ambayo yatatunzwa na maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kodi za kufutwa, kodi za majengo zifutwe kwani ni kero na hakuna utaratibu mzuri wa kukusanya. Kodi za pikipiki (Bodaboda) zifutwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiasha wenye mtaji usiozidi shilingi 10 wasitozwe kodi.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa melli, serikali inunue meli mpya kwenye Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali iangalie upya muundo wake kwa madhumuni ya kuwa na Serikali

ndogo ambayo itajikita zaidi katika utendaji wa kubana matumizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu na timu nzima ya wataalam wa Wizara ya Fedha kwa maandalizi na hatimaye kuwasilisha Bajeti ya Serikali hapa Bungeni. Ninaamini wataalam, Waziri na wengine wote walioandaa na hatimaye kuwasilishwa hapa Bungeni dhamira yao ni kuona kwamba Mtanzania na hasa mwananchi wa kawaida walau sasa ataanza kuona nafuu katika maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa Wizara ya Fedha pamoja na kusema katika Bajeti lengo la kuona kwamba mtu wa kipato cha chini halipi kodi. Mapato chini ya shilingi 3,000,000/= kwa mwaka hatalipa kodi, tunapongeza jitihada ambazo Serikali yetu na Wizara kwa mwaka huu imeonyesha. Ombi langu kwa Wizara wakati wa majumuisho tunaomba iainishe wafanyabiashara ambao watahusika na msamaha huo. Mfano mamantilie, wakulima wadogo wadogo wachukuzi ambao wanafanya biashara katika magulio na masoko yetu vijijini. Kuendelea kuwatoza ushuru katika maeneo yao ya biashara ni sawa na kulipa kodi. Ni vizuri basi Serikali ikatoa kauli au tamko ambalo halmashari hazitawasumbua wakulima hao au mamantilie na wachuuzi wadogowadogo ambao katika biashara hizo watakuwa wanapunguza makali ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni katika michezo ya Bahati Nasibu *TIGO – VODACOM - CELTEL,* Serikali inajipangaje katika kukusanya kodi ambapo kampuni za simu zinapata pesa nyingi katika uendeshaji wa michezo hiyo ambayo Watanzania wengi wanasikitika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMEIR**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, namshukuru Waziri wa Fedha kwa kutuletea Bajeti nzuri kwa mwaka huu wa fedha. Maombi yangu kwa serikali yetu ni kukazania kubana kwenye sekta ya madini na gesi ili kuweza kukusanya kodi nyingi kwa maendeleo ya nchi yetu. Maana yangu ya kuwabana sekta ya madini na gesi ni Serikali yetu iweze kuwapunguzia kodi wananchi wa kipato cha chini na kuwaondolea mizigo ya michango.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko sana kuhusu barabara ya toka Kilosa hadi Mikumi haikutengewa fedha kabisa. Ilani ya chama chetu ipo na Waziri wa fedha aliepita alitoa ahadi mwaka jana kuwa atahakikisha barabara hiyo itakwisha. Naomba maelezo toka kwako kwa nini hakuna pesa iliyotengwa mwaka huu kwa ajili ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo kweli pesa iliyotengwa ni kidogo sana. Je, tutaweza kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza. Naomba ruzuku itolewe

kwenye mazao yote ya kibiashara pia sio baadhi tu ya mazao. Suala la kuondoa kodi kwa pikipiki za aina zote pamoja na za matairi matatu kwa kweli ni ukombozi wa wananchi wa vijiji kwa usafiri wa haraka kwa wananchi na pia za matairi matatu kwa usafiri wa mazao toka mashambani hadi kwenye maghala au majumbani mwao. Naomba sana Serikali ione pia ni ajira nzuri kwa vijana wetu na wengi wao tunashukuru kwa kujiajiri na ajira ni moja ya ahadi ya chama cha Mapinduzi (CCM). Chonde chonde Mheshimiwa waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, narudia kutoa shukrani na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kuipoingeza Serikali kwa kufanya mabadiliko makubwa katika Wizara ya Fedha kwa kumteua Dkt. Mgimwa, kuwa Waziri na Manaibu Waziri wawili ambao ni akina mama shupavu. Tunaamini kuwa watachapa kazi kwa kiasi zaidi na watatutoa Watanzania katika hali ngumu ya maisha tuliyonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchangia machache katika Bajeti Kuu. Kwanza, napenda kutamka kuwa siungi mkono hoja hii ya Bajeti kwa sababu zifuatazo:-

Ongezeko la kodi kwenye huduma za simu. Kuongeza kodi kwenye huduma za simu ni kumwongezea Mtanzania wa hali ya chini mzigo, kwa sababu huduma za simu sio anasa ni huduma muhimu

hasa kwa wakati huu tulionao wa Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, lakini hata haya makampuni makubwa ya huduma za simu kama *VODACOM, AIRTEL* na *TIGO*. Yalipe kodi kama inavyopaswa hivyo Serikali kupitia *TCRA* inatakiwa ifanye haraka kuhusu mchakato wa kupata kifaa ambacho kitasaidia kuhakiki mapato sahihi wanayopata ili serikali ikusanye kodi inavyostahili badala ya makampuni haya ya simu kutoa taarifa yenyewe.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa, linazidi kuongezeka kwa kasi japokuwa bado nchi yetu inaweza kukopa lakini kuongezeka kwa deni la Taifa ni ishara tosha kuwa nchi yetu inaelekea pabaya.

Mheshimiwa Spika, deni letu sasa limefikia shilingi 18,8194 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 12.6 kutoka shilingi 16,708.2 bilioni mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ni lazima serikali ijipange vizuri kuhakikisha kuwa deni letu haliongezeki kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Serikali ihakikishe kuwa kitengo maalum cha kubuni na kusimamia vyanzo vipya vya mapato sio kila mwaka ni kwenye vyanzo vilevile mfano Soda na Pombe. Lakini pia naunga mkono kwa Serikali kwa wazo la kuondosha kodi kwenye bodaboda (pikipiki) kwani ndiyo ajira kubwa kwa vijana wetu sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika sekta za kiuchumi na kijamii, naipongeza serikali kwa mpango mzuri na ishara ya mafanikio imeanza kuonekana la kuzingatia zaidi, vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa lolote, sekta inayo nafasi ya kuajiri watu wengi hasa vijana. Nashauri, Serikali iandae utaratibu wa kuwatambua vijana wote, Elimu yao sehemu walimu, shughuli wanazofanya, ujuzi walionao na kadhalika**.**

Mheshimiwa Spika, kuandaliwe *program* maalum kwa kuwashikisha vijana na shughuli za kilimo huko vijijini waliko ili kuzuia wimbi kubwa la vijana kukimbilia mjini. Kila mkoa na wilaya, kijiji itenge maendeleo maalum na kumilikiwa kisheria ili waweze kuzitumaia kwa kukopa. Sekta mbalimbali ziwe karibu kwa kufikisha miundombinu kama maji, pembejeo, utaalam na masoko.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi, Serikali bado haijalisimamia vya kutosha eneo la uvuvi. Iweke mpango maalum wa kuwapatia vifaa na mafunzo wavuvi wetu waweze kuvua maji ya kina kirefu badala ya kuharibu mazingira kwa kutumia vifaa nduni na kuharibu mazalio ya samaki. Hali kadhalika viwanda vya kusindika mazo ya baharini vianzishwe kuweza kuongeza thamani na ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero za Muungano zilizopo ni vyema mwaka huu ufumbuzi ukapatikana ili kuondosha manunguniko yasiyo na tija kwa maslahi ya

Muungano wetu. Asilimia kubwa ya vijana wamezaliwa ndani ya Muungano. Hivyo ipo haja ya kuwa na *program* maalum za kuwaelimisha wananchi umuhimu wa Muungano wetu hasa kwa wakati huu ambapo Dunia imekuwa kama kijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikaoi ni muhimu sana katika kutekeleza mipango ambayo imewekwa na kupangwa na serikali ili ikitimiza malengo yake ambayo ni kuinua maisha ya Mtanzania. Vipaumbele ambavyo vimewekwa ni muhimu na vimelenga kuinua maisha ya Mtanzania. Naomba katika utekelezaji wa Bajeti katika Jimbo la Mufindi Kusini, ikumbukwe kwa ahadi ya Rais ambayo ni umeme katika Kata ya Malangali. Ni muhimu sana, ni Kata yenye idadi ya watu wengi sana ambayo ina wakulima na wafanyakazi katika taasisi mbalimbali. *TANESCO* walishafanya upembuzi yakinifu na waliona kweli ni muhimu sana wananchi wa Malangali wapewe umeme.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyololo – Igowole – Twango - Mgololo, ni barabara muhimu sana katika uchumi wa taifa hili tukizingatia una watu wengi sana ambao wanategemea barabara hii. Wanafanya kazi za kilimo cha biashara kama vile Kilimo cha Chai, Kilimo cha Pareto na sasa tunaanza kilimo cha Umwagiliaji wa Mpunga. Pia kuna viwanda vikubwa vya Karatasi, Mbao na Chai. Waziri wa Ujenzi alishaahidi katika Bunge, katika kujibu swali mwaka jana, 2011 kuwa

mwaka 2012/2013 kazi ya kufanya upembuzi yakinifu itaaanza mara moja na mimi namwamini sana Waziri wangu wa Ujenzi kwa mwaka 2012/2013 kazi hiyo itaanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Mufindi Kusini, lina matanki ya maji ambayo yalijengwa na Serikali kwa kushirikaina na wananchi miaka ya 1970 - 1980, Matanki hayo yalikuwa yanatumika vizuri sana sasa hayatumiki kutokana na kuharibika kwa miundo mbinu yake ambayo hajawahi fanyiwa ukarabati kwa miaka mingi. Matanki hayo ni Kijiji cha Sawala, Kijiji cha Kibao, Kijiji cha Nyololo, Kijiji cha Maduma, Kijiji cha Nyigo, Kijiji cha Igowole. Wananchi wanapata tabu sana ya maji wakati mataniki yapo na mito ipo ambayo inatoa maji kwa wingi. Sasa naiomba serikali katika Bajeti hii serikali kwa kushirikana na Halmashauri ya wilaya ya Mufindi kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji katika Jimbo la Mufindi Kusini ili wananchi waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo wameshafanya *waring* ya umeme katika nyumba zao, sasa kuna tatizo la *transforma* wananchi wanalalamika sana. Naomba Serikali kupeleka transforma katika vijiji vya , Mninga na Kihanga.

Mheshimwa Spika, nitashukuru sana kama Serikali itatekeleza kero hizi ambazo ni kero kubwa katika Jimbo langu la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Spika, ahsante nawatakia kazi njema.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA**: Mheshimiwa Spika, maji yamekuwa ni kilio kikubwa kwa Watanzania lakini katika Bajeti ya mwaka huu sio kipaumbele kaika vipaumbele vitano vya Serikali. Hii ni hatari kwa taifa leo hii mkoa wa Kigoma maji ya yamepanda kutoka 5500 - 17500. Je, Serikali inaweza kutuambia ni vigezo gani vimetumika kupandisha bei hizi ilhali watu wa Kigoma ni masikini sana?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuijengea uwezo kamati ya Bunge ya sheria ndogo ili iweze kutembelea Halmashauri zote nchini na kushauri juu ya utungwaji wa sheria ndogo nyingi ambazo zipo hususan sheria ndogo za mapato?

Mheshimiwa Spika, maeneo na sababu ambazo inakosesha serikali mapato, 0.03 ya *turnover* ya migodi mingi ya madeni, *gas,* minara ya simu hivyo kukosesha mapato. Kama kodi ya Pombe imepanda mbona watu wa *TBL* Kigoma, Manispaa wameshtakiwa na Manispaa wanadaiwa takriban milioni 26 hawataki kulipa? Je, Serikali inachukua hatua gani? Kwa agent wa *TBL* Kigoma? Wenye hoteli nao hawataki kulipa kodi Serikali inachukua hatua gani. *Service levy* ya mabenki hususan Mikoa ya Lindi na Mtwara, wilaya zinatofautiana kupokea kodi hii wilaya moja inalipwa 400,000/= kwa mwaka huku nyinginezo zikipewa 250,000 kila mwezi hapo hakuna *uniformity* na Halmashauri zinakosa mapato yake kama inavyotakiwa. Kilio hiki pia kipo kwenye minara ya simu, kodi zinazolipwa kama kodi ya huduma hazifanani kabisa, minara ya simu inalipia kwenye Halmashauri vile inavyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa madini ya ujenzi hususani kokoto haulipwi kabisa katika Halmashauri nyingi, lakini mwisho kabisa hakuna *uniform bylaw.* Sheria ndogo za kukusanya ushuru (mapato) maeneo mengi ni chache sana, serikali iweke mkakati katika eneo hili hususani Mkoa wa Dar es Salaam, kuweka sheria ndogo za kulinda mazingira na kwa kuwa watu wengi ni wachaguzi wa kuwekewa ada Serikali itaingiza mapato mengi.

**MHE. PINDI H. CHAMA**: Mheslhimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwa niaba ya wananchi wameniomba niseme kwa nini bei ya vyakula (*consumables*) ni ghali. Mfano Sukari, Mchele, Mafuta ya kula na sabuni. Hivyo maisha kuwa gharama licha ya kilimo kwanza? Hata unga ilifika kilo 800; *why*? Nini mkakati wa Serikali. Mshahara kima cha chini 180,000/= hakitoshi kufika mwezi mzima wanafunzi wa *Loans Board* kwa siku wanapata 7500 x 30 = 225,000, ambao wanafunzi hawana hata familia. Mfanyakazi wa Serikali hasa wanawake kima cha chini 150,000/= kimeongezwa kwa 180,000/=. Je, ni sawa?

Mheshimiwa Spika, kwa siku atumie shilingi ngapi ana watoto, nauli, shule ada na kadhalika. kodi ya nyumba. Matokeo yake wakienda kazini inabidi wabebe biashara kama masecretary vitenge, maandazi na kadhalika. *As a result, productivity* kwenye kazi inapungua. Naomba majibu kwa niaba ya wafanyakazi hao wanawake kwa ujumla.

**MHE. MCH. DKT. GERTUDE P. RWAKATARE**: Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu na Watendaji wake wote kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya 2012/2013. Natoa pongezi kwa Serikali yetu kwa jitihada ya kufanikisha barabara, mashule, vituo vya afya na mipango mingi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kama ifuatavyo. Naomba umuhimu utolewe kwa barabara za vijijini za halmashauri,kwa mfano barabara ya Kidatu – Ifakara - Taveta Wilaya ya Kilombero. Ni barabara ya muhimu sana ila imetelekezwa, tangu miaka ya 1960. Mimi wakati ninasoma mpaka leo barabara hii ina madaraja na barabara ya muda *(temporary)* japo ni wilaya ambayo inaunganisha Ulanga na Kilosa. Kuna chakula, sukari, samaki na umeme. Waziri wafikirie kuzikumbuka kama zile za *Tanroad.*

Mheshimiwa Spika, naomba pembejeo iwafikie wakulima kwa wakati mwafaka. Naomba MBEGU ziwafikie wakulima kwa wakati muafaka tukizingatia tutapata matokeo bora.

Mheshimiwa Spika, mishahara kwa madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji ile kuwapa motisha kiutendaji tumeongea sana sasa tutekeleze. Serikali iliangalie suala la meli mbovu ambazo limesababisha vifo vingi vya Watanzania wenzetu.

**MHE. MARGARET S. SITTA**: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kwa nini serikali haisimamii matumizi ya *USD* katika matumizi ya kibiashara nchini ili fedha za Tanzania tu zitumike. Je, ni kitu gani Tanzania kinachokwamisha kupiga marufuku kutumia *USD* katika malipo ya biashara na ada za vyuo na shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya ndani kama chakula na nguo vilindwe ili kutunza na kulinda viwanda vyetu kwa kukuza ajira nchini.

**MHE. DEOGRATIAS ALOYCE NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza kwa kuandaa bajeti nzuri. Lengo kubwa la Bajeti ya Serikali ni kupuguza makali ya wale maadui watatu, Umasikini, Ujinga, Maradhi, lakini pia na kuweka, maandalizi kwa kuweka programu za kuiwezesha nchi kufika lengo letu kubwa (*Vision 2025)* la kuwa nchi ya uchumi wakati *(medium income economy)* ifikapo mwaka 2025. Pia Bajeti ya Serikali lazima izingatie Malengo ya *Millenium* na hasa lengo la kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Spika, je, Bajeti yako imezingatia malengo hayo, mimi nimekuelewa unaposema kwamba Bajeti ya Maendeleo ni asilimia 30 ya Bajeti nzima kwa sababu fedha za *Human Development* ambayo nayo ni *investment* lazima kwenye hiyo asilimia 30. Suala muhimu zaidi ni la kuongeza fedha za *Development* kwa *TRA* kukusanya zaidi mapato. *TRA* inaweza kukusanya bilioni 700 kwa mwezi lakini inakusanya bilioni 400+ chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu la kuzingatia ni kuhakikisha hiyo asilimia 30 kwa ajili ya maendeleo inapatikana na inawafikia walengwa wananchi wa kawaida *Disbursement* imekuwa tatizo kubwa. Kwa mfano mpaka sasa kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 *Council* ya Ngara imepokea asilimia 29 ya fedha za maendeleo. Kwa fedha zilizokuwa zimeidhinishwa. Siyo kwa Ngara tu ni kwa wilaya nyingi. Katika hali ya *councils* kukosa fedha za maendeleo tusitegemee kupunguza tatizo la umasikini.

Mheshimiwa Spika, wakati wastani wa *per capital income* kitaifa ni shilingi 800,000 + wastani wa kipato cha Mwana Ngara kwa mwaka ni shilingi 170,000 - 240,000. Watu hawa hawawezi kuondoka katika dimbwi la umaskini bila kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Fedha isimamie vizuri ukusanyaji wa mapato na *Disbursement* ya Fedha zilizoidhinishwa. *Paymaster General* awe mkali kwa *Accounting Officers.* Idara mbalimbali zisitumie zaidi ya fedha zilizoidhinishwa. Wizara yako iwe makini katika *negotiations* na *World Bank*, *IMF* na Wafadhili mbalimbali. Sera za *IMF* na *World Bank* za kuweka mashari magumu katika kukopa *we should be smart.*

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze kuwa *shareholder* katika madini na gesi. Botswana imefanikiwa sana kusimamia migodi yake ya Almasi na kufaidika nayo kupitia *shareholding*. Waziri wa fedha anatakiwa kuongoza katika mchakato wa kupunguza gharama za uendeshaji. Serikali Tanzania tuna tatizo la *consumerism before take off. Consumption* yetu ni

kama ya nchi zilizoendelea wakati sisi ni *least development country, very poor.*

Mheshimiwa Spika, mawaziri wa Fedha wa Kenya na Rwanda ndiyo waliosimamia zoezi la kuondoa mashangingi ambayo ni *big cost centre.*

Mheshimiwa Spika, nakutakia kila la kheri katika kazi hii yenye changamoto nyingi.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA**: Mheshimiwa Spika, nami napenda kutoa mchango wangu mdogo katika Bajeti hii iliyopo mbele yetu. Kwanza natoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri kwa Bajeti nzruri ambayo pamoja na ugeni wake amejitahidi sana kwani hii inaonyesha dhahiri ya kwamba yupo makini na kwamba anatuonyesha na kuwapa matumaini wananchi ya kuwa na imani kwake.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie machache juu ya jinsi wakulima wanavyoachwa nyuma kwa kuwainulia uchumi wao kupitia kilimo chao. Wakulima asilimia kubwa hali zao ni duni sana, kipato chao ni kidogo kulingana na uwezo, kilimo chao ni kile cha kizamani yaani cha mkono. Hawa ndiyo watoa mchango mkubwa katika kuleta maendeleo. Hutozwa kodi kupitia mazao yao ambayo Serikali haitaki kuwasaidia kwa kuwapa zana za kilimo pamoja na pembejeo ili kuweza kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, hawana masoko ya uhakika kwa mazao yao, hawapati mikopo hususani wale wa kiwango cha chini. Matokeo yake huzidi kuishi katika

maisha duni na kuwa maskini wa kutupwa. Napenda kuishauri Serikali iwaangalie wakulima hawa kwa manufaa ya uchumi wa taifa letu. Iwakopeshe matrekta na pembejeo kwa wakati muafaka. Pia kuwatafutia masoko bora kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, haki za watumishi, napenda kuzungumzia kwa masikitiko juu suala hili, hasa kwa upande wa Wabunge.Wabunge baadhi wanaishi katika maisha ya kubabaisha tu ukizingatia kwanza kwa kukosa nyumba za Serikali. Inafahamika kwamba baadhi yetu kama Mawaziri hupata huduma zote hususani nyumba za uhakika magari na hata mishahara na posho za uhakika. Je, isingekuwa vyema serikali ikatoa walau nyumba hata kama za hali ya chini ili kunusuru maisha yao. Maana wengi wetu huishi katika nyumba za kupanga ambazo bei ni za juu sana ukilinganisha na mishahara midogo Wabunge wapatayo na kwa kiasi kikubwa hakikidhi haja. Hivyo, walau kwa hilo serikali iliangalie ili iweze kupunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kutounga mkono Bajeti hii mpaka ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwanza kabisa, Waziri wa fedha achukue mapendekezo yote mazuri yaliyotolewa na wabunge wote ili kuboresha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa ni tatizo kwa kweli ukuaji wake ni wa hatari ni lazima serikali itafute mbinu mbadala ili kuweza kupata mkakati wa kupunguza deni hilo, tusisubiri kusamehe tu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wabunge wote waliochangia kuwa makampuni ya simu hayalipi kodi inavyotakiwa wanakwepa kodi hasa. Bajeti hii itakuwa haikuwatendea haki Watanzania kwa kuongeza kodi kwa mwananchi anayetumia simu. Napendekeza kodi hii isiongezwe badala yake ni lazima kutafuta mbinu mbadala za kuyabana haya makampuni ya simu ili yaweze kulipa zaidi.

Mheshimiwa Spika, makampuni haya ya simu ni wakwepaji wakubwa wa kodi na wanapata faida kubwa sana ni lazima tuwatumie *TCRA* ili kujua na kubaini ni kiasi gani cha kodi wanastahiki kulipa.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato bado ni kilio kwa Watanzania kwani kila mwaka vyanzo ni vile vile hakuna jipya. Mheshimiwa mimi napendekeza naomba Serikali kupitia *TRA* ione umuhimu wa kuweka mpango na viwango maalum vya kodi kwa kila *item* fulani. Kuwe na viwango vinavyofahamika kabisa na kuwa na vipeperushi vitangazwe. Kwa mfano wanao *import* kuwa na viwango vyao maalum kwa kila *product* na wanao *export* hali kadhalika. Badala ya kuwaacha maafisa wa *TRA* kufaidi sana kodi ya Watanzania kwa kuhongwa sana kwani wafanyabiashara hawazifahamu kodi halali wanazotakiwa kulipa. Lazima serikali ipanue wigo wa kukusanya kodi ili iongeze mapato kupitia sekta isiyo

rasmi badala ya kuwaaachia mgambo wakineemeka na serikali haipati chochote.

Mheeshimiwa Spika, mwisho, uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida ambayo ni asilimia 70 wakati Bajeti ya Maendeleo ni asilimia 30 haiwezeshi nchi kupiga hatua ya haraka ya maendeleo. Napendekeza Bajeti ya maendeleo iongezwe angalau asilimia 35 ili kuzingatia masharti yaliyowekwa na mpango wa maendeleo uliopitishwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu ibara ya 63(3)(c).

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa muda mfupi alioteuliwa kuwa Waziri wa Fedha ameweza kujitahidi kukabiliana na changamoto za uandaaji wa hotuba ya mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze mchango wangu kwenye viwanda. Nchi hii ilikuwa na viwanda vingi visivyopungua ishirini na kama leo vingekuwa vinafanya kazi, basi vijana wetu wengi wangekuwa na ajira. Serikali haioni kuwa hivi viwanda vya nguo kwa kuwa wanatumia malighafi inayozalishwa ndani ya nchi yetu kama vile pamba, hebu sasa tuondoe *VAT* kwenye ununuzi wa pamba, nguo kwenye viwanda vyetu vya ndani na kwa mahitaji ya ndani tu kwa uuzaji wa bidhaa hizi nje ya nchi, *VAT* iendelee. Hii tutaweza kuwapunguzia huu ukali wa maisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi viwanda vinne vya nguo vilivyobaki, vina suasua na kupunguza uzalishaji. Je, Serikali imefanya uchunguzi sababu ni nini? Kama sababu ni *VAT* basi punguzeni ili viwanda hivi viweze kuendelea na kulinda ajira ya hawa vijana wetu wanaofanya kazi kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SULEMANI NKAMIA**: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Bajeti ya serikali ya mwaka na fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la mafuta ya kula, Serikali imeondoa asilimia 10 ya *crude oil* kutoka nje, kitu ambacho kinafanyika kwa sasa makampuni mawili makubwa ya *MURZA OIL MILLS* na *MOUNL MERU* ndiyo yanaagiza mafuta hayo. Hata hivyo, hawaleti *crude oil,* matokeo yake wanaagiza *refined oil* na hivyo kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo kumekuwa na athari kubwa sana kwa wakulima wa alizeti wa mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara, Tabora na Morogoro na hata Iringa ambao ni wazalishaji wakubwa na ALIZETI. Ninaiomba Serikali irudishe asilimia kumi ya uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ambayo iliondolewa katika mazingira ya kutatanisha na aliyekuwa Waziri wa Fedha. Hatukubali kuona wananchi wa mikoa hii wanatumika kupiga kura tu na Serikali ikishaingia madarakani inawasahau, *this is not fair*.

Mheshimiwa Spika, pili, katika nchi zilizoendelea na hata nchi changa tu kama Ghana, zimeendesha mashirika ya utangazaji ya nchi zao kwa *Television Licence.* Naiomba Serikali ianzishe *TV LICENCE*, tuna TV zaidi ya milioni 16 hapa nchini ukianzisha *TV Licence* unaweza kukusanya *almost* 3.2 bilioni kila mwaka na nusu ukaipeleka kuendesha TV, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC)* na nusu ukaingiza kwenye *basket fund* tufanye hivyo jifunzeni, Ghana, Uingereza, *South Africa,* Marekani na Japan,

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali iachane na mpango wa kufanya 31 Desemba 2012, kuwa siku ya mwisho ya kuzima mitambo ya analojia. Tuna haraka ya nini? Mbona haya mataifa makubwa yameweka 2015 ndiyo *deadline* tuna harakisha nini? Leo kuna idadi kubwa ya *TV* zinazoingia ambazo Desemba 31 nyingi hazitafanya kazi. Tumekaa kimya; *why*?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR**: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuunga mkono Bajeti hii mia kwa mia. Serikali lazima ipunguze gharama zisizokuwa za lazima katika matumizi ya serikali. Kwa mfano, safari za ndani na za nje ya nchi zimekuwa nyingi mno. Pia misafara imekuwa mikubwa hii imesababisha pesa nyingi zitumike katika safari na misafara hii.

Mheshimiwa Spika, kuna ulazima wa kuhakikisha kuwa safari zinapunguzwa pamoja na ukubwa wa misafara. Jambo lingine linaloongeza matumizi ya Serikali ni magari ya kifahari wanayotumia Viongozi na

Maofisa wa Serikali. Magari haya ni ghali na yanatumia mafuta mengi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Serikali ikabadilisha sera na kuanza kuwakopesha fedha Maafisa wa Serikali ili waanze kujinunulia magari yao wenyewe. Hii itapunguza pia gharama za mafuta matengenezo na vipuri. Viongozi Wakuu wa Serikali pekee ndiyo waruhusiwe kupewa magari ya kifahari.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi bado haijafikiwa asilimia moja kama Serikali ilivyoahidi. Misamaha hii inaikosesha serikali fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi na Mashirika yanayopata misamaha hii hawaitumii kwa manufaa ya wananchi wenye kipato cha chini. Pia bidhaa au huduma zinazotolewa na taasisi hizi zina bei kubwa hivyo kunufaisha zaidi matajiri kuliko maskini.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa taasisi zote za aina hii hazipati misamaha ya kodi.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, Bajeti hii haijamsaidia mwananchi wa kawaida, kwanza, kwa kuwa hata zile gharama za mawasiliano ambazo zimeongezwa basi faida kubwa itakuwa kwa makampuni kwani mfanyabiashara hakubali kukosa faida hata siku moja lakini si hilo tu bali hata matumizi ya simu wananchi yatawashinda na hivyo kumzidishia umaskini kwani mawasiliano ni ajira, ni

biashara, ni elimu na ndiyo maisha kwa ulimwengu huu wa Sayansi na Teknologia.

Mheshimiwa Spika, kilimo kwanza, kauli mbiu hii haikutafsiriwa ipasavyo katika Bajeti kwani fungu lililotengwa halikidhi haja ya kutimiza kauli mbiu hiyo, kwa vile tutaendelea kuwa na ukosefu wa ajira kupitia kilimo na kusababisha ukosefu wa chakula na hivyo kuendelea kutawaliwa na umaskini uliokithiri. Kutokana na Bajeti hii hatujaweza kutatua tatizo la matibabu. Mwananchi anahitaji lishe bora na matibabu bora, leo hii wananchi bado wanahangaika na matibabu yasiyo na uhakika na kupelekea vifo vya mara kwa mara vinavyotokana na ukosefu wa huduma bora hospitalini, madawa sahihi na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu tunahitaji tuiangalie kwa umakini mkubwa kwani bila elimu tutazalisha Taifa duni. Vijana wetu wanakosa mikopo ya kujisomea, maabara zilizokamilika katika shule za sekondari hamna. Je, Bajeti hii au fedha ziizotengwa kwa Wizara ya Elimu zinaweza kutufikisha kwenye lengo.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya uchimbaji wa madini yanayotunyonya sana. Je, kwa nini Mikataba isifanyiwe rejea, badala ya asilimia tatu ikawa angalau Tanzania inapata asilimia 50. Inakuwaje hili haliwezekani?

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti, huu ni mwanzo

mzuri na hasa tukizingatia ugeni wao katika Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nilete mchango wangu wa maandishi katika maeneo mawili muhimu ambayo binafsi nimeona nitumie muda huu kuishauri Serikali na hususani Wizara hii muhimu ya fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kuhusiasna na mpango mzima wa kubadilisha sera za mapato ili kuiongezea serikali yetu mapato yale ya kodi na hata yale yasiyo ya kodi katika eneo hili. Naomba kuishauri serikali na hasa wizara irejee sheria ya uundwaji wa Mawakala mbalimbali wa Serikali *(Government Agencies Law).*

Mheshimiwa Spika, Wakala (*Agencies)* wa Serikali mfano, *TPA, TCRA, TICRA, EWURA, SUMATRA, TANAPA, Ngorongoro Conservation* na kadhalika*.* Hutakiwa kuchangia kiasi cha asilimia kumi cha mapato yao kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina lakini cha kusikitisha. *Government Agencies* hazichangii kiasi hicho kwenye Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita wa fedha 2011/2012 Agencies hizi hazikuchangia kwenye Mfuko Mkuu (Hazina), jambo ambalo limesababisha ku-*drop* kwa *performance* ya *budget* ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni sababu zipi zilisababisha *Agencies* hizi zisichangie kwenye Mfuko

Mkuu? Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa *Agencies* hizo?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na zao la pamba na bidhaa zake. Zao la pamba ni muhimu sana ka wananchi wa *Lake Zone.* Zao hili hutoa ajira kwa wakulima wadogo wadogo wapatao 500,0000 na kuwezesha maisha ya takriban ya asilimia 40 ya Watanzania wanaofikia milioni 16, kwa bahati mbaya sana zaidi ya asilimia 70 ya pamba huuzwa nje ikiwa ghafi jambo ambalo ni changamoto kubwa si tu kwa serikali bali pia hii asilimia 40 ya Watanzania ambao maisha yao hutegemea zao hili la pamba.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikalli ifikirie sasa kuongeza thamani kwenye zao hili *(value added product)* kwa kufikiria kuwekeza kwenye viwanda vya nyuzi majora ya nguo na mavazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzisha viwanda hivi si tu tutakuza ajira nchini bali pia tutaongeza kipato cha wananchi na kuendeleza kwa kiwango kikubwa ulimaji wa zao hili la Pamba ambalo kwa mtazamo wangu, endapo hatua nilizozitaja hapo juu hazitachukuliwa, basi zao hili laweza kutoweka, jambo ambalo litasababisha wananchi hawa wawe na maisha magumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda kutotoweka kwa zao hili napendekeza pia viwanda vyote vya nguo (*textiles)* nchini vibinafsishwe kwa wananchi wenye uwezo ili viweze kufanya kazi jambo ambalo litapunguza bidhaa za nguo zinazoingizwa toka nje.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia viwanda hivi vya nguo vyuzi na mavazi vipewe misamaha ya kodi la ongezeko la thamani *(VAT)* yaani *zero rated*.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itaongeza uzalishaji na ajira jambo ambalo pia litaongeza kodi ya *PAYE* ambayo ukusanyaji wake kwa sasa kutoka sekta hii ni shilingi bilioni 0.528 tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO**: Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bajeti ya mwaka 2011/2012. Serikali ilitenga tirioni 4.9 kwa ajili ya maendeleo sawa na asilimia 36 ya Bajeti yote. Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 imetenga trioni 4.5 sawa na asilimia 30. Mwaka 2011/2012 mapato yalikuwa madogo lakini matumizi yalikuwa makubwa. Mwaka wa fedha 2012/2013 mapato ni makubwa trioni 15 lakini matumizi ni madogo misingi yake ni ipi kama nilivyosema awali kwamba matumizi yalikuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, uongezaji wa mikoa mipya na wilaya mpya ni moja kati ya mambo ambayo yanaonesha kwamba fedha nyingi zinatumika katika matumizi ya kisiasa zaidi kuliko maendeleo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya milenia, vifo vya watoto wachanga na mama wajawazito vinaongezeka kwa kiasi kikubwa. Ugonjwa wa maradhi ya matumbo yamezidi. Hakuna vyandarua, hakuna madawa, laiti serikali ingalitilia maanani janga

hili kwa kipindi cha miaka mitano ikasambaza vyandarua na madawa lingalitoweka kabisa. Hata hivyo kwa upande wa serikali limebakia kuwa nyimbo hakuna ufanisi wowote.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa, wakati wa Rais Mkapa alijitahidi sana kupunguza Deni la Taifa, wakati tukiambiwa Deni la Taifa lina himilika mwaka 2011/2012 lilikuwa trioni 15. Mwaka 20102/2013 limefikia trioni 22, visingizio vikubwa vinavyotolewa ni nchi kukabiliwa na ukame wakati Taifa hili limebarikiwa madini ya kila aina ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba madini yanawanufaisha kwanza Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tuna dhahabu, *Ureniam,* Almasi, *Tanzanite,* madini ambayo hayapo popote duniani, tuna gesi, bandari, mito na maziwa. Tanzania imezungukwa na bandari karibu nchi sita zikiwemo wanachama wa Afrika Mashariki. Kwa nini nchi haina mapato leo tunalimbikiza madeni ya ndani tukidai kwamba yanahimilika hivyo serikali hii kama itaondoka madarakani itawarithisha nini Watanzania?

Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti uliofanyika ni kwamba safari nyingi za Rais Kikwete na viongozi wengine zinafanyika kwa visingizio vya dharura vinaathiri mwenendo mzima wa Bajeti ya nchi. Rais ana wajibu wa kukaa nchini kuwatumikia wananchi yeye sio waziri wa Mambo ya Nje au kama kazi za wizara hiyo alitaka kuifanya mwenyewe asingemteua waziri kutuongezea gharama za bure.

Mheshimiwa Spika, namwomba mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati atakapotoa majumuisho awaeleze Watanzania ni kiasi gani cha fedha atakachokitumia kwa ajili ya mkopo huu ambao katika kitabu cha *Budget* hakuainisha juu ya namna atakavyotumia.

Mheshimiwa Spika, kuna mfano hai, kwa kipindi fulani serikali ilikopa dollar milioni 400 lakini serikali ilitumia dollar milioni 40 kwa ajili ya kupata mkopo huo. Sasa ni wakati wa kuelezwa Watanzania kupitia Bunge hili fedha hizi zilitoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa ufahamu wangu ni kwamba karibu bilioni 79 zililipwa kutoka Uingereza fedha ambazo zilihusiana na Rada. Fedha hizi ni za Muungano katika kamati ya Fedha na Uchumi tulipata taarifa kwamba zimeshagawiwa katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara bila kuihusisha mikoa ya Zanzibar wasipate fungu lao. Ni wajibu wa serikali kuliangalia hili kwa kina kwani ni miongoni mwa mambo yanayoudhi katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, Bajeti haijatoa nafuu kwa mwananchi wa kawaida na kupunguza makali ya maisha, hivyo wananchi watakuwa katika hali mbaya ikiwa hawajatimiziwa yale wanayoyahitaji kwa kila siku.

Mheshimiwa Spika, Serikali isipendelee kuwa na vyanzo vile vile vya mapato hasa ukiangalia asilimia kubwa ya watu wa nchini ndiyo wanaoonewa, kuvuta

sigara na kunywa soda. Serikali ikiwabana sana wengi wao wataacha kulewa na kuvuta sigara mwishowe kupelekea Serikali kukosa mapato, hasa ukiangalia kuna matangazo mengi ya upigwaji vita wa sigara.

Mheshimiwa Spika, ili Bajeti ilete maana kwa wananchi wigo wa kodi na vyanzo vya mapato vinapaswa kubadilika na kuongezeka, kwani nchi zilizoendelea Bajeti zao zinaendana na uwiano wa matumizi ya kawaida na maendeleo. Serikali inapaswa kuweka fedha nyingi katika maendeleo pamoja na kupata vyanzo mbadala kama madini na rasilimali mbalimbali zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya fedha ya maendeleo inatarajia kukopa trilioni 4,527,839 kwa wahisani mbalimbali wa nje na ndani, ambayo fedha hii itumike kwa matumizi ya maendeleo. Je, tuna uhakika gani wa kupata fedha hii ya kupeleka maendeleo mbele ikiwa fedha zote ni za mikopo? Ikiwa wafadhili hawa wamekawia au hawakutoa kabisa. Je, Serikali itaendesha vipi miradi yake ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; ni vyema Serikali ikawa na *Plan B* ambayo itaweza kufidia hali hiyo, kupunguza fedha za matumizi na kuziweka kwenye maendeleo, asilimia 40 - asilimia 35 iwe ni Bajeti ya maendeleo na Waziri atakapofanya majumuisho ni vyema akaeleza *Plan*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo Kwanza, Bajeti haikueleza mkakati mzima wa kilimo cha umwagiliaji ambacho kingeweza kufanya Taifa kujihakikishia

uhakika wa chakula na pia kuwapa ajira vijana. Ingawa imeweza kuonesha itasaidia wananchi pembejeo. Bajeti ndogo iliyowekwa katika Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ambayo asilimia 90 ya Watanzania inategemea katika kuliingizia pato sekta hizo. Serikali ingeliongeza Bajeti katika sekta hizi ili kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Bajeti imetenga fedha ndogo ambayo haikidhi mahitaji ya walimu. Mfano, shule hazina vitabu, vikalio, vifaa vya maabara na kadhalika. Kama inavyoeleweka elimu ni uti wa mgongo wa nchi na wanadamu. Watu wanaweza kujiendeleza mara wapatapo elimu na pia itawapunguzia adha ya kutopata ajira, pamoja na Serikali kujikuta imejipunguzia mzigo mzito wa kutafuta kazi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tozo, suala la Serikali kuongeza kodi katika mishahara ya wafanyakazi ni kuwaongezea ugumu wa maisha na hapa haioneshi kwamba umewaongezea mshahara kwani kiwango cha *VAT* kitakuwa ni kikubwa kulingana na pato lao. Kwani umewapa kwa mkono wa kulia na kuchukua kwa mkono wa kushoto (yaani + - = -) .

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wakiwa wanawake na vijana ambao wamejiajiri wenyewe, hawa ni watu wa kupewa motisha na kujiingizia kipato na kujiondolea umaskini. Si vyema watu hawa kutozwa kodi, kwani wengi wao ni wale waliokopa benki na kwenye *saccos* na huko nako wanakatwa kodi ni

vyema mkawaacha kumoja ili waweze kuishi na kusomesha watoto wao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ni sekta ambayo itasaidia sana mapato ya nchi, lakini haitii tija kwa kuwasamehe kodi wawekezaji. Serikali iweze kufunga mianya yote inayojitokeza katika sekta hii hasa kwa kuwatoza kodi kubwa. Pia wawe macho kuangalia makontena ya mchanga wa dhahabu yasisafirishwe bila kutolewa ushuru.

Mheshimiwa Spika, tathmini juu ya uwezo wa kukopa: Kutokana na mikopo ya nchi yenye masharti ya kibiashara Serikali inatakiwa kufanya tathmini juu ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni, ili wakopeshaji wawe na imani ya kuwezesha Serikali kupata mikopo yenye masharti nafuu ya kibiashara kwa wakati. Ni vizuri lakini ikiwa tathmini imeonesha kwamba Serikali haikopesheki. Je, kuna mkakati gani wa Serikali juu ya hili? Naomba Waziri atakapokuwa kufanya majumuisho atueleze mikakati iliyowekwa au *Plan B.*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupeleka fedha kwenye Halmashauri: Kuhusu matumizi ya fedha za Halmashauri na marejesho yake kwa wakati ni jambo jema. Halmashauri hupanga Bajeti yake, Wizara hupanga Bajeti yake lakini Hazina huchelewa kupeleka fedha na kuzifanya Halmashauri na Wizara kutotekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wizara ya Fedha ni vyema kuwasilisha fedha hizi za miradi kwa wakati. Suala la kupeleka rundo la fedha kwa kota ya mwisho na kuwataka wairejeshe fedha hiyo kwa

wakati ni kutokuwatendea haki na hili limejionesha katika Wizara na Halmashauri nyingi.

Mheshimiwa Spika, Utalii ni moja ya vivutio vizuri katika nchi. Tanzania ina vivutio vingi ambavyo vinaweza kuingiza fedha nyingi na kusaidia kuendesha nchi, lakini utalii wa Tanzania unakosa mapato mengi ambayo wawekezaji wanaojishirikisha hutoza watalii fedha huko huko kwao na kuja Tanzania kwa kuangalia tu bila ya fedha halisi. Hii haitoshi ni vyema Serikali kuwa na sera nzuri ya kuwabana wawekezaji hawa ili fedha isiachwe nje.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa ni kubwa na bado Bajeti inategemea kupata mikopo kutoka nje, ijapokuwa deni hilo linahimilika lakini kwanini Serikali inapenda kujizidishia matatizo ya kubeba dhamana au kuwadhamini Mashirika na Taasisi za Umma ambazo zinakufa na kuiachia Serikali tabu. Naomba Waziri atoe tamko na kuliambia Bunge kwamba hivi sasa mashirika yote pamoja na taasisi watalipa wenyewe madeni yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013, katika mambo kadhaa yakiwemo, misamaha ya kodi, ongezeko la kodi katika vinywaji baridi na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, tunaendelea na kuona ni jinsi gani misamaha

ya kodi kwa Makampuni makubwa ikiendelea kuwa gumzo. Hivi Serikali hii haioni kuwa misamaha hii ambayo sasa inafikia asilimia 5 mpaka 6 ni hatari kwa uchumi wa nchi yetu? Kuelekeza kodi kwa wananchi walio na maisha duni ni kuwaonea na kuyaacha makapuni ambayo mengi yanachukua rasilimali zetu bila ya kuacha chochote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukusanya kodi kwa kutegemea wananchi ni kuwaonea Watanzania. Makapuni ya Madini yamekuwa yakipewa muda mrefu sana ambapo yanasema bado yanatafuta madini wakati huo huo ndege zikiruka na kutua bila kujua ni madini kiasi gani yanaondoka nayo hapa nchini. Mbaya zaidi kuna maafisa wa kodi ambao wapo katika migodi hiyo. Sasa hawa wanafanya kazi gani.

Mheshimiwa Spika, ni pesa nyingi sana ambazo zinapotea kutokana na uwekezaji wa madini huku makampuni hayo yakiwaacha wananchi wanaoyazunguka maeneo hayo katika umaskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, hili ongezeko la kodi katika vinywaji na sigara kila mwaka ndiyo imekuwa mtindo wa Serikali kila mwaka kwa nini? Ni kwa sababu kuna wateja wengi au ni kuwakomoa wananchi? Mie naona umefika wakati sasa Serikali ibuni njia nyingine ya kukusanya kodi mbali na kuongeza kodi kwenye vinywaji na sigara, kwa sababu moja wananchi watashindwa kununua pombe na soda na biashara ya gongo na juice isiyo na viwango vya *TBS* kushamiri hivyo kuhatarisha afya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kupunguza kodi kwenye mvinyo unaotengenezwa ndani ya nchi ni hatua nzuri sana na ninaipongeza Serikali kwa dhati kabisa. Hili litaongeza uzalishaji wa zao la zabibu na kuongeza ajira kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei umekuwa tishio katika nchi yetu. Kila kukisha hadithi ni mfumko wa bei tu hii hadithi itateguliwa lini? Wananchi wamekuwa wakilia maisha yamekuwa magumu lakini Serikali imekaa kimya kana kwamba haipo. Tumeona mfano kwenye sukari, Serikali imetoa vibali vingi sana lakini sukari hiyo bado inazidi kupanda bei siku hadi siku. Ninaomba sasa Serikali itafute ufumbuzi wa kudumu ili hili neno mfumko wa bei lipotee katika vinywa vya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana Serikali inategemea fedha za nje kwa matumizi ya maendeleo kuliko fedha za ndani. Hii ni hatari sana kwani kutegemea misaada kutoka nje ni hatari tuna rasilimali za kutosha kila kona ni kukosa udhubutu wa kusimamia rasilimali zetu. Serikali ikisimamia rasilimali zote zilizoko ndani ya nchi yetu, tusingetembeza bakuli la kuomba nje ya nchi. Tatizo tulishazoea kuomba nje hivyo hata hatufikirii ku-*utilize resources* tulizonazo na kuwaacha wageni wakiondoka nazo na kusubiri zirudi kama msaada tena.

Mheshimiwa Spika, swala la kilimo, napenda kuzungumzia zao la Pamba. Pamoja na Serikali kuimarisha masoko ya mazao kupitia Bodi ya Mazao

ambayo imeshaanza shughuli zake na Shilingi bilioni 192.2 zimetengwa katika eneo hili. Wakulima wa pamba bado hawatendewi haki kabisa mpaka sasa. Shilingi 450 kwa kilo kitu gani jamani? Au ni kuwakatisha tamaa wakulima hawa?

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala hili la bei ya pamba lishughulikiwe haraka kwani wananchi wameshaanza kukosa imani na Serikali. Pamba nyingi imepatikana msimu huu na hivyo bodi kuwapangia bei Sh. 450 ni kuwaonea. Ninaomba sana Serikali isimamie bei ya pamba ili mkulima anayetegemea zao hili aweze kupata faida. Shilingi 450 kwa kilo ni kumnyonya mkulima huyu. Kama wachangiaji waliochangia kuwa bila Shilingi 1000 hakuna kuuza pamba.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii mpaka hapo Waziri atakapokuja na majibu ya mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALIKO NIKUSUMA KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote walioshiriki kuiandaa hadi ikaletwa hapa Bungeni. Bajeti ni nzuri ila inahitaji marekebisho kadhaa kwa ajili ya kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, Waziri aseme Bajeti itafanya nini kwa ajili ya wakulima hasa kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu (mawasiliano) kazi ya kuifufua reli ya kati ni muhimu lakini baadhi ya watu wanasema hata reli kikarabatiwa, kama magari makubwa ambayo yanaharibu barabara zetu kwa kazi kubwa kila kukicha hatasitisha shughuli za kubeba mizigo mikubwa, na badala yake kuacha mizigo mizito kama bati, saruji, nondo, vyombo na vifaa vya ujenzi vibebwe au kusafirishwe kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wachangiaji wenzangu waliochangia kwamba kodi ya waendesha pikipiki (bodaboda) ifutwe.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali zikiwemo ya Mpemba – Isongole km 51.7 katika Wilaya ya Ileje/Mbozi uonyeshe dalili za kujengwa vinginevyo wananchi watakata tamaa na kutokuwa na imani na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maandalizi ya Bajeti kuna haja ya kubadilisha mfumo wa mchakato wa kuiandaa ili uwashirikishe wadau mbalimbali, kwa kuwa na mawazo na vyanzo vingine vya kodi vinaweza kuibuliwa na wadau wengine nje ya ofisi za Serikali na taasisi zake. Jambo hili pia litapunguza malumbano ndani na nje ya Bunge pindi kipindi cha kusomwa kwa bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la maji, mtu makini hutengeneza sebule ya nyumba yake kuwa nzuri kuliko vyumba vingine vya ndani. Mipaka yetu ni taswira ya usafi, ustarabu na ukarimu wa Taifa. Pendekezo miji ya

mipakani kama Tunduma, Isongole na Kasumlo Mbeya, Namanga na maeneo mengine yapatiwe kipaumbele cha kupatiwa maji ili kuleta taswira nzuri kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme nashukuru fedha imetengwa kwa ajili ya mgodi wa Kiwira ambao utaanza rasmi. Nashauri jambo hili lisije likaishia katika karatasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER MHOJA KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuipata fursa hii ya kuchangia hoja iliyoletwa na Serikali yetu ya kulitaka Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio hayo ya Mapato na matumizi ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Maswa Wilaya iliyoanzishwa na wakoloni hapo mwaka 1927, wamenizuia kuiunga mkono hoja hiyo kutokana na Serikali kutokuzingatia kilio cha wananchi wa wilaya hiyo kuhusu ombi lao maalumu la kujengewa kituo cha kisasa cha polisi wilaya kutokana na wilaya hii kutokuwa na nyumba bora za polisi tatu 1927 – 2012.

Mheshimiwa Spika, aidha kutokana na Serikali kuweka Bajeti ndogo kwenye Wizara ya Maji kuliko hata kiasi kilichokuwa mwaka 2011/2012. Hivyo hali hiyo wanaiona itaendelea kuwatesa kupitia uzoefu wa miaka miwili mfululizo walivyoteseka kutokana na Mamlaka ya Maji Wilaya na Wizara ya Maji kutokuleta umeme *TANESCO.* Kutokana na Serikali kuweka Bajeti ndogo kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi

badala ya Serikali kujirundikia Bajeti kubwa kwenye matumizi yake kitendo hiki nikikibariki cha kupitisha Bajeti ya aina hii nitakuwa nimewasaliti wananchi wa Jimbo langu la Wilaya ya Maswa Mashariki.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali ikiongeza Bajeti katika miradi ya maendeleo kufikia angalau asilimia 45, mimi nitakuwa tayari kuiunga mkono hoja ya kuipitisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ASHA MUHAMED OMAR:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Kilimo, kabla ya kuunga mkono hoja naomba ufafanuzi katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Bajeti kinaonyesha wazi kuwa fungu la kilimo limeshuka kutoka Shilingi 258.4 bilioni (2011/2012) hadi Sh. 192 kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Bajeti kimeeleza wazi kuwa ukuaji wa kilimo umepungua kutoka asilimia 4.2 ya mwaka 2010/2011 hadi asilimia 3.6 2011/2012. Kutokana na ukweli huo ipo haja ya Serikali kutenga fungu kubwa katika suala la kilimo na hasa katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania ni ukweli usiofichika. Ajira kwa vijana ni tatizo sugu hivyo basi naiomba Serikali katika nafasi za ajira zilizotengwa katika Bajeti hii ya Wizara ya Fedha katika nyanja za kilimo, elimu na afya. Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya

Muungano, basi vijana wa Zanzibar na wao wapatiwe nafasi hizi ili tuweze kupunguza mlundikano wa vijana wasio na ajira, ili tuepushe vijana wetu kukaa vijiweni na kula unga ili taifa liwe na vijana wazuri wapenda maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kueleza kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kupanua wigo wa mapato, kati ya jumla ya Bajeti ya Trilioni 15.1, fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani ni Trilioni 8 tu. Ukweli ni kwamba Serikali inaweza kukusanya mapato makubwa kuliko hayo. Baadhi ya maeneo ambayo yanayoweza kutoa mapato zaidi ni:-

(i) Nyumba zinazopangishwa wenye nyumba hizo hawatoi kodi japo wao wanakusanya kodi ya kupangisha *(house rent)* mamilioni ya fedha kwa mwaka. Serikali ifanye sensa kumtambua mwenye nyumba za kupangisha ili waingizwe katika wigo wa kulipa kodi.

(ii) Shughuli nyingi katika serikali isiyo rasmi zinaingiza mapato makubwa lakini hayatozwi kodi yoyote, shughuli hizo ni kama: ufugaji wa

kuku, ufugaji wa ng'ombe wa kisasa, ufugaji wa nguruwe, bustani na kadhalika.

(iii) Sekta ndogo ya uuzaji mafuta; petroli, dizeli, mafuta ya taa na kadhalika, ina ukwepaji mkubwa wa kodi, kwa hiyo, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya kodi katika sekta hii.

(iv) Suala la misamaha ya kodi nalo lifanyiwe uchunguzi wa haraka ili Serikali ifute misamaha isiyoleta tija katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulinda viwanda vya ndani. Moja ya changamoto katika uchumi wetu ni kuanzisha viwanda vipya na kuviwezesha vilivyopo vizalishe kwa tija ili kutoa bidhaa na pia kuongeza ajira. Namna moja ya kuwezesha viwanda vya ndani kushamiri na kupambana na ushindani wa bidhaa toka nje ni kuvipunguzia kodi na ushuru mbalimbali, hasa viwanda vinavyosindika mazao kama viwanda vya korosho, viwanda vya nguo, viwanda vya mafuta ya kula, viwanda vya nyama, ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira ya kuwezesha sera ya *PPP,* Serikali iendelee kuondoa vikwazo vinavyozuia kukua kwa sekta binafsi, hasa kupunguza gharama na bugudha ya kuwekeza na kufunga biashara *(cost of doing business).*

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya Serikali haijampa unafuu wowote mwananchi wa kawada na yule maskini kabisa pia hata mkulima haijamsaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania ina rasilimali nyingi. Lakini watu wake ni maskini pia lakini kuna nchi hazina uwezo kuliko Tanzania. Tanzania nchi tajiri lazima tutumie utajiri wetu tusijidhalilishe kama hatuna kitu tuna bandari, tuna misitu, mbuga kuu za hifadhi, maziwa, tuna madini, tuna vivutio hata nchi za ulaya zinaitamani Tanzania. Ni kwa nini Serikali inakusanya mapato kila siku na maeneo yote yenye ukusanyaji na hata kodi kwa wananchi bado Serikali haimjali mwananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kuwa kuwa nchi yetu ina wakulina na wafanyakazi, hivyo Serikali haimjali mkulima anayelima bila msaada wowote, mfano mbegu zinasemwa tu wengi hawazipati zinaenda kwa wachache tu. Hata pembejeo mpaka leo wananchi wengi wanalalamika hawazipati na wakizipata kwa uhafifu zaidi mkulima hana msaada na Serikali, bali Serikali ndiyo inanufaika na mkulima inamnyonya.

Mheshimiwa Spika, mkulima analima mwenyewe hajui bei ya mazao yake na Serikali nashindwa kumsaidia atayauza wapi akiyatoa shambani akiyapeleka mjini anakutana na geti anatozwa ushuru, akipeleka sokoni anatozwa ushuru bado analipa kodi. Je, ni lini Serikali itaona mkulima anastahili kutendewa haki?

Mheshimiwa Spika, utakuta maeneo ni migogoro ya ardhi, ukusanyaji mapato ni hafifu; je, ni kwa nini Serikali inaididimiza nchi yetu wakati wakiona?

Mheshimiwa Spika, siungi mkono Bajeti hii haikuzingatia maskini, mtu wa kawaida hata mfanyakazi, mkulima, kumpandisha mshahara si unafuu wa maisha. Kupandisha bei vitu au kupunguza na unaongeza mshahara bado tatizo lipo pale pale.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mgimwa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kushika hii Wizara nyeti ambayo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha Bajeti nzuri hii inayojilekeza kwenye kutatua matatizo ya wananchi kama yalivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita katika kuinua uzalishaji wa zao la pamba. Jimbo langu tunalima sana tumbaku, zao ambalo linapigwa vita sana na Shirika la Afya Duniani *(WHO).* Kutokana na hali hii tumelazimika kupitia Halmashauri yetu ya Urambo kuteua zao mbadala la biashara. Tumechagua pamba. Kwa muda mrefu sasa soko la pamba limekuwa na matatizo kutokana na kuyumba kwa soko la dunia. Kwa hiyo basi ni muhimu kabisa kujenga na kupanua soko la ndani kwa maana ya kuweka mazingira endelevu kwa viwanda vyetu vya nguo ambavyo ndiyo mtumiaji mkubwa wa pamba hii.

Tatizo linalokabili viwanda hivi ni ushindani wa soko usiokuwa sawa na bidhaa za nguo toka nje. Ili kuvisaidia viwanda hivi tuvipunguzie mzigo wa kodi ya *VAT.* Viwanda hivi vikistawi nina hakika vitaleta ushindani chanya wa bei ya pamba. Hii itakuwa ni faida kwa mkulina wa pamba akiwemo na mkulima wa Urambo. Matokeo chanya yatakuwa ni haya yafuatayo:-

(i) Wakulima wa pamba wataingia katika maisha bora.

(ii) Ajira kwa vijana wanaoingia katika kilimo chenye tija itaongezeka.

(iii) Ajira hii itapunguza msururu wa vijana toka vijijini kuhamia mijini.

(iv) Kilimo cha pamba kikishamiri katika eneo letu kitapunguza kiasi kikubwa cha ukataji miti unaoharibu mazingira kwa kutengeneza jangwa na kuleta ukame.

(v) Kuacha kulima tumbaku kutaimarisha afya zetu na pia itaondoa mgogoro kati ya Tanzania na Shirika la Afya Duniani *(WHO)*.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FELISTER ALOYCE BURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Naibu Mawaziri,

Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukabiliana na mfumko wa bei, naishauri Serikali kupunguza urasimu kwa kuwaruhusu wananchi wenye uwezo kuagiza vyakula pale upungufu unapoikabili Taifa bila kutumia vibali. Kipindi kilichopita tulishuhudia vibali vya uagizaji sukari vikiuzwa kama pipi mitaani. Utoaji vibali pia haikushusha bei ya sukari sokoni bali bei ilipanda maradufu. Nashauri Serikali kutumia vyombo vyake kama vile bodi ya mazao mchanganyiko, hifadhi ya chakula ya Taifa katika uagizaji wa chakula kukabiliana na upungufu unapotokea.

Mheshimiwa Spika, azma ya KILIMO KWANZA haijafanikiwa, Watanzania walio wengi bado wanalima kilimo cha mazoea kwa kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, wakulima asilimia kubwa hawatumii mbegu bora na kilimo cha kisasa haitambuliki wala kutumika. Msisitizo uwekwe kwa maafisa ugani kufuatilia kwa karibu kwa wakulima kutoa ushauri na wanaofanya hivyo wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, hatujanufaika na mifugo yetu na mazao yetu ya biashara kwa sababu ya ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na mazao ya mashambani. Tuna mifugo mingi maziwa mengi,

matunda mengi, mazao mengi lakini hatuna viwanda na Serikali ione namna ya kuweka vivutio kwa wawekezaji wa Sekta ya Viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi za ndani. Nashauri ranchi zetu zipewe mitaji ya kuanzisha viwanda vya kusindika vyama na maziwa.

Mheshimiwa Spika, umeme mbadala usiohitaji mafuta ni mkombozi kwa wananchi. Serikali ipunguze kodi kwa vifaa vya kuzalisha umeme wa jua na upepo ni miaka zaidi ya mitatu Serikali inazungumzia juu ya umeme wa upepo wa Singida. Je, uzalishaji umeme wa upepo Mkoani Singida umefikia hatua gani? Wananchi wanahitaji sana nishati ya umeme tatizo ni gharama kubwa ya ku-*install.*

Mheshimiwa Spika, kampuni za simu za mkononi zinatuibia. Wabunge wa Kamati ya *POAC* waliishauri *TCCRA* kufunga kifaa kitakachosaidia kujua mapato halisi ya Kampuni hizo za simu ili ziweze kulipa kodi stahiki. Serikali ikakubaliana na ushauri wa Wabunge wa Kamati ya *POAC* pasipo kuwakamua wananchi watumiaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie matumizi ya Shilingi yetu. Bado hoteli kubwa nchini zinatoza huduma kwa Dola ya Kimarekani. Suala hili tumelisema sana. Je, Serikali yetu ina maslahi gani katika hili?

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya reli ya kati, faida zake kwa Taifa zinajulikana. Reli hii ifanye kazi kwa

ufanisi sasa ni miaka 50 ya Uhuru hatuna reli ya uhakika ni aibu kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo kutekelezwa kwa asilimia 22 tu ni aibu. Hatuwezi kuendelea kwa haraka kwa hali hii. Naomba Serikali kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati na sio mwisho wa mwaka wa fedha kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya vitambulisho vya Taifa. Umakini mkubwa utumike katika utoaji wa vitambulisho hivyo kwani Tanzania tumewahi kuwa na wakimbizi wengi katika nchi mbalimbali na siyo wote waliorudi makwao.

Mheshimiwa Spika, deni kubwa la Taifa hupunguza uwezo wa Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Serikali iainishe vyanzo vipya vya mapato kukabiliana na mzigo mkubwa wa kukopa katika mabenki kila kukicha. Naishauri pia Serikali kupunguza matumizi yake ya kawaida ili itumie kulingana na mapato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake yenye kuelimisha wabunge na Jamii yote ya Watanzania, pongezi hizo ninazitoa pamoja na Manaibu Waziri pamoja na Wataalam wa Wizara ambao walijiandaa kutayarisha hotuba. Hata hivyo ninaunga mkono hoja, kwa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kwanza nimefurahi kuona pato la Taifa, Zanzibar limeendelea kukua, kwani katika mwaka 2011 ilifikia asilimia 6.8. Ingawa Karafuu imeshuka lakini utalii unakuza uchumi wa Zanzibar. Pia tunamshukuru Mungu kwa kipindi hiki thamani ya mauzo ya Karafuu kuongezeka, hii imesababishwa mauzo ya Indonesia kukosekana kutokana na ugonjwa ulioathiri zao hilo. Hata hivyo tunaiomba Serikali ya SMT kuisaidia Zanzibar jinsi ya kukuza uchumi wake kwa kutumia njia nyingine mbadala.

Mheshimiwa Spika, Pili, mapato inayopata Serikali kupitia *TRA* hivi sasa utaratibu uliopo wa kulipia benki ni mzuri, lakini Serikali lazima ifuatilie katika ofisi za *TRA* kwani wafanyakazi tayari wameanza mgomo baridi wa kazi, na hii inatokana kutopata fedha ambazo walikuwa wanazichukua binafsi. Utaratibu uliopo sasa mzuri na *TRA* ofisi iwe wanacheza na risiti za wateja tu.

Mheshimiwa Spika, tatu ongezeko kubwa la riba katika mabenki hasa *CRDB* na *NMB*, tunaiomba Wizara yako kufuatilia ili kupata unafuu kwa wananchi, kwani mapato wanayopokea na ukiangalia riba wanayopata kutoka kwa wananchi ni kubwa mno. Ombi kwa Mheshimiwa Waziri ajaribu kufuatilia kwa karibu ili kumwondoshea wananchi riba kubwa ya Benki hizo.

Mheshimiwa Spika, nne, misamaha ya kodi ya magari kupitia sheria za kodi na matangazo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 72 kifungu 103 kinatoa maelezo ya kodi ya msamaha wa kodi kwenye magari kwa watu mbalimbali ili kuwa na ukomo wa umri wa miaka minane badala ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri suala hilo kuliangalia tena iwe muda ule ule wa miaka kumi kama utazidi hapo ndiyo itozwe ushuru zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Wizara ya Fedha ya kuandaa Bajeti hii ni ukweli ni kwamba Bajeti hii haitoi majibu kwa matatizo ya wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii haijadhibiti mfumko wa bei, haijaonyesha ni namna gani itaongeza ukusanyaji wa mapato. Bajeti bado imerudia maeneo na vyanzo vile vile ambapo havina tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuona vyanzo vya mapato vitokane na bia, sigara hii haina tija kwa Taifa, matokeo yake wanywaji watakimbilia kunywa gongo na kuvuta bangi na kusababisha kuathiri afya zao na kupunguza nguvu

kazi ya Taifa. Hivyo lazima Serikali ibuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti imekuwa tegemezi asilimia 70 matokeo yake 2010/2011 Halmashauri nyingi zimeshindwa kumaliza miradi ya maendeleo, hivyo miradi yote itashindwa kupata thamani halisi kutokana na mfumko wa bei. Sasa Bajeti hii imejirudia kuwa tegemezi kwenye miradi ya maendeleo. Lazima tutoke huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpango kutaja Wilaya ya Kilombero iko kwenye mpango wa *SAGCOT* lakini haijapangiwa fedha za kutosha ili kukidhi miradi ya uzalishaji wa chakula. Taarifa ya mwaka wa fedha 2010/2011 ilieleza fedha zimetengwa kwa upembuzi yakinifu. Lakini cha kushangaza fedha za upembuzi yakinifu shilingi bilioni moja kwa kila mradi. Sasa napenda nipate majibu fedha za mwaka 2010/2011 zilifanya nini? Kwa nini Serikali inatangaza Kilombero, Mkoa wa Morogoro ni ghala la chakula na hakuna haraka ya kuzalisha na haipewi umuhimu na kutengewa fedha za kutosha ili uzalishaji wa chakula uanze mara moja, ili kuongeza chakula nchini na bakaa kuuza nchi za nje na kukuza uchumi ambapo ukiwekeza katika kilimo utapata matokeo ya haraka kwa miezi sita hadi nane tu na kukomesha upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema nini kuhusu miundombinu ya barabara, Reli ya Tazara na Daraja la Mto Kilombero. Kwa kuwa tunatoa kipaumbele kuzalisha chakula kwa wingi na ili chakula hicho

kisafirishwe ni vyema juhudi za kulima ziendane sambamba na uboreshaji wa miundombinu. Je, katika Bajeti hii Kilombero itatengewa fedha kiasi gani cha barabara na daraja. Pia kuendeleza kilimo ili mwaka 2013 mwezi kama huu tupewe taarifa ya tani za mpunga na siyo masuala ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kuhusu ukusanyaji kodi.

(i) Wizara irasimishwe kwa kila Mtanzania kusimamia ukusanyaji kodi kwa kila anaponunua bidhaa adai risiti halali na kila baada ya miezi mitatu ripoti ya *TRA* na apewe tuzo kulingana na thamani ya risiti kwa asilimia itakayopangwa.

(ii) Wizara kupitia *TRA* na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kutumia watendaji wa vijiji ipate idadi ya maduka na biashara zilizopo maeneo yao ili kwa kutumia watendaji wa vijiji waainishe biashara kubwa na za kawaida, muone namna ya kuweka makadirio ya kodi na nashauri angalau mlipa kodi apewe miezi mitatu ya matazamio baada ya hapo aanze kulipa kodi. Napendekeza ili kuepuka ulipaji kodi hasa kwa wenye *viosks* na maduka ya rejareja kodi ikadiriwe kwa faida atakayopata na si kama ilivyo sasa inakadiriwa kwa mtaji wa mfanyabiashara ambapo wengi wao wanakwepa kodi kwa kutumia leseni moja kwa maduka zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijikite kwa kuwekeza maeneo machache ya gesi ya

mchuchuma. Hivyo iachane kabisa na uchimbaji wa *uranium.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali nyingine tuziache kwa vizazi vijavyo na tujifunze kwa Mwalimu Nyerere (Marehemu).

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja iwapo Serikali itazingatia na kuboresha Bajeti kwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya kudumu na yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani pia kwa hayo niliyopendekeza.

Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. BENEDICT NGALAMA OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu wake na Wadau wote kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, bado yapo maeneo maalum yanayohitaji kutozwa kodi kama Madini, Magogo, Wanyama pori, (hasa uwindaji), Mahoteli, Majengo na Ardhi. Serikali itazame maeneo haya na kukata kodi ili kuongeza mapato

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa fedha kwenye Wizara na Sekta, Taasisi na Mamlaka tofauti siyo sawa na siyo *consistent.* Wizara moja kupatiwa fedha Trilioni na nyingine bilioni 54 ni sekta ya kiuchumi (mifugo na Uvuvi). Napendekeza Bajeti ipangwe ki-*ratio* (*percentages*) ili kila mwaka ijulikane kuwa kila mwaka

kila Wizara ijulikane kuwa inapata *percentage* ngapi katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya tatizo la kusimamia utekelezaji wa Bajeti napendekeza Wizara iandae mpango wa kuanzisha *Endowment Fund* kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti. Mfuko huu utunishwe na fedha kutoka *Reserves,* mikopo na *pre-financing* kutoka Sekta za Madini, Nishati ya Gesi, mkaa wa mawe, wanyamapori na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Tume ya Mipango itazame jinsi ya kuongeza fedha kwenye Bajeti ya Mifugo na Uvuvi, kwa ajili ya kutenga na kuendeleza maeneo ya ufugaji na hatimaye kuondoa migogoro kati ya Kilimo na Mifugo katika matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, fedha ibainishwe na kutengwa kwa ajili ya kukamilisha zoezi la kutoa kifuta machozi kwa wafugaji wa Longido, Monduli na Ngorongoro waliopoteza mifugo yao kwa ajili ya ukame.

**MHE. CHRISTOWAJA GERSON MTINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Deni la Taifa. Taarifa ya CAG inaoesha kuwa deni la Taifa linazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka na hiyo kutishia uhai wa Taifa na watu wake. Mfano deni hilo limeongezeka kwa asilimia 38 kutoka Sh. Trilioni 10.5 mwaka 2009/2010 mpaka trilioni 14.4 mwaka 2010/2011. Mpaka mwezi Machi, 2010 deni hilo limefikia Sh. Trilioni 20.3 kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na *BOT* taarifa yao ya Mei inaonyesha

deni hili limefika Sh. Trilioni 22. Hivi maana yake nini? Ni kweli tunakopa kwa ajili ya shughuli ya maendeleo au tunatoka kwa ajili ya mambo ya anasa? Ni kwa nini Serikali imekuwa ikifanya matumizi yasiyo na msingi na kusababisha wananchi wa kawaida kuishi kutoka umaskini uliotopea? Kwa nini Rais anasafiri kila kukicha na safari hizo mara nyingi zimekuwa zikiambatana na idadi kubwa ya watumishi? Watu wote hao wanaleta tija gani katika safari hizo? Safari za Rais zina tija au ndiyo sehemu ya kufuja fedha za Umma? Kwanini Serikali imeendelea kununua magari ya anasa kwa watumishi wote wa Serikali kuanzia Mkurugenzi wa Halmashauri mpaka kwa kada za ngazi ya juu? Kwanini magari ya bei ndogo yasinunuliwe kwa watumishi kada ya chini? Maana yake ni kwamba tunakopa ili kuendeleza anasa na si shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa fedha za Maendeleo, Bajeti ya mwaka jana 2011/2012 iliyopitishwa na Bunge hili ilidhinisha fedha za maendeleo katika Wizara mbalimbali. Lakini fedha hizo zilizopitishwa mpaka sasa hazijaweza kupelekwa kwa shughuli tajwa na leo tunaomba fedha zingine. Fedha hizo zilipelekwa wapi? Matatizo makubwa tunayoyapata kwenye halmashauri nyingi za wilaya ni ukosefu wa fedha za maendeleo. Sasa kwa maana hii tunategemea umaskini utaondoka vipi kwa wananchi wa Taifa hili?

Shule zinashindwa kuendeshwa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, vinashindwa kutoa huduma bora kwa wananchi maskini. Ni lini Serikali itatilia maanani ahadi inazotoa na kuheshimu matumizi ya fedha ili

kuwatendea haki wananchi wake? Serikali ibadilike katika Bajeti hii na ihakikishe inapeleka fedha za maendeleo kwa wakati na hivyo katika Bajeti hii Serikali itoe maelezo ya kina fedha zilizotengwa mwaka uliopita zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Misamaha ya Kodi, pamoja na umuhimu wa Serikali kutoa misamaha ya kodi kwa mashirika mbalimbali yanayotoa huduma hapa nchini; kuna haja ya kupitia upya sheria ya kodi ili kuokoa fedha nyingi au mapato yanayopotea kutokana na misamaha ya kodi. (mchango wangu nimeutoa kwa undani katika hoja ya Hali ya Uchumi). La msingi hapa naomba Waziri anieleze kwa kina kwa nini TRA imeendelea kutoa msamaha wa kodi kwenye maduka ya Jeshi ili hali hayauzi bidhaa hizo kwa *duty free?* Madhumuni ya maduka hayo kutozwa kodi ni kuwafanya wanajeshi na familia zao kumudu kupata mahitaji yao kwa bei nafuu kutokana na *nature* ya kazi yao ambayo inahitaji motisha wa kutosha. Maduka hayo ambayo yote yanamilikiwa na Watanzania wenye asili ya Kiasia, yamekuwa yakiwanyonya wanajeshi na kuuza bidhaa zao kwa bei kubwa sana kuliko hata ile ya sokoni au ya maduka ambayo yanatozwa ushuru/kodi. Maduka haya yamekuwa yakipata faida maradufu kwa unyonyaji huu na hivyo kwenda kinyume na madhumuni ya kuanzishwa kwayo. Ninaitaka *TRA* pamoja na Serikali kupitia upya misamaha hii na ikiwezekana ifutwe kabisa maana haiwanufaishi walengwa bali hao wenye maduka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Baada ya kuunga mkono naomba kuchangia baadhi ya maeneo ili kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miundombinu ya umeme, bila kuwa na miundombinu ya uhakika ya umeme maendeleo ya haraka na yaliyoendelevu siyo rahisi kufikiwa, naipongeza serikali kwa kulitambua hili na kulibainisha katika mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kuingiza mkakati wa kusambaza umeme wa Gridi ya Taifa kuanzia maeneo ya Nyakanazi, Kigoma, Mpanda, Sumbawanga, Tunduma, Mbeya, Makete hadi Iringa ni vizuri jambo hili likatekelezwa kwa kasi kubwa ili kufungua mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na Njombe ili kama Taifa tuendelee kwa pamoja na kuondokana na dhana potofu ya mikoa ya pembezoni ambayo imekuwa *disadvantaged.*

Mheshimiwa Spika, ili nia nzuri ya kuhakikisha kwamba nia njema ya kusambaza nishati ya umeme kwa maendeleo ya haraka ni vizuri vyanzo vingine vikatizamwa ili kuweza kuzalisha umeme utakaoingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, viko vyanzo vya uhakika vya makaa ya mawe yaliyopo Namwele na Nkomolo Mkoani Rukwa vyanzo ambayo vimeonesha kuwa na makaa ya mawe ya kutosha na machimbo haya yalishaanzishwa na Mtanzania Mzalendo ambaye

anachohitaji ni kuungwa mkono na Serikali na pia kuhakikishiwa umeme utakaozalishwa kununuliwa na shirika la umeme yaani *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa Serikali kuhakikisha kwamba pesa inatengwa kwa ajili ya mradi huu ambao ni muhimu kwa uzalishaji wa umeme kwa Mikoa ya Rukwa na Katavi na hivyo kuvutia kujengwa viwanda vya usindikaji wa mazao ya chakula pia mazao ya samaki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu ya barabara. Napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) chini ya uongozi imara wa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuamua kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Tunduma hadi Sumbawanga hadi Kasanga na Kasesya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza jitihada za Serikali nashauri Serikali ihakikishe barabara hizi zinatengewa pesa za kutosha na hasa kwa barabara zile zinazojengwa kutokana na pesa za ndani ili kuhakikisha pesa zinapatikana isije ikachukua muda mrefu na kuwaondolea matumani wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya sababu za kiusalama ni vizuri barabara zinazounganisha Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa kwenda Ziwa Tanganyika ziboreshwe na kupitika vipindi vyote vya mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la kilimo ili kama Taifa tuharakishe kwamba tunapata tija.

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na nia ya makusudi ya kufanya mapinduzi ya kilimo na hivyo kuwa ni kivutio cha biashara baada ya kuwa na *agrobusiness*. *Budget* ihakikishe kuomba utaratibu wa kuhakikisha mikopo ya zana za kilimo kwa maana ya matrekta yanayowafikia wakulima na hasa wale walio katika vikundi vya uzalishajimali na hasa *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kalembo, ipo *SACCOS.* Katika Kijiji cha Ulumi kata ya Ulumi ambayo ilichukua mkopo wake *SCULT* wa milioni 30 na kuweka amana ya kiasi cha shilingi milioni 10 kama amana.

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* hii ilifanikiwa kulipa mkopo huu pamoja na adhabu kwa kuchelewa kulipa mkopo kwa wakati cha kuchangaza tangu *SACCOS* hii ilimalize deni ni muda mrefu bila kurudishiwa pesa yao iliyotumika kama amana wamenituma pesa hii irudi mara moja ili waweze kuzitumia katika kukopa trekta kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mgimwa (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Janet Mbene (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Saada Salum Mkuya (Mb), Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye kuonyesha kuinua uchumi wa Watanzania hasa wenye maisha duni. Vile vile ninawapongeza Waziri na Manaibu

Mawaziri wote wawili kwa kuteuliwa kuwa Wabunge na kuteuliwa kushika wadhifa huo muhimu, tuna matumani makubwa kuwa watatekeleza majukumu yao vyema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi kuwa Sh. 170,0000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote Tanzania kwa juhudi zao za kazi za kila siku ingawa mishahara yao kuwa midogo sana mfano kima cha chini Sh. 135,000 na sasa Serikali inapandisha kima cha chini kutoka Sh. 135,000 hadi Sh. 170,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa bado Serikali haijamfikisha mtumishi kwenye maisha bora kwani mahitaji muhimu ya familia zao ni mengi na yote yanahitaji fedha. Mfano mtumishi wa mjini, mfano katika Jiji la Dar es Salaam watumishi mishahara yao huishia kwenye nauli ya daladala tu kwa ajili ya kwenda kazini na kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwahurumie walimu, wauguzi na wafanyakazi wote, Serikali iongeze mishahara ili kuondoa utoro, wizi na uzembe kazini. Naomba Waziri atoe maelezo ya kuwafariji wafanyakazi wakati wa kufanya majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya ndani kuondolewa *VAT;* napenda kuishauri Serikali kuondoa *VAT* kwenye viwanda vya ndani hususan

viwanda vya nguo na mavazi ili viwanda hivi viweze kuimarika, kuongeza uzalishaji na kuongeza ajira kwa vijana wetu na kadhalika utaratibu wa Serikali kuuza mali ghafi nje ya nchi haileti tija sana kiuchumi hivyo ni vyema malighafi mfano pamba itumike kwenye viwanda vyetu, viwanda ambavyo vitatoa ajira na faida nyingi kwa Watanzania kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ipokee hoja hii na kutekeleza kwa kuondoa *VAT* kwenye viwanda vya ndani ya nchi hususani viwanda vya nguo na mavazi ili viweze kuimarika kwa maslahi yetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nafanya majumuisho ndani ya Bunge la Aprili mwaka huu 2012 nilitoa ushauri wa ongezeko la kodi ya mafuta ya taa ambao utakuwa bilioni 50 kwa mwezi na shilingi bilioni 600 kwa mwaka mradi wa kupeleka umeme vijijini angalau zitengwe fedha hizi kwa asilimia 50 ili kuondokana na utaratibu wa kutegemea wahisani kwa asilima mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeona Serikali imekubali kupeleka asilimia ndogo sana. Kwa kuwa mradi huu unagusa maeneo mengi ya vijiji karibu majimbo yote nchini ninaamini Wabunge wote na Watanzania watafarijika kwani wakati natoa hoja Bungeni iliungwa mkono. Ninaomba Serikali kufikiria upya hoja hii ya kutenga asilimia 50 ya ongezeko la kodi ya mafuta ya taa kwa ajili ya *REA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama Kuu Singida pamoja na mahakama za Wilaya ya Iramba na Manyoni. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa imeanza kutoa ahadi mara nyingi hapa Bungeni azma yake ya kujenga Mahakama Kuu Singida pamoja na mahakama za Wilaya nilizozitaja hapo juu lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea naomba kuelezwa na Waziri wa Fedha azma hii itatekelezwa lini na kwa nini isiwe Bajeti hii ya 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyanzo vya mapato nchini kutazamwa upya. Ni ukweli usiofichika kuwa nchi ina bahati ya kuwa na vyanzo vingi vya mapato mfano madini, gesi, utalii, kilimo, bandari na kadhalika. Kulinganisha nchi nyingi duniani zilizoendelea mfano visiwa vya *Trinidad and Tobago* wanaotegemea gesi na mafuta tu. Hii inadhihirisha wazi kuwa vyanzo vingi vya nchi yetu mapato yake ni madogo sana. Hivyo kuna haja ya kuweka mikakati kabambe upya ili vyanzo vingi vya mapato viweze kuongezeka kwa lengo la kuinua uchumi na kupunguza utegemezi wa wahisani, nitahitaji maelezo ya Waziri, mfano kwenye madini na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia mchango kwa kuunga mkono Bajeti hii nikitegemea kabisa mchango wangu utapewa uzito unaostahili. Ninawatakia utekelezaji wenye kuleta tija kwa Watanzania.

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunga mkono, naomba nipate

ufafanuzi katika mambo muhimu yafuatayo: Kilimo, Umeme, Mshahara wa Madiwani kuongezeka, Posho kwa wenyeviti wa Serikali za vijiji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Kilimo, kumekuwa na kauli mbiu nyingi toka wakati wa enzi ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alianzisha kauli mbiu ya Azimio la Iringa - mwaka 1972, SIASA NI KILIMO, Kilimo cha Kufa na Kupona na sasa Kauli mbiu ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu zote hizi utekelezaji wake wote una kuwa ni kwa nguvu ya soda au moto wa mabua.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni kwamba mwaka jana katika Bajeti ya Kilimo ilikuwa ni 258.4 bilioni na kwa sasa Bajeti ya mwaka huu kilimo imetengwa Shilingi 192 bilioni. Sasa hii ni sawasawa na kuwa na mbiu ya nguvu ya soda au moto wa mabua. Hivi niulize swali. Je, kilimo kimefika kikomo cha kusonga mbele? Hadi kupunguza Bajeti yake naomba jibu. Je, Serikali imediriki kwamba asilimia 75 ya Watanzania ambao ni wakulima tayari wameshanufaika vya kutosha na wanaweza kusimama kwa miguu yao? Je, Serikali itaacha kuanzisha jambo na kuliacha kabla halijaleta manufaa ya kutosha?

Mheshimiwa Spika, kilimo bado kinahitaji kuendelea kupewa kipaumbele kwa kutenga Bajeti kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kuonekana bila kuwepo na nishati ya umeme na ndiyo maana hata ukiangalia mikoa iliyoendelea ina umeme wa kutosha, umeme unasaidia kuvuta wawekezaji kujenga viwanda na katika viwanda tunakuza uchumi, tunaongeza ajira, tunakuza uchumi wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, nije katika Mkoa wa Rukwa na Katavi, Mikoa hii haina umeme wa kutosha umeme wa Gridi ya Taifa japo kuwa mikoa hii inachangia sana katika kutoa chakula kwa nchi hii. Kwa nini mikoa hii isifikiriwe tena kwa haraka kuhakisha kuunganishwa umeme wa gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, niulize swali ni lini Serikali itaunganisha umeme katika gridi ya Taifa kutoka Nyakanazi- Kigoma – Mpanda – Tunduma – Mbeya – Makete – hadi Makambako. Nijibiwe ni lini mpango huu utakamilika?

Mheshimiwa Spika, mikoa hii ya Rukwa na Katavi inazo rasilimali nyingi. Yapo makaa ya mawe yaliyopo Namwele, Nkomolo na inasemekana makaa haya ya mawe yaliyopo yanaweza kutoa zaidi ya megawatt 100.

Mheshimiwa Spika, ukiachia makaa ya mawe tunayo mito mingi yenye maporomoko yanayoweza kutoa umeme na mojawapo ya mito iliyofanyiwa utafiti ni pamoja na Mto Nzovwe lakini rasilimali hiyo haijafanyiwa kazi. Je, ni lini rasilimali hizi zitatumika?

Mheshimiwa Spika, ongezeko la mshahara kwa Madiwani, katika Bajeti ya Bunge lililopita tuliomba Serikali iongeze mishahara ya madiwani Je, madiwani wameongezewa mishahara?

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa vijiji kulipwa posho/mishahara. Naomba Serikali ifikirie uwezekanio wa kuwalipa viongozi hawa posho/mshahara. Ikumbukwe kwamba maendeleo yetu tunayozungumza mtekelezaji wa mwisho na msimamizi wa mwisho ni viongozi hawa hivyo ili kuwafanya wasimamie vyema ni bora Serikali iwalipe haki yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Spika baada ya kufafanuliwa vizuri nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2011 na mwelekeo wa mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013, inaeleweka wazi kuwa Watanzania zaidi ya asilimia 75 wanategemea kilimo katika kipato chao, ili kuendesha maisha yao. Kwa maana hiyo kukua kwa uchumi wa wakulima hao ndiyo kukua kwa uchumi wa Taifa kwa sababu zifuatazo:-

Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara utaongezeka, kodi ya Serikali italipwa kutokana na kipato kizuri cha mazao, kutakuwa na chakula kingi nchini, mfumko wa bei ya chakula utashuka, ziada kubwa ya chakula itapatikana na itauzwa nje hivyo fedha ya kigeni zitapatikana kutokana na mauzo ya

mazao hayo. Malighafi ya viwanda tulivyonavyo nchini itapatikana, viwanda vyetu vitakuwa hai na ajira itaongezeka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu zote hizo ipo haja kubwa ya Serikali kutilia mkazo mkubwa suala la kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji ambacho bado Serikali haijatilia mkazo mkubwa. Kwani nchi yetu inayo mito mingi ambayo ina mabonde makubwa lakini hajatumika kikamilifu na mfano mzuri ni katika Wilaya ya Sumbawanga ipo mito mingi na mabonde makubwa mfano mto Momba, kuna bonde la Maleza, hekta 7,500 halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa umeme, ukiachia mfumo wa umeme toka gridi ya Taifa, ipo mikoa ambayo inaweza kupata umeme kutokana na maporomoko yaliyopo katika mikoa yao. Mfano mzuri ni Mkoa wa Rukwa ambao unavyo vyanzo vingi vya maporomoko ya mito ambayo inaweza kutoa umeme wa kutosheleza mahitaji ya umeme katika Mkoa, kuliko kutegemea umeme toka Zambia au umeme wa *Generator* ambao una gharama kubwa. Mfano mzuri ni mto Nzovwe una maporomoko yaliyokwisha kufanyiwa utafiti kuwa yana uwezo kutoa *watt 8* na zaidi mwaka 1972 na mwaka 1980 na kadhalika, cha kuchangaza Serikali haijachukua hatua zozote ila kuendelea kulalamika tu. Serikali chukua hatua kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mikopo, Serikali itoe mikopo kwa wakulima kwa masharti nafuu.

**MHE. ENG. HAMAD YUSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi ipangiwe mkakati wa kuipunguza. Bajeti hataonesha dhamira ya dhati ya Serikali kupunguza misamaha.

Mheshimiwa Spika, *impact* ya kilimo kuanzia kwenye mfumko wa bei ya chakula haitajionesha. Kuna haja ya kuangalia zaidi eneo la misamaha ya kodi ya sukari, ruzuku kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula na kufanikisha wimbo wa uanzishwaji wa Benki ya Wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala ya misamaha ya kodi ni muhimu likadhibitiwa ikiwemo kwa wawekezaji wa nje, taasisi za dini na kadhalika. Ingawa ni muhimu fursa hii adhimu kutumika katika maeneo yanayoleta tija kwa uchumi mpana ikiwemo *VAT* kwenye viwanda vya nguo ili kuongeza ajira na nyumba ama ujenzi ili kupunguza mzigo wananchi wa hali ya chini

**MHE. VICK PASCHAL KAMATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa William Mgimwa na Manaibu wake kwa kuteuliwa na Rais kuiongoza Wizara nyeti, Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa waheshimiwa hawa watafanya kazi kwa uwezo wao wote na kulifikisha Taifa hili pale linakotakiwa kufika.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya pongezi hizo naomba nisisitize suala moja tu kabla ya kuunga

mkono hoja hii. Pamba ni bidhaa muhimu sana katika uchumi wa nchi hii ukianzia uchumi wa ngazi ya familia inauma na inakatisha tamaa sana kuona zao hili muhimu halipewi kipaumbele kinachostahili kwa kuanzisha kuwawezesha wakulima wa pamba waweze kulima zao hili kwa nguvu zaidi na liweze kuleta tija kwa Taifa, kuwapatia soko zuri la mazao yao ni kuwakomboa wakulima.

Mheshimiwa Spika, bei ya pamba ni tatizo sana. Naomba sana sana Bajeti hii ikipita basi tuzingatie bei ambayo waheshimiwa wengi wameidai yaani bei ya Sh. 1,000/= kwa kilo moja ya pamba. Naomba sana bei hii izingatiwe kusudi tuweze kuwainua wakulima wa pamba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya mwaka 2012/2013 katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti na kuifanya sekta ya miradi ya maendeleo kuendelea kukosa fedha za kutosha naishauri Serikali kupunguza matumizi ya kiutawala ili fungu litakalopatikana liweze kuongezeka katika Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kiutawala hatuwezi kuyaepuka kwa jinsi yoyote ile lakini kwa umuhimu wa maendeleo yetu na ili miradi ya maendeleo izidi kupata nguvu ni vizuri sana marekebisho yakafanyika ili angalau Bajeti ya

Maendeleo iweze kufikia asilimia 35 kutoka asilimia 30 iliyotengwa sasa. Nadhani hili linaweza kutufanya tuweze kusonga mbele, japo kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya uvuvi, wananchi wengi wanaoishi maeneo ya *Coast Zone* na maeneo ya Maziwa ambao shughuli zao za kujipatia kipato hasa zinatokana na uvuvi. Wamekuwa na kilio cha muda mrefu kwa Serikali kutokana na kukosa mikopo ya vifaa vya uvuvi. Wananchi wakipata matatizo ya mara kwa mara na watu wa mazingira kutokana na vifaa wanavyotumia kuonekana havifai. Sasa naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kufungulia milango kwenye taasisi za fedha ili waweze kukopeshwa kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ni muhimu sana na ikisimamiwa vizuri serikali inaweza kuongeza Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa sana kutokana na hii sekta.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kwa kufufua shirika letu la Ndege la Tanzania, lakini ni vizuri Serikali iwe na uangalifu sana na hujuma ambazo zinaweza kujitokeza hasa kuangalia mashirika binafsi ambayo wanaliangalia kwa mtazamo hasi Shirika hili. Kwani kuwepo hai Shirika hili wanahisi ni kikwazo kwao katika ushindani wa kibiashara.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kuhusu bajeti hii ya mwaka wa fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza moja kwa moja kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, huduma ya maduka ya madawa. Kumekuwa na tabia ya wamiliki hawa wa maduka ya dawa kuchukua/ kuhamisha dawa katika hospitali zetu za Serikali ambako dawa hizo zinapatikana kwa bei nafuu na kuzipeleka katika biashara zao za maduka ya dawa baridi na kuziuza kwa bei ya ghali/juu kuliko katika hospitali za Serikali. Hali hii inawapa wagonjwa wakati mgumu sana wa kuhangaika kutafuta dawa hizo sehemu mbadala tofauti na hospitali hizo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili, elimu kwa Mafamasia, ni kweli usiopingika kuwa wahudumu wengi wa maduka haya. Hawana elimu ya kutosha *either* kwa kujua *or* kwa makusudi tu kwa ajili ya *cheap labour* kama baadhi ya Watanzania wengi walivyozoea bila kujali huduma hii inahitaji ufanisi na utaalamu wa hali ya juu kwani wana-*deal* moja kwa moja na maisha ya binadamu ambayo kitaalamu inajulikana kama afya.

Mheshimiwa Spika, tatu, kupanda kwa gharama za maisha ni pamoja na huduma za afya kuwa juu kwani kupanda kwa gharama hizi kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la bidhaa katika soko la Ulaya yakiwemo mafuta ya magari ambayo ndiyo yamekuwa yakitumika katika magari/ndege/treni katika kusafirisha bidhaa hizi za mahospitalini mfano dawa, vifaa vya upasuaji na vyote vinavyohusika katika hospitali zetu. Kwa sababu hiyo huduma za hospitalini zimepanda kwa kiwango kikubwa kiasi cha

mwananchi kushindwa kupata huduma hiyo kiurahisi katika hospitali zetu hapa nchini na kusababisha baadhi ya wagonjwa ambao hawana uwezo wa kutosha kuishia kununua dawa katika maduka ya dawa bila kujali anayewahudumia ana utaalamu wa kutosha wa uuzaji wa dawa hizo kwa maana ya kuwa na taaluma ya Kifamasia na kumsaidia mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo niliyoaandika hapo juu naomba kutoa changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa vifo, hii ni kutokana na hali ngumu ya maisha, uzembe wa wamiliki wa maduka kuajiri wahudumu wasio na elimu ya utabibu na kusababisha kuwapa wagonjwa dawa kinyume na matatizo yanayowasumbua na hata kusababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, katika maduka haya kumekua na ukiukwaji wa kanuni za huduma hii mfano, kuchoma sindano, kufunga vidonda wagonjwa n.k na kuleta matatizo zaidi kwa wagonjwa kutokana na baadhi yao wengi kukosa taaluma hii ya utabibu kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wengi wamekuwa wakijali biashara zaidi kuliko kutoa huduma ya afya kama lilivyo kasudi la kufungua maduka haya kama kibali kinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara na bila taarifa katika maduka

haya ili kubaini wanaoenda kinyume na maazimio ya huduma hii na kuwachukulia hatua madhubuti kama kuwanyang'anya kibali cha uendeshaji wa huduma hii ya dawa baridi ya binadamu kwani afya ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, lazima wamiliki wa maduka haya waambatanishe vyeti ambavyo vitaonesha elimu ya wahudumu wa maduka hayo pamoja na *CV* zao ambazo zitakuwa zinaonesha *experience* waliyonayo wauzaji hao ili kuwa na uhakika leseni inatolewa kwa mtu ambaye atakuwa na elimu ya kutosha ya utabibu wa ufamasia kwani afya ni muhimu sana katika maisha ya mwanadamu na kama hataweza kufanya hivyo asipewe leseni ya biashara hiyo. Watakaokamatwa na makosa yoyote, wanyang'anywe leseni na wasirudishiwe tena kwa kuwa afya siyo jambo la mzaha hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuishukuru Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* kwa kuandaa mafunzo na semina kwa wamiliki wa maduka haya baada ya tathmini iliyofanywa mijini na vijijini na kubaini kuwepo kwa matatizo ya upatikanaji wa huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake pamoja na ugeni wake katika Wizara lakini ameweza ku-*display talent* na *professional*

yake vizuri sana. Naunga mkono hoja lakini hata hivyo ninahitaji haya yafuatayo yazingatiwe:-

(a) Ukali wa maisha umekuwa juu sana. Mapato ukilinganisha na matumizi haviendani. Nchi inakua kiuchumi lakini wananchi wanazidi kuwa maskini kwa nini?

(b) Tunashukuru kuwa bajeti ya maendeleo sasa ni 30% na *OC* ni 70%, hii bado hatujawatendea haki Watanzania ambao zaidi ya 70% wanaishi vijijini - hakuna madawati shuleni, hakuna dawa hospitalini, damu salama ni kizungumkuti, zahanati vijijini chini ya mpango wa MAM hakuna, reli, barabara shida tupu. Kwa nini Serikali itenge bajeti ndogo ya maendeleo yanayohusu wananchi moja kwa moja.

(c) Tanzania ni nchi inayotegemea sana wahisani zaidi ya asilimia 30, Kenya mfano ni asilimia 5, Uganda ni asilimia 20, naomba *clarifications* ya kwamba chetu ni kipi? Mapato ya ndani na ya nje, misaada ya nje inapanda au inashuka? *Total* bajeti yake ni ipi na kwa kiwango gani?

(d) Misamaha ya kodi Tanzania ni mikubwa sana *(massive exemptions tax relief)* zipo juu sana. Hivi hii mikataba mibovu ya madini na Tume ya Mzee Bomani vimefikia wapi? Nchi inapoteza, hapa ni *win-loose situation*. Wanapopewa *tax relief exemptions* mfano miaka 10 ikibaki mwaka mmoja tu aidha migodi, kampuni zinauzwa kubadilishwa majina na kuondoka nchini kabisa hivyo nchi kupata hasara. (Hizi ni *foot loose companies)*. *Review* nyingine ifanyike kwa hawa

wawekezaji ili kuwepo na *winwin situation*. *Incentives on mining* ni *zero import duty, this is unbelievable!* Kama tunashindwa kupata mapato hayo kwenye madini *as per cost benefit analysis*, sasa kwenye *gas and oil* tutawezaje? Tujali kwanza Watanzania walio wengi.

(e) Makampuni ya simu 2010 yalipata zaidi ya shilingi sita trilioni lakini kodi yakalipa 2.7 bilioni i.e. Kenya, Rwanda, Uganda, Serikali inapokea mara kumi zaidi ya Tanzania. Kwa nini makampuni ya simu na madini yanatengeneza faida kubwa ambayo hailingani na kodi wanayolipa? *Corporate social responsibility* pia haiendani na pesa kubwa wanayopata.

(f) Naipongeza Serikali kwa *innovation* ya jinsi ya ukusanyaji wa mapato ya *number plate* na *willingness* ya majina binafsi kwa kutoza shilingi milioni tano kwa miaka mitatu. *However* hii sio nzuri kwani inaleta matabaka ya walionacho na wasionacho kwa nchi, *if that is the case* katika kukusanya mapato ni vyema basi hiyo shilingi milioni tano ikawa kila mwaka yaani shilingi 15 milioni kwa miaka mitatu. Serikali iliangalie suala hili upya.

(g) Naipongeza Serikali kwa kuleta *Capital Gain Tax*, *however withholding tax* bado iendelee kuwepo kwa nini iondolewe? Asilimia 10 *withholding tax* ya nyumba – *proper control* ifanyike ili Serikali iendelee kupata mapato maana kodi nyingi zipo kwa wapangishaji nyumba na isiwe tu baadhi ya maeneo fulani, i.e *prime areas* iwe ni kote.

(h) Serikali inatakiwa kutoa vipaumbele zaidi vitano kama ilivyokuwa kwenye mpango wa miaka mitano uliozinduliwa mwaka jana kuliko kushika hiki na hiki, mwisho wa siku *deliverables* inakuwa ngumu kujua *mables*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naunga mkono hoja hii ya bajeti.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa mambo mawili makubwa. Kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni imani kubwa kwa Rais juu yao. Pili, nawapongeza kwa kuwasilisha bajeti ambayo ni ya matumaini kwa wananchi wa Tanzania ambao imani yangu kubwa wananchi hawa wanaridhika na hali ya amani na utulivu uliopo kulingana na nchi jirani na nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida, bajeti hii ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji kuangaliwa kwa ukaribu sana na kusimamiwa katika utekelezaji wake na usimamizi ulio makini. Haitapendeza hata kidogo jitihada zao za kupanga na kuweza ku-*allocate fund* kwa Halmashauri zetu na Serikali za Mitaa kusikia kumetokea wizi wa fedha na kutotekelezwa kwa mipango na miradi ya maendeleo katika maeneo hayo. Kama hili halitoshi, ni busara kuimarisha kitengo cha ufuatiliaji wa matumizi hayo kabla *CAG* kutoa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, ni suala ambalo limezoeleka kusikia kwamba fedha zinachelewa kuingizwa katika kasma ama mafungu ya Wizara na kusababisha Wizara kuwa na visingizio vya kutotekelezeka kwa majukumu ya Wizara. Naishauri Hazina ijitahidi kadri iwezavyo kuingiza fedha hiyo mapema ili Wizara ziweze kutekeleza majukumu hayo na kusita kutoa visingizio vya utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho si kwa umuhimu ila ni mpangilio, miongoni mwa kero ambazo zinasababisha vurugu na kupoteza imani kwa Wazanzibar, ni lini hatua za makusudi zitachukuliwa kuelimisha na kuweka wazi kabisa mgao wa fedha hizi? Je, kuna usiri gani wa aidha Tume ya J.F.C. au Hazina kutoa elimu na kutoa taarifa kwa Watanzania uhalali wa formula inayotumika kugawa fedha hizi kwa upande wa pili wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuunga mkono hoja na kuwatakia utekelezaji mwema wa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kuhusu hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/2013. Nampongeza Waziri na watendaji wa Wizara na hasa Tume ya Mipango kwa kuanda taarifa hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya mwenendo wa uchumi wa Taifa unaonyesha kuwa ukuaji wa pato la taifa ulikuwa ni asilimia 6.4 kwa mwaka uliopita pamoja na matatizo ya umeme ukame na kadhalika. Napenda kupongeza Serikali kwa jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia ukusanyaji wa mapato hasa mapato ya kodi *(TRA).* Bado naishauri Serikali ijenge uwezo kwa Halmashaui zetu ili pia ziweze kukusanya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingine vya mapato pia viongezwe ili kuongeza wigo wa mapato kwa:-

- Sekta isiyo rasmi irasimishwe ili iweze kulipa kodi.
- Kuongeza ushirikiano wa kikanda na mauzo ya nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Serikali kwa mwaka uliopita 2011/2012, nashauri nidhamu ya matumizi izingatiwe na Serikali ijenge utaratibu wa kuheshimu bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hali halisi ya nchi yetu bado tunashauri tujitahidi kubana matumizi na kuweka vipaumbele vichache kwa matumizi yenye tija. Vipaumbele vya kilimo, umeme, miundombinu viendelee kupewa pesa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri, ukurasa wa 17 unazungumzia masuala mtambuka. Ni vizuri Waziri akazungumzia pia suala la jinsia kwani ni muhimu sana

kuthamini makundi mbalimbali yaliyopo katika jamii yetu ili kuona fursa na jinsi ambavyo yanaweza kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Mfano ipo haja kubwa ya kuwekeza katika kundi la vijana na wanawake ambao kwa kweli wana uwezo na nguvu ya kuzalisha zaidi, hasa kwa kuwa makundi haya mawili yana mitazamo chanya na wenye matumaini ya maisha marefu.

Mheshimiwa Spika, malengo ya millennia ni vizuri yakafanyiwa tathimini ya kila moja na utekelezaji wake hapa nchini.

Mheshimiwan Spika, kuhusu uwezeshaji wa wananchi, nashauri Wizara ifanye utaratibu wa kufanya mikutano, mafunzo na warsha kwa wawekezaji wote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Kimkakati ya Taifa; naishukuru Serikali kwa Mradi wa Reli ya Mbamba Bay/Mtwara, njia ya umeme Makambako, Songea. Naomba Serikali ikumbuke kulipa fidia za maeneo maalum ya (EPZ) Songea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hotuba ya Waziri wa Fedha, naomba kuchangia hotuba hii kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii maeneo mengi ya muhimu yametajwa kwamba yatafanyiwa kazi. Kwa maoni yangu, nashauri Serikali ijitahidi kuwa na kasi kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo

iliyopangwa katika bajeti ili kuleta imani na hali nzuri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Serikali iongeze ushirikiano na sekta binafsi na hasa kuijengea uwezo ili kupunguza mzigo wa majukumu na miradi mingi kutekelezwa na Serikali. Serikali pia ipunguze misamaha ya kodi, huu ni mzigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ijitahidi sana katika kukusanya mapato na kwa kuwa wapo wadau wengi hasa *private sector* wapo tayari kutoa mawazo yao kwa Serikali juu ya vyanzo vipya vya mapato basi Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali katika mchakato wa bajeti. Hili liende sambamba na maboresho ya sekta ya fedha ili iwe ni sekta ya mfano kwa ufanisi.

Mheshimwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu na wote walioshiriki kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, suala la mfumko wa bei, ni wazi kuwa hali ya maisha kwa wananchi wengi inakuwa ngumu, chakula kimekuwa ghali hasa mchele, mahindi, sukari. Chakula ndicho kinachangia kwa sehemu kubwa katika kukuza mfumko wa bei sasa imefikia asilimia 18.7 kutoka asilimia 8.9 Aprili 2011.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na jambo hili, Waziri ameeleza nia ya Serikali kuteremsha mfumko,

njia mojawapo ikiwa kuagiza chakula na wafanyabiashara. Mimi nina hofu njia hii inaweza isifanye hivyo hasa kwa kuwa kuna tatizo la chakula katika nchi zinazotuzunguka za Kenya, Uganda, South Sudan na Rwanda. Kitachotokea ni chakula kikifika Tanzania kitasafirishwa kinyemela kwenda nchi hizo na hivyo Serikali kukosa mapato, bei kutoshuka, kunufaisha wafanyabiashara, mfumko wa bei kubaki na wananchi kutonufaika.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kupunguza mfumko wa bei ni kuweka msisitizo na bajeti kubwa kwenye kilimo na umeme hasa kilimo cha umwagiliaji lakini inashangaza kuwa bajeti ya kilimo iliyounganishwa na sekta ya uvuvi, misitu, wanyamapori, ufugaji ni shilingi bilioni 192.2 tu. Hii ni kidogo na kwa kuwa ukurasa wa 48, aya 78b, Waziri amefunika umwagiliji kwa kuzungumzia kilimo cha misitu, pembejeo kwa wakulima, maafisa ugavi kuwa na mashamba ya mfano, kuimarisha masoko ya mazao kwa kurasimisha ardhi, kuna mistari mitatu tu juu ya kilimo cha umwagiliaji katika mipango ya bajeti ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Waziri ameeleza juu ya mipango ya *Quickwins* itakayoleta mafanikio ya haraka kwa kushirikiana na sekta binafsi. Serikali itawekeza katika mabonde, hapa Serikali lazima i-*balance* kuhakikisha kuwa wakulima wadogo ambao ndiyo wengi nchi hii wanaendelezwa katika uzalishaji. Mabadiliko yanayopatikana katika ngazi ya kaya na kijiji yataweza kupunguza mfumko wa bei hasa upande

wa chakula wakati huohuo tukijua kuwa suala la ajira ya vijana litapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, wengi wamekosoa juu ya kukua kwa Deni la Taifa. Deni la Taifa limekua kutoka shilingi trilioni 10.7 March 2011 mpaka shilingi trilioni 2.00 mwaka 2012. Kuna aina kuu mbili ya Deni la Taifa, lile la ndani na lile la nje. Kati ya March 2011 na March 2012 Deni la Taifa la ndani lilikuwa kwa asilimia 10.5. Nafikiri kuwa na deni ni jambo lisiloepukika na si jambo baya kutegemea na aina ya deni linatumikaje na matokeo yake na sio tu kuhimilika kwa deni. Kukua kwa deni la ndani naona ni hatari kwani kama tunataka kuendeleza sekta binafsi katika uwekezaji hawataweza kupata mikopo kwa haraka na pia uwezekano na kuwa na riba kubwa. Katika mwaka huu, Serikali inakusudia kukopa shilingi trioni 1.6 kutoka soko la ndani kati ya hizo shilingi bilioni 483.9 sawa na asilimia moja ya pato la Taifa, ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kiasi cha shilingi 1.48 tirioni kwa ajili ya kulipia hati fungani za Serikali na dhamana za Serikali. Hapa ina maana kuwa fedha zinazotumika kwa maendeleo za mkopo ni ndogo ukifananisha na za dhamana. Kuna haja kuangalia kwa uangalifu suala la dhamana za Serikali ili kutozidi kuongeza deni, pale wale wanaopewa dhamana kushindwa kulipa deni lao.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Naibu Mawaziri na Watendaji

wote walio chini yao kwa mawasilisho mazuri waliyofanya hapa Bungeni. Bajeti hii itapita *inshaallah* na nasema tangu awali kuwa naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Sera ya ubinafsishaji. Wapo wanasiasa wengi, wakiwamo Waheshimiwa Wabunge wanaoikejeli sera hii wakisema haina faida kwa Taifa, hivyo ifutwe. Nilifurahishwa sana na majibu ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Janet Mbene, aliyoyatoa hapa Bungeni, nami naongeza yafuatayo:-

Kama ubinafsishaji haufai ina maana kinachofaa ni utaifishaji ili sasa Serikali ijiingize kwenye uzalishaji na usambazaji (biashara) wa bidhaa na huduma. Lakini kama Taifa tukumbuke kuwa kilichotusababisha tubinafsishe mashirika na viwanda vya umma ni kushindwa kwa utaifishaji uliofanyika kuanzia 1967 hadi 1973. Uzoefu umeonyesha kuwa Serikali haiwezi kuzalisha na kusambaza bidhaa na huduma huku pia ikitimiza jukumu lake nambari wani la kutawala. Kuyalundika majukumu haya kwa Serikali ndiko kulisababisha mashirika na viwanda vya umma kuzorota kama siyo kufa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano viwanda 74 vilivyokuwepo wakati huo, vilionesha kuzorota kwa kiwango kikubwa. Bidhaa ziliadimika madukani na misururu ya watu ilikuwa ya kawaida pale bidhaa kama sabuni au sukari ilipopatikana, waliokuwa na shughuli muhimu kama harusi waliwajibika kupeleka

maombi *breweries* angalau mwezi mmoja kabla ya shughuli yenyewe ili kupata katoni chache za bia. Enzi hizo ukitaka kujenga, lazima ujenge mahusiano na mfanyakazi wa kiwanda cha simenti ili upate mifuko michache ya simenti. Uhaba huu wa bidhaa ulichochea vitendo vya rushwa, jambo lililosababisha Serikali kuanzisha Taasisi ya Kupambana na Rushwa mwaka 1973. Viwanda kama *Southern Paper Mills Limited* vilisitisha uzalishaji wa karatasi na kukawa na tishio la kemikali kutoboa makontena na kutitirika kwenye Bonde la Mto Rufiji na kuleta maafa makubwa kwa binadamu na bioanuai wengine.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo hali iliyokuwepo mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990. Ndiyo hali iliyolifanya Taifa liamue kubinafsisha viwanda hivi ili kuongeza mitaji, kuboresha menejimenti, kuingiza teknolojia mpya na kuongeza ajira. Isitoshe ufufuaji wa viwanda ungeongeza mapato ya Serikali na kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuingiza bidhaa hizo nje. Matokeo ya kubinafsisha uzalishaji na utoaji huduma yako wazi. Leo hii simenti inapatikana, bia sigara, sukari, karatasi na kadhalika. Leo hii kwa sababu ya ubinafsishaji, mapato ya *TRA* yameongezeka kutokea shilingi 27 bilioni kwa mwezi hadi shilingi 600 bilioni kwa mwezi, ambalo ni ongezeko la zaidi ya mara 22; ajira zimeongezeka. Nikitolea mfano sekta ya viwanda, kati ya viwanda hivyo 74 vilivyobinafsishwa, 42 vimekidhi viwango na kuzidi yaani makubaliano kati ya *PSRC* na viwanda hivyo yalikuwa, viwanda hivyo viongeze uzalishaji hadi viwango fulani. Leo hii viwanda hivyo 42 vimeshavuka viwango hivyo, haya si mafanikio ya kubeza. Kama

wanafunzi 42 kati ya 74 wanapata *divison one,* wazazi hupongeza utawala wa shule badala ya kudai shule ifungwe.

Mheshimiwa Spika, viwanda 17 vinasuasua yaani havijafikia viwango vya makubaliano japo vinazalisha. Sababu kubwa ni mbili; upatikanaji wa malighafi umekuwa na shida mfano kiwanda cha viberiti moshi (*Kibo Match*) kinasuasua kwa kukosa chanzo cha kuaminika cha miti husika na pia masoko kubadilika mfano viwanda vilivyokuwa vinazalisha bidhaa za katani vina changamoto kubwa baada ya walaji *(consumers)* kupendelea zaidi bidhaa zitokanazo na *jute, synthetic fibres* na *nylon*.

Mheshimiwa Spika, viwanda 15 vimekufa kabisa kwa sababu mbalimbali hasa aina ya ubinafsishaji uliofanyika ambapo vingi ya viwanda hivi vilibinafsishwa kwa mtindo wa *Management Employees Buy Out (MEBO).* Mtindo huu haukuongeza mtaji, haukubadili menejimenti na wala haukuleta teknolojia mpya. Jitihada zinafanywa na mrithi wa *PSRC* (ambaye ni *CHC*) ili kurekebisha kasoro hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi basi, sera ya ubinafsishaji ni nzuri na pale ambapo utekelezaji wake unafanyika vizuri, mafanikio ni makubwa, pale ambako utekelezaji haukufanyika vizuri, dawa siyo kutaifisha viwanda na makampuni bali dawa ni kurekebisha kasoro za utekelezaji. Wanaosema sera ya ubinafsishaji imefeli watambue kuwa tukiachana na ubinafsishaji itabidi wenye daladala wote wanyang'anywe hiyo biashara *UDA* irejee kazini. Wafanyabiashara wa

kariakoo itabidi waondolewe *RTC* irudi kazini. Viwanda vya sukari virejeshwe Serikalini foleni za sukari zianze. *Precision Air* wafukuzwe, tutegemee Air Tanzania kwa safari za ndege. Wanaopinga ubinafsishaji watueleze ni shirika lipi ambalo linaendeshwa na Serikali lenye ufanisi? Ni *Air Tanzania*? Ni *TRL*? Ni *TAZARA*? Pengine Bandari (*TPA)*? Kama haya yote yanasuasua, ni kwa vigezo vipi wanapendelea turejee kwenye utaifishaji?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia kuwa Tanzania ni mwanachama wa *Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA)* inayokataza kutaifisha mali zilizowekezwa na raia wa nchi nyingine ndani ya nchi mwanachama. Wabunge wanatuambia tutaifishe viwanda na migodi ya wageni halafu nchi yetu itaonekanaje machoni pa mataifa? La maana hapa, ni Serikali kuhakikisha kuwa uwekezaji unakuwa wa tija kwa Taifa na siyo kuwafukuza wawekezaji wa nje kwa kutaifisha mali zao.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi, ni kuwajengea Watanzania wapende ku-*save* badala ya kutumia sana mali zao kwa sherehe na walio-*save,* watumie fedha yao kuzalisha bidhaa badala ya kuuza bidhaa za nchi nyingine. Tujenge mazingira ya wao kuzalisha badala ya kuuza vya wengine. Kwa hiyo, suala la *incentives* kwa wenye viwanda vya ndani na *import duties* ziongezwe kwa bidhaa zinazotoka nje na kushindana na bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake wawili kwa kuteuliwa na Rais kushika nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kuchangia, kila mwaka tunashindwa kutekeleza bajeti yetu kiuhalisia wake kwa sababu zil zile za matatizo ya uchumi duniani, kushuka kwa thamani ya shilingi ya nchi, ukame na mengineyo kila mwaka ni hayohayo. Naishauri Serikali itafute njia za kudumu za kuyakabili matatizo hayo, wananchi wanateseka, wanakufa na kudhalilika. Kwa hiyo, Serikali lazima itafute mbinu za kudumu ili visingizio vya matatizo hayo vipungue au kuondolewa kabisa. Bajeti kimaandishi na uwasilishwaji ni mzuri lakini mara zote tunakuwa na matatizo ya utekelezaji. Kwa hiyo, tatizo kubwa ni utekelezaji wa yale tunayoyapanga na tukitoka hapa Serikali na watendaji wake wanafanya wanavyopenda.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa *'Cigars',* napendekeza uondolewe kabisa kwa kuwa wanaovuta *Cigar* Tanzania hawafikii hata watu kumi. Kwa hiyo, sioni kama hapo patakuwa na mapato au labda Waziri atuambie kwa mwaka Tanzania tunakusanya kiasi gani kutokana na sigara hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napendekeza kwenye utaratibu wa kumiliki usajili wa namba za magari zenye utambulisho wa taarifa za mtu binafsi kwenye gari lake kwa ada ya shilingi 5,000,000/= kwa miaka mitatu, ada hiyo ipungue kwa kuzingatia *theory* ya kiuchumi ya '*Economic of Scale'* kwa maana kuwa tuweke ushuru

mdogo ambao atawavutia na kuwafanya watu wengi kupenda na kujiunga na huduma hiyo na hivyo waweze kukusanya pesa nyingi zaidi. Kiwango cha shilingi 5,000,000/= itakuwa ni Watanzania wachache wataitumia huduma hiyo na pia kitakachokusanywa kitakuwa kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti na mapendekezo ya vima vya ushuru, sekta ya madini bado itakuwa tumeigusa kwa kidogo sana. Nchi yoyote itatakiwa kutumia rasilimali zake katika kuboresha mapato yake ya ndani, sisi Tanzania ni kwa nini tunasuasua na kuogopa kutoza ushuru wa juu kutoka katika utajiri wetu wa madini tulionao. Naomba na napendekeza Serikali iangalie upya mchango wa sekta ya madini katika kuweka pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia, ahsante.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumu kwa kuwakilisha hotuba yake kwa umakini mkubwa. Aidha, nawapongeza Manaibu Waziri, Makatibu wakuu na wote waliohusika kwa kutayarisha bajeti nzuri. Hata hivyo, nina ushauri ufuatao kuhusiana na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika**,** kwanza, bajeti ya kilimo ipewe kipaumbele kwa kuongezewa bajeti na kuongeza tija ili hatimaye kupunguza mfumko wa bei, kuongeza ajira na usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani hususani kwenye makampuni ya madini na mashirika ya kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwabana wakwepaji wa kulipa kodi, iangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa kuwa sekta ya usafirishaji na uchukuzi imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1,382.9 kwa mgawanyiko wa; barabara shilingi bilioni 1,000, uchukuzi shilingi bilioni 382.9 tu. Je, Serikali haioni bajeti kubwa ingekwenda kwenye uchukuzi na shilingi bilioni 382.9 zingekwenda kwenye barabara?

Mheshimiwa Spika, nne, nashauri ushuru wa muda wa maongezi *(airtime)* usiongezwe kutoka asililmia 10 hadi 12, badala yake Serikali ikusanye kodi ya uhakika kutoka makampuni ya simu kwa kuhakikisha makampuni haya yanajiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE).*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza kwa kuleta bajeti nzuri ya mwaka 2012/2013 na hususani vipaumbele vitano vilivyowekwa kubwa likiwa miundombinu ya barabara, reli na bandari. Aidha, vipaumbele vya nishati na pia rasilimali watu ni muhimu sana katika kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ianze utekelezaji wa kuikarabati reli ya kati ili ifanye kazi vizuri na kuweza kuchangia kukuza uchumi wa Taifa. Nchi

jirani za *DRC*, Rwanda, Burundi na Uganda zilitegemea sana reli hii muhimu na bandari zake za Kigoma, Mwanza na Dar es Salaam. Ni aibu kuona kwamba kipaumbele muhimu kama reli kimepuuzwa kwa muda na kuzorotesha uchumi wa nchi yetu. Hasara ya kutozingatia umuhimu wa reli hii na ile ya *TAZARA* na ya Dar es Salaam – Tanga, Arusha, ni uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu ya barabara na kupelekea gharama kubwa ya matengenezo ya barabara nchini. Naiomba Serikali ijenge barabara ya Itigi - Mbeya kwa kiwango cha lami ili kukuza uchumi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwekeze zaidi katika kumaliza tatizo sugu la nishati ya umeme ili kunusuru uchumi wa Taifa. Uhakika wa uzalishaji bidhaa hivi sasa haupo kutokana na tatizo la umeme. Aidha, Serikali ihamasishe ujenzi wa bomba la gesi kuja Dar es Salaam kunusuru viwanda.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato uimarishwe zaidi kuliko huu wa sasa kwa kupanua wigo wa vyanzo vya mapato. Naipongeza Serikali kwenye bajeti hii imepanua wigo wa vyanzo vya mapato. Serikali ione uwezekano wa kupata mapato kutoka kwa mwananchi anayepata mapato, misamaha yote ya ushuru iangaliwe upya ili kuziba mianya ya ukwepaji ushuru. Eneo la madini linapoteza kwa kiasi kikubwa mapato ya sekta hii, hakuna kificho kuwa sekta hii inahujumiwa sana kwa wawekezaji kutokuwa waaminifu na kupora madini yetu *at the expense of our nation*. Serikali inapata kiduchu ingawa inasemwa

kwamba sekta hii ni kati ya sekta zinazoongoza katika kuliingizia Taifa mapato.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu kumegundulika madini muhimu ya *uranium* (urani). Nitapenda kujua mipango ya Serikali imeandaliwa vipi katika uchimbaji wa madini hayo na je, wananchi wangu watanufaika vipi? Tanzania inataka kufanana na Nigeria nchi tajiri lakini mafuta yake hayanufaishi wananchi wake. Hali kadhalika nchi hii inashindwa kutumia fursa ya utajiri wake kuwaletea wananchi wake maendeleo ya haraka. Mfano mzuri wa nchi inayotumia vizuri rasilimali zake za madini ni nchi ya Botswana ambayo imeweza kuinuka kiuchumi na kuwa nchi yenye uchumi wa kati sawa na Uturuki na Mexico hivyo kuinua pato lake la Taifa. Mara baada ya uhuru mwaka 1968, Botswana ilianza na *GDP capital income* ya dola 70, leo hii *GDP/capital income* ni dola 14,000. Mipango mizuri na uadilifu imeifikisha Botswana hatua hiyo muhimu kiuchumi pamoja na kwamba sehemu kubwa ya nchi ni jangwa. Tanzania ni nchi tajiri zaidi lakini tumeshindwa kutumia fursa tulizopewa na Mwenyezi Mungu pamoja na mipango mizuri lakini utekelezaji wake unakwamishwa na watendaji wasio waaminifu na wanaoshirikiana na wageni na mafisadi kuiba na kupora rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu lina mbuga za hifadhi (Akiba) za Rungwa, Mhesi na Kizigho na kwa mwaka mbuga hizi zinachangia takribani shilingi bilioni mbili kwa mwezi kwenye mapato Hazina. Lakini Idara ya Wanyamapori inailipa Wilaya ya Manyoni kiasi kidogo tu cha shilingi milioni 200 kwa mwezi. Zote

shilingi 1.8 bilioni zinapelekwa maeneo mengine na kuwaacha wananchi wa eneo husika katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iunde haraka Mamlaka ya Mbuga za Wanyamapori na Bodi yake iweze kusimamia vyema mbuga hizi za Selous, Rungwa na kadhalika ili rasilimali zitumike kwa manufaa ya watu wake.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu *Carbon Trading*, kwa vile nchi zinazosababisha uchafuzi wa mazingira duniani takribani asilimia 80 ni China, USA, Australia na nchi nyingine na asilimia 20 ni kutoka nchi zinazoendelea, ni kwa nini hali ya utekelezaji wa uamuzi wa *Kyoto-Japan (Kyoto Protocol 1991)* kuwa nchi hizo tajiri duniani zichangie kuboresha mazingira katika nchi zinazoendelea. Je, pia Tanzania tunao mpango wa kuboresha kupitia *Carbon Trading*?

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi, kwa vile nchi yetu imefanyiwa upimaji kwa asilimia moja tu, kwa nini Wizara ya Ardhi imepewa fedha kidogo na hakuna mpango wa haraka wa kuondoa migogoro ya ardhi iliyokithiri. Pia upimaji wa ardhi utarahisisha wananchi kupata fursa ya kuwekeza, kukopa na kufanya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali imekuwa kimya kwa ajili ya maslahi ya Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji? Hawa ndiyo wasimamiaji wakuu wa maendeleo katika ngazi ya jamii. Suala hili mwaka jana Serikali iliahidi.

Mheshimiwa Spika, kilimo, utaratibu wa pembejeo ni vizuri utazamwe upya kwa sababu ya udhaifu mkubwa uliopo mfano wananchi wengi hawana fedha ya kuwatosha hata kujikimu lakini wanapelekewa pembejeo kwa shilingi 141,000/= kwa ajili ya mbegu (mahindi), mbolea ya kupandia, kukuzia na unyunyuziaji. Wananchi wanasainishwa kupokea pembejeo zote kumbe ni mbegu peke yake na ushahidi uliopo unaonyesha kuwa upo udhaifu mkubwa na upoteaji mkubwa wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, umeme *(Generation-mix Hybrid),* upatikanaji wa umeme wa uhakika ufanyiwe kazi kikamilifu na siyo kutegemea chanzo kutoka sehemu moja, ni vizuri vyanzo vingine kupitia mwanga wa jua, upepo, gesi, taka mbalimbali na makaa ya mawe vikatumika! Mfano Mkoa wa Mara hususan Serengeti kuna chanzo kikubwa sana cha gesi na maji ya moto. *Tanzania Oxygen* walionyesha nia kwa kuchukua eneo hilo la majimoto kwa ajili ya kuanzisha wingi wa gesi na kutoa umeme *(Geo-Thermal)* lakini hakuna kinachoendelea. Naishauri *'TOL'* wawalipe fidia wananchi wa Majimoto – Serengeti kwa kuwanyang'anya eneo lao bila kuliendeleza tangu mwaka 1992? Ni vyema chanzo hiki na vingine katika Mkoa wa Mara kama vile Nyekunguru na Kogaja - Panyakoo viendelezwe na kuzalisha umeme ili waingize katika "*grid*" ya Taifa na Serikali kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato, hali ya ukusanyaji wa mapato yako chini mno hasa kutokana na utaratibu wa *'self assessment',* hii inachangia sana

kutoa makadirio ya chini, pia kwa kushirikiana na watumishi wa *TRA* walio dhaifu kwa kuchukua rushwa. Kenya *(KRA)* wanakusanya mara 30 ya *TRA* inavyokusanya ndiyo sababu bajeti ya Kenya ya mwaka 2012/2013 ni shilingi tirioni 26, Uganda mwaka 2012/2013 ni shilingi tirioni 10, Tanzania kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi trilioni 15. Mkazo zaidi uwekwe kukusanya kodi, maoteo ni chini ndiyo sababu *TRA* imefikia asilimia 105.

Mheshimiwa Spika, Wachina wafuatiliwe kwa ukwepaji mkubwa wa ushuru na wasifanye umachinga na bidhaa zao nyingi ni feki.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kama hakuna nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na ukusanyaji wa mapato bado maendeleo katika nchi hii itakuwa ni ndoto. Kumekuwepo na matumizi makubwa yasiyo na maelezo ya kutosheleza ya matumizi ya fedha zaidi ya shilingi trilioni moja ambazo hazikuidhinishwa na Bunge jambo hili kama litaachiwa liendelee linahatarisha mipango ya maendeleo ambayo imeidhinishwa na Bunge. Ipo haja sasa Bunge kuweka ukomo wa matumizi ya fedha ya mfuko mkuu wa nchi na zaidi ya kiwango kitakachoidhinishwa iwe ni lazima kuwasilisha maombi hayo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, aidha, ipo haja sasa ya kuangalia upya Sheria ya Ukaguzi *(National Audit Act)* ili impe *CAG* mamlaka ya kupeleka moja kwa moja dosari ambazo ana mashaka ni ya kijinai kupeleka Mahakamani badala ya kuleta ripoti na kuiachia TAKUKURU, kwanza kutapunguza urasimu na

kuwezesha hatua kuchukuliwa kwa wakati. Hii itasaidia kuwepo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa bidhaa *(VAT)* kwa muda wa maongezi hadi asilimia 12 toka asilimia 10 ili kuoanisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki, ni kuwaongezea mzigo Watanzania maskini bila kujali hali za kiuchumi wa nchi zetu na uimara wa sarafu yetu ambayo inatetereka kila kukicha na hakuna jitahada za lazima na makusudi za kuinusuru sarafu yetu ili iwe na nguvu na usawa na sarafu nyingine za nchi za Afrika Mashariki kama ilivyokuwa wakati wa *EAC* kabla ya kuvunjika kwake.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa bidhaa kwa vinywaji baridi, ni kuwafanya sasa watoto, hata watu wengine wasitumie tena soda na kukifanya sasa kinywaji hiki kuwa cha watoto wa matajiri tu, haiwezekani. Leo soda kabla ya marekebisho haya Mpanda inauzwa kwa shilingi 700, kwa maana hiyo sasa Mpanda itauzwa kwa shilinig 1000/= au zaidi kwa chupa. Ninachoamini ni kwamba sasa uzalishaji utapungua na pengine hata makusanyo ya kodi kutokana na eneo hili yatapungua.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kuchelewa kupeleka fedha za maendeleo katika Wizara na Halmashauri zetu, hali hii imejitokeza kwa kujirudiarudia kwa miaka kadhaa mfululizo na hakuna hatua madhubuti ya kurekebisha dosari hii hadi sasa fedha za maendeleo hazikufika katika Halmashauri zetu kwa asilimia 100 na kwa wakati. Ni vyema sasa Wizara ikatazama tatizo ni nini. Wakati mwingine fedha yote

inapelekwa mwezi wa mwisho wa mwaka wa fedha *(June),* hili nalo linahitahji maelezo kwa nini hali hii inajirudia.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri ni pungufu ya mahitaji halisi ya Halmashauri zetu. Ili kukuza uchumi wa nchi hii, ni lazima tuweke mkazo katika kuimarisha uchumi vijijini na mojawapo ni kuwa na barabara za uhakika vijijini *(feeder roads).* Ni vyema sasa kuangalia eneo hilo kwa umuhimu unaostahili kwa kuwekeza katika barabara za vijijini kwa kuziongezea uwezo Halmashauri zetu kwa kuwapa fedha za kutosha. Fedha za Mfuko wa Barabara, nazo zifikishwe katika kipindi muafaka ili kazi za ujenzi wa barabara ziweze kufanyika badala ya kutuma fedha wakati wa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa linakuwa na kuongezeka pia deni la ndani kwa kutolipa malimbikizo ya madai ya watumishi. Hii ni aibu kwa Taifa kushindwa kulipa malimbikizo haya, jitahada za makusudi zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa uchumi katika tarakimu kunaonesha unakuwa kwa viwango tofauti mwaka hadi mwaka kama inavyosomeka katika hotuba ya Waziri lakini kukua uchumi hakuna mahusiano na hali ya umaskini wa watu. Ni vyema kukua huku kuonekane kwa kupunguza umaskini wa wananchi ndipo wataelewa dhana ya kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, mwisho tujitazame upya katika mfumo wetu wa kuandaa bajeti kwa kuzingatia ushirikishaji na muda wa kuiandaa bajeti vyema kuliko hivi sasa bajeti inakuwa kama jambo la utamaduni tu. Ifikapo Februari kila mwaka, Bunge lipitie mwelekeo wa bajeti na kuishauri Serikali mapema tofauti na ilivyo sasa tunalipua tu bora liende, hatuitendei haki nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kuhusu makadiro ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013 na mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa ni kubwa mno, limeongezeka kufikia shilingi bilioni 20.276.6 katika kipindi kinachoishia March 2012 kutoka shilingi bilioni 17,578.9 Marchi 2011. Serikali ijitahidi kutumia rasilimali zilizopo vizuri na ijitahidi kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, posho na chai maofisini inaweza kupunguzwa. Vyanzo vingine vya mapato vibuniwe na wananchi wahimizwe kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kujikomboa kutokana na umaskini huu uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa kodi pia usimamiwe vizuri ili wale wote wanaotakiwa kulipa kodi waweze kulipa viwango sahihi vinavyostahili bila kuipunja Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua fursa ya ajira na hasa kwa vijana, nashauiri Serikali ipanue huduma za fedha kwa kutenga fedha na kuanzisha benki ya vijana, ili vijana waweze kuwa na chombo chao cha kifedha ili wanapojiunga katika *SACCOS* zao waweze kukopesheka na kufanya shughuli zao za kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, ili kuwaandaa vijana kujiajiri, natoa ushauri kwamba masomo ya ufundi yafundishwe tangu shule za msingi ili wanafunzi wajijengee mtazamo wa kujiajiri pindi wamalizapo masomo badala ya mtazamo uliopo sasa hivi wa kuajiriwa na kupata kazi za ofisini. Hii itasaidia sana kuinua uchumi wa nchi yetu kwa vijana kujiajiri na kuzalisha kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho natoa ushauri kwamba dhana ya Kilimo Kwanza iimarishwe na wananchi wahimizwe kutumia ardhi kwa kilimo cha kisasa na cha kibiashara. Nchi yetu imejaliwa kuwa na hekta milioni 44 za ardhi inayofaa kwa kilimo lakini ni asilimia 23 tu ndiyo inayotumika. Kuna hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na maji ya kutosha yapo lakini ni asilimia moja tu iliyo chini ya umwagiliaji. Napendekeza Serikali ione umuhimu wa kuweka kipaumbele katika matumizi ya ardhi ya kilimo cha kisasa na cha kibiashara ili wananchi walio wengi asilimia 80 waishio vijijini waweze kujikomboa na kujionda katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa (MB) kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Fedha. Hotuba hii ya *budget*, Serikali imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa katika sekta mbalimbali za kilimo, viwanda, ajira, umeme, barabara, bandari, reli na kadhalika kwa lengo la kukuza uchumi wa Taifa, kupunguza uhaba wa chakula, kupambana na mfumko wa bei na kadhalika. Mimi naunga mkono *budget* hii asilimia 100 lakini mashaka yangu mimi ni kwenye utendaji na utekelezaji wa haya yaliyopangwa. Upungufu uliojitokeza katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, si vyema ukajitokeza tena katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, tumeshaona kwamba kilimo kinaajiri asilimia 75 ya Watanzania wote na kinachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa. Ushauri wangu, Wizara ya Kilimo itengewe *budget* ya kutosha na hasa kwenye ruzuku ya pembejeo. Sekta ya kilimo inagusa maeneo mengi na inawagusa Watanzania wengi, sasa ruzuku ya pembejeo zinapokuwa hazitoshi au haziwafikii wakulima kwa wakati na pembejeo nyingine zinafika zime-*expire* na wakati huohuo wakulima tayari wameshaandaa mashamba yao, huku ni kuwakwaza wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mkoa wa Mtwara na Lindi tulipata shida ya kupata *sulphur* na matokeo yake, uzalishaji wa zao la korosho ulipungua ukilinganisha na mwaka 2010. Mwaka huu sasa tatizo ni lilelile *its even more worse*, wakulima mpaka sasa

hawana pembejeo aina ya *sulphur* na msimu wa kupulizia mikorosho ndiyo huu. Wakulima wanahangaika kutafuta *sulphur* ya ruzuku ya shilinigi 10,000/= haipo na badala yake *sulphur* iliyoko ni kwa wafanyabiashara wa kawaida ambayo inauzwa shilingi 35,000/= kwa mfuko, wakulima wangapi wanaweza kununua mfuko wa *sulphur* kwa bei ya shilingi 35,000/=? Katika hali ya namna hii, tunategemea nini kwenye mavuno ya mwaka huu? Namwomba Waziri wa Kilimo na Chakula achukue hatua za haraka za kuhakikisha kwamba *sulphur* inawafikia wakulima wa korosho wote katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda na ajira kwa vijana, Serikali imeonesha nia njema kabisa katika maeneo mbalimbali katika *budget* hii ya mwaka 2012/2013 ya kuwapatia vijana ajira za kutosha. Mkoa wa Mtwara na Lindi una viwanda vingi sana vya kubangua korosho ambavyo kwa sasa vimeuzwa na kuishia kufanywa magodauni na mahali pa kufanyia minada ya korosho. Wakati viwanda hivi vimeanza kufanya kazi katika miaka ya 1978/1979, vilichukuwa idadi kubwa sana ya wafanyakazi karibu Wilaya zote za Mtwara na Lindi, nina uhakika viwanda hivi vilipunguza uhaba wa ajira katika Mikoa hiyo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, rai yangu, naiomba Serikali iangalie viwanda hivi vyote kwa upya ama Serikali ivichukue ama iwasimamie wamiliki wa viwanda hivi sasa vibangue korosho na sio kuvifanya viwanda hivi magodauni na magulio. Kwa kufanya hivyo, Serikali

itakuwa imeongeza ajira kwa vijana wetu na pili thamani ya zao la korosho itakuwa imeongezeka kwani hatutakuwa tunauza *raw material* kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, vijana wa bodaboda, mimi nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuwapunguzia kodi vijana hawa, mara ya mwisho nilipokuwa Jimboni niliwaita vijana wa bodaboda wapatao 80, nikakaa nao, vijana wale waliyoyaomba kwangu pamoja na mambo mengine waliomba niwafikishie kilio chao kuhusu kupunguziwa kodi pamoja na adha nyingine mbalimbali. Vijana hawa nakumbuka mpaka *statement* yao ya masikitiko waliyoitoa, kijana mmoja alisimama na kusema, Mheshimwa tunaomba mtusaidie, mtusimamie, hatupendi kurudi katika kazi zetu za mwanzo. Unaweza kuelewa *statement* hii ilikuwa na maana gani. Sekta hii ya bodaboda imeongeza ajra kwa vijana wetu, kwa kiasi kikubwa vijana ambao zamani walikuwa hawana kazi sasa wana kazi, wazururaji sasa wana kazi, wezi sasa wana kazi, vibaka sasa wana kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kuishukuru tena Serikali kwa ajili ya vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt.William Mgimwa, Waziri wa Fedha pamoja na wataalamu wake kwa jinsi walivyoiandaa bajeti hii ya mwaka 2012/2013 kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, bado bajeti hii ina maeneo ambayo yanatakiwa kuangaliwa kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni eneo la umeme ambao ni mhimili muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na Serikali kuweka suala la umeme katika vipaumbele, bado Serikali haijaonyesha nia ya dhati ya kutaka kutatua tatizo hili ambalo lilisababisha Serikali kutopata mapato makubwa kwa mwaka wa fedha uliopita. Serikali kama ina nia ya kweli ya kutatua tatizo la umeme, ielekeze nguvu zake pia kwenye umeme wa kutumia makaa ya mawe ambao ndiyo rahisi kuliko vyanzo karibu vyote vya umeme. Ndani ya mwaka mmoja, Serikali ingeweza kupata *mgt 120* kutoka Ngaka kama ingeamua kwa dhati kutoa shilingi bilioni 70 tu kwa ajili ya kujenga *transimission line* kutoka Makambako mpaka Songea ambao *mgt 40* zingetumika katika Mkoa wa Ruvuma na *mgt 80* zingepelekwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali inapaswa kuliangalia, ni suala la viwanda na haswa *SIDO* ambayo inaweza kutambaa nchi nzima na ingeweza kutoa ajira kwa vijana wetu ambao ni bomu kubwa. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo inaweza kuendelea kama haijaamua kwa dhati kuwekeza katika eneo la viwanda, lakini Serikali yetu bado haijaamua. Naishauri Serikali iliangalie eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika hotuba ya Waziri Serikali inakusudia kupunguza mfumko wa bei pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi yetu. Pamoja na maelekezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Serikalli haijaonesha nia ya dhati katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali idhibiti matumizi ya fedha za kigeni hapa nchini haswa matumizi ya *dollarization.* Katika nchi nyingi duniani, zinaheshimu matumizi ya fedha zao, pale unapofikia uwanja wa ndege tu matumizi ya fedha ya nchi mama ndiyo yanapoanza kuchukua mkondo wake lakini kwa nchi yetu hili halipo. Lingefanyika lingeiongezea kipato kwa maana ya biashara pia ajira kwa Watanzania na mwisho kulinda thamani ya pesa yetu. Namtaka Mheshimiwa Waziri anieleze mkakati gani Serikali imeweka katika kuondoa matumizi ya *dollarization*.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali inapasa kuliangalia, ni eneo la kodi haswa pale kodi inapoelekezwa kutozwa kwa bidha za nje kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani. Kwa kawaida na utaratibu uliopo duniani ni kuwa, kila nchi inapenda kulinda viwanda vyake vya ndani lakini kwa Tanzania hilo halipo. Mfano, pale Serikali inapoamua kuongeza Kodi ya Thamani ya *(VAT)* kwa bidhaa za nguo na kuifanya nguo inayozalishwa hapa nchini kuwa bei juu kulinganisha na nguo zinazotoka nje ya Tanzania. Ikumbukwe Tanzania kulikuwa na viwanda 21 vya nguo na sasa tumebakia na viwanda vinne tu. Hapa hakuna ushindani halali matokeo yake tunazidi kuuwa zao la pamba na hatimaye kuwafanya wakulima wetu wa pamba kupata shida ya kuuza pamba yao. Ushauri

wangu Serikali ifute Kodi ya Thamani kwa bidhaa zote zinazozalishwa hapa nchini ili kuwafanya wazawa na *(investor)* wawekezaji wote wenye nia ya kutaka kuwekeza katika zao hili wawekeze.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninashauri Serikali ni mgawanyiko wa rasilimali. Kuna baadhi ya maeneo yanaonekana kupendelewa na kupewa vipaumbele vya kwanza kuliko maeneo mengine. Naishauri Serikali kuwa na uwiano wa mgawanyo wa rasilimali ili kila eneo liweze kupata maendeleo yanayolingana, kuliko kuona baadhi ya Mikoa, Wilaya na Miji, ina maendeleo makubwa kuliko mengine na bado bajeti kubwa inaendelea kuelekezwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuvisaidia viwanda vya ndani, Serikali inapaswa pia kuangalia upya kodi za malighafi zinazoagizwa na hivyo viwanda. Hii itasaidia kuvifanya viwanda viweze kuzalisha bidhaa kwa bei ndogo na kuwa na uwezo wa kushindana na bidhaa kutoka nje, viwanda kama vya sabuni, mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema. Pia nachukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimwa Waziri, kwa kuchaguliwa kwake kuiongoza Wizara ya Fedha pamoja na wasaidizi wake, nawatakia utendaji mwema wa kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika bajeti hususani kwenye eneo la kusamehe ushuru. Nchi yetu ili ipate mapato ya kutosha tunahitaji tukusanye kodi kwa wingi na tumeona kuwa kodi ambayo tunakusanya bado haitoshelezi. Katika kusamehe kodi, Serikali inatakiwa iwe makini sana katika kusamehe kodi kwani wafanyabiashara wengi wamekuwa wakikwepa kodi. Kumekuwa na ukusanyaji wa kodi ambao sio waaminifu na kupelekea kuingizia hasara Serikali. Namwomba Mheshimiwa Waziri kama tuna nia ya dhati ya kujenga nchi yetu basi afanye marekebisho *TRA* huko ndiko kunakovuja mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nijikite katika matumizi ya Serikali, matumizi ya Serikali yaangaliwe vizuri. Tunakubali kuwa kuna matumizi ya lazima katika Serikali pia kuna matumizi siyo la lazima, yale ambayo siyo ya lazima tungeomba matumizi hayo yapunguzwe ili fungu hilo lipelekwe kwenye fungu la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, napenda nipongeze Wizara ya Fedha kwa kuandaa bajeti nzuri japo ina upungufu madogomadogo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa juu ya kodi za magari ambayo yana umri mkubwa kuongezwa ushuru, kwa kuwa watumishi wa Serikali kwa ngazi ya Madaktari na Walimu pamoja na wanafunzi wanaosoma nchi za nje hawana uwezo wa

kununua magari mapya. Naomba Serikali iangalie upandaji wa ushuru huu vizuri kwa kuwasaidia wananchi wenye kipato kidogo. Pamoja na yote kuzungumzwa lakini bado tuangalie mizigo inayotoka bandarini pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uvujaji wa mapato kutokana na wafanyakazi wasio na uaminifu. Serikali sasa iangalie vyanzo vya mapato vingine tofauti na kupandisha bei za soda. Soda kwa mwananchi wa kipato cha chini inawasaidia watoto wanapoumwa (malaria) mtoto anakataa kula lakini anaweza akatamani *fanta orange* kwa kuona.

Mheshimiwa Spika, kwa wakazi wa mijini, wajasiriamali, wafanyakazi, wanafunzi hawana tank za *fresh water*, wananunua maji ya kunywa, ni vyema pia Serikali ikaangalia upya bei za maji.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na wenzangu nisingependa kurudia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wote waliohusika kuandaa kwa aina yoyote bajeti hii ya mwaka 2012/2013. Vilevile nampongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake wote wawili, pamoja na ugeni walionao katika Wizara hii, lakini kwa kipindi kifupi wameweza kuonesha matumaini kwa Watanzania kutokana na mikakati mingi waliyoitangaza katika kuweka hali ya uchumi wa

nchi vizuri pamoja na uchumi wa wananchi, kwa kuwapunguzia mizigo ya hali mbaya ya kiuchumi na hasa mfumko wa bei za vyakula na vitu mbalimbali ambao unalikabili Taifa letu kwa kiwango kikubwa na kuwa kero isiyo na tiba kwa muda mrefu na kuwaondolea wananchi wa hali ya chini matumaini mengi, nitayazungumza kwa kuongea lakini nitachangia kidogo kuhusu vyanzo vya mapato vya nchi. Maana bila kodi ina maana vyote tunavyotaka havitawezekana, itakuwa ni kupiga kelele zisizo na maana, ni wajibu wa wa Mbunge kueleza au kutoa ushauri pale anapoona kuna chanzo cha kupata kodi au kuna upotevu wa kodi ili wigo wa kodi uongezeke na nchi kupata pesa ya kutosha na kuweza kujitegemea na kuondoa kero kwa wananchi na hasa kama fedha hizo zitatumika vizuri bila ufujaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwa leo napenda kutoa ushauri kwa ufupi katika biashara ya mafuta. Nimekuwa nikitoa michango mingi sana na yenye maslahi kwa Taifa, kwa mfano, tangu mwaka 2007 nilizungumza sana kuhusu Serikali kukosa mapato kutokana na tofauti kubwa ya bei za *diesel, petrol* na *kerosene* na niliainisha kiwango cha pesa inayopotea kwa mwezi na mwaka lakini tuliendelea kupoteza fedha hizo hadi 2011 Serikali iliposikia rasmi baada ya kupoteza pesa kwa miaka zaidi ya minne nilipochangia kwa kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, sasa wizi huu umehamia kwenye kodi ya mapato *(Income Tax)* kwa vile hakuna mpango mzuri wa ununuaji wa mafuta katika makampuni makubwa yenye maghala, yaani katika

makampuni yanayouza mafuta kwa vile hakuna utaratibu nani anayefaa kununua mafuta kutoka kwenye makampuni hayo. Kwa sasa kila mtu anaweza kununua mafuta kwa wauzaji hawa wa jumla bila kujua anapeleka wapi pamoja na kuwa mafuta ni hatari bila kujali anaweka au kuhifadhi sehemu gani na ina usalama gani. Hatua hii imesababisha Serikali kukosa mapato ya wazi bila kujali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi kila mwenye gereji ya kutengeneza magari au kuweka magari makubwa utakuta ndani ana *tanks* na *pamp* za kujiwekea mafuta na hata kuwauzia wengine. Hii inasababisha Serikali kukosa kodi kwa vile inakusanya kodi ya mafuta kwa wauzaji wa rejareja ambao ni wenye vituo vya mafuta ambao wao wapo kwa mujibu wa sheria na wana kumbukumbu za uchukuaji mafuta na uuzaji na kuweza kulipa kodi *(income tax)* bila shida. Sasa unaporuhusu kila mtu ajinunulie mafuta na kujiwekea mwenyewe, hamuoni kwamba tayari ameshakwepa kodi *(income tax).* Llazima Serikali iliangalie hili na biashara hii ipitie mlolongo wa kisheria kutoka muuzaji wa jumla kwenda muuzaji wa rejareja *(petrol station)* ili ulipwaji wa kodi uweze kuwa sawa sio kuuza hovyo na kusababisha ukosefu wa mapato ya waziwazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Watendaji wa Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya ya

kuandaa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na baadhi ya hatua ambazo zimependekezwa ambazo utekelezaji wake utafanya kufikiwa malengo ya MKUKUTA, Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hasa katika masuala yahusuyo maendeleo ya jamii hasa wanawake, watoto na vijana.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa mtaji wa Benki ya Wanawake, utaiwezesha Benki kujitanua na hivyo kuwafikia wanawake wengi zaidi hasa walio vijijini. Bado wanawake wengi zaidi hasa walio vijijini hawana *access* na *financial credits*, hivyo uimarishaji wa Benki ya Wanawake utachochea upatikanaji wa mikopo nafuu na ya haraka kwa wanawake wajasiriamali wadogowadogo. Uwezeshaji wa wanawake ambao utabadilisha maisha yao, familia zao na jamii kwa ujumla ni uwezeshwaji katika biashara na elimu. Hivyo, ushauri kwa Wizara ya Fedha ni kuhakikisha kuwa pesa iliyotengwa kwa ajili ya kuimarisha Benki ya Wanawake inatolewa kwa wakati na kama ilivyotajwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, nimefurahishwa sana na mapendekezo ya Serikali ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vitakavyotumika kwa ajili ya gesi ikiwemo vifaa vya kupikia majumbani na majiko yaliyotengenzwa kwa ajili ya matumizi ya gesi pekee. Hatua hii kwa kiasi kikubwa itapunguza mzigo mkubwa wa kazi/majukumu kwa akina

mama/wanawake ambao wanakabiliana nayo kila siku katika kuhudumia familia zao. Kuongezeka kwa matumizi ya majiko ya gesi majumbani hasa vijijini itawezesha wanawake wengi kupata muda zaidi wa kujishughulisha katika shughuli za maendeleo/kujiongezea kipato badala ya kupoteza muda mwingi wa kutafuta kuni za kupikia majumbani.

Hatua hii pia itachochea kufikiwa kwa malengo ya usawa wa elimu kwa watoto wa kike ambao wengi wao ndiyo wanalazimika kusaidia kutafuta kuni kwa ajili ya matumizi ya familia au kutumia muda wao mwingi zaidi kutumia mkaa kwa ajili ya kupika chakula cha familia badala ya kujisomea. Nashauri Serikali iwe na mpango kabambe wa kuhimiza, kuhamasisha matumizi ya gesi kwa ajili ya kupikia majumbani hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuondolewa kwa ushuru wa forodha kwa vyakula vya watoto wachanga. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wa kutoza ushuru wa forodha wa asilimia sufuri ili kuwezesha watoto wachanga na wagonjwa wengi kuweza kupata vyakula vyenye virutubisho kwa bei nafuu. Tanzania inakabiliwa na tatizo kubwa la utapiamlo *(malnutrition)* ambapo asilimia 42 ya watoto wa Tanzania wamedumaa kutokana na kukosa lishe. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha imefanya jambo jema sana

kuanzisha Kitengo cha Manunuzi (PPU). Hiki Kitengo ndiyo kinatoa Sera za Manunuzi ya Umma na pia kinasimamia manunuzi nchi nzima. Kitengo hiki kiimarishwe sana mpaka kiwe na Maafisa wa Kanda. Watasaidia sana kusimamia manunuzi ya umma hasa kwenye Halmashauri. Ili kufanikiwa, Kitengo hiki kisiwe kwenye *Vote 50* ya Wizara, kiwekwe kwenye *Vote* yoyote yenye mtazamo wa Kibajeti na wa Kitaifa, yaani Kitengo hiki kipewe nguvu kama Kitengo cha Ukaguzi kinavyoanzishwa na kupewa nguvu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Randama Namba Tatu inayoonesha Makadirio ya Mikoa, kuna kosa ambalo linahitaji kurekebishwa kwenye Mkoa wa Mbeya. Wilaya ya Chunya ina ukubwa kieneo ambao ni asilimia 46 ya Mkoa wa Mbeya, karibu asilimia 50, lakini ukiona Makadirio ya Wilaya ya mafuta ya magari, utaona Chunya inapata kidogo kuliko Wilaya zote Mikoani. Wilaya yenye eneo kubwa la utawala ndiyo inapata mafuta kidogo! Naomba Serikali irekebishe hii kwa Wananchi wa Chunya.

Mheshimiwa Spika, hali ya maisha kwa Watanzania ni ngumu sana. Mfumko wa bei ni mkubwa mno na umechangiwa zaidi na chakula kwa maana ya sukari na mchele. Pamoja na kuwa sasa ni wakati wa mavuno lakini bei imeshuka kidogo sana. Hii kwa maoni yangu ni sababu majirani zetu wote wanataka chakula toka Tanzania. Naiomba Serikali inaposhughulikia suala hili la mfumko wa bei upande wa chakula, ichukue hatua madhubuti za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Serikali ijue inatatua matatizo ya uhaba wa sukari na mchele, si kwa

Tanzania tu, bali pia Kenya, Zambia, Congo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, miradi ya miundombinu hasa barabara inachangia sana ukuaji wa uchumi. Kwenye bajeti za miaka miwili iliyopita, kuna *"back log"* kubwa sana ya kukamilisha miradi ya barabara na reli. Naiomba Serikali isianze miradi mpya kwenye maeneo haya bali ikamilishe kwanza miradi ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua *"bold"* kabisa kupunguza misamaha ya kodi ili nchi yetu ifanane na majirani zetu katika eneo hilo. Fedha zote zitakazopatikana katika hili ziende kwenye sekta za maendeleo. Serikali isiogope kelele na malalamiko toka kwa wale ambao wananufaika na misamaha kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tumejifunza sana kutokana na nchi ilivyofaidika na madini ya dhahabu na almasi. Waliopata zaidi ni wawekezaji siyo Serikali na wananchi. Sasa tuna gesi, urani na madini mengine, Serikali ichukue hatua madhubuti ya kusomesha wataalam wengi ili nchi ifaidike na madini. Ndiyo maana Mwalimu Nyerere hakutaka nchi ichimbe madini bila kuwa na wataalam wananchi. Pia kuna uwezekano mkubwa sana wa kupata mafuta. Nchi ikiwa na wataalam wake katika maeneo haya na Serikali ikijifunza kwenye nchi ambazo zinafaidi vizuri madini yake, nchi na watu wake wataneemeka na rasilimali hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono *budget* iliyowasilishwa na Waziri kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni nchi inayoendelea. Mahitaji ni mengi na uwezo wa Taifa kifedha ni mdogo, kwa sababu hiyo kubwa, lawama zitakuwa nyingi kulipa pongezi kwa yale mema yaliyofanywa. Mimi naomba nisisitize mambo mawili tu. Kwanza, kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii ili astahili malipo atakayolipwa na pili kila mtu azingatie sheria za nchi. Tuondokane na tabia inayojitokeza baadhi ya Watanzania kudai haki ya kuvunja sheria.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi anayeshughulikia mipango kwa matayarisho na mawasilisho makini ya bajeti ya Serikali, naomba niunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi waone miradi ya maendeleo inatekelezeka huko ilikopangwa, ni lazima kama Taifa tutafute njia mbadala namna ya kulipa madeni ya miradi ambayo mpaka sasa ni mikubwa sana hasa katika ujenzi wa barabara na miradi ya maji. Kwa hiyo, tusipokuwa makini bajeti hii na hasa bajeti ya maendeleo itaishia kulipia sehemu tu ya madeni ya kazi iliyofanyika nyuma na kufanya kutokuwepo fedha za kuendelea na ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya *VAT* ifanyiwe marekebisho ili watu wengi zaidi walipe kodi hii. Watanzania wanaouza kati ya Shs.10m na 20m ni wengi sana kuliko wale wanaozidi 20m. Kwa hiyo, kundi hili la kati linaweza kutuongezea mapato makubwa. Watanzania wengi hawalipi kodi kutokana na sheria hii kutokulenga kundi hilo kubwa na ambalo fedha zao hata benki hawapeleki.

Mheshimiwa Spika, ukienda Ethiopia, ukiagiza chai kwenye mgahawa lazima watakupa risiti yenye kodi ya Serikali. Faini kwa mtu asiyetoa risiti kwa biashara yoyote ni kubwa sana na hivyo kufanya wafanyabiashara kutoa risiti hata kama hujaomba yaani ukimpa fedha tu anakupa risiti, vivyo hivyo nimeona nidhamu ya aina hiyo nchini Angola.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kubadilisha fedha za kigeni ifanyiwe marekebisho ili Benki Kuu idhibiti hifadhi ya fedha ya kigeni. Katika sheria hiyo, mtu asiruhusiwe kuhamisha fedha nchi ya nje au kusafiri na fedha zaidi ya $10,000 pasipokuwa na kibali cha Benki Kuu. Ukienda China ni rahisi kuuza dola kwenye benki au mawakala lakini kununua dola iliyo *ring fenced* unapata Benki ya Taifa tu. Kwa nini nchi hii maskini tusiige mifano hii ili nchi yetu iweze kusonga mbele kimaendeleo?

Mheshimiwa Spika, lazima turejeshe nidhamu ya matumizi ya fedha ya Serikali iliyopangwa, iwe ni kinyume cha sheria kutumia zaidi ya kilichopo kwenye

fungu husika au iwe marufuku kukopa huduma kwa niaba ya Serikali kama fedha haipo.

Mheshimiwa Spika, nimalize hotuba yangu kwa kusema Mpango wa Miaka Mitano hautekelezeki. Kuna tatizo la madeni na miradi mingi kwenye Hamashauri zetu ipo mingine zaidi ya miaka kumi (10) haijakamilika. Mpango ulioletwa haukuzingatia "*commitments*" ambazo zipo kwa miradi isiyokamili kutokana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Sheria inarekebishwa ili kuweka pamoja na mambo mengine, kiwango cha chini cha mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo cha shilingi 3,000,000/= kisichotozwa kodi. Ni hatua nzuri ambayo naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa bahati mbaya sana wafanyabiashara wa pikipiki maarufu kama bodaboda ambao kwa maoni yangu ni wafanyabiashara wadogo, wanakadiriwa kodi kubwa sana, kati ya Shs. 3,000,000/= hadi Shs. 7,500,000/= kwa wenye kumbukumbu na asilimia mbili ya mauzo yanayozidi Shs. 3,000,000/= kwa wafanyabiashara wenye kumbukumbu zinazoridhisha. Angalia jedwali la pili, ukurasa wa 62 kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza zaidi ni kwamba wafanyabiashara wa gari ndogo maarufu kama “*Tax*”, ikumbukwe kwamba bei ya vyombo hivyo ni tofauti sana na hata ubebaji wa abiria ni tofauti pia. Bodaboda hubeba abiria mmoja tu wakati gari “*Tax’* hubeba wastani wa abiria wanne. Hata ukubwa wa *Engine (CC)* wa vyombo hivyo ni tafauti kabisa iweje kodi itozwe sawasawa! Inashangaza sana!

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba wafanyabiashara wa bodaboda, kwanza wachukuliwe kama wafanyabiasha wadogo na hivyo watozwe asilimia sufuri kwa mauzo yasiyozidi Shs.3,000,000/=. Ikumbukwe kwamba wafanyabiashara hao kwa sasa ni jeshi kubwa sana nchini, hivyo ni busara kwa Serikali inayoongozwa na CCM kusikiliza kilio chao na kuwafutia kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mifumo ya kodi yetu ni mibovu sana kwani inamnufaisha mwekezaji kuliko maslahi ya nchi yetu. Kodi katika sekta hasa za madini na utalii zinamnufaisha zaidi mwekezaji kuliko nchi. Katika sekta ya utalii mathalani kodi za uwindaji wa wanyama ni ndogo sana ukilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, eneo lingine ambalo kodi hazitozwi kwa kuzingatia hali halisi, ni sekta ya mawasiliano hasa simu za mkononi. Kwa maoni yangu, Serikali inapoteza pesa nyingi sana. Napendekeza Serikali ipitie upya sheria zote za kodi ili kuwianisha mapato halisi ya taasisi husika na kodi zinazolipwa. Pili, napendekeza itungwe sheria itakayolazimisha wawekezaji wote kutoka nje ya nchi waingie ubia na

wawekezaji wazalendo, hii itapunguza kama si kumaliza wizi wa rasilimali zetu. Nchi ya Ethiopia imefanya hivyo na imepiga hatua kubwa sana. Tusione aibu kwenda kujifunza huko.

Mheshimiwa Spika, kilimo kutengewa pesa kidogo. Inasikitisha na kushangaza sana kuona kwamba kilimo ambacho huajiri Watanzania zaidi ya asilimia 80, kimepewa Shs.192.2 bilioni tu lakini ziko Wizara ambazo zimepewa zaidi ya Shs.300 bilioni! Hivi kweli ipo dhamira ya kweli ya kuinua kilimo, hivi ipo dhamira ya kweli ya kutekeleza dhana ya Kilimo Kwanza? Hivi ni lini bajeti ya kilimo itafika angalau asilimia 10 ya bajeti ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, ushuru wa bidhaa kwa simu za mkononi. Kuongeza ushuru wa bidhaa kwa simu za mkononi kutoka Shs.10 kwenda Shs.12, ni kuwaumiza Watanzania walio wengi. Kuongeza ushuru kwa sababu za kuwa ni ushuru wa pamoja kwa nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki, siyo kuwatendea haki Watanzania walio wengi. Ni vizuri ifahamike kwamba simu siyo anasa, ni chombo muhimu sana kwa mawasiliano, kuongeza bei ni sawa na kuwatenga Watanzania walio wengi hasa wakulima na wafugaji vijijini pamoja na wanafunzi vyuoni. Napendekeza, mfanyabiashara ndiye abebeshwe mzigo huo na siyo mwananchi wa kawaida. Kama nilivyosema, hili ni eneo ambalo halitozwi kodi stahiki kwa biashara wanayofanya na mapato wanayopata.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti ila naomba nipatiwe maelezo ya maeneo niliyoyaelezea, ahsante sana.

**MHE. ANNA MARYSTELLA P. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima na afya, pia nashukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sina uchungu kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Rukwa na Katavi kama nitaunga mkono *budget* hii ambayo haiendi kutatua matatizo kwa wananchi maskini wanaoendelea kuishi kwa kukosa huduma muhimu za kijamii, maisha magumu, wanaumia na kuteseka ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwanza tujiulize, hivi unaweza kupanga *budget* ya kulisaidia Taifa ukiwa una matumizi makubwa kuliko pesa unayokusanya ndani ya nchi yako au ndiyo tunaendelea kuwahadaa na kuwapa moyo wananchi kwa kuwadanganya kwa kuwapa matumaini hewa? Maana nashangaa kuona *budget* hii tunaambiwa mapato ya ndani yameongezeka kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.5 huku matumizi ya kawaida yakipanda kwa kiasi cha trilioni 1.9. Hapa tunawadanganya wananchi maana tunajadili *budget* isiyotekelezeka na isiyokuwa na faida kwa maendeleo tuyatakayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni matumizi makubwa ya Serikali tena yasiyo na tija kwa Taifa letu wakati Watanzania wengi wanakufa kwa kukosa matibabu, madawa hospitalini na zahanati hakuna,

wananchi vijijini wanatembea umbali mrefu kufuata huduma za afya wakati wengine wakipoteza maisha njiani kutokana na umbali kufuata huduma za afya. Watoto wetu wanakosa elimu bora, wanasoma katika mazingira magumu. Wapo wanafunzi mpaka leo hii wanakaa chini mashuleni hawana madawati na darasa moja wanakaa zaidi ya wanafunzi mia moja na hamsini. Walimu wanaishi katika mazingira magumu, hawana nyumba za kuishi, majengo ya shule mabovu. Naiomba Serikali ipunguze pesa kwenye safari za nje na ndani, mawasiliano na badala yake zielekezwe kwenye huduma muhimu za kijamii kama elimu na afya ambayo imekuwa tatizo kubwa linalowatesa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 50, kipengele D kinachoelezea maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii, Serikali imetenga Shs. Bilioni 84.1 eti kwa ajili ya kuboresha viwango vya elimu katika ngazi zote. Huku ni kushusha elimu, maana katika sekta nyeti kama elimu huwezi kuboresha kwa kutenga fedha chache kiasi hicho wakati fedha nyingi zikielekezwa kwenye matumizi yasiyo ya lazima na yanayoepukika. Niiombe Serikali kuangalia upya *budget* hii tuhakikishe tunapunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuhakikisha tunaandaa Taifa lenye mwonekano mpya kwa maisha ya vizazi vyetu vijavyo na vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa suala ambalo linaleta vifo vingi mpaka sasa vya Watanzania, nalo ni suala la maji. Serikali imetenga Shs. Bilion 568.8 huku pato kubwa la Taifa likielekezwa kuendesha Serikali

kwa matumizi kama posho, safari, mafuta na ununuzi wa magari, sherehe na kadhalika, mambo ambayo hayana faida kwa Watanzania wanaoteseka. Kwa suala hili, naomba Serikali itupie macho kwa Mkoa wa Katavi na Rukwa hasa vijijini, Bunge la *budget* lililopita nilivitaja vijiji ambavyo wananchi wanahangaika sana kupata maji safi na salama. Wananchi wanakunywa maji ya mabwawa wakichangia na wanyama kitu ambacho ni hatari kwa afya zao. Naiomba Serikali ipunguze matumizi yasiyo ya lazima, watangulize maslahi yenye tija kwa faida ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia namna bora ya kuimarisha bei ya pamba na kujenga imani ya Serikali kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa. Itakumbukwa kuwa bei ya pamba imekuwa ikiyumba mwaka hadi mwaka na kuilazimisha Serikali kuchangia fedha kuokoa soko la zao hilo vivyo hivyo hali ya bei mwaka huu 2012 siyo nzuri na iwapo Serikali italazimika kuchangia ili bei ibakie kama ilivyokuwa mwaka jana ya TZS.1,000/= basi itabidi kutenga walau TZS bilioni 100 kwa ajili hiyo. Hiki siyo kiasi kidogo cha fedha ikizingatiwa kuwa bado kuna mahitaji makubwa ya fedha kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Simiyu, wananchi bado wanakumbuka kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati akizindua Kiwanda cha

Kusindika Pamba cha Nsagali, Wilaya ya Bariadi katika Mkoa wa Simiyu tarehe 27 Agosti, 2007, aliposisitiza umuhimu wa kujenga viwanda vya nyuzi na nguo ili kuifanya pamba inayozalishwa Tanzania iweze kusindikwa nchini na hivyo kuimarisha soko la zao hilo kwa wakulima. Rais alitoa mfano kuwa kilo moja ya pamba inaweza kuzalisha mashati manne ambayo thamani yake aliikadiria kuwa USD 50. Lakini pia pamba yetu inaweza kutumika hata kwa kutengeneza mataulo yanayoweza kuuzwa katika soko la Afrika Mashariki na Maziwa Makuu na kutosheleza soko. Hata hivyo, hili litawezekana tu iwapo wafanyabiashara watawezeshwa kuanzisha viwanda vya nyuzi kama hatua ya awali. Kutokana na kauli ya Rais na ahadi yake ya kuweza kuwasaidia, wafanyabiashara wa pamba katika Mkoa wa Simiyu walitenga eneo tayari kwa ajili ya kujenga kiwanda hicho (eneo hilo bado lipo).

Mheshimiwa Spika, ili azma hii iweze kutimia, wafanyabiashara wanahitaji dhamana ya Serikali ili waweze kukopa katika taasisi za fedha. Inakadiriwa kuwa kiwanda kimoja cha nyuzi (kutoka Japan) kinaweza kugharimu takribani TZS billion 50. Inakadiriwa pia kuwa walau viwanda vinne vingeweza kutosha kabisa kusindika pamba ya Tanzania kuwa nyuzi. Ieleweke pia kuwa karibu asilimia 70 ya pamba yote nchini huzalishwa katika Mkoa wa Simiyu. Hivyo kauli ya Serikali ya kukubali kuwawezesha wafanyabiashara kuanzisha viwanda kutokana na dhamana ya Serikali siyo tu itaongeza imani ya wanunuzi wa pamba mwaka huu bali itasaidia kupandisha bei kwa mkulima bila ya Serikali kulazimika kuweka nyongeza ya bei.

Muhimu pia ni kuwa wakulima wa Kanda ya Ziwa wanaotegemea pamba wapatao karibu milioni 14 watapata hamasa na imani kwa Serikali yao. Bila kutafuna maneno, Vyama vya Upinzani vinasubiri kwa hamu maamuzi ya kikao cha Wadau wa Pamba kinachofanyika leo Jijini Mwanza ili kuamua bei kwa msimu huu. Wangependa kutumia bei ya pamba kama rungu la kisiasa. Kujengwa kwa viwanda vya nyuzi Simiyu pia vitafungua ajira mpya kwa vijana na wanawake na kuufanya Mkoa unufaike na zao hilo muhimu la kibiashara. Naishauri Serikali ifanyie uamuzi suala hili haraka na kulitolea kauli kabla au wakati wa kuhitimisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza haja ya kuondoa punguzo la kodi ya mafuta ya kula kutoka nje ili kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta hapa nchini kama vile alizeti, pamba, ufuta na karanga.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, bajeti haikidhi mahitaji muhimu ya Watanzania. Jambo la kwanza ninaomba sana Serikali ipanue wigo wa kukusanya kodi. Kwani walipa kodi wa nchi hii ni wachache sana ukilinganisha na idadi kubwa ya Watanzania ambao wengi wao hawalipi kodi. Ni muhimu sana Serikali ikaangalia kwa undani sana kwani hata tukipiga kelele hatutaweza kufanikisha kama hatujakuwa na mpango mkakati wa kupanua wigo wa kukusanya kodi kwa kuangalia

maeneo mengine kama kwenye kodi ya majengo na kodi ya madini ambako kuna fedha nyingi sana ambazo tutaweza kukusanya.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo litapanua wigo wa kodi ni kuviwezesha viwanda vya ndani ambavyo vikiwezeshwa, vitaweza kuchangia pato la Taifa na kuwafanya wananchi waweze kupata ajira ambazo zitasaidia kukusanya kodi kupitia zalisho la viwanda hivyo lakini unapopata wafanyakazi, ni chanzo cha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine Serikali inatakiwa kuwekeza ni katika suala la kuwekeza kwenye umeme. Huwezi kuendelea kama hauna umeme wa kutosha kwani huko vijijini kuna umaskini mkubwa lakini kama tutawekeza kwenye *energy* tutaweza kuwawezesha wananchi walio wengi wanaoishi huko vijijini ambao wana mazao wanayotegemea yasindikwe lakini hawana jinsi ya kusindika mazao yao na matunda yanayozalishwa na wakulima wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwenye eneo la kilimo bajeti hii ni ndogo sana kwa kilimo. Nchi hii ni ya kilimo, tunaomba apunguze maeneo hasa ya posho ya Serikali zielekezwe kwenye suala la maendeleo haswa kuwawezesha wakulima kupewa ruzuku ya pembejeo ni pamoja na kuweka masharti nafuu ya kupewa zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi mabaya ya Serikali, ni muhimu Serikali iandae taratibu za kudhibiti matumizi mabaya yanayofanywa na Serikali. Pesa

nyingi hasa zinazopelekwa Halmashauri, Wilaya zinatumika vibaya kuliko zinazoelekezwa kwenye shughuli za maendeleo. Tunaiomba Serikali iwachukulie hatua wale wote watakaoonekana wamefuja mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali iache tabia ya kutoa msamaha wa kodi kwa makampuni na mashirika kadhaa ambayo hayalipi kodi. Nchi haiwezi kuendelea kama misamaha ya kodi ya holela itaendelea.

Mheshimiwa Spika, kama haya niliyoshauri yatatekelezwa, nitaunga mkono hoja hii.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na ugeni wake kwenye Wizara hii nyeti ametuletea bajeti ambayo nianze kwa kuiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nijikete kwenye mfumko wa bei wa bidhaa zote muhimu haswa chakula. Nianze kwa kutoa maelezo kidogo. Ulimwengu wa sasa umekuwa mdogo kama kiganja. Tunao mwingiliano kiuchumi, kisiasa na kadhalika. Mfumko wa bei ni tatizo kubwa la kidunia. Hakuna nchi hata moja duniani ambayo haina tatizo la mfumko wa bei. Mahali popote penye njaa, amani inapotea kidogo kidogo. Vurugu zote zinazotokea leo duniani mfano Syria, Misri, Tunisia na kwingineko kote, chanzo kikuu ni uchumi kuzorota na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, nakiri kabisa kama kila nchi duniani inalo tatizo kuu la mfumko wa bei, la msingi la kufanya, Taifa lijikite kwenye kutafuta ni jinsi gani itapata njia za kupunguza ukali wa maisha. Kila taifa duniani sasa hivi limejikita katika kutafuta utatuzi na kupunguza mfumko wa bei, ugumu wa maisha na kudorora kwa uchumi kwa ujumla. Naiomba Serikali iangalie kwa makini ni jinsi gani itawaondoa Watanzania hapa walipo.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja nikipata maelezo ya kutosha ya kujibu ni jinsi gani itawaondoa Watanzania hapa. Ahsante sana.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi katika kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelewa ni kwa nini hadi leo Serikali inashindwa kabisa kubaini namna ya kupanua wigo wa mapato na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo muhimu sana katika sekta ya uchukuzi hasa Bandarini, kuhusu *ICD*. Uanzishaji wa *ICD* binafsi ni jambo jema sana lakini nia imekuwa vinginevyo. Kuna *ICD* ambazo zimekuwa zikitoa *hidden charges* ambazo zimekuwa zikiwekwa kwenye utoaji wa mizigo na mwishowe gharama hizi huwekwa kwa mlaji na hii imesababisha bei za bidhaa kuwa juu na kufanya maisha ya *individual* kuwa juu na kupelekea watu wengi kushindwa kulipa kodi na kukosesha mapato ya Serikali. *SUMATRA* wameacha

kufanya kazi ya kusimamia *ICD* na wamekuwa wakikimbizana na daladala na kuacha *ICD* kuendelea na gharama zilizojificha na pia ningependa sana kuona hizi *Regulatory Authorities* kama *SUMATRA, EWURA, TFDA, TBS* na nyingine zingekuwa *under one roof* (bandarini) au *longroom.*

Mheshimiwa Spika, bado sikubaliani na utaratibu wa hizi *Regulatatory Authority* kulipwa na *importer* moja kwa moja ambayo imepelekea rushwa na ukaguzi makini kutofanyika. Napendekeza hizi *Regulatory Authority* zilipwe kupitia *TRA* wakati wa uingizaji mizigo ili fedha za nchi ziwe na sehemu moja tu ya ukusanyaji katika *importation*.

Mheshimiwa Spika, bado pia sikubaliani na huu utaratibu wa *TBS* kukagua magari nje ya nchi na kupelekea fedha nyingi kubaki nje ili hali bado ukaguzi huu haufanyiki. Napendekeza makampuni haya yaje na kufanya kazi hapa ndani kwa fedha za Kitanzania na pia kuongeza ajira za Watanzania ambao watapata kazi na kulipa kodi humu ndani.

Mheshimiwa Spika, pia napinga utaratibu uliotumiwa kwa vigezo vya miaka ya utengenezaji wa magari (*year of manufacture)* kwa ajili ya uchakavu. Utaratibu huu uangaliwe upya maana yapo magari yaliyotengenezwa hivi karibuni yamechakaa. Upo utaratibu wa *Used Car Grading* ambao nchi ya Japan na nyingine hufanya kuna *Grade* 5, 4.5, 4, 3.5, na 3 hii ni kutokana na ukaguzi wa viwango. Bado ninao uwezo wa kukaa na Mawaziri wa Fedha na yule wa Viwanda

na Biashara ili kusaidiana nao na kuwaelekeza namna bora ya kusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wakisaidiana na wakaguzi wa magari wamekuwa wakidanganya miaka ya utengenezaji wa magari kwa kubadilisha mikanda au hata kugonga namba za *chasis* upya ili kukwepa sheria au utaratibu huu unaowekwa. Kama tutaweka utaratibu huu wa *used car grading* utasaidia sana na kuepuka udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Vitambulisho vya Taifa uharakishwe ili tuwe na watu wengi wanaotambulika rasmi kwa ajili ya ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kama nikipata nafasi nitashauri zaidi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuweka mpango kabambe wa ujenzi wa bomba la gesi ambalo litasaidia kutatua tatizo la umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mpango huu utawasaidia wananchi maskini kuweza kupata umeme kwa bei nafuu zaidi na umeme wa uhakika haswa kwa wafanyabiashara ndogondogo kuweza kuendelea kujiajiri katika nyanja mbalimbali kama vinyozi, mama lishe na mafundi chuma.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuweka mkakati wa kuajiri vijana 71,000 katika nyanja mbalimbali na pia nitoe angalizo ajira hizi zitolewe kwa

vijana wenye sifa mbalimbali na wa kada mbalimbali ili kuleta fursa kwa vijana wetu walio mijini na vijijini, kujuana isiwe sifa ya kuajiri ili kuleta usawa kwa wenye nacho na wasio nacho.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuonyesha nia ya kuboresha reli ya kati ambayo itapunguza gharama za kufanya biahsara na kuongeza tija katika uzalishaji pia itasaidia miundombinu yetu ya barabara kuepukana na uharibifu ambao unaletwa na magari makubwa yanayopita humo, reli itasaidia maana mizigo mingi itasafirishwa kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa bajeti hii iliyolenga kukabiliana na changamoto zinazokabili uchumi pamoja na kuongeza fursa za kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutoongeza bei ya utumiaji simu kwa wananchi wake. Sababu wanaotumia simu hizi ni wananchi wote mijini na vijijini. Serikali inapoongeza bei, haiwatendei haki wananchi haswa maskini, mawasilianao ni muhimu kwa kila mwananchi. Serikali isisababishe wananchi wakashindwa kuwasiliana kwa sababu ya gharama za mawasiliano.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza pendekezo la Kamati ya Fedha la *ku-zero rate VAT* kwenye bidhaa za nguo ili kulinda viwanda vya nguo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, ninafuta pendekezo la *COSOTA* kusimamia *Stiker* za kazi za wasanii. Nakubaliana na Serikali kwamba *TRA* waendelee na utaratibu waliouanza. Pendekezo lililopo kwenye bajeti mbadala kuhusu *COSOTA* lisingatiwe, uamuzi wa Serikali uendelee.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ili niweze kusimama na kutoa mchango wangu mdogo kuhusu hoja iliyo mbele yetu ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Naibu Mawaziri wa Fedha; Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa ndiyo waongoze Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Pia napenda kuwapongeza wote walioshiriki wakati wa maandalizi ya bajeti hii ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika kuchangia hoja ya bajeti kwa kuunga mkono hoja ya bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa sababu ni bajeti nzuri ambayo vipaumbele vyake vimelenga kuimarisha uchumi wa Tanzania. Kwani ni ukweli usiopingika kuwa wananchi hawawezi kufikia maishi bora kama nchi yetu ina uhaba wa chakula, mfumko wa bei, ukusanyaji wa mapato na usimamizi

wa matumizi kuwa hafifu, ukosefu wa ajira hasa kwa vijana na wanawake, kuwekeza katika miundombinu ya nishati, elimu na afya havijaimairika. Kwa hiyo, Serikali kuchagua vipaumbele hivyo ni katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kukusanya mapato bado jitihada za ziada zitahitajika katika mambo yafuatayo:-

1. Bado wapo baadhi ya Watanzania wanakwepa kulipa kodi mfano ushuru wa magari.

2. Serikali iwe macho na watendaji wasio waaminifu wanaokusanya mapato bila kuyafikisha katika Mfuko wa Taifa badala yake wanaweka mifukoni mwao.

3. Serikali ichukue hatua kwa baadhi ya watendaji ambao wanafanya makadirio ya chini kwa baadhi ya wafanyabiashara, mtu aliyepaswa kulipa kodi ya shilingi milioni 100 anakadiriwa kulipa shilingi milioni 10 tu.

4. Bado misamaha ya kodi ni mingi sana, Serikali itazame upya.

5. Bado Serikali haijabuni vyanzo vipya vya kuongeza mapato kwa kiasi cha kuridhisha, eneo hili liangaliwe upya. Mfano Serikali

ianzishe kodi za majengo yanayopangishwa.

6. Serikali ijitahidi kuwekeza kwa kiasi cha kutosha katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji na kuongeza matumizi bora ya pembejeo za kilimo katika Kanda ya Ziwa. Mabonde ya Mto Kagera, Mto Simiyu na Tarime yaongezwe kwenye mipango ya uzalishaji.

7. Serikali ijitahidi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kufufua viwanda. Mfano viwanda ambavyo vimeshindwa kujiendesha virejeshwe Serikalini mfano Viwanda vya Pamba na Korosho.

8. Serikali ipeleke fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyopitishwa na Bunge tena kwa wakati.

9. Serikali iondoe kodi ya madawa ya maji ili wananchi waweze kupata maji safi na salama.

10. Serikali iongeze kodi kwa wawekezaji kwa wachimbaji wa madini na makampuni ya simu za mkononi.

11. Wakati wa kuandaa bajeti ya mwaka 2013/2014, nashauri Kamati ya Bunge ishirikishwe mapema katika kuandaa vipaumbele vya bajeti. Nashauri kikao

hicho kifanyike mwezi Februari, 2013 badala ya Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni sekta ya uvuvi. Ukurasa wa 48 *paragraph* ya 79, umeelezea nia ya Serikali kuendeleza shughuli za ufugaji na uvuvi lakini kwenye bajeti *itself* haijatafsiri hali halisi ya maneno ya Waziri kwa vile:-

- Bado mvuvi na wamiliki wadogowadogo wa vifaa vya uvuvi (mitumbwi, boti za mbao na madau) hawafaidiki na hawasaidiwi chochote.

- Vifaa vya uvuvi kila leo vinapanda bei mfano *roll* moja la nyavu ni Shs. 600,000/= - 700,000/= na ili uwe na nyavu kamilifu ya kuvulia utahitaji *Rolls* 10 -12, angalia ni bei gani?

- *Engine* moja ya *in board* ni kati ya 14,000 USD – 16,000USD. *Used* ni 7,000 USD – 9,000 *USD* geuza kwa Tshs ni kiasi gani?

- *Outboard engine 40 HP* ni *seven million shillings*.

- Hujanunua; *small generator*, *sport lights 240,000/= each,* maboya, *life jackets,* karabai, *fire*

*extinguishers, pumb*, kamba, nanga na kadhalika. Je, mvuvi atapona?

- Mvuvi maisha ni maskini na atakufa maskini licha ya juhudi zake za kulala baharini usiku na mchana, bahari tulivu au chafu.

- Samaki mzuri mezani akishapikwa ila namna nyepesi ya kumpata hilo hakuna mwenye kujali ya kuwasemea wavuvi wadogo wadogo.

- Wananchi wa kipato cha chini wanaishi kwa kula dagaa na kauzu wanaovuliwa na wavuvi wadogo wadogo. Huku samaki wakubwa wakivuliwa kwa *trollers* ambazo zinaishia bahari kuu na samaki wao hata hawafiki sokoni na hao ndiyo wanaofaidika na *exemptions* na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza, wavuvi wanaotumia vyombo vya mbao basi wapunguziwe kodi kwenye nyavu, *engines* za boti, *life jackets*, taa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pili, kupanua fursa za ajira. Napongeza juhudi za Rais Kikwete na Rais Karume za kuanzisha mfuko wa JK na AK, ila fedha hizo nyingi hazikuwafikia walengwa. Mifuko hii ingetumika vizuri basi ingesaidia sanasana wajasiriamali wadogowadogo ambao nao wangeweza kuondokana na dhiki zao. Ajira nyingi zinaweza kupatikana pia kwa nia ya ujasiriamali. Wazidi kuwezeshwa, tusitegemee ajira za Serikali tu.

Mheshimiwa Spika, tatu, ongezeko la kodi kwenye maongezi ya simu. Hebu tuangalie ipasavyo, makampuni ya simu kweli wanalipa kodi wanazotakiwa kulipa? Wao sasa wanajiingiza kutoa huduma nyingine nyingi na hatujui ni kiasi gani kodi ya Serikali inakusanywa au la. Kwa mfano, huduma za kupeleka pesa, huduma za kuwa wakala wa kukusanya madeni/malipo toka kwa wateja kwa niaba ya mashirika na taasisi mbali bali kwa mfano *bill* za *TANESCO*, maji na taasisi mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, makampuni haya yanaajiri wafanyakazi wa kada ya chini ambayo nchi yetu wapo na wana uwezo wa kufanya hivyo. Sina uhakika iwapo *skill development levy* inakusanywa kwani mara nyingi kelele zitokanazo na suala hilo zinapopigwa na wananchi basi wafanyakazi hao wageni huhamishwa kwa muda na kupelekwa kwingine hadi hali ikiwa shwari wanarudi kwenye *business plan* zao wanaandika *staff development* na wanaipangia bajeti je, wanafanya? Je, kama hawafanyi ile bajeti waliyotenga si inakuwa ni *gain* kwao? Aidha, makampuni haya yana-*change hands* bila ya Serikali kufaidika, ni wajanja kweli.

Mheshimiwa Spika, nne, maamuzi yetu kutoendana na utekelezaji halisi. Viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vimebadilishwa matumizi yake na kukosa mapato, Serikali mbona haichukui hatua? Vile viwanda vilivyokuwa vinahitaji kufufuliwa ili vifanye kazi na kutoa *products* za kusaidia jamii uzalishaji, vimekuwa mabehewa, mbona hatuchukui hatua?

Mheshimiwa Spika, tuangalie *taxation on service provision* kwenye maeneo mbalimbali mfano *construction industry, tourism, consultancy*, *feasibility study, tution (planned) and saloons* na kadhalika.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE**: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja mia kwa mia. Napongeza bajeti ya mwaka huu ambayo inajali Watanzania wanyonge walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza ni katika ukusanyaji mapato. *TRA* kila mwaka wanapewa siha nyingi, wamepindukia lengo lakini je, tumeangalia uhalisia wa makusanyo maana siku zote wanasema hivyo, sasa iko haja ya kuiangalia sehemu hii ya *TRA*, maana naamini sisi tuna uwezo wa kukusanya zaidi ya trilioni 10 badala ya hizo trilioni 8.5 zilizosemwa. *TRA*, kuna upotevu mkubwa wa mapato ya nchi hii, iko haja ya kutupia macho wafanyakazi wa *TRA*, mfano kila mfanyakazi ana mali nyingi kuliko mshahara anaolipwa, vijana wengi wanalilia kufanya kazi *TRA*, sasa tujiulize kuna nini? Kwa ajili ya kupata mapato halisi, naomba wafanyakazi wa *TRA* wafuatiliwe kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, kwa vile viwanda vyote ambavyo vilipewa sekta ya watu binafsi na ambao hawakufanya Serikali ilivyotaka, sasa nashauri Serikali ivichukue ili wapewa ambao wanaweza kufanyakazi ilivyokusudiwa ili Watanzania walio wengi wapate kazi ili tupate kupunguza mrundikano wa vijana wasio na kazi.

Mheshimiwa Spika, kuondosha *VAT* katika viwanda vya mafuta ya kupikia pamoja na viwanda vya korosho, hii itatusaidia kununua mafuta yetu ya hapahapa nyumbani na itasaidia kuwapatia kipato wakulima wa alizeti. Pia korosho zitabanguliwa hapa nyumbani Watanzania wengi watapata kazi na pia tutauza kwa bei iliyokuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za Rada, zimeamuliwa kutumika kwa ajili ya vifaa vya skuli zetu, kwa hivyo ushauri wangu fedha hizi zingegawiwa katika Mikoa yote ya Tanzania. Kwa vile fedha hizi zilinunuliwa "Rada", nina imani Wizara ya Ulinzi ndiyo inayohusika, pia iko katika sehemu ya Muungano, kwa hiyo, naomba Zanzibar nayo ipate sehemu yake katika mgawo wake wa elimu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bei ya vyakula. Tatizo kubwa la mfumko wa bei ya chakula lililopo hapa Tanzania linatokana na kutokuwa na uzalishaji wa chakula kinachopendwa na watu wengi mfano mchele. Ushauri wangu, Serikali inunue mchele mwingi ambao utasaidia kushusha bei ya chakula kama walivyofanya wenzetu wa Zanzibar na wamefanikiwa kupunguza mfumko wa bei, pia sukari inunuliwe kwa wingi.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuondoa ushuru kwa vifaa vinavyotumia gesi, ikiwa ni pamoja na majiko yaliyotengenezwa mahsusi kwa ajili ya matumizi ya gesi pekee. Hii itasaidia kupunguza gharama na mzigo wa kazi kwa wanawake sababu wanawake

wengi mijini na vijijini wao hutumia kuni. Kwa mujibu wa Tanzania *Household Survey* kuni zinatumika zaidi ya asilimia 90 hivyo hatua hii itasaidia kupunguza mzigo na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuondoa kodi tu haitoshi bali Serikali inapaswa kuwa na mpango kabambe ambao utahimiza na kuhamasisha matumizi ya majiko ya gesi majumbani. Hili la kutumia *gas* tunaweza kuliona dogo lakini litapelekea kufikiwa malengo yetu ya kuwa na usawa wa jinsia katika elimu kufikia asilimia 50 sababu wanaotafuta kuni ni watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kuamua kutoza ushuru zero (sifuri) katika virutubisho vya chakula na madini *(food supplements and mineral premix)* vinavyotumika katika kutengeneza chakula cha watoto wachanga na kuzitoza ushuru wa forodha wa asilimia sifuri. Hatua hii inalenga katika kuwezesha watoto wachanga na wagonjwa kuweza kupata vyakula vyenye virutubisho kwa bei nafuu na kuimarisha afya zao. Hii itasaidia sana nchi yetu kupunguza utapiamlo kwa watoto. Kwa mujibu wa Tanzania *Demagraphic and Health Survey* watoto katika 100, 42 wamedumaa (asilimia 42) hivyo baadaye tutakuwa na Taifa la viongozi ambao akili zao zimedumaa, hali hii ni mbaya sana katika maeneo ya Mikoa ya Dodoma asilimia 56, Lindi asilimia 54, Iringa asilimia 52, Mbeya asilimia 50 na Rukwa asilimia 50. Naishauri Serikali pia ianzishe programu maalumu ambayo itawapa uelewa kina mama umuhimu wa kutumia vyakula vya watoto vyenye virutubisho vilivyo maalum ambavyo huwapa afya watoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri na watendaji kwa kuitafakari bajeti na mazingira ya Taifa na kuja na mapendekezo ya Bajeti, kwa mawazo yangu itasaidia sana kutuondoa tulipo na kutusogeza mbele kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nitoe msisitizo kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nchi yetu inaendelea kupata taarifa nzuri za kugunduliwa kwa visima vya gesi asilia. Jambo hili sasa linapelekea nchi yetu kuzidi kuwa na uchumi mpana – *diversified*. Naomba nishauri kwa Serikali kwamba umefika wakati wa kulijua hili na kuweka mazingira ya kuwa na uchumi wa gesi. Serikali inahitaji kuchukua hatua za haraka ili kujipanga na kuupanga uchumi na wananchi kuelekea huko. Masuala ya kuandaa rasilimali watu ili kuongeza uchumi unaokuja ni muhimu. Aidha, kwa sasa macho ya Serikali yawe karibu zaidi na mradi wa bomba la gesi kwa kuamini kwamba huo ni mradi wa kwanza muhimu katika mabadiliko niliyoyasema. Bomba la gesi litapunguza *inflation*, uharibifu wa mazingira na litasaidia zaidi katika usambazaji wa nishati rahisi.

Mheshimiwa Spika, pili, ajira. Nchi yetu hivi sasa inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira hasa kwa vijana wanaomaliza shule na vyuo. Tatizo la msingi hapa ni pamoja na kushindwa kwetu kukifanya kilimo kisitowe nafasi za ajira hasa kutokana na tija ndogo pamoja na teknolojia duni. Hata hivyo, ni lazima tuelewe kwamba hatuwezi kwa muda mfupi, kuongeza nafasi za ajira kama tutakidharau kilimo. Ni kilimo ambacho kitaajiri watu, ni kilimo kitakachotoa nafasi za ajira kupitia uchakataji wa mazao viwandani. Nashauri kwamba *let us walk the* Kilimo Kwanza *in it's entirely* ili uchumi na ajira ziende sambamba.

Mheshimiwa Spika, tatu, misamaha ya kodi, ni kipindi kirefu sasa tumekuwa tukikariri haja ya kupunguza misamaha ya kodi na haja ya usimamizi wa karibu kwa wale ambao ni lazima wapatiwe misamaha. Chanzo kikuu cha misamaha ya kodi ni vivutio vya wawekezaji. Wakati umefika kwa Tanzania kuachana na kutumia kodi pekee kama kivutio cha wawekezaji. Nashauri tuangalie vivutio vingine ikiwa ni kuboresha mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara. Hapa nakusudia kupunguza urasimu, kuondoa rushwa, kurekebisha miundombinu (umeme, barabara na kadhalika). Naamini misamaha ya kodi na mapato yake ikitumika kutengeneza miundombinu niliyoitaja, ni kivutio bora kuliko misamaha. Aidha, kuna tatizo kubwa la matumizi ya misamaha inayotolewa hasa kwenye mafuta na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nne, *PPP*, kuna kila dali ya kuashiria kwamba mapato yetu hayatoshi mahitaji yetu

na hili linathibitishwa na mikopo na utengaji wa fedha chache karibu kwenye kila sekta. Katika jitihada zetu za kuendeleza nchi na hasa kwenye miundombinu tujielekeze kwenye *PPP*. Mpango huu umewekewa sheria na kanuni zinazohitajika. Pamoja na hatua hizi hadi sasa hakuna mradi wowote ambao umetekelezwa. Nashauri tuongeze kasi ya *negotiations* ili tuweze kutumia fedha na rasilimali kutoka sekta binafsi katika kuimarisha miundombinu yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mungu, muweza wa yote.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia dhana ya kukua kwa uchumi nchini ilhali wananchi walio wengi hali zao ni ngumu na zinarudi chini. Suala ni kwamba, uchumi unakua au kupanda wakati hali za watu ni za chini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kutilia mkazo zaidi kwenye kilimo ambacho ni ajira inayoshirikisha zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania, lakini wakulima wadogowadogo wamekuwa wakisahaulika katika kupewa msukumo unaostahiki kama vile pembejeo, mikopo, wataalam na pia kusaidiwa kupata masoko mwafaka kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, ili maendeleo ya nchi yetu yaonekane na wananchi waone maisha yao yanaboreka ni lazima Serikali iende sambamba na

zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaojiendeleza katika kilimo cha wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi katika nchi yetu hauonekani kuondoa umaskini kwa Watanzania kwa sababu sekta zinazokuza uchumi huo hazina ushiriki wa watu wengi; mfano, Sekta ya Madini na Utalii, hivyo bado tunabakia katika kilimo ambacho kina washiriki wengi.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imekuwa mjadala mkubwa katika nchi yetu kwamba, kuna kiasi kikubwa cha fedha zinazopotea katika misamaha ambayo pesa hizo zinaipunguzia nchi yetu pato la kukuza uchumi. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kufuta misamaha isiyokuwa ya lazima. Naishauri Serikali katika suala zima la ukusanyaji wa kodi, jambo hili lisifumbiwe macho hata kidogo, vyombo husika ni lazima viwajibike juu ya ukusanyaji wa kodi na kudhibiti mianya ya wajanja fulani katika kukwepa kulipa kodi. Hakuna lisilowezekana penye nia njema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la rushwa, naishauri Serikali ifunge mikanda juu ya rushwa. Jambo hili limekuwa mazoea kwa wananchi kwamba, hata jina limebadilishwa watu hawajui tena kuna majina mengi ya kupunguza ukali wa jina hili, wengine huita chai, bakshishi, bahasha ya bosi, kitu kidogo, ili mradi kuonekana kwamba jambo hili halina madhara yoyote. Ukweli wa mambo ni kuwa, rushwa inaumiza haki za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa William Mgimwa (Mb), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Fedha. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri wa Fedha; Mheshimiwa Janet Mbene (Mb) na Mheshimiwa Saada Salum, kwa uteuzi huo.

Naomba nichangie hoja ya Bajeti katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mapato yatokanayo na Sekta za Kiuchumi ni pamoja na kilimo na mifugo. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa jitihada inayofanya kupitia *TRA*, jitihada hiyo inatakiwa kuongezwa kwa kuziba mianya ya rushwa katika kilimo. Serikali, kwa njia yoyote ijielekeze katika kilimo cha umwagiliaji. Mataifa yote yaliyochagua Sekta ya Kilimo kama msingi wa uchumi wao, wameimarisha kilimo cha umwagiliaji. Mchango wa kilimo cha umwagiliaji unaweza kukuza uchumi kwa kuuza mazao nje hasa chakula na kutosheleza chakula ndani ya nchi. Pamoja na umuhimu huo wa umwagiliaji, bajeti hii haijielekezi sana katika suala mtambuka la kuhifadhi mazingira, ikiwa na pamoja na vyanzo vya maji ili kuhifadhi misitu, kuzalisha maji yatakayotumika katika umwagiliaji. Naomba kushauri kwamba, umefika wakati sasa Serikali iangalie suala la kilimo kuunganishwa na suala la kuhifadhi mazingira kama nguzo kubwa ya kiuchumi.

Serikali iangalie kwa undani mkubwa juu ya ukwepaji wa kodi unaofanywa na makampuni mbalimbali hapa nchini hasa makampuni ya simu,

hoteli na hata uwekezaji wa mashamba. Tabia ya wawekezaji hawa kubadilisha majina ya makampuni kila baada ya miaka mitano ni ukwepaji wa kodi. Kila inapotokea kampuni kubadilisha jina ni dhahili kuna mabadiliko ya mwekezaji ambaye angelazimika kulipa kodi lakini wanafichwa. Kwenye hoteli kubwa nako kuna matatizo kama haya. Nashauri uchunguzi mkubwa ufanyike kuhusu ukwepaji huu wa kodi.

Ukwepaji wa ongezeko la kodi katika mauzo ya bidhaa bado ni mkubwa. Bado wafanyabiashara wengi wanaendelea kutotoa stakabadhi kwa wateja na hivyo kujinufaisha badala ya kuongeza mapato kwa Serikali.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali ijiimarishe na kukamilisha mipango yake na kuimarisha miundombinu muhimu hasa ya uimarishaji wa reli ili usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani kama Zambia ufanyike kupitia reli kwenda Kigoma, Mwanza na kadhalika. Kutorekebisha usafiri wa reli kutaendelea kudidimiza uchumi kwa kuikosesha Serikali mapato yake.

Serikali inajitahidi kupeleka fedha nyingi katika Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Vilevile ni muhimu kuhakikisha Kitengo cha Manunuzi Sera kianzishe Ofisi za Kanda badala ya kuratibu kutoka Wizara ya Fedha Makao Makuu. Kuna ufujaji mkubwa wa fedha za umma hasa wakati wa manunuzi ambayo wakati mwingi hutumika vibaya na ubadhirifu.

Nashauri hoja hizi zifanyiwe kazi na naunga mkono bajeti na namtakia heri Waziri wa Fedha katika utekelezaji kwa mwaka 2012/2013.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais. Pia nawapongeza kwa Hotuba nzuri iliyowasilishwa.

Pamoja na pongezi hizi, ninayo mambo machache ya kuishauri Serikali ili kuboresha Bajeti kwa manufaa ya wananchi. Nitajikita katika sehemu nne muhimu zifuatazo:-

Kwanza, Sekta ya Kilimo: Zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania waishio vijijni, wanategemea Sekta hii ya Kilimo. Ninaishukuru Serikali kwa mpango wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo. Hata hivyo, wanaopata pembejeo hizi ni wachache; hivyo, Serikali iongeze bajeti ili wananchi wengi waweze kunufaika.

Kwa kuwa baadhi ya Mikoa katika Kanda ya Ziwa inakumbwa na ukame wa mara kwa mara na kusababisha upungufu wa chakula, mfano, mwaka 2011/2012, kumekuwa na tatizo kubwa la njaa. Ninashauri ianzishwe Programu Maalum ya Umwagiliaji katika Bonde la Ziwa Victoria. Programu hii itainua hali ya uchumi kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa sababu uzalishaji utaongezeka na bei ya chakula itapungua.

Takriban ni miaka mitatu sasa bei ya pamba inasuasua kutokana na kutegemea Soko la Dunia. Hii

inaathiri zaidi ya asilimia arobaini ya Watanzania wanaotegemea uchumi wao kutokana na kilimo cha pamba. Ili tuweze kunusuru kuanguka kwa bei ya pamba ni vyema Serikali itenge fedha kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda au ifufue viwanda vilivyopo kama vile *MWATEX* kilichoko Mwanza, *MUTEX* kilichopo Musoma na Viwanda vingine vya aina hii. Hii itaimarisha bei ya pamba, kwa kuwa viwanda vyetu vitanunua pamba hii. Vilevile viwanda vyetu vipewe msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* kwenye bidhaa za nguo na mavazi. Hatua hii itaongeza uzalishaji na ajira.

Pili, Sekta ya Mifugo: Bajeti haijatenga fedha za kutosha katika Sekta ya Ufugaji, ninapendekeza kuwepo na ruzuku kwa ajili ya madawa na chanjo za mifugo; hii itapunguza umasikini wa watu wetu hasa wafugaji. Serikali iwekeze katika uanzishwaji wa viwanda vya usindikaji wa nyama na mazao ya mifugo katika maeneo ya wafugaji. Kwa viwanda hivi, tutaweza kuuza bidhaa hizi kwa wawekezaji hasa walioko migodini; mfano, *GGM, Kahama Goldmine* na Migodi ya Tarime. Hii ingeongeza ajira kwa wananchi na pia uchumi wa wananchi wetu utaongezeka.

Tatu, Sekta ya Madini: Mkukuta II uanzishe Programu Maalum kuwasaidia wachimbaji wadogo. Sekta hii imeajiri wananchi wengi sana hasa vijana. Katika bajeti zilizopita, fedha zimekuwa zikitengwa lakini utekelezaji wake bado haujafanyika. Ninashauri mwaka huu utekelezaji ufanyike.

Nne, Utaratibu wa Kodi: Utaratibu wa kodi uangaliwe upya hasa kwa makampuni yanayotoa huduma migodini. Kodi hizi zinalipwa Makao Makuu ya Makampuni ambapo ni Dar es salaam au Mwanza. Halmashauri hazipati kodi hizi pamoja na kwamba shughuli zenyewe zinafanyika katika maeneo yao. Mfano halisi ni Geita, Halmashauri inapata mrabaha wa shilingi milioni 200 kwa mwaka kutoka *GGM,* lakini makampuni yanayotoa huduma mgodini hayalipi kodi yoyote kwenye Halmashauri pamoja na kwamba wanafanya shughuli zao ndani ya Halmashauri. Utaratibu wa kodi ukiruhusu kulipa kodi hizi kwenye Halmashauri, utaboresha huduma kwa wananchi hasa wanaozunguka migodi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii na mimi kumshukuru Mungu, kwa neema ya uhai.

Baada ya kusema hayo na mimi nachangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi naanza na maendeleo. Taifa lolote Duniani ili liendelee linahitaji kuwa na mipango madhubuti na endelevu na sisi tunahitaji kuboresha miundombinu yetu kama Barabara, Reli, Bandari na Viwanja vya Ndege ili kuwavutia wawekezaji ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, fungu la maendeleo katika bajeti hii angalau litengewe asilimia arobaini.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi kwa makampuni yanayowekeza nchini ni mkubwa sana na unapoteza pato kubwa la Taifa hili hasa sehemu ya uchimbaji madini; hivyo, nashauri upunguzwe au uondolewe kabisa.

Mheshimiwa Spika, viwanda ni sehemu kubwa ya ajira kwa vijana wa nchi yetu kama wangekuwa wanafanya kazi, Serikali imebinafsisha viwanda lakini vingi vyao havifanyi kazi. Huku ni kulipotezea Taifa mapato. Vijana hawana ajira wanabaki kuzurura. Mimi nashauri viwanda vyote ambavyo havifanyi kazi, virudishwe Serikalini haraka sana. Serikali ijipange kuviendesha kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, lingine, bajeti haikuzungumzia usafiri wa bahari, usafiri wa maziwa na usafiri wa mito, ambao ni muhimu sana kwa watu na mizigo.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri wa meli Dar es salaam, Mtwara na usafiri wa meli Ziwa Victoria, naiomba Serikali iliangalie kwa makini sana kwa sababu ni muhimu sana kwa Pato la Taifa na kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei umekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi hasa wa kipato cha chini. Huduma muhimu kama *petrol, diesel* na mafuta ya taa zikipanda, basi bidhaa zote muhimu zinapanda.

Mheshimiwa Spika, bei za vyakula zimepanda sana na kusababisha hali mbaya kwa wananchi. Ofisi

ya takwimu inaonesha mwezi wa Julai, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 14.8 na kuendelea hadi mwezi Novemba 2011 kufikia asilimia 24.7.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Bajeti ya Mwaka 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Nianze kuipongeza Serikali kwa kuanzisha tena Mpango wa Maendeleo ambao ulianza kutumika katika kipindi cha bajeti kinachomalizika (2011/2012). Katika kipindi hicho, changamoto zilikuwa nyingi na jitihada za kuzikabili nazo zilikuwa nyingi kama zilivyoainishwa katika Taarifa za Wizara, Benki kuu na Taasisi nyingine husika. Pamoja na ukweli kuwa kiwango cha pesa zilizotengwa kutekeleza bajeti hiyo hasa zile za Miradi ya Maendeleo hazikupatikana zote, bado Vitengo vingi na viashiria vya ukuaji uchumi vilikuwa chanya ingawa kasi ilipungua ukilinganisha na mwaka 2010/2011.

Ninaipongeza Serikali kwa jitihadi hii na hasa kwa kubaini sababu za upungufu wa kasi ili zifanyiwe kazi. Naomba kuchangia mawazo kuhusu cha kufanyika siyo kwa mwaka 2012/2013 tu bali pia kwa miaka ya mbele. Naipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi kwa uchambuzi na nasaha zake kuhusu bajeti, nasaha ambazo ninakubaliana nazo kwa kiwango kikubwa.

Vilevile naungana na wachangiaji wengine kuwa uwiano wa bajeti haukidhi lengo na dhamira ya kuendeleza nchi kivitendo kwa mazingira ya ushindani yaliyotuzunguka na azma ya kuibadilisha nchi hii iwe ya

maendeleo zaidi ya tulipo. Sasa ingetubidi tutenge siyo chini ya asilimia arobaini ya bajeti kwenye Miradi ya Maendeleo na tupunguze sana matumizi ya kawaida. Nchi zinazosifiwa kupiga hatua kwa kasi kama Korea ya Kusini ilibidi zifanye hivyo kwa kujinyima na kuchangia kwa pamoja hadi akina mama kunadi pete zao za ndoa kuchangia jitihada za maendeleo. Kwenye Ukombozi wa Afrika tulifanya zaidi ya hivyo; vipi leo tusifanye kwa maendeleo ya nchi yetu wenyewe? Sasa tusifike huko bali tupunguze matumizi ya kawaida.

Vivyo hivyo ili Taasisi za Serikali zichangie mapato, tuanzie na kuimarisha mishahara ya taasisi hizo iendane na hali halisi wanayoishi Watanzania wengine. Haiyumkini kumlipa Mkurugenzi Mkuu wa taasisi moja mshahara ambao ni mara tano ya Mkurugenzi Mkuu wa taasisi nyingine au mara tatu ya Naibu Mkurugenzi wake. Suala la uwiano wa mishahara na posho liangaliwe hata ikibidi kubadilisha sheria husika zilizotufikisha kwenye tofauti kubwa hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo; nchi yetu imeingia katika hatua muhimu sana ya kuupindua uchumi wetu ukue kwa kasi kubwa na pia uboreshe maisha ya wananchi yawe ya uchumi wa daraja la kati na baadaye daraja la juu katika jitihada za kuboresha maisha ya kila Mtanzania. Azma hii ni muhimu lakini utekelezaji wake unahitaji jitihada za ziada na kujitolea kwa hali ya juu kwa kila Mtanzania, kwa kupunguza matumizi na kuchangia fedha za maendeleo kwa kiasi na kwa mujibu wa sheria. Pamoja na mipango iliyowekwa na Wizara na Serikali kupunguza matumizi

na kukusanya kodi, ninapenda kushauri kuwa Wizara ifanye marekebisho katika sehemu zifuatazo:-

(a) Posho za US$504 kwa siku zinazolipwa kwa safari yoyote nje ya nchi ni kubwa ukilinganisha na uchumi wetu na hasa ukichukulia kuwa ni kubwa kuliko zile za Taasisi za Umoja wa Mataifa na nchi zilizoendelea. Ushauri wangu ni kupunguzwa posho hizi zilingane na zile za Umoja wa Mataifa, ambazo pia zinategemea miji na hata hoteli anayokaa msafiri. Hii itatupunguzia matumizi kwa zaidi ya shilingi bilioni mbili. Pia kwa kuamua kuwa safari zote za nje wasafiri watatumia daraja la kawaida la ndege, tutaweza kupunguza gharama hizo kwa wastani wa shilingi milioni nane kwa kila msafiri, ambapo kwa jumla ya wasafiri wote kitakuwa ni kiwango kikubwa.

(b) Ninaunga mkono azma ya Serikali ya kuzitaka taasisi zake zichangie bajeti zaidi ya wanavyofanya hivi sasa. Ili hili lifanikiwe, itabidi kuongeza tija za utendaji kazi katika taasisi hizi moja moja na zote kwa jumla, kwa kuondoa tofauti kubwa zilizopo kati ya mishahara ya taasisi hizo na hata ndani ya taasisi zenyewe. Haiyumkini kuwa katika nchi hii baadhi ya Wakurugenzi Wakuu wanapata mishahara ambayo ni zaidi ya mara tano ya Mawaziri, ukiachilia mbali Maafisa Waandamizi Wizarani, ambao wanatakiwa wawasimamie moja kwa moja. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuainisha mishahara hii kwa kuipunguza ile mikubwa bila kuathiri utendaji kazi. Vilevile taasisi hizi zisiruhusiwe kujipangia posho ambazo ni kubwa zaidi ya zile za Serikali.

(c) Uwekezaji kupitia Sheria ya Ushirikiano wa Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partneship),* uharakishwe kwani muda mwingi unatumika tangu Julai 2010, kuutayarisha tu badala ya kuanza kutumika. *PPP* ilivyo sasa irekebishwe isiwe imejaa ukiritimba na mlolongo wa idhini zisisokuwa na mashiko kama ilivyo sasa. Tathmini iliyofanywa na mamlaka ya viwanja vya ndege kuhusu Mradi wao mmoja itachukua takriban miaka mitatu kufuata taratibu za *PPP* zilivyo sasa kabla hata Mradi wenyewe kuanza.

(d) Imani yangu ni kuwa Mapinduzi ya Viwanda Tanzania yamo ndani ya Mapinduzi ya Kilimo na hii inawezekana tu kwa kushughulikia kuanzishwa viwanda kwa nchi mbili, kabla ya kulima na baada ya kuvuna. Tuanze kuangalia siyo tu viwanda vya kusindika mazao ya shamba, bali pia vile vya kutengenezea pembejeo za ukulima yakiwemo matrekta. Hatuwezi kufanikisha kilimo kama tunaendelea kuagiza nyenzo za ukulima kutoka nje. Nilitarajia bajeti hii ianze kulifanya kazi hilo. Ninaunga mkono ushauri uliotolewa na Wabunge wengine kuhusu kuendeleza Zao la Pamba na Korosho. Nami naomba niongezee Zao la Mkonge ambalo bado lina nafasi kubwa kuendelea kuwa mkombozi wa nchi hii kupitia wakulima wadogowadogo, wenye tija, hasa pale ambapo bei yake inapanda na faida zake ni nyingi zaidi ya yale ya kamba ya zamani, kiasi ambacho karibu asilimia tisini ya zao hili inatumika kwa faida mbalimbali kulingana na asilimia kumi tu hapo zamani.

(e) Tumewekeza kwenye taaluma bali hazitumiki kikamilifu kwa vile wataalamu hao hawawezeshwi kutumia taaluma zao kwa maendeleo ya nchi na hasa kuwa wabunifu. Nchi hii ina wahandisi zaidi ya elfu saba bali hatutengenezi hata baiskeli zetu wenyewe. Katika Mifuko ya Benki zinazoanzishwa, kingeanzishwa Kitengo cha kulenga kuwakopesha wataalamu hawa ili wapate pesa za kutumia taaluma zao waweze kujiajiri kwa tija na kuzalisha ajira kwa Watanzania wengine ili kuchangia vitendea kazi na bidhaa zizalishwazo nchini. Vyote hivi vikishughulikiwa, tutakuwa tumeweza kuelekea kwenye maendeleo ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuwapongeza Waziri Fedha na Waziri wa Mahusiano na Uratibu, kwa uwasilishaji wao mzuri wa bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie hoja kama ifuatavyo:-

Kwanza, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi ya makubaliano ya Muungano ni mapato ya Muungano, ambayo Zanzibara ilitakiwa kupata asilimia nne nukta tano. Je, mbona Serikali kupitia Wizara ya Fedha haikueleza kuhusu mapato haya ya mgao wa mapato ya Muungano? Naomba maelezo ya kina.

Pili, naipongeza Serikali kwa kuwa na Mpango mzuri ambao ukitekelezwa kwa umakini na uadilifu, utaweza kubadilisha hali ya nchi na watu wake mara moja. Kwa hiyo, naomba Serikali ijifunze kutokana na upotevu wa fedha uliotokea hasa kwenye Miradi yetu ya Maendeleo. Hivyo, wakati umefika sasa tujielekeze katika kufuatilila fedha za maendeleo zinavyotumika na pia zitumike kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo.

Tatu, Serikali ijitahidi kutekeleza ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. Mradi huu uharakishwe ili uweze kuleta ajira kwa wananchi, kuondoa tatizo la umeme na kuondoa tatizo la uharibifu wa mazingira, kwani wananchi wengi watatumia gesi kwa matumizi ya majumbani, viwandani na matumizi mengine.

Nne, naishukuru Serikali kwa kutenga Fedha kwa Benki ya Wanawake. Hivyo, ningeshauri Serikali itekeleze hili kwa haraka, kwani itasaidia sana wanawake wenye kipato cha chini ambao ni wengi.

Tano, naishauri Serikali ifute au iondoe kabisa tozo kwenye bodaboda. Serikali ifahamu wanaofanya kazi hii ni vijana wanaotafuta ajira kupitia kazi hii na hawana njia nyingine ya kuwaingizia kipato, lakini pia usafiri huu unasaidia sana wanyonge ambao wana kipato cha chini katika shughuli zao za kuendeleza maisha ya kila siku. Hivyo, Serikali iondoe kabisa kodi kwa wenye bodaboda.

Mwisho, naishauri Serikali izidi kuboresha Bajeti ya Wizara ya Kilimo ukizingatia asilimia themanini ya

Watanzania ni wakulima na wanaotegema kilimo kwa ajili ya kuendesha maisha yao; hivyo, iongeze Bajeti ya Kilimo. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba ni-*declare interest,* familia yangu ipo kwenye biashara nyingi kama pamba, katani, korosho, mahindi, viwanda na sukari.

Mfumko wa bei: *I advise the government to use hedging instrument in the world commodity future markets and take positions in fuel mainly.*

Viwanda vya nguo na mavazi: Sera ya Serikali ya Sekta ya Pamba na Viwanda vinavyotengeneza bidhaa za pamba ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa zenye ongezeko la thamani kama vile nyuzi na majora ya nguo. *There is unfair competition from China and India. Their governments are giving subsidy to their cotton farmers or industries. Due to unfair competition, factories have been shutting down over the years. There were 22 factories but now there are only five factories are working that buy local cotton. Please note; textile is one of the largest employer in Tanzania.*

Nashauri viwanda vipewe msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye bidhaa za nguo na mavazi *(zero rated)*. Hatua hii itaongeza uzalishaji wa ajira na ukuaji wa ajira utaongeza kodi ya *PAYE.* Kuna hoja ya wataalamu; *how wili we defferenciate*

*between important cloth or kitenge and local product (orated VAT).*

*For example, if you import kitenge from India you have to pay fifty + VAT input at entry so therefore when you sell the kitenge you have no choice but to charge the consumer the VAT or else you loose your input. While if local textiles get zero rated. They will sell without VAT and be more competitive.  Currently, the same system works in edible oil industry.  Imported oils are charged VAT while local seeds oils are orated VAT. Therefore, I see no problem in the implementation.*

*Production:  All the textile mills can produce 150 million mefas per year, enough to feed the whole country.*

*Edible oil – crude palm oil:  Our local seed production can only contribute to 10% of the total consumption. We still import 350,000 tons a year.*

*By putting a duty of 10% on crude imported oil; automatically the price of oil in Tanzania will increase by 10% creating future inflation.*

*We will become uncompetitive with East African States where we have agreed to have a common external tarrif. Kenya is 0% and 50 is Uganda. We will not be able to sell and compete in bordering cities like Mwanza, Arusha or Moshi and therefore I project Tanzania will import only half the quantity.  This will cause the government a big loss on revenue that is:-*

*Volume/m*

*Current 350,000 Price 1,000 Value 350 m*
*Proposal 10% Price1,000 Value125m*
*If 10% were to be put volumes will fall to half.*
*18%VAT = 63 million collection currently.*
*10% Duty and 12.5 m and 24.7 m Vat and 37 million.*
*Revenue loss, almost 50 billion.*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Nampongeza Rais, kwa umahiri wake wa kutuletea Waziri na Naibu Mawaziri wa Fedha, wenye uwezo wa hali ya juu na wachapa kazi. Nampongeza Waziri na Manaibu wake, kwa kazi kubwa waliyoifanya hatimaye kutuletea bajeti yenye kukidhi haja ya Watanzania walio wengi. Ushauri wangu; kwanza, Serikali isikubali matumizi yatakayojitokeza nje ya bajeti. Matumizi ya fedha za Serikali lazima yawe na nidhamu. Serikali iongeze juhudi katika Sekta ya Kilimo kwani huko ndiko kwenye ukombozi wa kweli kwa nchi yetu. Faida zitakazopatikana ni kama zifuatazo:-

Kupunguza wimbi kubwa la vijana kukimbilia mijini. Ajira nyingi zitafunguka kwa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Kwa hiyo, vijana watakuwa na shughuli za kufanya na kuondokana na ukosefu wa ajira kwa vijana hao. Kuhusu suala la kodi, hii ni sehemu nyingine

ambayo inahitaji marekebisho makubwa yafanyike, ikiwezekana misamaha yote ya kodi iondolewe mara moja. Kwa upande wa madini ni lazima mikataba iangaliwe upya na ile iliyokuwa haina tija ifutwe kwa maslahi ya Taifa na tusiogope kitu. Maeneo ambayo bado hatujafunga mikataba basi tuwe makini kwenye kufunga mikataba hiyo au tusubiri kwanza, kwani hayo madini hayaozi ila yanaongezeka thamani na yatakuja kutusaidia hapo baadaye.

La mwisho, tuimarishe Sekta ya Viwanda vidogovidogo ili kusaidia wananchi vijijini kuongeza thamani mazao yao na kuepukana na unyanga'nyi wa wafanyabiashara wanaokwenda kununua mazao yao kwa bei ya chini kabisa na kuwakatisha tamaa wakulima hao.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, bajeti haielezi kwa uwazi ni namna gani Serikali itawasaidia wastaafu. Serikali kupitia Waziri wa Fedha aliyepita, aliahidi kuwapandishia *pension* wastaafu lakini mpaka leo bado. Lazima Waziri atoe kauli nzito juu ya kupandisha *pension* za wastaafu. Viwanda vilivyouzwa hasa vya kubangulia korosho vimekongolewa na kuuzwa vyuma chakavu *(scrappers).*

- Serikali iwachukulie hatua kali za kisheria wale wote walionunua viwanda na wakashindwa kuviendeleza.

- Bei ya umeme ni kubwa sana na imekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi wanaotumia nishati hii.

Bajeti ipo kimya juu ya adha hii na baya zaidi ni pale watumiaji wanapotozwa kodi *(VAT)* nje ya malipo ya *service charge*.

- Mishahara ya kima cha chini bado ni kidogo kulingana na ukali wa maisha.

- Uangaliwe uwezekano wa kuongeza Bajeti ya Elimu, kiwango cha sasa hakitoshi.

- Suala la Vitambulisho vya Taifa halikupewa kipaumbele kwani hata hizo shilingi bilioni ishirini zilizoahidiwa mwaka jana, wamepewa kiasi kidogo tu cha shilingi bilioni moja nukta sita tu.

- Kiwango cha shilingi bilioni saba kilichotolewa J.K.T. hakiendani na ahadi ya Serikali ya kupeleka vijana elfu ishirini kwenye Makambi ya JKT na huenda watapeleka vijana elfu tano tu.

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Manaibu wake. Naomba Bajeti na Mpango uzingatie yafuatayo:-

Kwanza, mishahara ya Watanzania ni midogo *(across)* sana. Hii pia inawafanya wastaafu wapate mafao madogo sana na hivyo wastaafu hata waliokuwa na madaraka makubwa, maisha yamekuwa ya wasiwasi sana. Mishahara ikiwa mizuri, masuala ya posho ambayo inanufaisha wachache, yatapunguza sana.

Pili, Tume ya Mipango iwe na nguvu zaidi na meno pia na iongeze ajenda ya kuendeleza nchi yetu na Wizara ziwajibike kwa Tume hii kwa utekelezaji wa Mpango. Taarifa ya robo mwaka itolewe na kila Wizara na Tume itoe taarifa kwa Bunge na Rais.

Tatu, madeni ya ndani yote yalipwe ya Walimu na Wanaushirika kwa mfano, *MBICU* – Mbinga wanadai milioni shilingi 400.

Nne, uwekezaji: Sifurahishwi na pia sielewi kwa nini maeneo yaliyochukuliwa na *NDC*, ubia unaofanyika hauridhishi; kwa mfano, Mradi wa Makaa Ngalu.

(a) *Shareholding* ni *70* tutoe *energy 30 NDC*, inaaminika kwamba *NDC* au Serikali haijatoa mchango wowote lakini mkaa ulioko chini ya ardhi hauna thamani. Huu ndiyo mtaji tunaopaswa kukaa nao mezani na kusema tuna hili (mkaa), nawe mwekezaji toa fedha ya kazi. Hivyo, inawezekana kabisa kuwa *equal partners.* Naomba mikataba hii iangaliwe upya.

(b) Umeme: Mradi wa Ngalu umeiva mkaa unachimbwa. Napendekeza *TANESCO* wawe na *shares* katika Mradi huu, pamoja na Mashirika kama *NSSF* na *PSPF* ili tuwe na sauti juu ya Mradi huu.

*Transmission line* ya *132 KV* – Makambako – Songea - Mbinga iwe *upgraded* angalau kufikia *200 KV* na ikiwezekana *400KV* ili umeme ufike wa MW 400 - 600. Mradi huu ndiyo unaweza kutatua tatizo la umeme kwa haraka na siyo bomba la gesi. Napendekeza kwa nguvu sana, pengine *Interministerial Committee*

ingeundwa kuona namna ya kupata fedha ya kuanzisha kampuni ya kufua umeme na mkaa huu.

Tano, Serikali ni lazima iwalipe Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji mshahara na siyo kufanya kazi kwa kujitolea. Huu ni unyonyaji na Mungu hapendi.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kupanga na kuweka mpango mkakati mzuri wa maendeleo. Vile vile naipongeza kwa kuweka bajeti inayoendana na mkakati kama wa mwaka huu wa bajeti. Nitoe mapendekezo machache yatakayoiwezesha Serikali kuwafanya wananchi waone inawatendea haki na kwamba bajeti hiyo ni ya wananchi *(ownership).*

Katika kuwasilisha ni vizuri kuoanisha vizuri *own fund* na *donor fund.* Katika *own fund* tuimarishe fedha za makusanyo ya kodi na tozo mbalimbali, mikopo ya ndani na mikopo ya nje na kwa *donor fund* tuimarishe zile za kusaidia bajeti na zile za maendeleo. Hii itaondoa hali inayojitokeza juu ya fedha za Miradi kuonekana kuwa za *donor* nyingi wakati tunakopa na tutalipa baadaye.

Vilevile ili kuondoa hali ya kutoifanya bajeti ya uwekezaji katika nguvu kazi isionekane kama ni bajeti ya maendeleo, maelezo ya awali yawe yanatolewa kuondoa utata huu.

Nakumbuka pale Benki Kuu kuna *balance sheet* za aina mbili; inayowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Fedha

kwa kuzingatia *(IFRS);* na ile inayoitwa *re-arranged balance sheet* inayowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Uchumi na Sera. Hii ya Mkurugenzi wa Uchumi na Sera inatafsiriwa ya kiuchumi zaidi. Mheshimiwa Mgimwa, najua unalikumbuka hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri wa Fedha haijagusa Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa. Naomba kwenye majumuisho Waziri atoe kauli. Suala la ubinafsishaji ni zito na lenye nafasi kubwa katika uchumi wa Taifa. Mwenyekiti wa Bodi ya *Exim Bank* alipewa Mgodi wa Chumvi Uvinza akalipa shilingi milioni 90, sasa ameng'oa mitambo yote ya *plant* ya *(PVD)* iliyokuwa ikizalisha chumvi kwa umeme ameuza nchini Irani na nyingine Dar es salaam. Hii ni kashfa kubwa na *CHC* wanatambua.

Ajira zinaweza kuongezwa kwa kufufua viwanda vya ndani. Tunataka *exemptions* ziwe kwa wazalishaji wenye uwezo wa kuzalisha ajira. *Textile industries* zilizokufa zinapaswa kufufuliwa dhidi ya ushindani toka Bangladesh na India. Ondoeni au punguzeni kodi kwenye *textile* kwani tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa tunaweza kufufua ajira za wakulima 500,000 na viwanda hivi vinaweza kuajiri watumishi siyo chini ya 10,000.

Kampuni za simu zianze kulipa kodi za hakika. Mpaka sasa mchakato wa kupata mashine ya kurekodi *transactions* hii itasaidia kuokoa takriban shilingi trilioni moja kwa mwaka.

Deni la Taifa siyo tatizo kwani mpaka sasa ni asilimia 56 ya *GDP*, tatizo hapa matumizi yaliyopelekea Deni hilo. Naomba iwe mwiko kutumia mikopo kwa Miradi isiyo na *impact.* Tuendelee kukopa kwa Miradi ya Maendeleo tu; reli, bandari, elimu na kadhalika.

*Rural Development Agency:* Tatizo la maendeleo vijijini linachangiwa na miundombinu vijijini. Hali ya sasa ya kuziacha Halmashauri kusimamia Miradi ya Barabara, inaathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa miundombinu vijijini na hivyo kuathiri uzalishaji na soko.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2012/2013 haijazingatia wananchi wanaoishi vijijini au watu wa hali ya chini sana, imejali watu wa kati na juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti inategemea uwezo wa Taifa lake katika kuhudumia watu wake, basi ningeshauri Serikali ipanue wigo wa ukusanyaji kodi. Watanzania wengi hawalipi kodi, mianya ni mingi ya ukwepaji kutokana na rushwa iliyokithiri katika sekta mbalimbali ambazo zingesaidia kuongeza kodi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imezidi, irekebishwe. Kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana kikatiliwa maanani ili kuifanya ile Dhana ya KILIMO KWANZA iweze kuleta manufaa na hii itasaidia siyo kuongeza mapato ya Taifa tu, bali pia kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ufanyike utaratibu wa kutosha kuhakikisha kampuni za simu za mkononi zinalipa kodi stahiki. Mazingira ya ushindani ya kibiashara yatengenezwe ili kuweza kuvutia wale wote wenye nia njema na nchi yetu kufanya biashara au uwekezaji wenye tija utakaoongeza mapato hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha afuate ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwa kurekebisha vipengele ambavyo vinaifanya bajeti ionekane ina matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa mchango wangu kwa kutoa kilio changu kwa kutotekelezwa kwa ahadi nyingi ambazo zimekuwa zikitolewa hapa Bungeni kama sehemu ya utekelezaji wa bajeti lakini kwa ujumla wake hakuna utekelezaji uliofanyika mpaka sasa. Bajeti kubwa imekuwa tegemezi kwa pesa ya ahadi, ambayo tunajua kwa uhakika pesa hiyo hailetwi yote au haitolewi kabisa na mbaya zaidi pesa hizo za msaada toka nje ndizo tunazoelekeza katika maeneo muhimu sana wakati wahisani hao hawana pesa hiyo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana kulikuwa na ahadi ya kujenga Vyuo vya Ufundi *(VETA)* kila Wilaya, lakini mpaka dakika hii ni chuo kimoja tu kimejengwa nchi nzima. Sasa suala la kujiuliza wakati tunaazimia suala hili na kulitengea fedha tulikuwa tunawaridhisha akina nani? Vijana wengi leo hii wanamaliza Kidato cha Nne katika nchi nzima; je,

wangapi wanapata fursa ya kujiunga na Kidato cha Tano na asilimia ngapi wanabaki vijijijni au majumbani bila kupata fursa za kujiendeleza?

Bajeti hii haijaonesha kuna mkakati gani kwa ambao hawapati fursa za kujiendeleza watasaidiwa nao! Vyuo vya *FDC* havina walimu. Pia hakuna vifaa vya kufundishia *VETA!* Sasa kwa utaratibu huu tunawasaidiaje hawa vijana? Leo hii Serikali haioneshi kwenye taarifa zake ni kiasi gani cha fedha za *EPA* zimerudishwa na kiasi gani cha fedha za Rada zimerudishwa na fedha hizi zimefanya nini au zimepangiwa kazi ipi katika bajeti hii!

Mheshimiwa Spika, leo hii usafiri wa reli umekuwa ni hadithi au ndoto ambayo kutekelezwa kwake haiwezekani. Fursa za maendeleo zimekuwa nyuma kwa sababu suala la uchukuzi limeachwa nyuma sana. Usafirashaji wa mazao ya biashara haupo. Usafiri wa nafuu wa tabaka la wananchi walio wengi haupo na hii inapelekea kutoa fursa kwa uchangiaji mdogo wa uzalishaji na ukuaji wa Pato la Taifa. Ahadi za mwaka jana ilikuwa ni kuimarisha Reli yetu ya Kati lakini jaribio la kushangaza mpaka sasa hakuna hatua za makusudi na za kimkakati za kufufua shirika hilo. Tutenge pesa zetu za ndani ili tuokoe shirika hili ambalo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la ubinafsishaji lazima liangaliwe upya; leo hii viwanda vingi vimekufa au kuchakaa, wawekezaji wapo kwa ajili ya kuimarisha soko la bidhaa zao na kuua bidhaa zetu au kutoa fursa za ajira kwa wananchi wetu. Watu hawa wapo kwa

ajili ya kutengeneza faida tu na siyo kumsaidia Mwananchi wa Tanzania. Nashauri kuwa, wataalam tunao, viwanda hivyo virudishwe Serikalini na wataalam wetu wapewe uwezo na Serikali iwaamini. Naamini kwa hili tutafanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali kuandaa mazingira wezeshi kwa wananchi wake, leo hii usimamizi wa Miradi yetu mingi haufanyiki kwa usahihi na hii inatokana na walio wengi kutokuwa na dhana ya uzalendo na kuona kuwa Miradi hii ni sehemu ya maendeleo ya wananchi hivyo ni mali yao. Rai yangu ni kuwa bajeti iangalie mahitaji, wananchi wa tabaka zote na rika zote. Kuwepo na ushirikishwaji wa ngazi zote katika mipango ya bajeti na kuwepo na vipaumbele ambavyo vinalenga moja kwa moja maisha ya mwananchi wa ngazi ya chini na si wale wachache wenye maisha ambayo yana hali ya unafuu mkubwa. Kwa misingi ya bajeti tunayojadili, naomba iangalie yote niliyoshauri hapo juu ili iwe endelevu na yenye manufaa kwa wananchi wote.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri na imepokelewa vizuri na watu wa makundi mbalimbali. Mimi ninampongeza sana Waziri wa Fedha na Wasaidizi wake, kwa kutayarisha bajeti hii nzuri hasa kwa wakati huu ambapo uchumi wa dunia unashuka kwa kiasi kikubwa. Tumeshuhudia nchi nyingi duniani zimepata mtikisiko mkubwa kiuchumi. Bajeti hii imeonesha ya kwamba, uchumi wetu upo imara.

Bajeti hii ya shilingi trilioni 15 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo italeta huduma na miundombimu muhimu ambayo Watanzania wana kiu nayo. Pia bajeti hii itafungua milango kwa wawekezaji. Bajeti hii itapunguza umaskini, mimi ninataka kuchangia kwenye Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Tunaishukuru sana Serikali kwa kutenga pesa kwa ajili ya TEHAMA. Sekta ya Mawasilianao inakua kwa kasi kubwa, kwa hiyo ni muhimu sana kuwekeza kwenye Sekta hii. Kwa sasa Sekta hii inachangia asilimia 2.2 ya *GDP.* Mimi ninaamini Sekta ya Mawasiliano ina uwezo wa kuchangia mpaka asilimia 55 ya *GDP* kama itasimamiwa vizuri.

Kwa upande wa simu, haitakuwa na tija yoyote kuweka *SIM card registration fee* ya shilingi 1,000 kama ilivyopendekezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha. *Registration free ya SIM card* haitasaidia sana kwenye bajeti. Mapato ya *SIM card* mpya hayatazidi shilingi bilioni 3.6 kwa mwaka. Je, hii itasaidia kweli kwenye bajeti?

Ninaishukuru sana Serikali kwa kuwekeza kwa Sekta ya Sayansi na Teknolojia. Bila ya kuwekeza kwenye Sekta hii, hakutokuwa na maendeleo endelevu.

Ninaipongeza Serikali kwa kupunguza asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwenye ving'amuzi kwa ajili ya digitali. Hii itawapunguzia wananchi wetu mzigo mkubwa. Mpango huu utawawezesha wananchi

wengi kupata matangazo ya TV ya kisasa na bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kwa maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona Deni la Taifa linazidi kuongezeka kwa asilimia 38 kutoka shilingi trilioni 10.5 mwaka 2009/2010 hadi shilingi trilioni 14.4 mwaka 2010/2011 kufikia 2012. Nashauri *special audit* ifanyike katika Deni hilo ili Watanzania wajiridhishe kwani ndiyo walipaji wa deni hilo. Wakati Serikali inatoa majibu itueleze pesa hizo zimetumikaje na mchanganuo uletwe Bungeni ili Wabunge tujiridhishe, lakini umuhimu wa kufanya *special audit* upo palepale.

Bajeti ya Serikali inaonesha kuwa Serikali itakopa fedha zenye masharti ya kibiashara ndani na nje, yenye thamani ya shilingi trilioni 2.89 kwa kipindi cha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya aina hii ina riba kubwa lakini Serikali imeeleza mkopo tu bila kujumuisha italipa lini na kwa muda gani na kwa riba ya kiasi gani. Nashauri Serikali iachane na mikopo ya aina hii bali ijikite kuangalia vyanzo vingine vingi vya mapato ili kuongeza wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2012/2013 haimgusi Mtanzania wa chini kwani haijibu maswali yake ya ugumu wa maisha unaosababishwa na mfumko wa bei unaoongezeka kila siku, ambapo sasa

umekuwa kero kwa Watanzania wa kipato cha chini kabisa. Inasikitisha kuwa karibu shilingi trilioni 5.1 itakopwa na madeni hayo yatatokana na mkopo wa kibiashara ambayo ni mikopo ghali mno. Bajeti hii ni ya kulipa madeni zaidi kuliko kuchochea maendeleo ya nchi. Inatia uchungu kwamba, Serikali ya Tanzania inamiliki magari ya zaidi ya shilingi trilioni tano. Halafu inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.1; kwa nini Serikalli imiliki magari ya kifahari wakati haina uwezo hata wa kujiendesha? Ushauri magari ni kwamba, yote yapigwe mnada halafu uwepo utaratibu wa kuwakopesha magari watumishi wanaostahili kuwa nayo ambao watayatunza kuliko gharama za uendeshwaji wa magari hayo. Kwa kufanya hivyo, tutaepuka matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa bajeti hii ya sasa unaonesha asilimia 70 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 30 kwa bajeti ya maendeleo. Je, nchi hii itaendelea kweli? Kwa nini Serikali imetayarisha bajeti hii bila kuzingatia masharti na mapendekezo ya Bunge katika kupitisha Mpango wa Maendeleo uliopitishwa kwa mujibu wa kifungu cha 63(3)(c). Mpango wa Maendeleo ulisema kuwa, asilimia 35 ya mapato ya ndani ya Serikali itatengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo lakini haikutengwa. Nashauri na naitaka Serikali, kwa mujibu wa Katiba yetu inayolipa Bunge mamlaka ya kuisimamia Serikali, ije na majibu kwa nini imekiuka Mpango wa mwaka wa Maendeleo wa kutenga asilimia 35 ya pesa za ndani kwa ajili ya maendeleo yetu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusoma Bajeti ya 2012/2013, kumeibuka hisia na maoni mbalimbali kutoka kwa watu wa kada tofauti kote nchini. Binafsi napenda kutoa hoja zifuatazo:-

Kumeibuka hali ya ushindani wa kisiasa wa kila mmoja kwa nafasi yake kuonesha umwamba wa kubishana na kutukana badala ya kujikita katika hoja mahususi kwa manufaa ya wananchi.

Pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutoa hoja za matusi, bajeti ya maendeleo ni ndogo sana ukilinganisha na fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kupungua kwa bajeti ya maendeleo kunakwamisha sana utekelezaji wa maendeleo hasa Miradi mipya na ya zamani.

Serikali imeendelea kutegemea au kuegemea vyanzo vilevile vya vya mapato vya siku zote. Kwa mfano, Sekta ya Madini imeachwa au haijaguswa kana kwamba haigusi rasilimali za nchi. Sekta hii imefanyiwa au imeainishwa kuwa ya hiari aidha kuchangia uchumi wananchi au la.

Katika bajeti hii Serikali inajisifia kuwa Deni la Taifa linalokua linastahimilika. Hili siyo jambo la kujivunia na inasikitisha sana kuona Serikali inafurahia deni kukua bila kuchukua hatua madhubuti za kulipunguza. Ni vyema Serikali ikajizatiti katika kuongeza wigo wa mapato ili nchi ipunguze kabisa hali ya ukopaji nje au ndani na hivyo kupunguza mizigo ya deni kwa taifa.

Mfumko wa bei unaendelea kulitesa Taifa na bado Serikali inaendelea kurudia mipango ile ile iliyotumia mwaka jana, mwaka juzi na kadhalika kushughulikia tatizo hili. Kitendo cha Serikali kuondoa au kufuta kodi kwa waagizaji wa baadhi ya bidhaa mfano sukari na mchele, imeleta hasara kwa namna mbili: Moja, Serikali imepoteza mapato kwa kuwaamini walaghai hawa waingizaji. Pili, bado bei ya bidhaa hizi ilipanda tena kwa kasi kubwa sana na hivyo kutokuwepo na ile mantiki ya unafuu wa bei ya mazao haya. Ni vyema Serikalli ikawa makini katika utoaji wa vibali vya uingizaji bidhaa kwa wafanyabiashara ambao watafanya kila wawezalo kujinufaisha na huku Serikali na wananchi wake wakibaki kulaumiana na kutoaminiana.

Hitimisho katika maelezo haya ni kama ifuatavyo:-

Serikali ni vyema ikasikiliza hoja zinazotolewa na wadau mbalimbali kuhusu upungufu wa bajeti na kuufanyia kazi ili kufikia malengo yaliyotarajiwa. Ni vizuri Serikali ikajiepusha na ushabiki wa kisiasa na badala yake iwe makini katika kuchukua hoja ambazo zina manufaa kwa Taifa bila kujali aliyetoa hoja husika. Itapendeza Serikali ikihoji yenyewe kwa nini kila mara inarudia mambo yale yale katika bajeti?

Pili, ni lini rasilimali zilizojaa Tanzania zitawanufaisha wananchi?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti. Naipongeza Serikali kwa kupunguza kiwango cha ushuru wa mvinyo utokanao

na mvinyo unaozalishwa humu nchini. Wakulima wa Dodoma, tunapongeza sana hatua hiyo na tungeliomba zao la zabibu liendelee kuangaliwa kila mara na hata ikibidi tupatiwe ruzuku ya kuzalisha zabibu kwa kuwapa motisha wakulima waweze kuzalisha zao hili la zabibu ambalo litawaongezea kipato wakulima wa Dodoma kwa kuwa moja ya zao la biashara. Kwa kuongeza kilimo cha zabibu, tutaongeza viwanda vya mvinyo na kuongeza ajira pia.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu kwa Serikali kuweka misingi mizuri ya uanzishaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)*. Inavyoonekana sasa, *SACCOS* nyingi zinaachiwa zijiendeshe zenyewe bila kuwa na usimamizi wa karibu. *SACCOS* zikisimamiwa vizuri zitakuwa ni chanzo kizuri cha kuanzisha Benki za Wananchi. *Community Banks* imara ambazo zitafanya kazi karibu sana na wananchi na kuwatengenezea wananchi mazingira ya kujiwekea akiba na kujipatia mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Benki ya Kilimo uharakishwe kwa kuwa kukosekana kwa Benki hiyo wakulima wanakosa benki ya uhakika ya kuwapatia wakulima mitaji ya kuendeleza kilimo. Masharti yaliyopo kwenye dirisha dogo la kilimo chini ya *TIB* hayavutii na yanakatisha tamaa.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, suala la bodaboda kweli waondolewe kodi lakini naiomba Serikali iangalie hili kwa makini ili matajiri wasikimbilie kwenye biashara hiyo ya bodaboda kwa

kuweza kumiliki zaidi ya vyombo vitano na kuwakosesha vijana wetu ajira kama azma yetu ilivyokusudia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke mkakati wa nguvu ili makusanyo ya kodi yasisuesue tukakosa fedha za maendeleo. Naomba sana upungufu kama huu usitokee katika Bajeti ya Mwaka huu wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja mia kwa mia, Bajeti hii ipite bila kupingwa. Ninaipongeza Wizara kwa Bajeti nzuri; ninaunga mkono.

Maoni yangu ni kwamba, iongezwe pesa katika uzazi wa mpango, lishe, Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Jinisia na Watoto na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, swala la bodaboda liangaliwe upya.

Sherehe za Serikali ni nyingi mno, ziangaliwe upya. Kitendo cha Wizara mbalimbali kuzunguka nchi nzima kufanya sherehe za Wizara zao, kinapoteza fedha; kuwepo Sherehe Maalum za Kitaifa tu kama Kilimo (Nane Nane), Biashara (Saba Saba) na UKIMWI. Chagueni chache tu.

Mheshimiwa Spika, majumba yanayotumika kwa makazi yasitozwe kodi watu wanashindwa kulipa,

yatozwe yale yanayotumika kwa biashara tu kama *guest house,* hoteli na kadhalika.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, nina machache ambayo ningependa nipatiwe majibu kwani ninafahamu juhudi ya Serikali yetu katika kuletea maendeleo ya nchi na wananchi wake. Tunaona ujenzi wa barabara, vituo vya afya, zahanati, hospitali, shule za sekondari na msingi, kilimo na viwanda. Pia huduma za maji safi na salama, yote ni kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Sasa hoja yangu ni kuomba bajeti ya maendeleo iko kwenye asilimia 30; kwa nini isingesogea kufikia asilimia 35 – 40? Matumizi ni shilingi trilioni kumi, wakati bajeti halisi haikufika huko; sasa fedha za ziada tutazipataje?

Mheshimiwa Spika, kuna viporo vingi vya Miradi ya Maendeleo, kwa mfano, Mkoa wa Pwani, Ujenzi wa Barabara na hata Miradi ya Umwagiliaji na Umeme. Je, kwa kiwango hiki cha bajeti ya shilingi trilioni nane na matumizi ya shilingi trilioni kumi; hizo 2.8 trilioni tutazitoa wapi ili kuweza kuendeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo hususan kwa ile ambayo imebaki?

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu ili niwaeleze vizuri wananchi wangu wasipotoshwe na wapinga maendeleo.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Mgimwa, kwa kuteuliwa kubeba dhamana ya nchi hii, kwa kuwa ndiyo Kiongozi wa

maisha ya Watanzania kiuchumi. Pili, nawapongeza Manaibu wake, kwa kuteuliwa kuwa Wabunge na baada ya hapo kuwa Naibu Mawaziri wa Fedha. Hii ni wazi kuwa wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye Bajeti yetu, napenda kusema kuwa bajeti hii haina tofauti sana na Bajeti iliyopita ya 2011/2012. Kwani iko wazi kwamba, tunachotumia sicho tunachokusanya, tunakusanya kidogo na tunatumia kingi. Huu ni udhaifu; ni wakati mwafaka sasa tuongeze makusanyo ili yaweze kupita matumizi. Pia Bajeti ya Maendeleo tunayopitisha mara nyingi hutegemea fedha za wahisani na mikopo. Tumeona wazi katika Bajeti ya 2011/2012 ambayo pesa za maendeleo hazikukimu bajeti ambayo tuliidhinisha katika Wizara, hawakupata Bajeti halisi. Katika kila Wizara hawakupata Bajeti halisi ambayo tuliidhinisha; hivyo, hali ilikuwa mbaya katika utekelezaji wa Miradi yake. Angallia Bajeti ya Ujenzi, Miradi yote imesimama labda ambayo hatutengenezi sisi. Naiomba Serikali isimamie vizuri ukusanyaji wa mapato kwa uwazi na kwa wafanyakazi wengi zaidi ili tuweze kukusanya mapato ya kutosha pia tuangalie zaidi eneo la madini na uvuvi wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, katika Bahari ya Hindi kuna meli nyingi zinavua bila kulipa kodi na hasa zitokazo nje ya nchi; ni wajibu wa Serikali kufuatilia meli hizo kwa kufanya doria kwenye bahari katika maji marefu (kina kikubwa), ndiko meli hizo ziliko kwani ni za kisasa zaidi na zinavua katika kina kirefu.

Mheshimiwa Spika, pia ni bora Serikali hii ikafanya bidii ya makusudi kuweza kurekebisha kodi ya madini na misaada ya wawekezaji wa madini. Kuamua kwa dhati kuongeza mrabaha na pia kama mrabaha umeongezeka kidogo kwa Serikali; nini ongezeko la wakazi wanaozunguka migodi hiyo? Hali za miradi ya kijamii siyo nzuri sana; ni bora ongezeko hilo likitokea litawasaidia sana wananchi wanaozunguka migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia zao la pamba hapa Tanzania ni adhabu kulima kwani wakati wa mauzo ni tabu tupu; hivyo, tuwe na nia ya dhati ya kuhuisha viwanda vinavyotumia zao la pamba ili kutengeneza bei bora ya pamba na kuwapatia wakulima wake maisha bora kwa faida ya zao lao. Wakulima wa korosho na kahawa lazima tukae na tujitathmini kama nchi, tukifanya hivyo tutaongeza viwanda; ni wazi ajira zitaongezeka na kodi pia itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kama Tanzania, ni bora sasa tukaangalia maeneo mengine ambayo yanaweza kuongeza mapato na siyo kila kukicha soda, pombe, sigara; hivi siku watu wakigoma kunywa pombe na kuvuta sigara hali itakuwaje? Sasa tuangalie madini, uvuvi na mambo ambayo yanaleta kodi kwa wingi. Hivi sasa kila ardhi ya Tanzania ina madini mengi. Tukiamua tutaweza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, naanza na kusema kuwa suingi mkono hoja hii.

Nasema hivi kwa sababu bajeti hii haikulenga kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kuhusu mfumko wa bei. Mfumko wa bei umekuwa ukiongezeka siku hadi siku kutoka asilimia 13.0 Julai 2011 hadi kufikia asilimia 16.8 Septemba hadi kufikia asilimia 19.8 Desemba 2011. Hii yote inasababishwa na kuporomoka kwa shilingi, upandaji wa bei ya mafuta, upungufu wa nishati ya umeme na ukame. Takwimu zinaonesha kuwa, mfumko huu wa bei ni matokeo ya matumizi makubwa ya Serikali yasiyokuwa na kipimo. Mapato yote ya ndani shilingi trilioni 4.7 hayakidhi hata matumizi ya kawaida, matumizi ya kawaida yanakuwa makubwa kwa sababu Serikali inaongeza matumizi ya kiutawala kuliko ya maendeleo.

Kama kweli Serikali imekusudia kupunguza ukali huu wa maisha kwa wananchi wake, basi ingeliipa kipaumbele Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo katika bajeti ya 2011/2012 ilitenga asilimia 2.92 ambapo haifai na maisha yamezidi kuwa magumu. Kilo moja ya mchele ni shilingi 2,600 wakati mchele huu unalimwa hapa hapa Tanzania. Sekta hii ya Kilimo ingepangiwa angalau asilimia 10.0 ili chakula kilimwe kwa wingi na bei ya chakula ipungue na wananchi wajikwamue kiuchumi.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nianze na kutounga mkono Bajeti hii na kuungana na wachangiaji wengine kuwa Waziri wa Fedha airudishe na kuifanyia marekebisho kwa baadhi ya maeneo kama kilimo, ufugaji, afya,

miundombinu, elimu na misamaha ya kodi. Kwa nini mfumko wa bei uko juu sana ambapo unazidi kumkandamiza Mtanzania?

Bajeti ya 2011/2012 ilikuwa asilimia 35, Bajeti ya 2012/2013 itakuwa asilimia 30; kwa nini ishuke badala ya kupanda?

Mheshimiwa Spika, nami siungi mkono Bajeti irudishwe na kurekebishwa upya.

**MHE. SARA MSAFIRI ALLY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara – Dar es Salaam hadi Tanga kupitia mkopo kutoka *Exim Bank* ya China. Naamini itapunguza mgawo wa umeme, itaongeza uzalishaji viwandani na pia itapunguza makali ya gharama za maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya kugharamia Miradi ya *SAGCOT* ambayo ni Mpanga Ngalimila, Itete, Sonjo na Lupiro. Fedha hizi ni kwa ajili ya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro ambapo kila Mradi umetengewa shilingi bilioni moja tu.

Mheshimiwa Spika**,** sikubaliani kabisa na Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Umwagiliaji ya *SAGCOT.* Kwanza, fedha zilizotengwa hazitoshi, jambo ambalo linapingana na Mpango wa Maendeleo ya Taifa ambapo kipaumbele cha kwanza ni kilimo. Aidha, tumeahidi kwa Watanzania wakiwemo wapiga kura wangu kwamba, Serikali imedhamiria kuzalisha

chakula cha kutosha kupunguza gharama za maisha. Hivyo, fedha zilizotengwa na kazi zinazofanywa ni dhahiri bado Serikali haijadhamiria kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo ya Kilimo imetengewa shilingi bilioni 76 tu. Fedha hizi ni chache sana, hazitoshelezi kwenye utekelezaji wa Maazimio ya Serikali ya kufanya kilimo kiwe cha kisasa cha kuwanufaisha wakulima, chakula cha kutosha na kuongeza ajira hasa kwa vijana.

Nashauri fedha ziongezwe kwenye kilimo na fedha hizo zipunguzwe kutoka kwenye Miradi ya *EPZ* ambapo shilingi bilioni 50 zimetengwa kulipa fidia wananchi, jambo ambalo lingeweza kufanywa na hao wawekezaji kwani hii ni *private sector,* ambapo baada ya kufanya uzalishaji basi gharama hizo za fidia ziingizwe kwenye *production cost* na siyo Serikali kuchukua fedha za walipa kodi kuzipeleka kwenye *private sector*. Serikali inatakiwa kupeleka miundombinu kwenye maeneo ya uwekezaji tu. Maswala ya fidia yakatwe kwenye gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezeka ushuru wa bidhaa kwenye muda wa maongezi *(airtime)* kwenye simu za mkononi kutoka asilimia kumi kwenda asilimia 12; nashauri hizo gharama ziongezwe kwenye makampuni ya simu siyo kwa walaji (wananchi) kwa sababu Makampuni ya Simu ya Tigo, Voda na Zantel, hayapo katika orodha ya walipa kodi bora kutokana na Taarifa ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa Bungeni.

Kampuni ya Chibuku ipo kwenye kumi bora. Kampuni za Simu za Kenya zinachangia Pato la Taifa kwa asilimia tisa, Uganda asilimia tano, Tanzania asilimia mbili na nusu. Hii haikubaliki kabisa, lazima Serikali idhibiti mapato yanayotokana na makampuni haya ya simu kwani ni dhahiri kabisa upo uzembe katika kudhibiti mapato.

Mheshimiwa Spika, aidha, wananchi wanalipia huduma za M-PESA, kupitia kampuni hizi za fedha ambapo pia nako wanatozwa. Serikali inakata inachukua asilimia 18 *VAT,* asilimia 10 *exice duty,* ambapo jumla ya tozo wanazotoa wananchi katika kupata huduma ya kupiga simu ni asilimia 26. Hivyo, siyo sawa kuwaongezea gharama wananchi.

Mheshimiwa Spika, mkulima anapiga simu kuuliza bei ya soko la bidhaa anazozalisha, wanafunzi wa vyuo vikuu na sekondari wanatumia huduma za simu kutafuta taarifa mbalimbali zinazowasaidia katika masomo yao na kufanya *research.*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya simu siyo anasa ni kichocheo cha maendeleo na kinapunguza gharama na kuokoa muda. Nashauri gharama zisiongezwe kwani Watanzania tunatarajia gharama hizo zishuke chini zaidi kutokana na kuanza kwa matumizi ya Mkongo wa Simu wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naamini patakuwepo marekebisho ya Bajeti, mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapohitimisha Hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES F. MBATIA**: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwa hapa leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete, kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 66(1)(e).

Mheshimiwa Spika**,** napenda kutoa salamu zangu za pole kwa Mheshimiwa Joseph R. Selasini (Mb), kwa kupata ajali mbaya ya gari, mnamo tarehe 24 Mei, 2012 iliyopelekea kupoteza uhai wa mama yake mzazi na ndugu wengine watatu. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi; amina.

Ajali hiyo pia ilimsababishia majeraha makubwa yeye na mke wake, Ndugu Digna Kavishe. Nawatakia wote wapone haraka ili waendelee kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na Wanachama wa CHADEMA, kwa msiba wa kuondokewa na Mwasisi wa Chama hicho, Mzee Mohamed Ally Nyanga (Bob Makani). Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika**,** nianze kwa kusema kupanga ni kuchagua, Bajeti nii imeandaliwa kwa ajili ya kutekeleza sehemu mojawapo ya mipango ya kuleta maendeleo ya Taifa letu; maendeleo ya kukuza Utu wa Mtanzania. Bajeti hii ni kioo au kivuli cha utamaduni wetu wa kuwa na matumizi yanayozidi kipato. Asilimia 70 ya Bajeti yetu ni matumizi ilhali asilimia 30 tu ni kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Matumizi yanayozidi kipato yanakinzana na asili ya mwanadamu. Siasa za kulalamika zinadidimiza Utu wa Taifa letu. Hivyo, napenda kushiriki katika kuboresha Bajeti hii ili kukuza Utu wa Taifa letu badala ya kulalamika na kupoteza muda tuliopewa wa kulitumikia Taifa. Pamoja tutashinda.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuongeza mapato yetu kwa kiasi kikubwa kwa kubadilisha vipaumbele vilivyowekwa katika bajeti hii na pia tunaweza kupunguza matumizi yetu kwa kiasi. Penye nia njema pana njia!

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na upande wa kuongeza mapato ya Taifa. Jambo hili linaendana moja kwa moja na kubadilisha utamaduni wetu wa kutowajibika hasa katika kutumia rasilimali watu; ujanja wa kukwepa au wa kutokulipa kodi zinazostahili; ubadhirifu wa fedha na mali za umma na matumizi mabaya.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano michache:-

Kwanza, kwa kushughulikia tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam tutapunguza

upotevu wa rasilimali za Taifa zenye thamani ipatayo shilingi bilioni 1,460 kwa mwaka na kuanzisha mpango wa kutengeneza ajira za kudumu hasa kwa vijana watakaopenda kufanya kazi za kilimo.

Mheshimiwa Spika, msongamano huo husababisha upotevu wa nishati ya mafuta yanayotumika kwenye magari, rasilimali muda, uchafuzi wa mazingira na pia husababisha msongo wa mawazo. Ni ukweli usiopingika kwamba, katika dunia ya leo njia kuu za usafirishaji zipo nne; maji, reli, barabara na anga. Njia inayotumika zaidi ni maji, ikikadiriwa kuwa na asilimia 92 katika kukuza uchumi wa nchi kwa kuwa na uwezo mkubwa wa kukuza na kuendeleza Biashara za Kimataifa kupitia bandari, ikifuatiwa na reli, halafu barabara na mwisho ni njia ya anga.

Pili, kwa kufuta baadhi ya misamaha ya kodi isiyokuwa na tija kwa Taifa na kwa Watanzania ili kukuza Utu wa Mtanzania. Takwimu zinaonesha kuwa, kwa mfano, mikataba ya kutoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya *NGO,* zilizopewa hadhi ya upekee tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza bila kikomo; mojawapo ya *NGO* hizo ni *Agha Khan Foundation*.

Mheshimiwa Spika, *Agha Khan Foundation* huduma zake hutolewa kwa gharama kubwa na hivyo kutowafikia walengwa ambao ni Watanzania wa kipato cha chini. Badala yake hutoa huduma zake kwa tabaka la walionacho. Mwenendo huu unakatisha tamaa *NGOs* nyingine za wazawa wa Taifa letu.

Pili, misamaha inayotolewa kwa makampuni ya uchimbaji wa madini itathminiwe upya kwa kuangalia maslahi yenye kuleta tija kwa Watanzania. Takwimu zinaonesha kuwa msamaha wa kodi wa zaidi ya shilingi milioni 109,886 kwa mwaka 2010/2011 na shilingi 92,658,000 hadi kufikia mwezi Februari, 2012 kwa makampuni ya uchimbaji wa madini ilitolewa.

Takwimu za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka unaoishia Juni 2011, misamaha ya kodi kwa ujumla wake iliyotolewa imefikia shilingi 1,016,320,300,000. Taarifa hiyo inaonesha kuwa, misamaha ya kodi imeongezeka hadi kufikia shilingi 335,652,400,000 au sawa na asilimia 49 kutoka shilingi 680,667,900,000 kwa mwaka 2010.

Taarifa hiyo inazidi kueleza kuwa, kama misamaha hiyo ya kodi isingetolewa, Taifa lingeweza kupata kiasi cha shilingi 717,431,844,378. Mapendekezo yangu katika kutoa misamaha ya kodi izingatie hasa katika Sekta ya Kilimo kwa ujumla wake, vifaa vya usindikaji wa maziwa na mazao mengine katika viwanda vya ndani. Katika kusisitiza hili la usindikaji wa maziwa na mazao mbalimbali, Serikali ingetoa msamaha wa kodi sifuri ili kufanya maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa na mazao mengine kuwa katika ushindani wa usawa na nchi zingine za Afrika Mashariki hasa nchi za Kenya.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi sifuri ulenge pia kwenye usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini. Hii itasaidia katika

kuendeleza uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi na kufanya bidhaa zetu kushindana Kimataifa na kuweza kulipatia Taifa hili mapato makubwa. Kwa kuweka mkakati madhubuti wa kuhamasisha wananchi kuhusu mpango wa kuzuia upotevu wa maji katika mabomba makubwa, kampuni za usambazaji maji nchini zitaongeza mapato yake. Kwa kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kutolipa kodi mfano: (a) Sheria ya *Tanzania Investment Centre (TIC),* (b) kodi ya mapato ya mali na (c) kodi ya kipato.

Mheshimiwa Spika, nitaelezea kwa kifupi Sheria ya *TIC.* Msamaha wa kodi chini ya Sheria hii unatumiwa vibaya na baadhi ya wawekezaji na hivyo kusababisha upotevu wa shilingi milioni 228,514 kwa mwaka 2010/2011. Hii inatokea wakati mwekezaji anapoingiza nchini au kufanya manunuzi nchini ya bidhaa za ujenzi ziitwazo "*Deemed Capital Goods*" kwa kiasi kikubwa kuliko mahitaji ya Mradi husika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza unafuu wa kodi katika bidhaa za mitaji (*Deemed Capital Goods),* uwekewe utaratibu wa kutambua baadhi ya vifaa kwa wawekezaji tofauti na hali ya sasa ambapo kibali cha uagizaji kikishatolewa na *TIC,* wawekezaji wamekuwa wakiingiza bidhaa nyingi tofauti na kibali kilichotolewa na *TIC*.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ninapendekeza kuwa, *Tanzania Revenue Authority (TRA)* kwa kushirikiana na *TIC,* wapewe nguvu ya kisheria ili kufuatilia na kuratibu machakato wa utoaji wa unafuu, pamoja na kufuatilia kama misamaha hiyo ya kodi,

inatumika kwa usahihi kudhibiti na matumizi yake wakishirikiana na wataalum wa tathmini wa vifaa *(BQ).*

Kodi ya mapato ya mali: Mpaka sasa Sheria ya Mapato ya Mauzo ya Mali haijaweka masharti yenye kueleweka ya kutathmini kwa uhakika ukuaji wa thamani ya majengo. Hivyo, wamiliki wanauza majengo yao kwa kukadiria. Pia hakuna taaluma ya kutosha inayotumika kukadiria kwa usahihi thamani ya majengo yanayouzwa. Mpaka sasa hakuna utaratibu mzuri wa kisheria wa kusajili ardhi na majengo. Kupatikana kwa Hati ni jambo gumu sana, lenye kero kubwa, japo bila hati ya umilikaji ardhi, uchumi wa nchi utaendelea kuwa wa kusuasua.

Kodi ya mapato: Ninachelea kusema kuwa, vyanzo vya mapato katika nchi hii viko vingi sana, kama Serikali na Idara zake watakuwa wabunifu wa kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kubuni njia mpya na endelevu za ukusanyaji wa kodi bila kutoza kiwango kikubwa cha kodi kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongeza kima cha chini cha kutozwa kodi *(threshold)* kwenye mapato ya ajira kutoka shilingi 135,000 hadi 170,000. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, hatua hii itaongeza kipato kwa mfanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama hatua hii itamsaidia Mtanzania. Kwa kutumia mwanya huu, makampuni yamekuwa yakimnyonya mfanyakazi na kumsababishia Mtanzania kuishi maisha yasiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kuwa kiwango cha chini cha kodi ya mapato ya mfanyakazi kipunguzwe kutoka asilimia 16 hadi asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, kuziba mianya hii kutafanyika sambamba na kutoa elimu ya maadili ya ulipaji wa hiari wa kodi na kuboresha utoaji huduma za msingi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika**,** naomba sasa nizungumzie upande wa kupunguza matumizi. Tunaweza kufanya hili kwa kuzingatia yafuatayo:-

Kwanza, kupunguza matumizi ya Viongozi wa Serikali yasiyo ya lazima; kwa mfano, ziara za Viongozi zipunguzwe, ukubwa wa sherehe za Kitaifa upunguzwe, ukubwa wa sherehe za Taasisi mbalimbali za Serikali upunguzwe, ukubwa wa misafara ya Viongozi katika ziara upunguzwe, magari ya kifahari yapigwe marufuku na yaliyopo yapigwe mnada na kadhalika.

Pili, kuwepo na udhibiti mkali katika kulipa madai mbalimbali ya watumishi na wazabuni hasa mishahara hewa.

Tatu, kuwepo uwazi katika gharama za matengenezo ya mali mfano; nyumba, magari, samani za ofisi za Serikali na kadhalika.

Nne, Shule za Serikali zinazotumia kuni kwa shughuli za jikoni zianze kutumia teknolojia mpya ambayo itapunguza matumizi ya nishati hiyo.

Tano, kuwepo kwa uhamasishaji kwa watekelezaji wa sheria za kudhibiti ubadhirifu wa mali na fedha za umma.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kuwa bajeti iliyopo ni ya matumizi, zaidi ya kuzalisha, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuwa na mipango ya sera elekezi za maendeleo *(Development Directives Policies).* Hii itasaidia kuwa na mtazamo wa kuboresha vyanzo vya maendeleo vilivyowekwa katika mipango mikakati inayotekelezeka. Kutokana na kutokuwepo kwa sera madhubuti za mipango mikakati ya maendeleo elekezi, kumekuwa na matumizi elekezi yasiyojulikana.

Pili, kuwa na sera madhubuti ya kubuni vyanzo vipya vya mapato. Matokeo ya Bajeti tuliyo nayo sasa yanaonesha waziwazi kuwa, bado hatuna mikakati ya kubuni vyanzo vipya vya kuongeza Pato la Taifa na lenye kujali Utu wa Mtanzania.

Tatu, kuwa na mfumo wa kuchunguza na kupunguza malipo hewa ya Watumishi wa Umma. Kutokana na hali hii, kumekuwa na upotevu mkubwa wa pesa za umma.

Nne, uaminifu wa ukusanyaji kodi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya kuleta maendeleo ya nchi kama Tanzania lazima iegemee katika kuzalisha zaidi ya kutumia. Bajeti hii haitaweza kukuza Utu wa Mtazania bila ya kubadilisha utamaduni wetu wa kuwa na matumizi makubwa kupita mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maamuzi yoyote hasa katika Bajeti ni lazima kujiwekea vipaumbele ambavyo unategemea kuvifanyia kazi. Hivyo, ninapendekeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sekta ya Kilimo: Uchumi wa Taifa hili hutegemea zaidi kilimo kwa asilimia kubwa (wastani wa asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima). Sekta hii ya kilimo pamoja na kuwekewa Sera ya KILIMO KWANZA na kupewa kipaumbele cha kwanza kwa mwaka wa fedha uliopita (2010/2011), lakini inaonekana kupiga hatua kidogo na kutoendelezwa kuwa kipaumbele kinachotakiwa kufikia dira na dhamira ya Sera hiyo. Hiki ni kipaumbele cha kwanza katika kuliingizia Taifa mapato na kuinua hali za kiuchumi za wananchi.

Mambo yafuatayo yatasaidia kuikuza Sekta hii na kuweza kuinua Utu wa Mtanzania na kumfanya aishi maisha safi na bora:-

- Kukifanya kilimo kuwa kipaumbele cha kwanza hadi pale kitakapofikia dira na dhamira ya sera zake.

- Kuwatumia wataalamu wa kilimo ili kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mbegu bora na utunzaji wa mazao na mifugo yao.

- Kuwa na bei elekezi za mazao zenye kuendana na hali halisi ya maisha ya sasa na hali ya soko.

- Kuwa na Benki ya Wakulima ambayo itakuwa na Matawi katika Wilaya zote nchini.
- Kuwa na misamaha ya kodi sifuri kwa shughuli zote za kilimo ikiwepo usafirishaji, ununuzi wa bidhaa na vifaa vyake na usindikaji.

- Kuwepo kwa mashamba ya kilimo ya mfano.

- Mikopo nafuu kwa wakulima na kadhalika.

Hivyo, ni busara Sekta hii muhimu katika nchi yetu ikatengewa bajeti kubwa kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Miundombinu ndiyo kiungo cha sekta zote katika uchumi wa nchi yoyote ile duniani. Katika kuifanya sekta hii kuwa na tija kwa taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa majini: Tanzania tumejaliwa kuwa na Ukanda wa Bahari wenye urefu wa km 1,424, Maziwa na Mito ambavyo katika kukuza uchumi wa nchi, njia hii ni ya uhakika hasa kwa kusafirisha bidhaa za aina mbalimbali. Inakadiriwa kuwa, Biashara za Kimataifa kupitia njia hii ni asilimia 92. Njia hii ikitumiwa ipasavyo hasa katika Ukanda wa

Bahari ya Dar es Salaam, tunaweza kupunguza msongamano wa magari Jijini na pia kusaidia kutunza barabara zetu. Bajeti hii lazima izingatie kuboresha bandari na vivuko vilivyopo na kuanzisha bandari na vivuko vipya ili kukuza uchumi wa nchi kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, njia hii ya usafiri ni ya haraka, uhakika na yenye kuchukua mizigo mikubwa. Njia hii ya usafirishaji pia ni kiungo kikubwa cha Biashara za Kimataifa. Bajeti ya nchi lazima izingatie umuhimu wa njia hii ya usafirishaji kwa kuangalia miundombinu yake, ukarabati na uendelezajii wake hasa kufikia mpango wa kuwa na reli za kisasa ziendazo kasi ili kuendana na kazi ya ukuaji wa uchumi duniani kote. Kuna haja kubwa ya kuzifufua reli zetu na kuzifanya kuwa za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa Tanzania imekuwa ikitumia usafiri wa barabara kwa usafirishaji wa abiria na mizigo ndani ya nchi hadi nchi jirani. Serikali imekuwa ikijitahidi kutengeneza barabara mpya na kurekebisha zilizopo. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, lakini bado barabara zilizopo zinazidi kushuka viwango vyake na kushindwa kufikia Hadhi za Kimataifa na hali huwa mbaya hasa kipindi cha masika. Hii husababishwa na usimamizi mbovu, kuajiri makampuni yasiyo na viwango, kutoboresha na kutunza hadhi za barabara hizo na magari yenye uzito mkubwa kupita kwenye barabara bila kuzingatia viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza Mamlaka na Wakala wa Barabara kuziboresha barabara zetu hasa

za Miji Mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Miji mingine inayokua ili ziweze kufikia Hadhi za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni yangu.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika vipengele vifuatavyo katika Bajeti ya Mwaka 2012/2013:-

Mheshimiwa Spika, riba ya kukopea inapokuwa kubwa, huathiri dhana nzima ya mwananchi kupata mkopo.

Angalizo: Mfumko wa bei uliopo kwa sasa umesababishwa na upungufu wa uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali mfano; sukari, unga, umeme na upandaji wa bei za mafuta. Mkakati wa kupunguza mfumko wa bei lazima ulenge chanzo halisi cha mfumko wa bei. Ieleweke kuwa mfumko wa bei unatokana na upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula na kupanda kwa bei ya mafuta duniani na sababu zingine zinazofanana na hizi. Ushauri wangu ni kuwa ni vyema Serikali ijipange imara kukabiliana na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato 2011/2012: Serikali iliendelea kukopa na kulipa madeni. Kitendo kiki cha Serikali kuendelea kukopa na kulipa madeni kinapelekea kuonesha kuwa Serikali mapato yake siyo stahimilivu. Ninaishauri Serikali kuwa ni vyema kuboresha mifumo

ya ukusanyaji mapato ya ndani ili yatumike kulipia madeni na si mikakati inayotumika ya kukopa na kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu akaunti za Halmashauri (kifungu cha 38), naipongeza Serikali kwa kupunguza na kuanzisha akaunti sita kwa kila Halmashauri kwa kuwa jambo hili litasaidia kutoa huduma kwa ufanisi na urahisi. Serikali inapaswa kuongeza nguvu ya usimamizi wa akaunti hizi ili zilete ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo (kifungu cha 42); Serikali inaonesha imetoa fedha jumla ya shilingi 22.9 bilioni kwa ajili ya *SACCOS*, Kampuni na Vikundi mbalimbali vya ukopeshaji fedha. Lengo la utoaji wa fedha hizi ni kuhakikisha ajira zinatengenezwa hususan kwa vijana wetu wanaomaliza elimu ya sekondari na vyuo, lakini gharama za kukopea na masharti ya ukopeshaji wa fedha hizi kutokana na wakopeshaji yanakuwa magumu mno kiasi cha kutofikiwa kwa lengo lililokusudiwa. Serikali inapaswa ku-*facilitate* vikundi vya uzalishaji vya vijana ili kuwarahisishia upatikanaji wa mikopo kwa maeneo yote ya mijini na vijijini. Natumai Halmashauri za Wilaya zina jukumu la kusimamia hili kwa kushirikiana na taasisi binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii (kifungu cha 55); Serikali ifikirie jinsi ya kuanzisha *ageing benefits,* yaani mafao ya uzeeni kwa wale wasiokuwa waajiriwa. Hii inamaanisha kuwa, wazee wetu vijijini na mijini, kimsingi wanaishi maisha magumu mno na wengi wao hawana familia au ndugu wa

kuwahudumia. Nchi nyingine duniani, jukumu la kuhakikisha wazee wanapata *basic flow of income* ni la Serikali. Lengo liwe ni kuhakikisha tunakuza kipato chetu ili tuweze kuwahifadhi wazee wetu. Serikali iangalie upya jinsi ya kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu badala ya kuwaachia sekta binafsi. Tatizo hili ni kubwa kwa sasa na linahitaji Serikali kuingilia kati si Kisera tu bali kuwa na miundombinu thabiti Kikanda au Kiwilaya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha *Electronic Physical Device* kuwa *zero tax* kwa kuwa hili ni jambo zuri na litawasaidia walengwa kupata vifaa hivi kwa urahisi. Pia litasaidia udhibiti wa ukusanyaji wa mapato na kuipa Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332); naipongeza Serikali kwa kuongeza kima cha chini cha kutozwa kodi kwenye mapato ya ajira kutoka shilingi 135,000 hadi shilingi 175,000. Pia tulitegema Serikali ije na kiwango cha kodi ya *PAYE* ambacho ni chini ya ile inayotozwa sasa kulingana na malalamiko mengi yaliyotolewa na wafanyakazi katika kilele cha kuadhimisha Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani. Punguzo la kodi kwa wafanyakazi linaweza kuwa na manufaa yafuatayo:-

Litawaongezea kipato chao na kustahimili mfumko wa bei uliopo hivi sasa. Pia itawapa motisha ya kufanya kazi kwa saa za kazi. Vilevile itapunguza kuacha kazi kwenye Sekta ya Umma ambapo mishahara yake mara nyingi inaonekana midogo ukilinganisha na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu: Kumekuwepo na migomo mingi katika vyuo vya elimu ya juu. Aidha, migomo mingi husababishwa na wanafunzi kucheleweshewa mikopo hiyo na au baadhi ya wanafunzi wenye vigezo kukosa kabisa kupatiwa mikopo. Serikali itambue kuwa suala la kuhakikisha watu wanapatiwa elimu bora ni jambo la msingi na ni jukumu lake. Mikopo hii itolewe katika fani zote na mikopo ya wanafunzi itengewe fungu maalum na si kuweka katika fungu la matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya maendeleo hususan Miradi ya Miundombinu ya Kilimo mfano, majosho na mifumo ya umwagiliaji, imesahaulika na pesa nyingi kuonekana kutumika katika Miradi ya Umeme na Barabara tu. Tunahitaji kuwa makini na jinsi ya kuboresha Sekta ya Kilimo kama kweli dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kuendana na Mkakati wa Kilimo Kwanza. Serikali inapaswa kuliona jambo hili ni *economic vehicle* ya kuinua kipato cha nchi kwa kujikita katika kuzalishaji zaidi kupitia kilimo.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti 2013/2013, kifungu cha 78(iii), maji safi na salama: Serikali imetenga shilingi 568.8 bilioni ili kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini. Serikali ifanye upembuzi yakinifu ili kutambua ni maeneo gani ya vijijini yenye uhitaji mkubwa wa maji. Pia Serikali iweke mpango mkakati madhubuti kwa kuanzia na maeneo yenye matatizo sugu ya maji na siyo kurudia maeneo ambayo angalau yana unafuu wa shida ya maji.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 79 – 80; uzalishaji wa mpunga na sukari: Serikali haihitaji kuweka nguvu tu katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga na sukari. Ikumbukwe kuwa, bidhaa hizi kwa kiasi kikubwa zinatumiwa na watu wenye kipato cha kati na cha juu. Serikali itumie mazao yanayotumiwa na watu wa kipato cha chini ambao ndiyo walio wengi, mfano, Serikali inapaswa kujikita zaidi katika kuzalisha mazao ya maharage, uwele, mtama, mahindi, alizeti, karanga na kadhalika.

Serikali imetenga shilingi 192.2 bilioni kwa ajili ya kilimo; fedha hizi ni kidogo sana kwa kuwa kilimo kinategemea kuchangia kwenye Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 75. Hii inamaanisha kuwa, kama tunahitaji kuinua Pato la Taifa, tunahitahji pia kuwa na *capital investment* kubwa katika Sekta hii ya Kilimo.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa Bajeti hii. Utekelezaji ukifuatiliwa vizuri, itatekelezeka na itamsaidia mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotokana na utalii wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni asilimia 38 ya mapato ya *TANAPA;* ni takriban asilimia 40 ya mapato ya Wizara ya Utalii na kila mwaka mapato yanayotokana na utalii wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni bilioni 80 (USD 50,000 milioni), inayotokana na fedha zinazolipwa na watalii 35,000 wanaopanda mlima kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, ili pato hili liwe endelevu, Hifadhi inatakiwa kulindwa kwa kutokukata miti, kulinda vyanzo vya maji, kupanda miti na kuzuia kuwasha moto. Yote haya yanahitaji fungu la fedha. Fedha iliyotengwa, shilingi bilioni tano, haitoshi kwa kutunza mazingira ya Hifadhi zote za Taifa kwa mwaka. Pamoja na matunzo mazuri ya *TANAPA* na *KINAPA,* zipo Halmashauri za Wilaya za Siha, Hai, Koshi Vijijini, Moshi Mjini na Rombo na Uongozi wa Mkoa, wanafanya kazi usiku na mchana kuondoa wavamizi haramu wanaokata miti, kuvuna mbao, kuchoma moto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na Uongozi wa Mkoa ili ziendelee kulinda Hifadhi hii yenye kutoa pato kubwa kwa Taifa.

Naishauri Serikali kuwa, badala ya bomba la gesi kutoka Mtwara kuishia Tanga kama Mpango wa Taifa ulivyosema, bomba hili lifike Arusha ili watu watumie gesi kupikia na waache kukata misitu na kuchoma mkaa kwa ajili ya matumizi ya kupikia. Mkoa wa Arusha pia unatoa pato kubwa linalotokana na utalii kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika**,** katika Mkoa wa Kilimanjaro, *square metre* moja ya ardhi ina watu 126; ni *the third densely populated region* baada ya Dar es Salaam na Mwanza. Kwa sababu ya uwingi wa wakazi hawa, eneo la hifadhi linakuwa *encroched.* Watu wanawasha moto katika mashamba yao na hatimaye

unaingia katika hifadhi, unafukuza wanyama na kuua uoto wa asili.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iweke umuhimu wa kuwaondoa watu katika eneo la Hifadhi na watengewe eneo lingine zuri la kilimo. Nakumbuka Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, miaka ya 1970 aliwahi kuhamisha wananchi wa eneo hilo akawapa maeneo Kilombero. Baba wa Taifa aliona umuhimu wa kulinda chanzo hiki muhimu cha Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria na 19 ya 2010 ya *Public Private Partnership*. Nashukuru Serikali kuiwekea mkakati katika Bajeti ya 2012/2013. Naipongeza pia Serikali kwa sababu *NHC* tayari imeanza kujenga nyumba kwa kushirikiana na watu binafsi na hali ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa viwanda unachangia Pato la Taifa kwa asilimia nane na Sekta hii inaajiri asilimia saba kati ya nguvu kazi nchini ya takriban milioni 22. Hata hivyo, ubinafsishaji na *trade liberalization* vimechangia mdororo wa viwanda nchini. Tanzania (viwanda au mashirika 170 vilivyostaafishwa, 41 tu ndiyo vinafanya kazi) na hii ni kwa sababu pia ya uingizaji nchini bidhaa wakati mwingine bidhaa feki za bei nafuu kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Dira yetu ya Taifa 2025 (*National Strategic Master Plan)* inasema, tunategemea Tanzania iwe *industrial country by 2025* au *semi-industiralized by 2015.*

Mheshimiwa Spika, ili Dira hii itekelezeke, nashauri Serikali iharakishe mchakato na Halmashauri za Wilaya kuwa na ubia wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwenye maeneo yao baada ya kufanya *feasibility study* za kutosha, kutambua bidhaa zinazotakiwa kuzalishwa ili zikidhi mahitaji ya soko lililopo.

Mheshimiwa Spika, nashauri viwanda vilivyotaifishwa ambavyo havizalishi (129), Serikali ifute mikataba yao na Halmashauri na Wilaya zipewe mashirika na viwanda hivi, wafanye na wabia.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo *potential* kwa mazao fulani mfano, maeneo yalimayo mahindi mengi waanzishe viwanda vidogo vya kukoboa, kusaga na ku-*pack* unga. Maeneo yenye matunda, vianze viwanda vya kutengeneza *concentrates juice* na kadhalika. Maeneo yenye ndizi mvinyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizi zitakuwa zimeongeza thamani na hivyo bei itakuwa nzuri. Nashauri viwanda vya *SIDO* viendelee kupewa uwezo wa kifedha ili waweze kutengeneza mashine za viwanda vidogo vidogo na ikiwezekana vitoe mkopo kwa Halmashauri za Wilaya na wabia husika. Inawezekana pia Benki ya Kilimo au *TIB* ikatoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vidogo vinaweza kuajiri nguvu kazi asilimia 80, ukiondoa nguvu kazi ya kilimo; viwanda vya kati na vikubwa vinaweza kuchangia takriban asilimia 50 ya Pato la Taifa kwa kodi vinavyolipa mfano ushuru wa forodha na kodi za mapato *(corporate tax)* na kadhalika. Vyema viwanda

vyetu vya *textile* vipewe nafuu ya kodi ili vishindane na nguo za nje. Hata hivyo, vifuatiliwe visibadilishe matumizi pale ambapo wanapunguziwa kodi.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa viwanda vidogovidgo vya kusindika mazao tofauti utaleta ajira kwa wananchi wetu. Kwa sababu ya upungufu wa chakula Afrika na Duniani, soko la bidhaa zitakazotengenezwa lipo na tutaanza na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambalo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, wakulima tulionao takriban asilimia 80 ambao wanachangia Pato la Taifa kwa takriban asilimia 50, wanatumia zana duni za kilimo. Wengi wao bado hawajui kanuni bora za kilimo. Maeneo machache wanatumia trekta, *power tillers* na majembe ya kukokotwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya bilioni 192.2 kwa kilimo ikilinganishwa na idadi ya wakulima na idadi ya hekta milioni 5.1 zinazolimwa ni kidogo. Serikali iliajiri maafisa ugani takriban 5000; ni hatua nzuri sana itakayoelimisha wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo na ufugaji bora.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye mpango wa kukarabati mabwawa, malambo na sehemu zote za umwangiliaji popote zilipo nchini ili wananchi wapate maji walime. Hakuna haja ya kujenga mabwawa mapya wakati ya zamani Serikali imeshindwa kuya-*maintain;* mfano, Bwawa la Nyumba ya Mungu – Mwanga, Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kaskazini (Kilimanjaro Arusha na Manyara), imekumbwa na mfululizo wa ukame na *impact* ya *climate change* kwa takriban miaka mitatu sasa. Hata mwaka huu wa 2012, mazao yaliyokuwa yavunwe Juni na Julai yote yamekauka katika Ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iweke mkakati wa kupambana na changamoto ya mabadiliko ya Tabia nchi. Itafutwe njia mbadala ya kusaidia wakulima badala ya kutegemeea mvua. Ipo *technic* ya *drip irrigation.* Mikoa ya Ukanda wa Kaskazini haiwezi kutegemea chakula cha msaada kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeweka katika Mpango na Bajeti, Mkakati wa Kilimo katika Mabonde ya Kilombero na Malagarasi. Mabonde haya tayari yamevamiwa na mifugo kutoka Ukanda wa *Lake Zone.* Nashauri Serikali irudishe ushuru iliyofuta katika kuagiza *crude edible oil*. Kuondoa ushuru unawanyima wakulima wadogo wa alizeti kuuza mafuta yao. Ikumbukwe kuwa, alizeti inalimwa pamoja na mahindi. Popote panapovunwa mahindi, inawezekana pia kuvuna alizeti. Wananchi katika Mikoa mingi wanalima alizeti na wana mashine ndogondogo za kukamua alizeti.

Mheshimiwa Spika**,** taarifa zisizo rasmi zinasema kuwa, wafanyabiashara wanaosamehe ushuru huwa wanaagiza *refined oil* kwa jina la *crude oil*.

Mheshimiwa Spika**,** umefika wakati Tanzania tulinde wakulima na viwanda vyetu. Nchi za Ulaya *(EU)* zinalipa ruzuku kwa wakulima na wafugaji wao na hii inazuia nchi za *African Caribbean and Pacific Countries (ACP),* kushindwa kuuza bidhaa zao za kilimo na mifugo huko *EU*. Hii ni wazi ni mikakati ya kulinda viwanda, wakulima na wafugaji wao. Tulinde viwanda vyetu na wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika**,** katika bajeti hii, sijaona mikakati ya Serikali ya kuvuna samaki vina virefu vya bahari *(Deep Sea Fishing).* Rasilimali zinazopatikana katika vina virefu vya eneo la Bahari la Tanzania zinavunwa na Mataifa ya nchi za nje.

Mheshimiwa Spika**,** nashauri Serikali iliwekee mkakati, samaki watakaopatikana pato lake litakuwa tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeje.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa niaba ya Waziri Mkuu, niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge hususan katika eneo la uwekezaji na uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, mnamo miaka ya 1990, Serikali ilitoa Sera na Taifa likakubaliana kwamba, Serikali inatoka katika biashara ipate muda zaidi katika mambo ya Utawala na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kutoa mchango wake kwenye uchumi wa Taifa. Uwekezaji wa ndani na wa nje ni muhimu kwa Taifa lolote linalohitaji kuendelea kwa kasi kutokana na faida zinazotokana na uwekezaji huo. Uwekezaji unaongeza ajira, mapato ya nchi na vilevile upatikanaji wa fedha za kigeni na teknolojia na pia tunatoa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu ambao tunauhamasisha na kuuwezesha ndani ya nchi, kama Waheshimiwa wengi walivyosema, unapaswa uwe na manufaa kwa nchi yetu na hivyo hatuna budi kujenga uwezo katika majadiliano ya mikataba ya uwekezaji ili kulinda maslahi ya Taifa letu, sambamba na kuhakikisha kuwa wawekezaji wanatimiza masharti yanayoambatana na uwekezaji kama vile kulipa kodi na kuepuka udanganyifu wa aina yoyote unaotokana na mikaba husika. Kutokana na umuhimu huu, Serikali itahakikisha uwekezaji wa ndani na wa nje vilevile unakua kwa kasi sambamba na mahitaji ya nchi yetu. Katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2012, jumla ya Miradi 6,602 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 49 imesajiliwa katika Kituo chetu cha *TIC* na imesaidia kutoa ajira kwa Watanzania wapato 950,108. Idadi ya wawekezaji wa ndani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na katika kipindi husika jumla ya Miradi 3,345 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani ambao ni asilimia takriban 52. Miradi inayomilikiwa na wageni

kutoka nje ni 1,569, ambayo ni asilimia 24 na Miradi ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje ni 1,688, ambayo ni sawa na asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona jinsi tunavyohamasisha uwekezaji wa ndani kwa sababu ndiyo ambao unatuhakikishia uchumi endelevu na kuimarika kwa nchi yetu na kujitegemea. Uwekezaji vilevile unaongeza biashara ya nje. Ukitaka Wachina wanunue kutoka Tanzania, inabidi utengeneze vitu ambavyo vinakubalika China na kwa ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, tunapowakaribisha wawekezaji kutoka huko kwa mfano watazalisha yale ambayo wanajua wakiyapeleka yatapokelewa na hivyo kuongeza biashara. Changamoto kubwa tuliyonayo ni kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Ripoti zinazoshindanisha nchi zote duniani kama Benki ya Dunia na nyingine zinaonesha kuwa, mazingira yetu ya uwekezaji bado hayavutii sana wawekezaji ukilinganisha na nchi jirani katika Afrika na Dunia kwa ujumla. Changamoto mbalimbali ambazo zinafanya wawekezaji wasivutiwe ni pamoja na kukosa nishati ya uhakika, bandari yetu bado haina ufanisi wa kutosha, reli barabara na maji, kama Wabunge walivyochangia humu ndani. Kutokana na vivutio hivyo vya kodi, Tanzania imeweza kupata mafanikio ambayo nimeyaeleza katika uwekezaji ikiwemo kukua kwa Miradi kutoka 178 mwaka 2000 hadi 826, kukua kwa mitaji kutoka kiasi cha Dola za Marekani milioni 824 hadi dola bilioni 7.2 na vilevile kuongeza ajira mpya kutoka 19,000 hadi 87,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona manufaa ambayo yanatokana na uwekezaji, lakini bado narudia kwamba lazima tuongeze uwezo wetu wa kujadiliana na kujipanga vizuri ili tuweze kupata manufaa hayo, kwa sababu kila mwamba ngozi anavutia kwake; mwekezaji anataka *return on investment* sisi tunataka ajira, tunataka bidhaa, teknolojia na kutoza kodi pale ambapo wanaleta faida. Baadhi ya Wabunge wamependekeza kuondolewa kwa misamaha ya kodi ya uwekezaji kama njia ya kuongeza wigo wa kodi. Ili wigo wa kodi uongezeke, nchi inahitaji kuwa na mikakati kabambe ya kuvutia biashara. Tunapoweka kodi kwenye Miradi ya Uwekezaji bado mitaji haijafika, kwa hiyo, yule mwekezaji ana hiari ya kuja au kutokuja. Kwa hiyo, unaondoa kodi kwenye kitu ambacho unakingojea, lakini kinapokuja kinatoa manufaa.

Mheshimiwa Spika, ni sawasawa unapotaka ndege zitue Tanzania kama hakuna kiwanja cha ndege hakuna ndege itakayotua. Kwa hiyo, ukitaka ndege itue Tanzania lazima utengeneze uwanja wa ndege lakini na wewe upate manufaa na kiwanja chako cha ndege. Hayo ndiyo mambo ambayo tunayasema sisi Serikali.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitaje madhumuni ya misamaha misingi ya kodi kwa wawekezaji ambayo mingi imelalamikiwa na baadhi ya Wabunge na hata Watanzania kwa ujumla na hasa ningependa kushukuru kwamba watu wanapotoa maoni siyo mara zote watazikataa. Kuna hili la *one billion dollar question*, tumepata *document* ile tunaifanyia kazi. Vilevile ni

wajibu wa Serikali yenu kutoa ufafanuzi pale inapohitajika. Kwanza, maeneo mengi ya nchi yetu hayapo katika hali ya kuvutia kama nilivyosema na ndiyo maana tuna Miradi ya *EPZ* na *SEZ* ili hatimaye wawekezaji waje, lakini ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo tunahitaji sisi kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *deemed capital goods incentive;* hili limewanufaisha wawekezaji wa ndani kuliko wa nje na ndiyo maana wengi wamejenga hoteli za kitalii na bado kuna Miradi ambayo inawanufaisha wawekezaji wa ndani ili tujenge kada ya kati ya Watanzania ambao watatumia fursa kutokana na wawekezaji wakubwa wa nje. Kwa hiyo, utaona mwaka 2009 tuliweka kodi ya *deemed capital* ikapunguza wawekezaji ghafla. Mwaka huu tunaiweka tutaangalia italeta athari gani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ningependa wote tujue kwamba ni muhimu kwa nchi yetu kuvutia wawekezaji na ni muhimu zaidi kwa nchi yetu kuwawezesha wawekezaji wa ndani kwa sababu faida inayotokana na uwekezaji wa ndani inabaki ndani ya nchi yetu wakati wawekezaji wa nje inakwenda kwenye nchi zao. Hatuwezi kulifumbia macho, hata Marekani ambao ni tajiri bado inavutia wawekezaji wa nje na sisi lazima tupate *share* yetu ya wawekezaji wa nje. Manufaa yanayotegemewa kutokana na faida baada ya uwekezaji ni kama ajira, malipo ya kodi, mapato ya mauzo ya nje na teknolojia mpya. Haya tunayahitaji lakini hayatabiliki kwa sababu inategemea uwezo wetu wa kujadiliana na wawekezaji. Kinachotakiwa sasa hivi na tunachokifanya ndani ya Serikali ni kuweka mikakati ya kuanza kutoa misamaha

kwa kuangalia faida tutakayopata sehemu ya mitaji ya uwekezaji kwani hii inatabirika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge waiunge mkono ili tuhimize uwekezaji na faida za uwekezaji zije Tanzania. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata fursa hii kujaribu kuchangia mengi, lakini naomba Wabunge wasikilize kwa makini sana hotuba yangu ya tarehe 24 na 25 mwezi ujao ya Nishati na Madini. Hata hivyo, kuna vitu ambavyo nadhani inabidi nitoe ufafanuzi wake kama ifuatavyo:-

Kwanza ni umeme. Wazungumzaji wengi wameongelea jambo la umeme na napenda kuwahakikishia ninyi Wabunge na Watanzania wote kwamba, kuna mikakati kabambe ya kutatua hili tatizo. Tunajua kwamba, tukitaka kutekeleza kwa uhakika na ufanisi mkubwa ajenda yetu ya maendeleo kwa mwaka 2025 ni lazima tuwe na umeme ambao wingi wake siyo chini ya megawati 3000 na 5000 na huo mkakati nitaueleza siku hiyo. Kata hivyo, kwa sababu Serikali ya CCM na Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeeleza wazi kwamba, itakuwa ni vizuri kuongeza watumiaji wa umeme na mimi kwa siku chache nilizakaa pale Wizarani karibu mwezi na nusu, napenda sasa hivi kutoa agizo ambalo nimeshalitoa ni amri na ninyi Wabunge jaribuni kuwasaidia wapigakura wenu kwamba wale wote ambao walikuwa wamelipa kuunganisha umeme na malipo yao yamefanyika kabla ya tarehe 31 Mei, wanapaswa kuwa

wameunganishiwa umeme ifikapo mwisho wa mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani ikifika tarehe 30 Juni, 2012 hawajaunganishiwa umeme, itabidi watoe taarifa Wizarani na ikiwezekana kwangu mwenyewe na namna ya kutoa hizo taarifa imewekwa kwenye magazeti ya leo, usiku mtasikia kwenye vyombo vya habari. Kwa hiyo, Wizara yangu mambo ni kwa vitendo na wale watu wa *TANESCO* hawana mjadala ni aidha wanatekeleza, wanaiweza kazi au hawaiwezi kazi. Kwa hiyo, mengi mtayapata kwenye magazeti.

Mheshimiwa Spika, pili, limekuja suala la makaa ya mawe Nakagulo; napenda kukutaarifu kwamba, Msemaji aliyetoa hii hoja inaonekana vile vile yeye ni mwakilishi wa kampuni moja ambayo ipo Dubai; kwa hiyo, sitapenda kuongelea watu wanaoshindana kibiashara humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa gesi; wengi vile vile wameongelea sana mambo ya gesi. Napenda kuwaeleza Wabunge na Watanzania wote kwamba, kweli gesi imekuja imetukuta Watanzania tulikuwa hatujajitayarisha lakini hiyo siyo dhambi, sidhani kama mambo yote yanayowapata kila Taifa huwa limejitayarisha. Napenda kuwahakikishia kwamba, kwa wakati huu *draft* ya kwanza ya Sera ya Gesi tumeshaipata tumeipitia imerudi, ifikapo mwezi wa saba Watendaji wa Sekta mbalimbali ambazo nishati inahusiana nazo, wataipitia baadaye wakimaliza. Sisi ni wawazi sana, tutaita kitu kinachoitwa *Public Hearing*; yaani Watanzania wote, watu binafsi, *NGOs* na

makampuni, tutaitisha kikao tutaiweka hiyo sera mbele yenu mtaichambua tukitoka hapo tutaenda kwa watu wa Lindi na Mtwara ambao nao wanasema hawajui manufaa ya gesi, tutaongea nao baada ya hapo kufika mwezi wa kumi hiyo Sera itakuwa ipo mbioni kuja kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, tutaifanya kwa uwazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Sera ya Nishati Mbadala *(Policy Renewable Energies)*, ambayo nayo ni mpya haijatengenezwa lakini kama nilivyotoa pendekezo siku za kwanza nikiwa Wizarani; napenda kuwataarifu kwamba hii kazi nimewapatia wataalam wa ndani, *Members* wa *Tanzania Geological Society*, ambao wapo Vyuo Vikuu na kwenye makampuni binafsi, watatengeneza hiyo Sera ya *Renewable Energies;* inamaanisha namna tunavyoweza kutumia *solar energy, wind energy, geothermal* na *bio-energy*. Kwa hiyo, nayo nataka kuwahakikishia kwamba, kabla ya mwisho wa mwaka huu hiyo Sera itakuwa ipo tayari.

Mheshimiwa Spika, niwapatie *breaking news* ni kwamba, juzi tarehe 20, saa tatu asubuhi saa za Tanzania, ambayo ilikuwa ni saa tisa mchana kule China, tumeweza kuwekeana mkataba na wenzetu Wachina; kwa hiyo, ile *pipe line* mali yetu itaanza kujengwa. Kwa hiyo, hapo ndugu zangu ndiyo watu ambao wanahoji mambo ya mikopo kidogo lazima mjiulize hii gesi tumechukua mkopo wa dola bilioni 1.225, hizo fedha hatuna ni lazima tukope. Kwa hiyo, msiojua maana ya mikopo kidogo inabidi mrudi nyuma mjifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, tatizo la nishati nchini tukubali kwamba ni Taifa linasonga mbele, ile mikakati haikuwepo au iliyokuwepo ilikuwa imetengenezwa na Shirika moja tu la *TANESCO.* Ukienda kote duniani, utakuta Sera na mikakati ya nishati ya kila nchi ni mali ya Serikali siyo mali ya shirika binafsi. Kwa hiyo, tutatengeneza ambayo ni *energy mix 2013-2023,* hii mikakati huwa inachukua miaka kumi na mitano au miaka ishirini duniani kote. Kwa hiyo, hilo nalo nawahakikishia kabla ya mwisho wa mwaka huu litakuwepo.

Mheshimiwa Spika, wengine wameongelea madini, nadhani mmesikia matangazo; kesho nitaonana na wachimbaji wa madini ambao wanawakilisha mikoa yote na tunaweka mikakati namna ya kuboresha uchimbaji wao kwa manufaa yao. Vile vile ni chanzo kingine cha makusanyo ya kodi kwa ajili ya Taifa. Huu umiliki wa madini nitauzungumzia pia tarehe 25.

Mheshimiwa Spika, niongelee bajeti kwa ujumla; unajua bajeti yetu imetengenezwa ikiwa siyo kwamba; imejikita au imejiweka kwenye Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na sisi tumesema itakapofika mwaka 2025 tunataka tuwe watu wa nchi ambayo ina kipato cha kati, ambayo ni dola kati ya 3,800 na dola 12,000. Wakati tunafanya hivyo, Dunia haikulala; kwa mfano, nchi za Brazil, Russia, India, China na South Africa, hizi nchi pekee zinahodhi asilimia themanini ya Pato la Dunia *(80 percent of the World's GDP).*

Kwa hiyo, tusikae hapa tukaumizana wengine kule hawakulala. Afrika kama unajidharau wewe Tanzania, Afrika kwa ujumla wetu sisi tuna *account for two percent of the Worlds GDP.* Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia kwamba, Nchi za Afrika ikiwemo Tanzania, bado tuna safari ndefu, bajeti zetu ni mambo ya ushindani, huwezi kufanya bajeti ya nchi bila kujua uchumi wa dunia nao upo namna gani na ndiyo maana napenda muunge mkono kwa sababu bajeti yetu hii inatuelekeza kufika kwenye Malengo yetu ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye.

**T A A R I F A**

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkono.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana msemaji aliyemaliza kuzungumza, ndugu yangu Profesa Muhongo.

**SPIKA:** Toa taarifa jamani kuheshimiana hakupo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, taarifa ni kwamba, jana wakati nazungumza,

nilizungumza kwa kipindi kifupi lakini kwa maandishi nimesema nina-*declare interest* chini ya Kanuni ya 61. Nakala ya hiyo *speech* ipo hapa na Mheshimiwa Mtaalam aliyezungumza anayo nakala, kwa hiyo, naomba atoe kauli hiyo.

**SPIKA:** Ile kauli ya kwamba kuna mtu ana maslahi, katika hilo ilitakiwa na wewe kabla ya kusema ungesema mimi nina-*declare interest* kwa mujibu wa Kanuni ya 61.

**WABUNGE FULANI:** Alisema!

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nilisema kwa maandishi lakini nafasi haikuwepo.

**SPIKA:** Kama alisema hakuna kilichoharibika; alisema hakusema?

**WABUNGE FULANI:** Alisema.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nilisema.

**SPIKA:** Sasa Waziri amesema hawezi kujibu kitu ambacho watu wana-*interest* nacho; si basi?

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, hapana!

**SPIKA:** Hakumtaja mtu, jamani tuelewane tusitumie muda kwa kitu kidogo. Kama Mheshimiwa alisema sawa na huyu anasema sitajibu kwa sababu mtu ana *interest* nacho si basi na hakumtaja mtu.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mimi nilitaka kuuliza huyo mtu ni nani.

**SPIKA:** Sasa jamani tusipoteze muda kwa ajili ya kubishana, kitu alisema au hakusema kama amesema *Hansard* ipo, kama ameandika maandishi yapo, Waziri anasema siwezi kusema kwa sababu hakuona hiyo kitu. Tunaendelea.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mimi sipendi neno mwongozo kwa sababu halina hata msingi, hebu eleza sasa, niongoze.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea iwapo linaruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini wakati anachangia hoja, jambo linalohusu Kiwira amesema hawezi kutoa majibu kwa sababu mhusika aliyelizungumza ana maslahi. Sizungumzii hilo suala la maslahi, nataka kujua iwapo inaruhusiwa kwa mujibu wa taratibu za Kibunge, jambo ambalo lina maslahi ya Taifa Waziri asilijibu kwa sababu tu msemaji ama ana maslahi au ana nini?

Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako ili Waziri au mtu mwingine wa Serikali aweze kujibu

kuhusiana na suala hilo la Kiwira na mambo yote yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, si ndiyo hili tulikuwa tunabishana hapa? Suala hili amesimama Mheshimiwa Mkono anasema yeye ali-*declare interest,* mimi sina ushahidi nitaangalia kama ndiyo hivyo anavyosema. Mimi hamnilazimishi, kama sijaridhika kwa nini nijibu hivyo. Nitaangalia kama aliyoyasema Mheshimiwa Mkono yana msimamo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika nakuomba.

**SPIKA:** Tafadhali Waheshimiwa, Mheshimiwa Zitto naomba tuendelee na kazi. Nimesema kwamba, tutaangalia na mimi ni lazima nijiridhishe kwenye Meza hii kwamba hilo jambo linalozungumzwa lipo sawa, kwanza sijui Waziri alikuwa anajibu nini.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ole-Medeye.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufafanuzi kwa hoja chache ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha. Yapo mambo kadhaa ambayo

yalizungumziwa, lakini kubwa ambalo Wabunge wengi wamezungumza ni kuhusiana na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kwamba, wanatoa rai kwa Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, hadi sasa Serikali imekwishaandaa Mpango wa Taifa wa matumizi bora ya ardhi kwa nchi nzima, ambao unatarajiwa kupitishwa hivi karibuni na Serikali. Kwa hiyo, rasimu ipo tayari, tunatarajia kuwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri na mara itakapokuwa imepitishwa basi itaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya Wilaya 30 na Vijiji vipatavyo 932 vimekwishaandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi na katika mwaka wa fedha 2012/13, tunatarajia kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango hiyo, ambapo tunategemea kwamba takriban Wilaya nane na vijiji 1,300 vitaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Kwa hiyo, napenda niwahakikishie Wabunge kwamba, tumetengewa fedha za kutosha katika eneo hilo kwa mwaka huu unaokuja kiasi kwamba tutaweza kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la kwamba, pengine Sekta ya Ardhi haijapewa kipaumbele sana na Serikali; nipende kukiri jambo moja, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Fedha na niipongeze sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa jinsi ambavyo wameisaidia Wizara kutoa mwanga juu ya

umuhimu wa rasilimali ardhi na haja ya kuipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tutakapowasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, napenda kuwahakikishia kwamba, tumetengewa fedha za kutosha kwa mwaka huu unaokuja kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ikiwemo kulipa fidia kwa wananchi ambao wanatakiwa kupisha maeneo ya uwekezaji kama vile Kurasini, Kigamboni, Bagamoyo, Kigoma na maeneo mengine nchini ambayo *EPZ* imeyaona na kuelezea nia ya kuyachukua kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa migogoro ya ardhi, kumekuwepo na hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna migogoro mingi ya mipaka baina ya vijiji na vijiji, baina ya Wilaya na Wilaya na pia kuna migogoro baina ya baadhi ya Vijiji na Hifadhi za Taifa. Nikitoa tu mfano, kuna Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ambayo hoja ilitolewa kwamba mipaka yake imeingiliana na baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba ni kweli Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kama tunavyojua, ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 160 la tarehe 19 Juni, 1970. Hifadhi hii inapakana na Wilaya za Monduli kwa upande wa Kaskazini na Kaskazini Mashariki na pia Simanjiro kwa upande wa Mashariki na Kusini Mashariki, Kondoa kwa upande wa Kusini Magharibi na Babati kwa upande wa Magharibi na Kaskazini Magharibi. Kwa upande wa Kusini, Hifadhi hii inapakana na Pori la Akiba la Mkungunero na kwa upande wa Kusini Mashariki inapakana na Vijiji vya

Loibosireti na Kimotoroku vilivyoko katika Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda mipaka ya Hifadhi hii, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* mwaka 2004 iliomba Wizara ya Ardhi kwamba, isaidie kuhakiki mipaka ya hifadhi hiyo. Wakati wa kufanya uhakiki iligundulika kuwa katika baadhi ya maeneo mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ilikuwa imekosewa. Katika maeneo ya Kijiji cha Loibosireti, mipaka ya Hifadhi ya Tarangire ilikuwa imeingia ndani ya eneo la kijiji na katika Kijiji cha Kimotoroku, Hifadhi ilikuwa imeacha eneo lake na hivyo eneo hilo kuonekana kuwa ni sehemu ya Kijiji. Wataalam walirekebisha kasoro hizo kwa kurudisha eneo la Loibosireti kijijini na vile vile kurejesha eneo la Hifadhi lililokuwa katika Kijiji cha Kimotoroku na marekebisho hayo yalifanyika kwa mujibu wa Tangazo la Serikali ambalo nililitaja awali, Namba 160 la Mwaka 1970.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo tunaamini kwamba, yakizingatiwa yatafanya sasa Hifadhi hiyo kwanza wananchi waweze kutambua mipaka baina yao na Hifadhi na pia iweze kuendeleza eneo lake kama ilivyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa wito kwanza, kwa Hifadhi za Taifa na Hifadhi za Misitu kwamba, waweke mipaka inayoonekana katika maeneo yao kwa kuzingatia Sheria iliyoanzishwa na Hifadhi hizo. Pili, kwa upande wa mipaka ya Wilaya, tumekuwa na mgogoro baina ya Wilaya na Wilaya Wilaya zote zinapogawanywa au zinapoanzishwa,

hutolewa Tangazo la Serikali ambalo linaelezea bayana mipaka ya Wilaya hizo, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ili kuhakikisha kwamba, Wilaya zote zinawekewa mipaka inayoeleweka ili kuepusha migogoro baina ya Wilaya na Wilaya.  Pia tungetoa wito kwamba, Halmashauri za Wilaya zihakikishe kwamba kuna mipaka inayoeleweka baina ya Vijiji na Vijiji ili kuepusha migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo machache, maelezo ya kutosha na ya ufasaha tutayawasilisha wakati wa Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, basi ningeomba Wabunge tushirikiane kupitisha Bajeti hii ya Serikali ili tuweze kutekeleza kazi ya kulinda Mipaka yetu ya Kimataifa, kulinda mipaka ya Mikoa na Mikoa, Wilaya na Wilaya na Vijiji na Vijiji ili kuepusha migogoro.

Pia tuweze kutekeleza mpango huu wa kupanga matumizi bora ya ardhi ili kuepusha migogoro baina ya makundi na pia mwananchi na mwananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia.  Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mgimwa na Manaibu wake wote wawili, kwa hotuba nzuri ya mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba vile vile nitumie fursa hii kuwatoa wasiwasi Watanzania wengi wanaofuatilia kwa karibu mjadala huu wa bajeti kuwa, pengine mara nyingine huwa joto kubwa sana linajitokeza hapa; nataka kuwaambia kwamba, halitokani kabisa na ubaya wowote wa bajeti hii, bali hamasa na shauku kubwa ambayo Wabunge wote wanayo, kutaka maendeleo hata ya miaka mitano wayaone leo. Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Miaka Mitano iwepo katika bajeti ya mwaka mmoja na itekelezwe leo. Kwa hiyo, hiyo ni hamasa ya kawaida ambayo binadamu anategemea pale ambapo anahitaji maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hoja kali sana hasa kutoka upande wa Upinzani dhidi ya Serikali, pamoja na kwamba Upinzani haujawahi kutawala nchi; hivyo unatumia zaidi nadharia kuliko uzoefu na hii ni kawaida sana hata kwa maisha ya kawaida tu ya binadamu na nadhani ni ya afya, yanachangamsha na yanaifanya Serikali pia iangalie hizo *alternatives.*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano wa kawaida sana, tuchukulie mfano wa mchezo wa mpira ambao watu wengi wanaupenda sana. Ukiamua kwenda uwanjani kuangalia mchezo wa mpira au ukakaa kwenye *TV* kuangalia mchezo wa mpira, unakaketi na watu waliokwishawahi kucheza mpira kama akina Mheshimiwa Waziri Sitta au Mheshimiwa Ismail Aden Rage au Mheshimiwa Captain Komba, utaangalia ule mpira mpaka mwisho bila maneno mengi. Ukikaa na mtu ambaye hajawahi kugusa mpira utasikia ahaa Ronaldo pale angedokoa tu kwa kisigino angefunga,

ukimwangalia mtu mwenyewe unakuta hata pengine kisigino hana, ashakum si matusi; aah, Mercy bwana angetia *cross* pale sasa unamwangalia mtu mwenyewe hii *cross*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kueleza kwamba, hii hata kwa maisha ya kawaida ni sawa na mifano mnayoiona hapa leo. Mtu ambaye hawajawahi kuongoza Serikali anajua zaidi kuiongoza Serikali kuliko hata Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja mdogo alioutoa mdogo wangu hapa kwenye Bajeti Kivuli, ukurasa wa 31, inapoongelea kutenga shilingi bilioni 443 kwa mwaka ujao wa fedha ili kukarabati Reli ya Kati. Mimi nafurahi ni mawazo mazuri sana, ni fedha nzuri ambayo ningeifurahia kweli kweli, lakini misingi yake imekosa ule uhalisia maana kiasi hicho kilichopendekezwa hakijazingatia *absorption capacity* ya *TRA* na *RACO* na hata mchakato tu wa *procurement* na uwezo wa utekelezaji kwa fedha hiyo kwa hayo mashirika na *nature* ya hiyo *industry* yenyewe ya reli.

Leo hii nikiagiza vichwa vipya vya treni na mabehewa nitapata katika miaka miwili ijayo. Nikitaka kuagiza vichwa vya treni vilivyotumika nitasubiri kwa miezi sita mpaka miezi 12. Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba, *solution* siyo fedha tu *as such,* tunatoa kwa wingi, utatoa mwanya tu kuanza kuzitamani hizo fedha kuchukua maana hazitatumika kwa haraka hivyo. Ninachosema ni kwamba, tatizo kubwa tulilonalo hapa siyo fedha yake, lakini vile vile

hata kubadilisha *mindset* ya viongozi na wafanyakazi wetu. Mimi namwomba Mheshimiwa Kabwe Zitto na wenzangu rafiki zangu upande wa Upinzani, waunge mkono bajeti hii na ninawahakikishia usafiri wa reli kwenda kuchukua migebuka kila wiki *brother* utapata kila siku kwenda Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdallah Masoud amelalamikia uchakavu wa vyombo vya usafiri baharini na kwenye maziwa yetu na ametaka kujua mikakati ya Serikali katika kulinda usalama wa wananchi. Pamoja na kwamba, Serikali imetenga fedha ya kutosha kukarabati meli za kampuni ya huduma za meli *MCL* katika bajeti ambayo tunawasilisha sasa hivi, tuna Mradi wa ujenzi wa meli mpya na tulishalieleza hili Bunge lako Tukufu kwa Maziwa yote matatu tukisaidiwa na Serikali ya Denmark. Vile vile hata meli ya MV Liemba sasa hivi imeingia kwenye mchakato wa kukarabatiwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani na vyombo hivi vyote vitakuwa tayari kufikia mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile mamlaka ya Udhibti na Usafiri wa Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA)*, imekuwa ikifanya kazi vizuri sana kuhakikisha meli zetu ni salama hasa kwenye maziwa na baharini. Ndiyo maana mpaka sasa *mandate* ya *SUMATRA* ni kusajili tu meli zile ambazo ni za Tanzania na zile ambazo zinamilikiwa na Watanzania kwa zaidi ya asilimia 51 ndizo zinapewa usajili na kupepea Bendera za Tanzania. Vile vile meli yoyote haiwezi kupata usajili Tanzania bila kuwa na umri wa miaka 15 na kushuka chini, ikizidi hapo hatusajili.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba, katika kipindi hiki cha Bunge nategemea kuonana na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi wa Zanzibar, tuweze kujadiliana hili ili tuwe na utaratibu wa pamoja, maana wenzetu Zanzibar wana *open registry* wanasajili meli za dunia nzima kama Liberia na hawana ukomo wa umri. Kwa hiyo, meli zote chakavu zinakimbilia Zanzibar kusajiliwa, hilo tutaliongea tutaliweka sawa, nina uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kabisa nimesikia kengele imegongwa. Mheshimiwa Sabrina Sungura, amehoji kwa nini Uwanja wa Kigoma umepewa shilingi bilioni 3.5 tu, Uwanja wa Songwe shilingi milioni 10, naelewa anafikiri sijui nimejipendelea. Uwanja anaouongelea wa Songwe huu ni mwaka wa 12 haujakamilika. Nataka nichukue fursa hii kuwapongeza Wananchi wa Mikoa ya Kusini kwa uvumilivu mkubwa kwa Serikali yao. Nawahakikishia mwaka huu tunamaliza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe. Uwanja wa Ndege wa Kigoma umeanza kukarabatiwa mwaka huu wa fedha unaokwisha sasa na tayari tumetoa karibu nusu ya fedha tunayohitaji kuchangia kwa sababu upo chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Uwanja wa Mpanda anaouongelea tulishaujenga, mkandarasi anatudai na hiyo fedha tuliyoitenga ni ya madai ya mkandarasi tumeweza kukaa kimya kama waungwana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naona nimegongewa kengele, naomba kuunga hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimesema atakuja Mheshimiwa Saada Salum, sasa tumefikiri kwamba, kwa sababu ataungana na Waziri wake wakati wa kujibu mchana, basi aingie mchana, kwa hiyo, tumwite mtoa hoja Mheshimiwa Stephen Wasira, atakayetumia zaidi ya saa moja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru sana kwa kunipa fursa nyingine tena ili niweze kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha hapa Bungeni Siku ya Alhamisi, inayohusiana na Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2012/2013. Napenda kutumia nafasi hii, kukushukuru sana kwa jinsi unavyoongoza Bunge letu, mwanzoni damu zilichemka sana lakini baadaye ukazipoza. Naona tunaendelea vizuri na nina imani tutafika vizuri. Kwa hiyo, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika na Wasaidizi wako wote.

Kabla sijasema lolote, ningependa niwatambue Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao wamechangia hoja hii. Jumla yao ni 229, karibu Bunge lote wamechangia ama kwa kusema au kwa maandishi. Kwa hiyo, ningependa niwatambue waliochangia kwa mdono kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Christina Mugwai, Mheshimiwa Kabwe Zitto - Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Sarah Msafiri, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Letecia Nyerere, Mheshimiwa Lutengano Kigola, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Amina Amour Abdallah, Mheshimiwa Mwigulu Madelu, Mheshimiwa Ali Salim, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Rita Mlaki.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Mustafa

Akunaay, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Muhammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Dustan Kitandula - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Cecilia Parreso, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Seleiman, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Salim Hassan

Abdallah Turky, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Mhandisi Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Mheshimiwa Goodlack Ole-Medeye na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Wengine ambao hawakuwa wameandikwa mapema wote nimeshasoma majina yao yapo, kama kuna ambaye sikumsoma na alichangia kwa kuongea basi atanijulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na ambao hoja zao tumezichukua na tunazo ni Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Abas Mtemvu, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Aisha Mohamed Amour, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mheshimiwa Anjellah Jasmin Kairuki, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro,

Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Cecilia Parreso, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa John Mipata, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Titus Kamani, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Kheir Ali Khamis, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne

Mchuchuli, Mheshimiwa Letecia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Gertrude Lwakatare, Mheshimiwa Bernard Lutengano Kigola, Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed Dewji, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Mwanakhamisi Kassim Said, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Profesa Juma Athumani Kapuya, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rukia

Kassim Ahmed, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mheshimiwa Sylvester Muhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo na Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu. Niliyekuwa nimemwacha lakini amechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Assumpter Mshama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasoma wote walioshiriki na kuwashukuru sana kwa mchango mkubwa ambao wameutoa bila kujali kama waliunga mkono au hawakuunga, lakini nawashukuru kwa kuunga au kutokuunga mkono ni sehemu ya kuchangia. Mwisho wa siku tutafika mahali tu maana hata kule tulikopigiwa kura siyo watu wote waliotukubali. Wengine walikukataa lakini uko huku na waliokubaliwa hawakuja, kwa hiyo, Bunge hili haliwezi lote likawa na mawazo yanayofanana. Lazima tukubaliane kwamba, wengine watasema hapana na wengine watasema ndiyo. Kazi yangu hapa ni kuwashawishi waliosema hapana waseme ndiyo. Wale

waliosema ndiyo sina *problem* nao maana wao wameshatuelewa hawana matatizo na Mpango.

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka nitumie fursa hii kabla ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nina mambo matatu ninataka kuyasema ya jumla na yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Ninaomba wale waliosema hapana wanisikilize zaidi kwa sababu kazi yangu hapa ni kuwafanya wakubali kwamba Mpango huu ndiyo ule ule tulioupitisha mwaka jana wakati wa Bajeti na hii ni sehemu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, sasa huwezi kukubali mwaka jana, halafu ukianza kutekeleza baada ya miezi 12 tena ukakataa. Lakini unaweza kusahau kwa sababu sisi binaadamu tumeumbwa kusahau. Tungekuwa tunakumbuka kila kitu, tungekuwa tunaishi maisha magumu sana, maana tungekuwa tunakumbuka kifo, halafu tunaanza kukosa usingizi. Kwa hiyo, nadhani kusahau nayo ni sehemu ya uumbaji wa Mungu. Lakini nataka kusema kwamba vipaumbele vilivyoelezwa katika mpango huu wa mwaka 2012/2013 ni vile vile ambavyo tulipitisha katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Tena nitawasomea sasa hivi kwa kumbukumbu tu.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha Mpango. Ukisoma humu kwenye hiki kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano, utaona *strategic intervention,* tuna-*intervene* katika maeneo gani. Tumeeleza vizuri, lakini kwa ajili ya kumbukumbu, ningependa kusema tulikubaliana kwamba katika Mpango wa Maendeleo

wa Miaka Mitano, tutaweka vipaumbele mahsusi vitano na viko katika Mpango wetu wa Maendeleo.

Tulisema kwanza, tutafikiria uwekezaji katika miundombinu, kwa sababu shabaha ya mpango huu ni kuondoa vikwazo vinavyozuia kukua kwa uchumi, ndiyo shabaha kubwa. Mpango wote wa miaka mitano unakusudia kuondoa vikwazo vinavyozuia kukua kwa uchumi. Tulisema *priority* namba moja itakuwa miundombinu. Watu wote, hakuna haja ya kusoma Chuo Kikuu kuelewa kwamba nchi ambayo haina barabara, reli yake haifanyi kazi, haina umeme, haiwezi kukua kwa kasi kwa uchumi. Kwa sababu hivyo peke yake ni vikwazo vinavyozuia kukua kwa uchumi na hii ni hakika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu anayelima mahindi Rukwa, ambaye hana barabara ya kufikisha mahindi Shinyanga, ataendelea kulima *on subsistence* kwa sababu mahindi yake hayapati soko na hakuna barabara ya kumuunganisha na soko. Kwa hiyo, uchumi unakuwa wakati soko liko *smooth*. Kwa hiyo, miundombinu ni jambo la msingi katika ukuzaji wa uchumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukasema nini? Tukasema tutashughulikia miundombinu na miundombinu ya kwanza ni nishati, tulikubaliana. Mwaka jana kwa kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, tulikuwa na mgao wa umeme miezi 12 iliyopita na ndiyo ilikuwa msingi uliofanya tukashindwa kupitisha bajeti ya nishati, tukae hapa tuzungumze namna ya kuondoa kikwazo kwa uchumi. Ndiyo tulikubaliana kuweka mpango wa

dharura, kuzalisha *megawatt* na kuondoa mgao wa umeme na tulijua kwamba tunaweka wa dharura, lakini wa gharama. Lakini tulikubaliana kwamba umeme utakuwa wa gharama, lakini itakuwa gharama kubwa zaidi kutokuwa na umeme na hili tulilisema wote bila kujali chama. Tukakubaliana.

Sasa tumeweka nishati kama moja ya vipaumbele na tunasema nini? Tunasema umeme sasa unaozalishwa, unazalishwa kwa gharama kubwa kwa sababu tunatumia mafuta. Sasa tunataka kuweka kipaumbele cha kujenga bomba la kutoa gesi asili kutoka Mtwara na Songosongo kuja Dar es Salaam ili umeme unaozalishwa pale Dar es Salaam na mahali pengine uwe wa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa umeme wanatuambia sasa wanatumia senti 42 za Kimarekani kuzalisha *unit* moja, lakini tukitumia gesi, itashuka mpaka senti saba. Lazima tukubali kwamba hiki ni kipaumbele. Ukizungumza *inflation* halafu ukakata bajeti inayotaka kushusha bei ya umeme, unapata taabu sana kujieleza. Unasemaje sasa? Kwa hiyo, tukakubaliana umeme, tukakubaliana usafirishaji tehama, maji safi na maji taka katika sehemu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sasa nitakuja kueleza jambo lingine tena baadaye. Tukakubaliana tuweke mkazo katika kilimo, tukakubaliana kuweka mkazo katika viwanda na hasa vile viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya wakulima ili kuondokana na

tatizo la soko kama lile linalotukabili sasa kwenye zao la pamba hivi sasa. Halafu tukakubaliana kipaumbele kingine ni kuendeleza rasilimali watu na tukakubaliana ya kwamba bila sayansi, tekinolojia na kuwa na ubunifu, hatuwezi kupiga hatua; na tano tulikubaliana kuendeleza huduma za utalii, biashara na fedha. Hayo ndiyo mambo tuliyokubaliana miezi 12 iliyopita. Mpango huu wa mwaka mmoja unazungumza suala la kutekeleza haya tuliyokubaliana.

Kwa hiyo, nasema, wale wanaosema hawaungi mkono, wamebadili tu mawazo, lakini walikubali mpango. Mpango huu ndiyo tunaotekeleza sasa na kwa sababu binadamu tuna hulka ya kusahau, kazi yangu ni kuwakumbusha halafu tuunge mkono, maana ndiyo mambo tuliyokubaliana.

Mheshimiwa Spika, sasa sitaki kupoteza muda mrefu kueleza vipengele vya kila mpango tunaotaka kutekeleza katika vipaumbele hivi kwa sababu vipo katika bajeti na sisi wote tunajua viko wapi na tunasema nini sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisema kabla sijajibu hoja, linahusiana na suala la kusema kwamba mpango huu eti unakataliwa kwa sababu ugharamiaji wa mpango eti hatukufika asilimia 35. Hapa kuna *version* nyingi. Kwanza nataka nikiri kwamba rafiki yangu Mheshimiwa Zitto alikuwa anasoma *version* ya mpango kwa tafsiri ya Kiswahili.

Ni kweli na nataka niseme wakati mwingine watu wanafikiri Kiingereza, halafu wanatafsiri Kiswahili au wanafikiri Kiswahili, halafu wanatafsiri Kiingereza. Sasa

mpango tuliopitisha *version* rasmi, ukitokea mgogoro wa tafsiri, *version* inayochukuliwa ni ile ya Kiingereza kwa sababu ndiyo *original* na ndiyo iliyopitishwa na Bunge hili. Ila Bunge likatuambia, nendeni mkatafsiri. Sasa kama tulitafsiri tukakosea, tutakwenda kutafsiri vizuri zaidi. Maana nitakueleza tafsiri na hiyo ni kawaida tu, hata ukiwa na Sheria ya China na ukasema Sheria inayosimama ni ya Tanzania, unasema ya Tanzania ni kawaida. Kwa hiyo, nasema *original version* ni hii.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Zitto anasema tunaweza kutumia fedha za ndani asilimia 35 kuendeleza maendeleo.Mimi nasema tungekuwa tunaweza wala hakuna tatizo. Lakini bajeti yetu mwaka huu, ni Shilingi trilioni nane. Ukitoa asilimia 35 ya Shilingi trilioni nane, inakuwa Shilingi trilioni 3.0 *something*. Halafu ukiondoa *wage bill* 3.3 *trillion* utakuwa una *six*, unabaki na 1.8. Huwezi kuendesha Serikali hii kwa trilioni 1.8 ununue dawa, uweze kulipa mshahara Mwalimu bila shaka, ulipe Dakitari bila dawa, umlipe dereva bila mafuta ya petroli. Uchumi namna hiyo hauwezi kwenda popote. Kwa hiyo, nataka kumsaidia tu kwamba, najua Mheshimiwa Zitto msomi, walibishana sana na Mheshimiwa Mwigulu, nilikuwa nawaangalia kwenye *TBC1* wanasema mimi nilipata Daraja la A. Mimi nataka kuwaambia wasomi vijana hawa, Daraja la A au la B siyo hoja, hoja, unatumiaje elimu hii katika mazingira yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimesoma uchumi ukubwani, na nilipata *distinction* kwenye *Development Economics*, lakini haisaidii kitu. Ninachotaka, mazingira ya sasa yananitaka nitumieje elimu hii kwa manufa ya

nani? Hiyo ndiyo hoja. Kwa hiyo, nataka kuwaambia bajeti hii imezingatia masuala ya msingi yanayotokana na mpango wa maendeleo na hilo ndilo jambo la msingi. Tuliposema asilimia 35, tulikuwa tunazungumza asilimia 35 ya *national budget* ambayo inaunganisha misaada, mikopo, fedha za ndani na kila kitu una-*convert* unapata asilimia 35. Lakini tulikwenda zaidi ya hapo, tukasema ili ku-*commit* bajeti ya kwetu wenyewe, iwe ya kodi au mapato yasiyo ya kodi, au mikopo ya ndani na kadhalika. Tukasema, angalau tusipungue asilimia *2.7 trillion*. Sasa hapo ndipo ninapotaka Mheshimiwa Tundu Lissu nimsaidie maana Mheshimiwa Tundu Lissu naye! Lakini yeye simlaumu kwa sababu ni Mwanasheria. Wanasema Wanasheria huwa hawajui sana hesabu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu alisema, kwenye kitabu kile tumesema tutakusanya Shilingi trilioni 8.6, hapana. Kwanza bajeti yetu haifiki Shilingi trilioni 8.6 kwa mwaka huu. Sasa tungesema eti hela zote Shilingi trilioni nane zinakwenda kwenye *development;* ah, Bwana, Mheshimiwa Tundu Lissu naye, lakini inawezekana ni hesabu au ni *oversight*. Lakini naona hayupo, mumsaidie tu safari nyingine awe anasoma vizuri kabla hajagomba.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninalotaka kulisema la jumla, linahusu kwamba wanasema, wako watu wanasema hawaungi mkono mpango kwa sababu mpango huu haujibu hoja na haufiki kwa wananchi. Wanasema wananchi wa kawaida hawafaidiki na mpango huu. Sasa mimi hapo tena nilikuwa nataka wanisaidie na wao maana nchi hii,

tuna shule 16,000 za msingi, tuna watoto 8,300,000 wanasoma Shule za Msingi, bajeti hii inakwenda kwenye hizo shule wasome, kama hawajui kusoma watajua, lakini lazima tugharamie wajue. Sasa ukisema watoto hawa 8,300,000 wote wazazi wao sio watu wa kawaida, watu wasio wa kawaida, hawa wanaishi wapi? Hebu, nisaidie na mimi niwatembelee hawa ambao sio wa kawaida. Lakini watoto 8,300,000 wamezaliwa na watu wasiokuwa wa kawada, wako wapi hawa? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuna watoto 1,500,000 wako *secondary school* katika sekondari 4,000 Tanzania nzima. Hawa watoto wote kweli watakuwa katika sekondari kila Kata, lakini bajeti inayokwenda kwenye hizi sekondari haiwafikii watu wa kawaida. Hao wasiokuwa wa kawaida, wanaishi wapi? Kata gani huko wanakoishi watu wasiokuwa wa kawaida? Tuambiane. *(Kicheko/Makofi)*

Bunda wote sisi wa kawaida pamoja na mimi, tuna Hospitali 231, tuna Vituo vya Afya 605, tuna Zahanati 5640, tunaomba pesa hapa kupeleka dawa. Mheshimiwa Mbunge anasema hii haiwafikii, watu wa kawaida hawatafaidika. Wanaotibiwa kwenye hizo Zahanati ni watu wasiokuwa wa kawaida, wa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani tuwe wa kweli. Lakini wala silalamiki. Kwa kawaida wanasiasa naona hapa Mheshimiwa Mrema ananiona, anajua. Wanasiasa tunapenda sana kutumia wananchi. Tunasema wananchi wamenituma, hata kama

hujaonana nao. Wote tuko hivyo, hata kama hujaonana nao unasema wananchi wote wa eneo hili wamenituma. Unamwuliz,a ulionana nao wapi mbona ni wengi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasema tuwe wa kweli katika jambo hili, kwamba bajeti hii kabisa kabisa haiwasaidii wananchi na wale wanaoitwa wa kawaida ambao kwa kweli ndio Watanzania wote hapo. Mimi napata taabu kwamba Shilingi trilioni nane, Shilingi trilioni 15, tuna bajeti na haziendi kwa wananchi hawa kwa huduma. Mimi nadhani hapa tuna matatizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani nimemaliza kazi hiyo ya mambo muhimu matatu niliyotaka kufafanua tena kwa nia ya kuwafanya wanaosema hapana, waseme ndiyo maana mpango huu, unajibu matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo limezungumzwa sana na kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Chenge - Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha kwa niaba ya Kamati yake, ametupa maelezo mengi sana ambayo ametoa ushauri wa namna tunavyoweza kusaidia kukuza uchumi na kupunguza mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei ni tatizo. Hakuna mtu yeyote anaweza akasema siyo tatizo awe wa kawaida au sio wa kawaida, mimi sijui wa kawaida wakoje na wasio wa kawaida wakoje, lakini ni tatizo ambalo sisi viongozi tunalijua na lazima tushirikiane katika kupambana nalo.

Mheshimiwa Spika, ushauri tulioupokea kutoka kule na sisi tunaukubali kabisa kwamba katika hatua za kwanza za muda mfupi kabisa, Serikali tuingize chakula, isiwe ndiyo msingi wa uchumi wetu, lakini kama kweli chakula kama mchele, bei zake ziko juu kwa sababu ndani ya nchi yetu hakuna mchele. Kwa hali ya kawaida, kwa miezi michache tu, itabidi tukubali, lakini msingi wetu lazima uwe kuzalisha. Lakini kama sasa hivi hamna chakula, lazima tutanunua tu kutoka nje ili tuweze ku-*suppress* upandaji hovyo wa bei na hiyo itakuwa kwa mchele, ngano, sukari, lazima tutazame uwezekano wa kuongeza mafuta ya kula kwa njia zozote zile za kodi ili tuhakikishe kwamba mafuta yanapatikana hapa nchini kwa ajili ya kula, na huo ushauri tunaukubali kabisa na sisi tunaamini hiyo inaweza kusaidia. Tunazungumza juu ya Sekta ya Fedha, kudhibiti ujazo wa fedha.

Hii Benki Kuu wanafanya kazi hii kabisa kupunguza au kusamehe kodi katika vifaa vya gesi tumependekeza hapa kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini hasa zaidi kutilia mkazo uuzaji wa nje. Kwa sababu tukiuza nje, ndiyo shilingi yetu ina-*stabilise*. Kama hatuuzi sana nje, tutapata matatizo.

Kwa hiyo, kwa kweli lazima tuongeze kasi ya kuuza nje ili kusaidia kupunguza mfumuko wa bei kwa maana, unaotokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi au kutokana na *pressure* ya bei za vyakula, hiyo ni hatua za dharura za muda mfupi katika dili na matatizo ya mfumuko wa bei. Lakini tunakubaliana na Kamati vile vile kwamba katika hatua za muda wa kati na muda mrefu, lazima tutilie mkazo kilimo cha mazao

ambayo yanaonekana ndani ya soko yanahitajika sana. Lazima tutilie mkazo kilimo cha mpunga ili kupata mchele unaohitajika, lazima tutilie mkazo mbegu za mafuta, lazima tutilie mkazo kilimo cha miwa na katika mpango huu tumetamka, tumeainisha mabonde ambayo tunataka kuwekeza sukari.

Wawekezaji wapo, ni watu binafsi, sisi Serikali tuna-*facilitate*, lakini bajeti lazima i-*facilitate* ili anapokuja kuwekeza mtu, basi akute kweli kuna ardhi imepimwa na inaweza kufaa kwa ajili ya kilimo cha miwa au kilimo cha mpunga. Kilimo hiki hatusemi walime watu wa nje, watu wowote tu, hata wa ndani wanaweza wakalima miwa. Vile vile wanapolima miwa kwenye mabonde haya, wajue kuna watu wanaozunguka yale mabonde, wawashirikishe katika kile kilimo kama ilivyo Kilombero *out growers* ili watu wa maeneo yale wakue pamoja na ile kampuni inayolima miwa na wao walime, lakini kampuni inunue miwa ya wananchi. Haya mambo yanaweza kusaidia kuongeza uzalishaji wa sukari na vile vile utatusaidia sana kuongeza uzalishaji wa mchele, ili basi tuweze kupunguza kasi ya ongezeko la bei.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyokwishasema na kama alivyosema Waziri wa Nishati na Madini, suala la kujenga bomba kutoka kule Mtwara kuja Dar es Salaam ni suala la msingi kabisa na nimefurahi Waziri wa Nishati na Madini amesema tayari wameshawekeana mkataba. Kwa hiyo, matumaini yetu ni kwamba bomba hili litaanza kujengwa na likianza kujengwa litatupunguzia kasi kubwa sana ya kupanda bei ya umeme, vile vile litatupunguzia

gharama ya uzalishaji viwandani kwa sababu viwanda vinatumia umeme na bei ya umeme ikishuka, uzalishaji gharama itapungua.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahimiza juu ya kuhakikisha tunasimamia suala la usafiri na usafirishaji, barabara, reli, viwanja vya ndege, na kadhalika na iko katika mpango. Mimi nadhani haya mambo ambayo yamesemwa na Kamati, hatuna sababu ya kubishana na Kamati hata kidogo kwa sababu, ni mambo ya wazi tu na kuendelea kuimarisha ununuzi wa mitambo na magari, kuimarisha hifadhi ya chakula ya Taifa ni mambo muhimu ambayo yatatusaidia katika muda mfupi ujao na wa kati, kuhakikisha kwamba, tunakuwa na chakula cha kutosha ambacho kimehifadhiwa hapa. Ili unapokuwa na soko huria tena, huria yenyewe ni nje ya nchi, chakula kinanunuliwa na nchi nyingine vilevile, sisi tuwe na hifadhi ili upungufu ukiwepo tuwe na chakula ambacho kinaweza kutusaidia hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahimiza sana kuwepo kwa vivutio vya wakulima. Nami nakubaliana kabisa na Kamati ya Uchumi, kutekeleza mfumo wa ruzuku na pembejeo, kuweka mfumo wa kilimo cha mikataba; wote ni ushauri ambao tumeupata kutoka kwenye Kamati, na sisi tunauzingatia. Vilevile, ni lazima kuhakikisha kwamba, mkakati wa kilimo unaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, watu wengine wamesema na wanasema kweli kwamba, uchumi wetu unakua, lakini maisha ya watu wetu bado ni duni na umasikini haupungui kwa kiwango kile kile cha

uchumi kukua. Hili tunalijua na tumelisema kwenye hotuba zote hizi kwamba, sekta zinazokua kwa kasi, kama Mawasiliano 19% kwa mwaka jana, 2011; watu wangapi wameajiriwa katika Sekta ya mawasiliano? Watu wengi zaidi wameajiriwa katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukitaka kupunguza umasikini *seriously,* ni lazima uwekeze katika kilimo. Hili ni wazo, tumelianza tangu mwaka 2007 kwamba, tuanzishe Benki, na tumefanya hatua zote. Sasa tumefikia mwisho, tunaanzisha Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Kilimo haitaweza kuanzishwa tu ika-*solve problem* kwa sababu kilimo ni kitu ambacho unawekeza kwa muda mrefu. Lakini namna ya kuwafikishia wakulima mikopo ni lazima tuwahimize wakulima wale waanzishe *SACCOS,* ili *SACCOS* zile zije zifanye kazi na Benki ya Kilimo, ili hata mkulima wa heka moja aweze kupata mkopo wa kuboresha kilimo chake.

Mheshimiwa Spika, ni kwa kufanya hivyo peke yake, tunaweza kuwafanya wakulima wapate manufaa zaidi kutokana na nguvu ya kazi yao na kupunguza kasi ya umasikini ambao unawakabili. Kwa hiyo, eneo la *SAGCOT* tumeshalifanyia mkakati, nadhani itatusaidia. Halafu vilevile kukamilisha zoezi la kuainisha maeneo ya kilimo kwa kila Wilaya, tunafanya hivyo.

Kuhusu Serikali iendelee kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula, nimeshalisema. Serikali ihamasishe uanzishaji wa viwanda na kusindika nyama. Ni kweli

tumesema katika mpango kwamba, kuweka viwanda na mazingira yatakayowezesha watu kuwekeza katika viwanda kwa ajili, ya kuongeza thamani ya mazao yetu kama ngozi, nyama, pamba, korosho, na kadhalika, ni mambo ya msingi kama tunataka kweli uchumi wetu ukue na uwe kwa manufaa ya wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia maoni yaliyotolewa na Kamati, yako maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Christine Lissu. Alizungumzia suala la 35%. Nimelijibu nadhani. Kuna kitu kinaitwa *physical development,* maendeleo ya vitu ambavyo ukienda unaviona, kama ni barabara unaikuta, kama ni reli utaiona, lakini yako katika mfumo wetu ule. Bajeti yetu katika mambo tuliyokubaliana ilikuwa ni pamoja na rasilimali watu. Hii rasilimali watu katika mpango wetu, katika *4.7 trillion,* hatukuingiza suala la rasilimali watu, ingawa ni kigezo na ni moja katika vipaumbele tulivyokubaliana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumejaribu kukokotoa. Ziko fedha katika bajeti ya kawaida ambayo tumejaribu kukokotoa, zina *nature* ya *development* kwa sababu, ya kuongeza *skills.* Tumegundua kule kuna Shilingi bilioni 841.4, ambazo kama zingerudishwa kwenye *development* na kutilia mkazo suala la *skills, then* bajeti yetu ya mwaka huu kwa ajili ya maendeleo, ingekidhi kigezo hicho cha 35%. Maana sasa tuna 30%, lakini ukiongeza 800 inakuwa trilioni tano nukta *something* ambayo, ni sawasawa na 35.5%. Sasa hayo ni mahesabu, lakini vipaumbele ndiyo vinaamua mahesabu.

Mheshimiwa Spika, sasa wachumi hawa wamebishana sana. Nilimwona tena Mheshimiwa Mwigulu na nilimwona Mheshimiwa Zitto kwenye *TV,* wanabishana wanasema *convetional approach* na *non-convetional;* aah, sasa mimi sijui. Lakini nilisoma uzeeni, mambo ya *convetional* na *non-convetional,* labda watanisaidia zaidi wenyewe. Lakini ninachosema, tulikubaliana *skills development* ni kipaumbele na ni lazima kigharamiwe. Hatuwezi kufanikiwa katika mpango wetu bila ku-*develop skills.* Hakuna nchi duniani ambayo imepuuza *skills* na ikafanikiwa, hamna! Zote hizi unazosikia zinasemwa.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu vilevile kwamba, hata ile 35% siyo kwamba, ni *arbitrary* na wala siyo lazima kwamba hii haiwezi kuzidi hapo. Inategemea hali ya uchumi tu. Hali ya uchumi ikiwa nzuri, tutazidi hapo kwa sababu, shabaha yetu ni kukuza zaidi uchumi. Sasa *development budget* ni mbegu. Mkulima anajiwekea mbegu, anasema hii mbegu siwezi kula hata nikikosa chakula leo, ili apande maana anajua akipanda itampa chakula zaidi. Kwa hiyo, ni mbegu. Sasa mkibishana unakula mbegu au unaweka mbegu; masuala ya uchumi, hata mkulima wa kijijini atakwambia, kuweka mbegu ni lazima. Kwa hiyo, hatuna ubishi sana juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba, mwezi Februari mwakani, Bunge hili litapitia tena Mpango wa Maendeleo wa mwaka unaofuata. Tutatumia mawazo tuliyoyapata hapa kuboresha zaidi na kuona ya kwamba, kama inawezekana kuweka

fedha zaidi za maendeleo, basi tutafanya hivyo. Nataka niwahakikishie hivyo, wala hakuna tatizo. Ni lazima tupunguze *dis-investiment* katika kilimo na Benki ya Kilimo, imekusudiwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Sera za Gesi, hizi tumeshazizungumzia na Waziri wa Nishati na Madini ametuambia ikifika Desemba, tutaanza kuona Sera ya Gesi. Maana gesi hii, inaweza kubadili sura ya uchumi wa Tanzania na kitu kikubwa kwa Tanzania. Kwa hiyo, itabidi tutengeneze Sera ya Gesi na mimi ninaamini kabisa tutafika hapo tunapotaka.

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine yametolewa na Mheshimiwa Zitto; nimeshajibu sehemu kubwa. Jana kulikuwa na kaubishi hapa, wanasema ni Bajeti Mbadala, ni Mawazo?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu ndio alitusaidia tena akasema hamna Bajeti Mbadala na Kiongozi wa Upinzani, akamuunga mkono. Mheshimiwa Zitto, hakuwepo. Sijui wamekueleza? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini chochote utakachokiita kwa mapenzi yako mwenyewe ni kwamba, lile ongezeko ukichukua mapendekezo ya matumizi yaliyokuwa yanapendekezwa na Mheshimiwa Zitto, katika hiyo inayoitwa Maoni au Bajeti Mbadala, ukifanya mahesabu ukiwa makini, maana mimi siwezi kulaumu, maana hata ukiwa mchumi namna gani, unahitaji msaada wa watu wengine. Kwa hiyo, inawezekana ilikuwa haraka, na Mheshimiwa Zitto, hakupata msaada sana. Lakini, ukichukua matumizi anayopendekeza na mapato, huwezi kuendesha

Serikali. Mheshimiwa Zitto, utawalipa vizuri sana watu wote, lakini hauwezi kupata vitendea kazi. Utawalipa Madaktari bila dawa? Utawalipa walimu bila vitabu? Madereva bila mafuta? Kwa hiyo, Serikali yako hiyo itakwama kabisa Mheshimiwa Zitto. Ni lazima ku-*check* vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya kuendesha Serikali unajua, lazima ku-*check* vizuri. Ama sivyo *your Government will run bankrupt,* wananchi wanataka huduma na wewe unasema tumelipa mshahara! Wakulima wanakuuliza mbolea, unasema hakuna, mshahara. Hatuendeshi hivyo Serikali, hapana. Kwa hiyo, ni lazima kabisa.

Mheshimiwa Spika, mengi yanayohusiana na hayo nimeshayaeleza. Halafu jambo lingine labda ambalo kabla sijaingia kwenye kujibu hoja za Wabunge wengine wote, nataka niseme, unajua tusitazame matumizi ya kawaida kama jambo baya. Kwanza, kimsingi ukiongeza matumizi ya maendeleo, *automaticaly* unaongeza matumizi ya kawaida, kabisa! Tena ni kama amri tu. Maana ukijenga sekondari 4,000 unapeleka walimu na ukipeleka walimu, unawalipa. Kwa hiyo, matumizi ya kawaida yanaongezeka. Ukijenga Hospitali kila Kijiji na Zahanati kila Kijiji na kila Kata Kituo cha Afya, utaongeza Watendaji wa Afya na utawalipa. Tena wenyewe unawasikia huko wanataka mishahara mikubwa kabisa. Kwa hiyo, matumizi ya kawaida yataongezeka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusije hapa tukawa tunasema matumizi ya kawaida ulaji tu, aah; Alooh, ulaji peke yake! Matumizi ya kawaida ni *grease* ya kuendesha Serikali. Huwezi kuya-*avoid* kabisa. Ila unachosema ni kwamba, usikope kuendesha Serikali kutoka nje, hiyo nakubali. Lakini kutuambia tusikope kujenga daraja la Kigamboni, aah tunakopa na Malagarasi tungejengaje bila kukopeshwa? Tutakopa. Ila tunakopa kwa uangalifu tu, kuhakikisha ya kwamba, hatukopi sana halafu tukarudi kuwa *HIPC,* hiyo tu.

Mheshimiwa Spika, vigezo vipo, Waziri wa Fedha, atatueleza tu, atavieleza vizuri. Maana yeye ndio mkopaji wetu mkubwa, atatueleza vizuri tu anakopakopaje? Lakini ni lazima tukubali kwamba, hakuna nchi inayokopa na kama tunakopa kuingiza kwenye *development,* kwamba vizazi vijavyo vitalipa, ni vizuri vitalipa. Maana hata kizazi cha sasa kinalipa hela alizokopa Mwalimu Nyerere mwaka 1962, ni kawaida tu. Huwezi kumlaumu kwa nini ulikopa, alah! Kwa nini wewe upo sasa? Ni kwa nini umesoma? Nimejenga *University* na wewe ukasoma, sasa si ulipe deni? Sasa unataka kufanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba ni lazima tukope, lakini tunakopa kwa uangalifu. Unakopa kuwekeza wapi? Ndiyo hoja tu hiyo peke yake. Lakini kama unawekeza katika miundombinu na wewe unakopesheka, kwanza kukopesheka ni heshima. Ndiyo. Kwamba, umejenga nchi yako, uchumi wako mzuri, unakopesheka, na daraja huna, unakopa unajenga daraja, aah. Uache kukopa ukae unakusanya kodi, zisipotosha, daraja hujengi? Huo

uchumi gani? Huo uchumi wa jembe la mkono, ni mgumu sana, haiwezekani. Hiyo ni *consumption economy.* Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wafanyabiashara wanajua vizuri jambo hili. Tena ukikuta wafanyabiashara nao wanatuambia usikope na huku wao wanakopa kila siku, unapata taabu kuwaelewa, lakini wanakopa hawa. Halafu wanakwambia wewe ukiwa na tatizo usikope. Wao ukitaka kukopa wanakwambia, una nyumba? Sasa kama bila kukopa ukajenga nyumba, halafu ukalipa pole pole, utakuja kupata wapi mtaji wa kuweka kwa watu?

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali machache ambayo tumehojiwa hojiwa hapa na mimi wajibu wangu ni kujibu. Mimi nadhani wale waliokuwa wanasema hawaungi mkono hoja, sasa wameanza kuunga mkono, maana wa kwanza ni Mheshimiwa Zitto, anaonekana sasa amechangamka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unajua ni *facts* tu. Ukweli ni ukweli, ukiupata tu unakufanya huru. Huwezi kugombana tu; unajua kugombana nayo wala haikusaidii sana. Maana kugombana na kukasirika na kutoa mishipa ni uendawazimu tu, lakini haukupi *thinking,* ni lazima ufikiri. Huwezi kufikiri umekasirika. Ukikasirika una-*stop* kufikiri. Nataka niwashauri, mnapotaka kuamua mambo makubwa, msikasirike kwa sababu, mtaacha kuamua vizuri mambo muhimu kwa nchi yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu, alisema Mpango wa Miaka Mitano ulisisitiza kupunguza misamaha ya kodi. Sisi tunakubali na bajeti yote inasema tutajaribu kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyambari, yeye aliuliza hii mipango ya *MKUKUTA, MKURABITA,* inasaidiaje maendeleo?

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya uchumi unaokua yanatokana na fedha zinazopita katika *MKUKUTA* na Mpango wa Maendeleo huu tunaouzungumza. *MKURABITA,* unafanya kazi katika baadhi ya maeneo. Nadhani haijafika Tarime. Lakini hii inasaidia tu kufanya thamani ya mali ambazo kwa Sheria, zilikuwa hazionekani kama zina thamani, sasa ziwe na thamani mbele ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kayombo, alizungumzia kwamba Mpango wa Maendeleo, umeeleza ukubwa wa riba katika Mabenki, lakini haujaeleza suluhisho.

Mheshimiwa Spika, nimesema katika bajeti ile kwamba, riba zimeanza kujirekebisha kwenda chini. Lakini mambo haya ya riba ni mambo ya mabenki binafsi, wakati mwingine yanaogopa kushusha riba kwa sababu ya *risk.* Lakini ni Wizara ya Fedha inayosimamia, nadhani itatusaidia katika kuona tunapunguza kiasi gani cha riba.

Mheshimiwa Spika, watu wengi waliosema kama Mheshimiwa Lissu, kama Mheshimiwa Mughway, kama

Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mwanamrisho na Mheshimiwa Abama, wamezungumza mambo ambayo tayari nimeshayajibu, yanahusiana na *ratio* kati ya Mpango wa Maendeleo na bajeti ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa kabisa ambalo nimeshalijibu na ambalo lilikuwa limesemwa na Mheshimiwa Rajab Mohamed; Mheshimiwa Gerson Mtinda; Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya; Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, tena huyu ni rafiki yangu, tena sio rafiki yangu wa utani utani, ni rafiki yangu hasa! Lakini tutaendelea kuzungumza naye, lakini kwa maelezo niliyoyatoa sasa hivi nadhani kwa sasa anakaribia kutuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Anastazia Wambura, kuna Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo; wote walizungumzia sana *ratio* kati ya *development budget* na *recurrent.* Nimeshalitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, wengine walioandika ni Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Elirehema Mkono na Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makala. Namshukuru sana Mheshimiwa Makala, alifanya kazi nzuri kusema kweli, alitusaidia sana katika kueleza hili suala la *skills.* Kwamba, huwezi kuwa na *development budget* na vipaumbele vyako vina *skills* lakini haviko katika bajeti. Aliona kweli kabisa viko kwenye *recurrent* na akatushauri tuvirudishe kwenye *development* ili tufikie lengo. Namshukuru sana Mheshimiwa Ramo, alieleza jambo hili vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kwa kweli ni kuongeza uchumi. Hawa wote niliowataja walisema lengo letu ni kuongeza uchumi kadiri unavyokua. Kadiri uchumi unavyokua, mapato yetu yakiongezeka, ni lazima sehemu ya mapato yetu iende kwenye maendeleo. Kwa sababu, hiyo ndiyo inayoweza ku-*fuel* kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid, alizungumzia sana suala la maendeleo na kama kweli Wizara na Halmashauri, zinaweza kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kwamba, Mpango huu wa Maendeleo, umetengenezwa kwa namna ambayo tunaweza kusimamia na tumejituma. Maana mambo haya ni kujituma. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zimeagizwa na Mpango huu kusimamia na kupokea ripoti za mambo yanayoendelea. Tume ya Mipango katika Ofisi ya Rais, itakuwa inafuatilia miradi ya kitaifa ambayo ni miradi ya kimkakati. Tutakuwa tunajaribu kuangalia kwa karibu zaidi, kuona mpango wetu unatekekelezwa, maana utekelezaji wa mpango huu ndiyo msingi wa maendeleo yenyewe. Kama hatutekelezi, hakuna mpango.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, alisema mapitio ya Bajeti ya Serikali, yaanze mapema ili utekelezaji wake uanze.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na hoja yake kabisa, ndiyo maana tunasema Februari, wala siyo

Aprili tena, tutaleta mapendekezo kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, lakini Profesa Kahigi, alikuwa mkali kidogo. Alisema tunaleta hapa mpango hautekelezeki. Profesa, Mpango unatekelezeka huu, ila mipango yote unaweza ukatekeleza *partly* na wakati mwingine ukapata *problem* kwa sababu, ni...

**SPIKA:** *Microphone, microphone.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, natafuta kitendea kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namshauri tu Profesa Kahigi, asome Sura ya pili ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2011/2012. Kuna maelezo pale yanayoonyesha barabara, nishati tumefanya nini, miundombinu yetu; utekelezaji umekwenda mpaka kurasa zote zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane na hofu ya Mheshimiwa Kahigi kwamba inawezekana tumetekeleza lakini hatukutekeleza kikamilifu. Nadhani ndicho alichokuwa anasema, lakini kusema hatutekelezi kabisa hiyo nayo itakuwa taabu, miezi, watu wazima tukae hapa halafu tutoke hatukutekeleza kabisa! Hiyo hapana. Hiyo Profesa, hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwa sababu kwenye *Local*

*Government* mwaka huu sisi tunatoka kule kule halafu tumechaguliwa huko tunafuatilia maendeleo, kulikuwa na *problem* mwaka huu unaokwisha. Tunataka mwaka huu unaonza tusimamie vizuri zaidi na Mheshimiwa Mgimwa tutamwomba atusaidie kupeleka fedha ili mipango midogo midogo inayohusu wananchi kule vijiji iweze kutekelezwa. Hiyo naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Devota Likokola, anasema Serikali ijitahidi katika kasi hii ya utekelezaji wa miradi. Nakubaliana naye kabisa. Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama naye anazungumza ni nani msimamizi wa miradi ya maendeleo ambayo Serikali inatoa fedha? Wako wasimamizi kila mahali katika ngazi ya Mkoa, kuna Sekretarieti ya Mkoa chini ya Mkuu wa wa Mkoa inasimamia pale katika ngazi ya Wizara, yuko Waziri Mkuu anasimamia utekelezaji na Ofisi ya Rais ina tume, ina mipango, inamsaidia Waziri Mkuu na Rais kuona kwamba mpango ule unatekelezwa. Kwa hiyo, usimamizi upo katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Amina Nassaro Makilagi alisema, kuwepo na vipaumbele na viwe vinalenga moja kwa moja maisha ya wananchi na mimi nakubaliana naye kwamba lazima tulenge, kwa sababu kwa kweli tunafanya bajeti, tunafanya mpango kwa ajili ya nani? Tunafanya mpango, tunafanya bajeti kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Hakuna Tanzania bila watu! Tanzania gani hiyo itakuwa haina watu na bado iwe inaitwa jina? Kwa hiyo, kwa kweli lazima tulenge kwenye huduma za maji, kilimo, umeme na huku mjini ambako watu wetu wengi wanaishi, sasa tunaanza kupeleka programu ya umeme ili kuboresha maisha na

tukieneza umeme kule vijijini *migration* ya vijana kuja mjini itapungua, kwa sababu watapata shughuli za kufanya kule vijijini na tunaweza tukapunguza kidogo uhamaji kutoka vijijini kuja huku. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, hiyo ni hoja ya msingi na mimi naiunga mkono kabisa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Makilagi alizungumzia vilevile suala la uchambuzi wa mabonde, na akataka zaidi mabonde yaingizwe katika Mpango na akatoa mfano wa mto Mara. Nami nasema, huu ni mwanzo tu, tumechagua mabonde machache, lakini shabaha yetu ni kukuza kilimo katika mabonde mengi zaidi nchini.

Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Makilagi itazingatiwa katika kutazama Mpango mwingine unaofuata ili tuone na mabonde mahali pengine kwa sababu ni kweli vilevile kwamba huwezi kutilia mkazo kilimo cha chakula kwenye *SAGCOT*, halafu watu wanaoishi nyanda za juu ambao hawana chakula wakategemea soko tu la kununua kutoka huko. Lakini ukiweza kufanya mabonde yale nayo yakazalisha gharama ya usambazaji wa chakula itakuwa karibu kwa sababu watakuwa katika maeneo hayo hayo. *(Makofi)*

Vilevile suala la umwagiliaji, wenzetu wa Kilimo watatazama kwa sababu maeneo yenye ukame yanahitaji vilevile kupewa fursa zaidi ya umwagiliaji ili tuweze kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza na Mheshimiwa Esther Matiko, walizungumza juu ya *small scale farmers* kwamba tuboreshe miundombinu ya barabara na mabwawa. Mimi nakubaliana nao. Kwenye Sekta ya Kilimo kuna *element* ya mabwawa, tena katika maeneo ya ukame, lakini ningependa kushauri tu yale mabwawa *multipurpose*, kwa sababu, mimi najenga la *irrigation* lakini pale kuna ng'ombe hawana maji. Una-*irrigate* na ng'ombe wanakunywa, mimi nadhani tukifanya hivyo tutafika haraka zaidi.

Mheshimiwa Sara Msafiri, anazungumzia Shilingi bilioni 50 zilizotengwa kwa ajili ya *EPZ,* zielekezwe kuendeleza kilimo. Sasa hapa Mheshimiwa Sara anataka tubadili vipaumbele. Kiupambele ni kipaumbele, lakini na viwanda ni kipaumbele, na ukilipa *EPZ* na kuweka miundombinu katika *EPZ* unakaribisha uwekezaji wa viwanda ambao na wenyewe ni muhimu kwa maendeleo. Kama unazungumza dira ya 2025 *then* huwezi kukwepa kuweka mkazo suala la viwanda.

Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Peter Msolla na Mheshimiwa Sylvester Francis Koka, wote wamezungumza kwamba kilimo tukipe umuhimu kwa sababu ndicho peke yake kinaweza kikasaidia vilevile kuleta mageuzi ya viwanda ili kuwa na viwanda vya kuongeza thamani. Hili ni jambo kubwa.

Nadhani Waziri wa Fedha amewasikiliza vizuri sana Waheshimiwa Wabunge, hili jambo limezungumzwa sana Waheshimiwa Wabunge katika vikao cha *Caucus* ya CCM hata wale ambao walikuwa wamechelewa

kuelewa walianza kuelewa baada ya kushauriana nadhani na *Caucus* ya CHADEMA nayo ikikaa vizuri na wenyewe wataelewa tu, kwa sababu ni mambo ya vyama haya. Wakati mwingine unaweza kuwa na msimamo wa Chama tu, lakini wanakuuliza sababu, unasema alaah! Chama, lakini *issue* siyo hiyo peke yake, *issue* ni pamoja na wewe kuelewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, zile *Caucus* ni shule na mimi naona shule ya *Coucus* ya CCM. Mimi mjumbe kule, naona kama ilisaidia sana kufanya Waheshimiwa Wabunge waelewe ndiyo maana wanaunga mkono. Siyo kwamba wanaunga mkono kwa sababu wao ni CCM, aah, wameelewa na mimi nawapongeza sana kwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mlaki alizungumzia sana kuhusu kuwapatia wakulima mikopo. Nakubaliana naye na ndiyo maana tunaanzisha Benki ya Kilimo ili kuanza kuwekeza hii.

Mheshimiwa Ritta Mlaki, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Desderius John Mipata na Mheshimiwa Meshack Opulukwa walizungumzia fedha zilizotengwa kwa ajili ya uendelezaji wa mabonde ya Kilombero kwamba ni kidogo. Lakini nadhani hapa hatuelewani vizuri. Mabonde yale siyo kwamba Serikali inakwenda kulima, tunawekeza; Serikali iweke miundombinu ambayo itawawezesha wenye uwezo wa kulima, walime. Siyo kwamba Serikali sasa imeanza kulima mabondeni aah! Watalima watu, lakini wanataka kujua ardhi ipo? Imepimwa? Sisi tunakwenda kule mabondeni kupima na wakulima siyo lazima wawe wa

kutoka nje, wanaweza kuwa ni wakulima wa Kilombero, wakulima wadogo wadogo tunawawekea misingi pale, halafu wanalima mpunga lakini kisasa zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri huu ni mwanzo mzuri wa kuwa na maeneo maalum ya uwekezaji. Mheshimiwa Rukia Hamad, Mheshimiwa Sara Msafiri naMheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, walisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya kilimo ni kidogo. Pengine wana hoja, lakini nilikwenda kukokotoa baada ya kusikia hili na mimi mwenyewe ni Waziri wa Kilimo wa zamani nikagundua kwamba bajeti nzima ya kilimo kwa maana ya Sekta ya Kilimo, Sekta ya Kilimo ni kilimo mazao, kilimo mifugo, kilimo uvuvi, na kilimo misitu, vyote kwa pamoja, ile sekta imepewa asilimia tisa ya bajeti ya Serikali, ila zimesambaa Mikoani huko. Kwa hiyo, ukija kwenye Wizara pengine usizione, lakini tulipojaribu kukokotoa, ndiyo tukakuta *nine percent* ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wakuu walishatuambia tufike *ten*, kwa hiyo, tutajaribu kuangalia mbele zaidi kabla ya mwaka 2015 tuweze kufika huko tukuze zaidi kilimo. Lakini nasema hata ukifanya bajeti ya Serikali iwe kubwa, kama hakuna *source* nyingine ya kufikisha mikopo kwa wakulima, bado ni *problem*. Ndiyo maana lazima wakulima wetu wakopesheke, ndiyo maana lazima mali zao zilazimishwe ili waweze kupata mfumo wa kukopa.

Mheshimiwa Chibulunje, Mheshimiwa Rebecca Mngodo na wengine walizungumzia suala la

kufunguliwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ni tarehe ngapi? Nimeshajibu kwamba hii benki itafunguliwa katika msimu huu sasa wa bajeti, mwaka 2012 mpaka 2013 wakati wowote hapo. Maana Benki Kuu ndiyo inasimamia uanzishwaji wa hii benki pamoja na Wizara ya Fedha na wameshamaliza karibu na ndiyo maana tumebajeti fedha za *seed money* kutoka Serikali kuanzisha benki hiyo.

Suala la mfumko wa bei nimeshalizungumzia. Mheshimiwa Amina Amour na Mheshimiwa Capt. John Komba walizungumzia kwamba Serikali ijielekeze kwenye uvuvi, na mimi nataka kukubaliana na Mheshimiwa Komba kwamba kwa kweli yeye yuko kwenye Ziwa Nyasa, lazima tufanye *something* ku-*develop* upande wa pili ili samaki wasiwe wanavuliwa upande wa Malawi na sisi huku hatuvui. Kwa hiyo, kwa kweli ni jambo ambalo ningeshauri Mheshimiwa Komba, kwa sababu sasa kuna Wilaya ya Nyasa kule na hakika na umeme utakwenda huko wa uhakika waanze kutafuta uwezekano wa kuwekeza kwenye Ziwa Nyasa, ili samaki wanaopatikana pale waweze kuvuliwa na kuuzwa kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Mnyika, wao walikuwa wanahoji juu ya msongamano wa magari Dar es Salaam. Mheshimiwa Magufuli alikuwa anaeleza jibu lake leo hii hii, hapa Bungeni. Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Magufuli anayo dawa ya jambo hili na limewekwa katika vipaumbele vyetu. Tumesema barabara zinazounganisha nchi zinazokwenda kwenye maeneo ya uzalishaji na barabara zinazoondoa msongamano katika miji na mji mmoja uliosongamana

sana ni Dar es Salaam. Kwa hiyo, nafikiri hili litatekelezwa katika eneo hilo. *(Makofi)*

Usafiri wa mazao na abiria, nadhani hili limezungumzwa vizuri na Waziri wa Uchukuzi, ndiyo nilikuwa nasema, ukisema bajeti hii haijibu matatizo ya mtu wa kawaida, mimi nashangaa. Maana Mheshimiwa Josephine Ngezabuke, yeye alisema, kwamba ile reli ikifika Kigoma, watu wa Kigoma wanaotaka kuja Dar es Salaam sasa wanalipa Sh. 55,000/=, ikifika watalipa Sh. 19,000/=. Sasa ukisema na reli nayo haitasaidia mtu wa kawaida mimi nitashangaa. Hivi wanaopanda reli ni watu wa namna gani?

Kwa hiyo, nakubaliana na hii hoja na kwa kweli nataka niwaambie watu wanaotegemea reli ya kati kwamba sisi kule katika Mikoa ya Ziwa inahudumiwa na ile reli. Sisi tuna *double inflation* kule kwa sababu bei ya mfuko wa *cement* unaotoka Dar es Salaam kwa *Fuso*, unafika kule kwa bei kubwa sana. Kwa hiyo, suala kutengeneza na kuifanya ile reli ipitike na nasema hapa na rafiki yangu Mheshimiwa Mwakyembe ananisikia vizuri kwamba, yaani ni suluhu kwa maisha ya watu wanaotumia ile reli. Sasa kuna watu wengine huko nje wanasema ooh, unajua kuna watu wana malori, kwa hiyo, hawataki reli. Kwa hiyo, nataka kuwaambia wenye malori, kama kweli hiyo reli ndiyo tatizo lao, waanze kuuza malori, maana sisi tunataka ile reli *seriously,* wala hatuna *compromise* katika hili. *(Makofi)*

Kama wewe una lori zako 40 na unafikiri reli hii itapunguza biashara, uza 20, uuze Kenya kule, lakini hatuwezi kuzuia ujenzi wa reli kwa sababu eti kuna watu wana malori, aah! Sisi wote kule tufe kwa sababu watu wa malori wanapata faida! Hicho kifo hatukubali. Kwa hiyo, tunaunga mkono suala hili, tumeweka Shilingi bilioni 134, tunajua siyo nyingi, lakini tumeweka zile kwa sababu inaweza kuifanya ile reli na treni ianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesema humu, kuna mabehewa, tunanunua mengine tunayakarabati, kuna vichwa cha treni tuna-*rehabilitate,* reli tunataka ifike Kigoma, Mwanza, Mpanda na nataka kumwomba Mheshimiwa Mwakyembe, siku reli itakapofika katika maeneo hayo, anialike twende tukasherekee. Kwa sababu huu ni ufumbuzi mkubwa kwa maisha ya watu wetu. Katika mambo ambayo ni *serious* hakuna utani, ni katika hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, alisema Serikali iimarishe miundombinu hiyo ya reli na yeye ndiyo Mwenyekiti wetu. Kwa hiyo, tunakubaliana naye na reli zijengwe ili kupunguza fedha nyingi zinazotumika kukarabati barabara na hiyo nayo ni hoja nzuri tu kwa sababu huwezi kutumia shaba, unasafirisha shaba kwa barabara. Shaba inasafirishwa kwa reli. Ukiisafirisha kwa barabara, barabara inakufa tu, maana uzito ule unaua ile barabara.

Kwa hiyo, ndiyo maana tunaitilia mkazo, tena katika bajeti hii tumeweka siyo reli hiyo ya kati tu, au ya *TAZARA,* tunataka reli zaidi na tumesema tutafanya

*feasibility study* kwa ajili ya reli ya kubeba chuma cha kutoka Mchuchuma kupitia kwenda Mtwara. Tumesema katika bajeti hii tutatengeneza *feasibility study* ya kufanya biashara na Uganda kwa kutengeneza reli inayotoka Tanga kwenda Arusha na kwenda Musoma. Tumeweka haya mambo maana reli ni muhimu sana kwa maendeleo kwa sababu ndiyo inayochukua mizigo mizito. Mengine haya, nguo na nini, lori zitaendelea kubeba tu, lakini mamizigo mazito yabebwe na treni.

Mheshimiwa Kafulila, yeye alikuwa anahoji tu kwamba, bajeti ya Uchukuzi ni ndogo. Tunaona ni mwaka mmoja, mwaka wa pili tutaiongeza mpaka tuwe na mfumo wa reli ya bandari na reli ya uhakika kuelekea kule ili iweze kufanya *trade* na kuhudumia watu wetu. Serikali ina sera gani ya kuendesha biashara? Nimeshasema kwamba tutatengeneza kwanza na gesi yenyewe tumegundua juzi halafu hatujaanza kuchimba, halafu huanzi leo, kwa hiyo, tuna muda wa kutosha kutengeneza sera, tuna muda wa kutosha kupitisha sheria ambayo itatu-*guide* katika makubaliano yetu na wanaochimba na sisi wenye gesi.

Sasa mimi naomba Wabunge tusije tukaja tena tukapitisha halafu tena tukaja kulaumu kusema hii sheria gani? Huku na wewe ulikuwa umekaa unapitisha. Tuangalie sasa tusirudi tena kwenye malumbano yasiyokuwa na msingi, halafu tutakuwa tunarithisha malumbano tu. *(Makofi)*

Mradi wa Ngaka hauonekani kabisa katika Mpango wa Maendeleo. Naomba Mheshimiwa

Gaudence Cassian Kayombo azungumze na Waziri wa Nishati na Madini, ili yale makaa ya mawe ya Ngaka maana anachosema yeye ni kwamba wanaweza kutengeneza umeme wa makaa ya mawe kule. Lakini hakuna mahali ambapo kuna *grid* ya Taifa karibu ambako wanaweza kuunganisha. Sasa *grid* tunayotoa Makambako kwenda Songea, ni ya 133Kv. Kwa hiyo, huwezi kuunganisha Makambako. Mahali unapoweza kuunganisha au ni Iringa ama Mbeya.

Sasa jambo hili liko *beyond my scope*, naomba aje azungumze na Waziri wa Nishati na Madini wafanye *calculation* waone tukitumia makaa ya mawe na Waziri wa Nishati na Madini anasema Makaa ya Mawe ndiyo *solution*, kama ni kweli, basi tutafute namna tunayoweza ku-*utilize* makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Leticia Nyerere alisema, tunasema ukame kisingizio, aah! Mheshimiwa Leticia tunaheshimiana sana. Ukame wewe huoni Kwimba pale pakame kweli kweli, hata Mheshimiwa Leticia anaishi katika maeneo makame kweli kweli. Kwa hiyo, ukitokea ukame, wala huna siri, maana huwezi kuficha ukame. Halafu kuna mmoja alisema kwamba tumesema kuna ukame, halafu tukasema mvua.

Ni kweli, nchi hii ni kubwa, kunaweza kuwa na ukame Mwanza, kukawa na ukame Kilimanjaro lakini kukawa na mtawanyiko wa mvua Kusini Nyanda za Juu. *Actually* hata miaka mibaya sana nyanda za juu zinazalisha chakula cha kutosha kabisa isipokuwa inapoingia kwenye soko huria, ndiyo kinapungua. Lakini

miaka miwili mfululizo tumezalisha tani milioni 12 na sehemu kubwa inatoka Nyanda za Juu Kusini, Kigoma pamoja na Morogoro. Kweli yote mawili, huwezi kukataa ukweli, tabia ya nchi hiyo mbaya kweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia teknolojia ya matone, ni wazo nzuri kwa maana ya kukubali kwamba lipo tatizo.

Serikali inatakiwa kuelekeza umeme katika maeneo ya vijijini, naunga mkono katika hili kwa sababu vijijini kule lazima tuwapatie umeme, tena tukiweza kufikisha umeme katika kila Shule ya Sekondari, Tanzania itabadilika sana kwa sababu pale kwenye Kata patakuwa ni *focal point* ya *development* ya nchi yetu. Tukiweka umeme katika kila Shule ya Sekondari, *whether* unaweka wa *solar* au wa kitu gani, lakini ukiuweka pale utakuwa kwa kweli Tanzania itabadilika. Maana tukiweka kila Wilaya, Wilaya zimeongezeka, nadhani watakuwa na mpango wa kupeleka. Lakini tukienda kwenye *level* ya Kata, na kila Kata ikawa na *focal point* mahali ambapo umeme umefika, mimi naamini Tanzania itabadilika kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, naunga mkono hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mlaki, anasema tuongeze mkazo katika kuuza nje, nimeshalijibu hilo na nakubaliana na Mheshimiwa Mganga Ndassa. Fedha zilizotengwa juu ya kuimarisha viwanda nchini zielekezwe katika ujenzi wa viwanda vitatu vikubwa, viwanda vya pamba, korosho na kahawa, hili tunakubaliana naye kabisa kwamba lazima sasa tuanze kuwekeza kwenye pamba kwenye korosho ili tuache huu utaratibu wa kuuza

malighafi kutoka nje, tuanze kufungua hatua kwa hatua. Haya mambo yalisemwa na Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Celicia Paresso na Mheshimiwa Anastazia Wambura, wote walisema maneno haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Msolla na wengine, walizungumzia kiwanda cha Mbolea. Vilevile na chenyewe kitakuwa katika mpango na suala la rasilimali watu limezungumzwa vizuri na mimi nimelijibu.

Mheshimiwa Spika, sasa nina mambo mawili madogo ambayo ningependa kumalizana nayo.

Moja, wako watu wanatudai katika *EPZ,* wanaidai Serikali katika maeneo mengi, wako Songea, Bagamoyo, Kigoma na mahali pengine na Bunda katika Kijiji cha Tairo. Nataka niwaambie kwamba jitihada zinafanyika na fedha mwaka huu unaokwisha, zimepatikana na mamlaka ya *EPZ* itaanza kulipwa na madai yale ya kusema wajaribu kutazama, maana wengine wamefanyiwa tathimini mwaka 2007; nataka wajue kwamba tunajua hilo na wajue wanawakilishwa vizuri sana katika jambo hili na haki zao zitalindwa. *(Makofi)*

La mwisho, nataka kueleza hali ya pamba ilivyo na msimu, watu wa pamba wale wangeshangaa, ningemaliza bila kusema pamba, maana mimi ndiyo wananiweka mjini wale watu wa pamba. *(Makofi)*

Mimi naelewa liko tatizo ambalo limechelewesha msimu. Naomba wawe wavumilivu, lakini nataka kuwaomba wanunuzi wa pamba na ninaomba wakulima wa pamba wanisikilize vizuri kwamba wanunuzi wa pamba wasipeleke *burden* ya kila kitu kwa mkulima inapotokea *crisis*. *(Makofi)*

Lazima tugawane *burden*, kama *profit ni ten percent*, lazima na wewe angalau upate *nine* au *eight*, kama *cost of transportation* kama unaweza ku-*manouver* au cost ya *marketing* unaweza ukapunguza, na hicho unachokipunguza unakipeleka kwa mkulima kwa sababu tusipofanya hivyo, sasa mkulima huyu kila shida inapotokea kwenye *World Market* yeye ndio anabeba. Sasa yeye huyu *shock absorber* zake ziko wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaambia sasa hapa, maana hakuna mipango kama watu hawalimi, na vilevile hakuna Uwaziri wa Wasira kama hakuna pamba. Kwa hiyo, nataka wakulima wa pamba wajue mimi najua wana matatizo na mimi niko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru tena kwa kunipa fursa na nataka kutuma nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono Mpango, kwa sababu kutouunga mkono ni kwamba nchi haipo sasa. Maana kama huungi mkono bajeti, sasa unafanyaje? Hata nauli ya kukurudisha kwako haipo. Maana ni hela zitakuwa zimekosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeangalia kwamba sasa hivi tuahirishe shughuli za Bunge hapa kusudi mchana tutakapoingia saa 11.00 wataanza kujadili Manaibu Waziri na kwa sababu Naibu Waziri Mmoja ana afya kidogo iliyotetereka, kwa hiyo Naibu mwingine atapata muda wa dakika 30 halafu Waziri mwenyewe nitampa saa moja. Halafu tutaanza kwenye saa 12.30 jioni au saa 12.45 jioni, kupiga kura kukubali bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo ni wito wangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wote popote waliko wafike kwa sababu ni wajibu wetu kupitisha bajeti kwa mtindo huu. Kwa hiyo, usije ukadhani watapiga kura wenyewe hapana. Huko mliko kama mko majumbani mje, hata wale wanaojisikia afya siyo nzuri sana, wafike hivyo hivyo. Wakae kwa muda wa kupiga kura, halafu waondoke. Kwa hiyo, nategemea jioni *the house will be full*.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine. Waheshimiwa Wabunge naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.27 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikali Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge mchana nilisema kwamba tutaanza na Naibu Waziri wa Fedha na tulisema kwamba atatumia dakika 30 kisha baada ya hapo Waziri wa Fedha mwenyewe mtoa hoja pamoja na kwamba atakuwa na majina atakayoyataja lakini muda wake ni saa moja.

Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa. Napenda kuunga mkono hoja iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii vilevile kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuendesha majadiliano ya bajeti kwa umakini wa hali ya juu. Nawashukuru pia Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa na pia Wenyeviti akiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, nina fahari kubwa mbele yenu kujibu hoja zilizowasilishwa na baadhi ya Wabunge na hoja nyingine zitakamilishwa na Mheshimiwa Waziri. Mimi nimekuwa mmoja wa wataalamu walioshiriki moja kwa moja katika kuandaa bajeti hii, kwa hiyo, nina uhakika bajeti hii imezingatia matakwa yote ya wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kwanza kuanza kujibu hoja ya kwanza iliyowasilishwa ambayo ilikuwa inahusiana na kilimo. Mtoa hoja alielezea kwamba kilimo kimetengewa fedha kidogo sana wakati sekta hii inaajiri zaidi ya watu 80%. Alisema kwamba bajeti ya kilimo iongezewe ifikie walau 10% ya bajeti ya Serikali. Sekta ya kilimo, ni moja ya sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu hasa ukizingatia kuwa inaajiri wananchi walio wengi. Sekta hii inajumuisha shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi, ardhi pamoja na misitu. Baadhi ya taasisi ama maeneo yanayohusika katika sekta ya kilimo ni kama Wizara ya Kilimo yenyewe, Wizara ya Chakula na Ushirika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tume ya Ushirika, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo huratibu miradi kama ya *MSDP* pamoja na *MIVAF*, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inahusiana na barabaraba za vijijini ambayo moja kwa moja ina-*link* na kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara pia ambayo inashughulika na uratibu wa masoko ya mazao ambayo wakulima wanazalisha. Kuna taasisi za mafunzo na utafiti kama *SUA* na *MUKOT* ambazo zenyewe zimewekewa fedha, kuna Wizara ya Maliasili ambayo yenyewe ina Idara ya Huduma za Misitu na Nyuki yaani ni *part* ya kilimo, Sekretari za

Mikoa ambazo zinatoa huduma za kiuchumi, vilevile Halmashauri ambapo ndani yake kuna Idara ya Mifugo, Kilimo, Ushirika na Uvuvi. Vilevile kuna Benki ya Kilimo na ile ya Rasilimali Tanzania, zote zinajishughulisha kwa ajili ya kuimarisha kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo basi, bajeti ya kilimo yenyewe imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kwa lengo la kuiboresha ili iweze kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi na hivyo kusaidia juhudi za Serikali katika kupunguza umaskini wa kipato na chakula. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1103.6 sawa na 9% ya bajeti yote ikilinganishwa na shilingi milioni 926.2 ambazo zilitengwa kwa mwaka 2011/2012 sawa na 8% ya bajeti katika sekta hiyo. Nia ya Serikali yetu ni kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya kilimo ili kufikia lengo la 10% ya bajeti nzima kama ambavyo tumekubaliana katika nchi za *SADC*. Kwa hiyo, mtaona ni jinsi gani Serikali inavyojitahidi katika kuongeza bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iondoe kodi kwenye mbegu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haitozi kodi kwenye mbegu. Sheria ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inatoa msamaha kwa ushuru wa Forodha kwa mbegu za aina zote. Kwa upande wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT* mbegu zimeorodheshwa kwenye Jedwali la Pili la sheria hiyo na hivyo kusamehewa kodi. Naomba

kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba mbegu hazitozwi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja inayosema kwamba Serikali inachukua hatua gani kupunguza kodi ya mapato yaani *PAYE* kwa watumishi kutoka 14% na kuwa 9%. Mfumo wa kodi ya ajira yaani *PAYE* katika Tanzania unazingatia misingi inayokubalika kimataifa ya utozaji kodi kadri kipato kinavyoongezeka. Mfumo huu una viwango tofauti vya kodi ambavyo hupanda kadri ya kipacho cha mfanyakazi kinavyopanda yaani kunakuwa na *progressive tax.* Serikali imekuwa ikirekebisha viwango vya kodi ya *PAYE* hatua kwa hatua kwa lengo la kutoa unafuu wa kodi kwa mfanyakazi hasa wa kipato cha chini kulingana na hali halisi ya uchumi na uwezo wake wa kulipa. Kwa mfano, katika mwaka 2008, Serikali ilipandisha kima cha chini kisichotozwa kodi yaani *personal income tax ratio* kutoka shilingi 80,000/- hadi shilingi 100,000/= kwa mwezi. Ongezeko hili pia lilikwenda sambamba na kushusha kiwango cha chini cha kodi kutoka 18.5% hadi 15%. Aidha, mwaka 2010, Serikali ilipunguza kiwango cha chini cha kutoka 15% hadi 14% na pia kupandisha kima cha chini kisichotozwa kodi kutoka shilingi 100,000/= hadi kufikia shilingi 135,000/= kwa mwezi. Hatua zote hizi zililenga kutoa unafuu wa kodi ya mapato kwa mfanyakazi kwa kada mbalimbali hasa wa kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, kupandisha kiwango cha chini cha kutoza mapato ya ajira, kina lengo la kuwapunguzia mzigo wa kodi watu wa kipato cha chini. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali

imeangalia suala hilo na hivyo kupandisha kiwango cha chini cha mapato ya ajira kutoka shilingi 135,000/= hadi shilingi 170,000/= kwa mwezi. Hatua hii ina manufaa zaidi kwa watumishi wenye kipato cha chini kwani inatoa unafuu wa kodi kwa 100%. Serikali itaendelea kupitia utaratibu wa kodi ya *PAYE* mara kwa mara ili kutoa unafuu kwa watu wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu wavuvi wanaotumia vyombo vya mbao wapunguziwe kodi kwenye nyavu, injini za bodi, *life jackets,* taa na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, vifaa vya uvuvi, nyavu, injini za boti na vyombo vingine vinavyofanana na hivi, vilishaondolewa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kodi ya vifaa hivi tayari ilishaondolewa. Vifaa hivi viliondolewa kodi ili kutoa unafuu kwa wavuvi na kuiendeleza sekta hii ya uvuvi. Vifaa vingine kama taa havitumiki kwa shughuli za uvuvi pekee, hivyo kuviondolea kodi kunaweza kupunguza mapato kwa sababu matumizi ya taa yako nje ya sekta ya uvuvi. Matumizi ya taa yenyewe yanatumika mbali ya sekta ya uvuvi, kwa hiyo, vifaa vingine ambavyo vinatumika kwa uvuvi tayari vimeshaondolewa kodi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linafanana na hilo kama Wajumbe walivyolielezea, ilikuwa ni kuondolewa kodi kwa vifaa vya umwagiliaji maji. Vifaa vya umwagiliaji maji ni miongoni mwa maeneo ambayo hayatozwi kodi. Sheria ya Forodha pamoja na ile ya Ongezeko la Thamani, zinatoa

msamaha wa kodi kwenye vifaa vya umwagiliaji maji. Hata hivyo, napendekeza wadau watuletee orodha ya vifaa na vipuri ambavyo havijaingizwa kwenye msamaha huu ili sisi Serikali tuangalie namna ya kuvisamehe kodi hiyo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba vipuri na vifaa hivi vinaweza kuwa na matumizi mbadala na hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali iwapo tutatoa msamaha wa ujumla moja kwa moja. Kwa hiyo, tunawaomba wadau washirikiane nasi katika kupata orodha hii ya vipuri ambavyo tutaviangalia na kuvisamehe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na wafanyabiashara ya Bodaboda, Mkoa wa Tabora. Ilielezwa kwamba wanatozwa kiwango kikubwa cha kodi cha shilingi 291,000/= badala ya shilingi 95,000/= ambayo ipo kwenye sheria. Kwanza, naomba nieleze kwamba misingi ya utozwaji wa kodi kwa wafanyabiashara wote imeainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na.332. Sheria hii haimbagui mtu, kundi au Mkoa anaotoka.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya ukadiriaji wa kodi, viwango vya kodi vimewekwa katika tabaka nne yaani *bands* ambazo hutumika katika ukadiriaji wa mapato hayo. Kodi hii haitozwi kwa kuangalia makundi ya watu au biashara bali hutozwa kutokana na pato la mtu analolipata kwa mwaka. Kwa hiyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichopita, kodi ya shilingi 291,000/= ilikuwa inatozwa kwa wafanyabishara wenye mauzo ya shilingi milioni saba na yasiyozidi shilingi milioni 14, wakati kodi ya shilingi 95,000/= ilikuwa inatozwa kwa wafanyabiashara wenye mauzo yasiyozidi shilingi

milioni tatu na yasiyozidi shilingi milioni saba. Kwa hiyo, suala la utozwaji kodi kwa wafanyabiashara wa vyombo vya usafiri katika Mkoa wa Tabora limekuwepo kwa muda mrefu lakini kwa sasa naomba kutoa taarifa kwamba limepatiwa ufumbuzi baada ya vikao kufanyika baina ya wawakilishi wa wafanyabiashara, *TRA* na uongozi wa Mkoa ambapo ilikubalika kwamba wenye pikipiki walipe shilingi 95,000/= na wamiliki wa magari madogo ya kubebea abiria yaani *tax* na daladala walipe shilingi 191,000/=, baada ya kukokotoa mauzo yanayopatikana kutokana na biashara hizo. Hata hivyo, kama tatizo hilo bado linaendelea basi Wizara inaahidi kuchukua hatua yaani tunatoa ahadi kwamba tutachukua hatua zifaazo kwa wafanyakazi wa *TRA* ambao wanaliendeleza tatizo hili katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja nyingine kuhusu ushuru wa hoteli yaani *hotel levy* ipunguzwe kutoka 20% hadi 18% au 16%. Serikali inakamilisha zoezi la kuhuisha Sheria ya Ushuru wa Hoteli ambayo ilifutwa na Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 iliyoanza kutumika mwezi Julai, 2009. Katika uhuishaji huo, Serikali itazingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kuweka kiwango cha ushuru kitakachoonekana kinafaa, tutaweka kiwango cha ushuru ambacho tutakiona kinafaa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, aidha, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyandarua vinavyotumika katika kilimo yaani *agro-net,* ilishauriwa iondolewe. Ukweli ni kuwa vyandarua vilivyotajwa vina matumizi mbalimbali ikiwa

ni pamoja na kujengea vibanda vya kuogeshea magari, kukinga jua pamoja na mvua. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa vyandarua hivi kwa wakulima wa maua na mbogamboga, pendekezo la Waheshimiwa Wabunge limepokelewa na tunaahidi kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ambapo Wabunge walitaka Serikali iwachukulie hatua watendaji wanaofanya makadirio ya kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara ili kukwepa kodi. Lengo la Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi kwa uadilifu. Kwa hiyo, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, mamlaka yenyewe ina sera ya uadilifu yaani *integrity policy* kwa ajili ya kudhibiti vitendo vya maafisa wachache wasio waadilifu ambao wanahatarisha mapato ya Serikali. Hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa mara kwa mara kwa vitendo vya aina hii pindi vinapobainika. Aidha, Waheshimiwa na wananchi wote tunawaomba kutoa taarifa mara vitendo vya namna hiyo vinapojitokeza ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine iliyohusiana na kutunga sheria ili kuhakikisha kwamba riba kwenye mikopo kutoka makampuni yanayohusiana haitaondolewa kwenye kutoza kodi. Kifungu cha 33 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na.332, kinazuia kupunguza riba ya ziada kutoka kwenye faida inayotozwa kodi endapo riba hiyo inalipwa kwa kampuni zinazohusiana kwa karibu. Riba ya ziada ni kiasi kinachozidi riba ambayo ingelipwa

kama mkopo ungetolewa na kampuni isiyo na uhusiano wa karibu. Aidha, kanuni za kudhibiti mbinu za kudhibiti kodi yaani *transfer pricing rules* kwenye makampuni yenye uhusiano ikiwemo riba zinazolipwa kwa kampuni yenye uhusiano huo zinaandaliwa na zipo kwenye hatua za mwisho. Tunapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba hizo *rules* zinaandaliwa na zipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kwamba Serikali ipunguze idadi ya *accounts* kwenye Halmashauri ili kupunguza mwanya wa upotevu wa fedha za taifa pamoja na mapato. Hili liliongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana lakini naomba kuwakumbusha kwamba tumelieleza hili katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2012/2013, aya ya 38 kwamba Serikali inaendelea na zoezi la kupunguza *accounts* za Halmashauri ili kudhibiti mapato na matumizi mabaya ya fedha za umma. Lengo la zoezi hili ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji, kuwezesha usuluhishi na utoaji wa taarifa za matumizi kwa wakati. Mwaka huu wa fedha Serikali imefungua *accounts* sita mpya katika kila Halmashauri. Aidha, zoezi hili litaziwezesha Halmashauri kutumia mfumo wa usimamizi wa malipo ya Serikali yaani *Intergrated Financial Management System.* Hivi sasa ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inaendelea kufanya usuluhishi wa *accounts* za zamani na mara utakapokamilika *accounts* zote za zamani zitafungwa na kuanza kutumia *accounts* hizi sita ambazo tayari tumekwishazifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine kuhusiana na vigezo vya mgawanyo wa mapato kwa mujibu wa Katiba viwekwe wazi, vigezo hivyo ni baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar viwekwe wazi kwa mujibu wa Katiba. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Kwa upande wa Serikali ya Muungano, suala hili limejadiliwa hadi ngazi ya Baraza la Mawaziri ambapo maelekezo yaliyotolewa yalihitaji kufanyiwa kazi zaidi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba maelekezo hayo ya Baraza la Mawaziri yameshafanyiwa kazi na yamerejeshwa upya katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi yake. Ama kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari maamuzi ya Baraza la Mapinduzi yameshatolewa. Kwa hiyo, lengo la mchakato huu ni kwamba Serikali mbili za SMZ na SMT ziwe zimeafikiana kuhusu mapendekezo ya Tume katika kipindi kifupi kijacho. Kwa hiyo, naomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato unaendelea na tutafikia malengo kama vile tunavyotarajia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na utekelezaji wa Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuchelewa kuanza. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kutekeleza Sera ya *PPP* yaani *Public Private Partinership,* Serikali imeanza na maandalizi muhimu yaliyopaswa kufanyika kwanza. Maandalizi hayo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Ubia ya mwaka

2010, kutoa Kanuni za Sheria ya Ubia ya mwaka 2011 na vilevile kutungwa kwa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kuanzishwa kwa vitengo vya *PPP* pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi. Aidha, hivi sasa maandalizi hayo yamekamilika na tayari Serikali imepokea mapendekezo ya miradi inayoweza kufikiriwa kwa ajili ya utekelezaji wa ubia. Sote tumemsikia Waziri Magufuli asubuhi alisema kwamba kwa mfano *linkage* ya *PPP* itaonekana katika ujenzi wa barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Ubia kwa kuwa maandalizi yamekamilika na fedha zimetengwa kwa ajili ya vitengo vipya vya *PPP* na miradi husika basi itaanza kuchambuliwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, muda wa kumpata mbia unaoidhinishwa na Sheria ya *PPP* ni mrefu kiasi cha kukatisha tamaa wawekezaji. Naomba kutoa ufafanuzi kwamba, sheria inasema kuwa muda wa mradi ambao uko katika hatua za kuidhinishwa haupaswi kuchukua zaidi ya siku 90. Aidha, Serikali itaendelea kuangalia muda wa kuidhinisha miradi ya ubia kwa kutumia mifano ya nchi nyingine zinazotekeleza miradi ya ubia katika ngazi za kikanda na kimataifa. Vilevile lengo la Serikali ni kuingia kwenye ubia wenye manufaa kwa taifa, hivyo, juhudi za kupunguza muda wa kumpata mbia zitazingatia lengo hilo.

**SPIKA:** Kuna mazungumzo mengi mno kati yetu. Waheshimiwa tuko ndani ya Bunge siyo nje. Mheshimwa Naibu Waziri endelea!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba, je, bajeti hii imejipanga vipi kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya mwaka 2015? Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya mwaka 2015 yanajielekeza katika kupunguza umaskini kwa kuweka mkazo katika huduma za afya, elimu, maji na masuala mtambuka yakiwemo jinsia, ukimwi, malaria pamoja na mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, bajeti yetu imezingatia azma ya kufikia Maendeleo ya Milenia kwa kutenga rasilimali fedha katika maendeleo husika. Mfano, mgawanyo wa fedha katika sekta ya elimu umeongezeka kufikia asilimia 23 ya bajeti ya mwaka 2012/2013, ukiondoa na deni la taifa kutoka asilimia 20 ya mwaka 2011/2012, wakati ambapo sekta za afya na maji zimetengewa asilimia 15 mwaka 2012 na 2013 kwa mtiririko huohuo. Aidha, hotuba ya hali ya uchumi, aya ya 46 na 47 imebainisha mafanikio yaliyofikiwa; Mawaziri wa sekta husika wataeleza kwa kina juu ya hatua zilizofikiwa na mikakati ya kufikia malengo hayo ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, moja kati ya Malengo ya Milenia ni kuwawezesha wanawake, kuweka usawa wa jinsia baina ya wanawake na wanaume katika ngazi zote. Kwa hivyo, nimefarijika sana kuona kwamba, hata

katika ngazi ya Bunge pia tunatekeleza Malengo ya Milenia. Nimeona jinsi wanawake tulivyo humu ndani na ninakwambia *we are the strongest gender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimependezewa sana na jinsi unavyoliendesha Bunge lako. Nawaomba Wabunge tupitishe bajeti hii. Bajeti hii inajali kumwezesha mwanamke. Mimi niko hapa ni mwanamke na hakuna mtu ambaye alijua kama nitakuwa hapa leo hii. Niko hapa na ninawaahidi Watanzania na Bunge lako Tukufu, nitafanya kazi zangu kwa uadilifu. Nawaomba Wabunge tupitishe bajeti hii ili kuendelea kutekeleza Malengo ya Milenia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine iliyosema Serikali ilipe malimbikizo ya madeni ya Walimu kwa wakati. Serikali imeendelea kulipa kwa wakati malimbikizo halali ya Walimu. Mwezi Januari, 2012 jumla ya shilingi bilioni 22.5 zilitolewa kwenda kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa ajili ya kulipia madai ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ambayo yamehakikiwa. Utekelezaji wa malipo ya Walimu husika utatolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa pamoja na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine iliyohoji sababu za Wakala na Mamlaka za Serikali kutochangia asilimia 10 ya mapato yao kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha unaoishia mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali ilizitaka Wakala na Mamlaka za Udhibiti kuchangia asilimia 10 ya mapato yao katika

Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika kutekeleza uamuzi huo, Wakala na Mamlaka zilichangia jumla ya shilingi bilioni 16.5 ambazo mchanganuo wake ni kama ifuatavyo; *TPA* (bilioni 5.5), *TCRA* (bilioni 6.5), *TANAPA* (milioni 400), *SUMATRA* (bilioni 1.2), *EWURA* (milioni 652), *TCAA* (milioni 800), *NCAA* (milioni 500), *Gaming Board* (milioni 382), *TIRA* (milioni 284), *STAMICO* (milioni 20), *NHC* na *Sugar Board* bado hazijachangia. Serikali inaendelea kuhuisha Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuipa nguvu za kisheria zaidi katika kusimamia Wakala na Mashirika ya Umma na kuongeza makusanyo katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihoji ni kwa nini Serikali inaruhusu uagizaji wa vilainishi (*lubricants*) kutoka nje wakati kuna viwanda vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo hapa nchini. Hivi sasa suala la kulinda bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa kutoka nje linawezekana tu pale ambapo uwezo wa uzalishaji wa ndani unakidhi mahitaji ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, uzalishaji wa vilainishi haukidhi mahitaji ya soko la ndani. Hata hivyo, kulingana na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, vilainishi vinavyoagizwa kutoka nje hutozwa ushuru wa forodha kwa asilimia 25. Hiki ni kiwango cha juu cha ushuru wa forodha ambacho kimewekwa kwa bidhaa timilifu (*maximum tariff*). Aidha, viwanda vya ndani tunavihimiza kuzalisha bidhaa zenye ubora na kwa wingi ili viweze kukidhi mahitaji na kushindana. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutaweka vizuri mazingira kwa ajili ya viwanda vya ndani ili viwezeshwe kuzalisha zaidi na kukidhi soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Maji ili kukidhi matarajio ya wananchi. Sekta ya maji ni moja ya sekta muhimu sana ambazo zinatoa huduma kwa jamii na pia kutumika kwenye shughuli zingine za maendeleo kama vile umwagiliaji. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Maji kutoka shilingi bilioni 446.1 mwaka 2011/2012 hadi kufikia shilingi bilioni 485.9 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia tisa (9%). Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 465.8 ni fedha za maendeleo. Kwa msingi huo, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mikoa na Halmashauri zimetengewa fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Vilevile, sekta binafsi tunazihimiza nazo kushiriki katika kuigharamia miradi ya maji kwa sababu kama ilivyoelezwa hapa labda Wabunge wengi walifikiria kuna njia moja tu ya kuweza kupata *financing* lakini tukiimarisha sekta binafsi, tukihuisha *Public Private Partnership* jamani sekta binafsi nayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine kuhusu kuchelewa kwa mafao ya kustaafu kwa zaidi ya miezi sita (6). Mafao kwa watumishi wanaostaafu hulipwa katika makundi mawili; kundi la kwanza ni wale wanaolipwa kupitia mifuko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono bajeti hii ya mwaka 2012/2013 na ninawaomba wote muiunge mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa maelezo. Waheshimiwa Wabunge wamevutiwa sana na namna ulivyoweza kujibu hoja zao kwa kujiamini na kwa uhodari mkubwa sana. Tunakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Sasa nitamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha lakini naomba utulivu maana kuna vikao vingi vinaendelea humu ndani, hata Mwenyekiti wake haonekani. Tunaomba utulivu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**SPIKA:** *Microphone*!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba uniruhusu niseme maneno machache ya utangulizi. Katika kipindi hiki cha wiki mbili, katika kuwasilisha bajeti ya taifa letu, nimegundua mambo manne(4) makubwa; la kwanza Wabunge mmeonesha nia kubwa na mnanipenda pamoja na wasaidizi wangu wawili. Nina imani kubwa na nyie. *(Makofi)*

Jambo la pili nimegundua kwamba, mna dhati kabisa ya kunipa ushauri. *(Makofi)*

Jambo la pili ...

**WABUNGE FULANI:** La tatu!

**WAZIRI WA FEDHA:** Jambo la tatu mmeonesha moyo wa upendo wa kusaidia na kuona kwamba bajeti hii ni ile ambayo itasaidia nchi yetu kusonga mbele. *(Makofi)*

Jambo la nne, nimegundua kwamba Wabunge mko makini, mnapenda viongozi wa Wizara tuwe makini, waaminifu na watu tunaowajibika. Ndiyo maana ushauri wenu wa dhati kabisa umeonesha kwamba umakini utanisaidia mimi na wasaidizi wangu, Naibu Mawaziri kuwajibika, kuongeza uaminifu na kuona kwamba Wizara inafanya kazi tuliyotumwa na taifa. Baada ya kusema hayo naomba niwaahidi uaminifu, uwajibikaji na kujituma katika kazi ambayo Mheshimiwa Rais amenipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa hoja, maswali, madodoso na ushauri wenu wote mlionipa mimi pamoja na wasaidizi wangu wawili. Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe *documment* yangu. Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Naibu Spika,

Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa na pia Wenyeviti wa Bunge: Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Sylivester Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kwa jinsi mlivyoongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja ya Serikali niliyoiwasilisha tarehe 14 mwezi wa Sita, 2012 kuhusu mapendekezo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka huu wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mtemi Andrew J. Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati yake kwa ufasaha. Aidha, nawashukuru Waziri na Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Mheshimiwa Christina L. Mugwai, Mbunge wa Viti Maalum kwa maoni na ushauri wao juu ya bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kadhalika napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mbunge wa Bunda kwa kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali zinazohusu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013. Vilevile, nachukua nafasi hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, kwa umahiri wa kazi yao na kwa nguvu na upendo katika kunisaidia kufanya kazi hii na vilevile kwa namna walivyochangia na kutoa ufafanuzi

katika baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mmeziwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na waliotoa maoni yao kwa maandishi. Nawashukuru wote kwa pamoja kwa maoni na ushauri wenu na yote tumeyachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi wakati wa utekelezaji wa bajeti hii ya mwaka 2012/2013 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2013/2014. Naomba muendelee kutupatia mapendekezo wakati wowote ule ili kuongeza tija na ufanisi katika kutekeleza shughuli mbalimbali zilizotengwa kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge 108 waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mtemi Andrew J. Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Christina L. Mugwai, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Sarah M. Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu, Mheshimiwa Omar R. Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki na Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Esther A. Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa David E. Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwigulu L. Mchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mbunge Solwa, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mbunge wa Chakechake, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini na Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde, Mbunge wa Mtera, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, Mbunge wa Dole, Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Dkt. Augustino L. Mrema, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Chiku A. Abwao, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola,

Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge Viti wa Maalum, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo, Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Dkt. Henry D. Shekifu, Mbunge wa Lushoto, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, Mheshimiwa Vita R. Mfaume Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mbunge wa Nkansi Kusini, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mbunge wa

Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Cecilia D. Parreso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Sylvester F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Salim Hassan Abdallah Turky, Mbunge wa Mpendae, Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Nimrod, Elirehema Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Aliko

Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje na Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Janet Zebadayo Mbene, Mbunge wa Kuteuliwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Kuteuliwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mbunge wa Kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 148 wamechangia kwa maandishi kama hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mhesimiwa Victor Kilasile

Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Hassan Athumani Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Mhandisi Gerson Hosea Lwenge, Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashairiki, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallack, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine ni Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mbunge wa Chumbuni, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge

wa Ngara, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Antony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Phillipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge wa Kikwajuni, Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa

Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani, Mheshimiwa Vick Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Slyvester Mhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki na Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Capt. John Zefania Chilligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa Juma Athumani Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje,

Mheshimiwa Waride Bakar Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Ritha Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga**,** Mbunge wa Misungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Dkt. Kwebe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Profesa Peter Mahmoud Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa

Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mbunge wa Amani na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Segerea, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Asha Mchimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, Mheshimiwa Kheri Ali Khamis, Mbunge wa Kwamtipura, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla, Mbunge wa Rahaleo, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini na Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mbunge wa Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Said Suleiman, Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda**,** Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Rajab Abdul Mteketa, Mbunge wa Kilombero na Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua wote waliochangia katika bajeti hii, naomba sasa niseme yafuatayo. Kwa namna ya pekee, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwa asilimia mia moja. Kuunga mkono huku ni ushahidi tosha kwamba bajeti niliyowasilisha imezingatia kutekeleza masuala muhimu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuunga mkono bajeti hii kutokana na sababu nzuri walizokuwa nazo na napenda niwahakikishie kuwa maoni na ushauri wao tumeupokea na tutaufanyia kazi kwa kadri itakavyowezekana. Naamini kuwa Waheshimiwa Wabunge wote mtaikubali bajeti hii na tutashirikiana kwa karibu katika kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo ya baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nirejee kusisitiza maeneo muhimu katika hotuba yangu ya bajeti. Lengo la kufanya hivyo ni kutimiza azma ya Serikali ya kupambana na changamoto za kiuchumi na kijamii ambazo Watanzania wanakabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo ni pamoja na ongezeko la bei za mafuta ya petroli, upungufu wa nishati ya umeme, upungufu wa chakula na upungufu wa ajira hususan kwa vijana wetu. Kamati ya Fedha na Uchumi kupitia kwa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge imeleta mapendekezo muhimu ambayo Serikali imeyazingatia.

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Hotuba yake ametoa mapendekezo mengi. Napenda kuihakikishia Kambi ya Upinzani kwamba baadhi ya maoni yao mazuri tumeyachukua na tutayafanyia kazi kwa maana ya kuyachambua na kuangalia namna ya kutekeleza mapendekezo yao mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni umuhimu wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi, hasa kupandisha kima cha chini cha mshahara. Napenda kusisitiza kuwa dhamira ya Serikali ni kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na uwezo wa uchumi wa nchi yetu. Katika miaka ya hivi karibuni kima cha chini kimepanda kutoka shilingi 80,000/- mwaka 2008 hadi shilingi 135,000/- mwaka 2010. Sambamba na kupunguza *PAYE* kutoka asilimia 15 mpaka asilimia 14, vilevile mapendekezo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzania ni kupandisha kima cha chini hadi kufikia shilingi 315,000/- kwa mwezi. Utekelezaji wa mapendekezo hayo utahitaji kiasi cha fedha kisichopungua trilioni 6.9. Hivyo itaongeza sana matumizi ya kawaida ya Bajeti. Aidha, hali ya mapato yetu ndani kwa sasa hayawezi kuhimili ongezeko hilo, lakini tunatambua wenzetu wa Kambi ya Upinzani wana dhamira nzuri. Hali tuliyonayo ya uwezo wa kiuchumi bado tunajenga nguvu, tutakapoboresha uchumi huko tutafika mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge wametoa ushauri kuhusu hoja ya kubadilisha mzunguko wa Bajeti ili kulipa Bunge fursa zaidi ya kushiriki katika mchakato

wa Bajeti. Serikali inakubaliana na hoja hii na kwamba mzunguko huu utatazamwa upya na kuanza utekelezaji wake katika mwaka huu unaoanza mwezi ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mzunguko huu wa Bajeti mpya kwa utaratibu mpya tutaanza miezi ya awali tunapoanza mwezi wa pili. Marekebisho hayo yanalenga kukamilisha mwongozo wa mpango wetu wa Bajeti wa mwezi Oktoba kila mwaka na kwamba vikao vya Kamati za kisekta vifanyike mwezi Aprili. Katika kila hatua Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Kamati za Kisekta zitahusishwa katika utaratibu huu. Lengo likiwa ni kuwa na vitabu vya Bajeti mwisho wa mwezi Mei kila mwaka kama Kanuni za Bunge zinavyotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie kwamba Wizara ya Fedha tutajitahidi kuona kwamba inapofika mwanzoni mwa mwezi Mei vitabu viwe vimetayarishwa Waheshimiwa Wabunge wasisumbuke kuchambua Bajeti bila kuwa na vitabu. Kuhusu usimamizi, nidhamu na ufuatiliaji wa Bajeti ya Serikali hatua mbalimbali zitachukuliwa na Serikali ambazo nimezieleza katika Bajeti yangu nilivyokuwa nasoma. Napenda kusisitiza kwamba hatua zifuatazo zitasisitizwa katika eneo hili wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu unaokuja wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaagiza kufanya vikao vya kila robo mwaka hivyo tutahakikisha kufanyika kwa vikao hivyo vya udhibiti wa mapato na matumizi kwa kila Wizara. Hatutaishia katika

Wizara tu tutakwenda katika kila Mikoa, taasisi na Halmashauri kama alivyoagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vikao hivi vinatakiwa viongozwe na Mheshimiwa Waziri kwa upenda wa Wizara na Mkuu wa Mkoa kwa upande wa Mkoa. Kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa vikao vitaongozwa na Mwenyekiti au Meya wa Manispaa au Jiji husika. Taarifa za vikao hivi ziwasilishwe Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Ofisi ya Rais Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha yenyewe. Hii ni kuhakikisha kwamba kuna ufuatiliaji unaojali maagizo ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti zitakazoandaliwa na Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango zitawasilishwa Serikalini na baadaye kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Hii itatuhakikishia kujua kuwa fedha zimepelekwa kwa wakati na zinatumika inavyotakiwa kama ilivyohitajika kwa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali atafanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa Wizara, Mikoa, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Halmashauri kuhakikisha kuwa Sheria za Fedha na Ununuzi wa Umma zinazingatiwa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi na kuwasilisha taarifa zake kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nne, ni matumizi ya IFMS *(Integrated Financial Management System)* itahimizwa kwa ngazi zote zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuepuka matumizi yasiyofuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tano, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaweka mkazo katika kusimamia utekelezaji wa hatua hizi na dhidi ya watakaokiuka taratibu hizi watachukuliwa hatua. Tufike wakati watendaji Serikalini tuwe na uwajibikaji, tuoneshe kwamba tunauaminifu na tunaweza tukaaminiwa ili waliotupa dhamana ya kuongoza waweze kuona kwamba thamani ya pesa walizotukabidhi inaonesha thamani ya matendo yanayostahili fedha tulizokabidhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja kuwa uhamisho wa fedha kwa mafungu mbalimbali ambao umesababisha kupunguza fedha kwa baadhi ya mafungu na hili limejitokeza sana huko nyuma. Katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 utaratibu huu utadhibitiwa kwa kuweka kiwango maalum cha uhamisho kwa mujibu wa Sheria na taratibu. Lengo la utaratibu huu ni kudhibiti uhamisho wa fedha ili kuepuka kuvuruga utekelezaji wa Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa za uhamisho zitawasilishwa kwa mujibu wa Sheria. Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kujadili taarifa za uhamisho wa fedha wakati unaostahili. Vile vile Maafisa Masuhuli wanaelekezwa kutekeleza Bajeti zao kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ya utangulizi, naomba sasa nijadili mapendekezo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge mliyawasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza inahusu kukusanya mapato na kudhibiti matumizi. Hoja hii imejitokeza kutokana na Wabunge wengi kutoridhika na hali ya mwenendo wa makusanyo ya pesa na matumizi ambayo yamepelekea wasiwasi wa matumizi ambayo huenda yamekuwa hayaendani na hali halisi ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu umuhimu wa kulipa kodi. Serikali inatenga matumizi yake kulingana na mapato yanayokusanywa hasa mapato ya ndani na ya nje. Kuna haja basi sasa ya kuongeza juhudi ya kupanua wigo wa kukusanya mapato kama Waheshimiwa Wabunge mlivyoshauri. Hatuwezi kuwa na Bajeti inayokidhi mahitaji ya matumizi ya Serikali na mahitaji yetu ya maendeleo ikiwa vyanzo vya mapato ya Serikali vitaendelea kuwa finyu, ni lazima tutazame kwa upana ili tupanue vyanzo vya mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna haja sasa ya kuongeza juhudi ya kupanua wigo huo wa kukusanya mapato kama nilivyosema. Naelewa kuwa Waheshimiwa Wabunge wana mawazo mazuri sana ya kuongeza vyanzo vipya vya mapato na kupunguza baadhi ya kodi kama walivyoshauri. Katika mwaka huu wa 2012/2013, tutahakikisha kwamba, tunafanya juhudi za ziada na nashirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kupanua wigo wa mapato na kuhamasisha wananchi kulipa kodi stahiki kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kuukumbusha umma kuwa mmoja wetu ajivunie kulipa kodi kwani ni wajibu na ni jambo jema kwa kila aliye raia mwema. Bila kodi hakuna maendeleo. Hivyo iwapo kila mmoja wetu atalipa kodi ipasavyo tutaiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma na ujenzi wa uchumi pamoja na ujenzi wa ujumla wa miundombinu inayotukabili ili nchi iweze kuwa na uwezo wa kuzalisha. Aidha, ulipaji kodi stahiki utaiwezesha nchi hii kujitegemea. Serikali itahakikisha kuwa fedha hizo zinatumika ipasavyo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Fedha na Ununuzi.

Mheshimiwa Spika na Wabunge wote, naomba sasa niseme juu ya hoja kubwa iliyoulizwa na Wabunge wengi kuhusu Deni la Taifa. Serikali imeendelea kutekeleza sera ya mkakati wa Taifa kusimamia madeni kudhibiti ongezeko la Deni la Taifa lisizidi kiwango kinachohimilika. Mwenendo wa uwiano wa deni la Serikali kwa pato la Taifa kutoka mwaka 2000/2001 ilikuwa ni asilimia 65. 2 ikilinganishwa na asilimia 52.1 ya mwaka 2005/2006. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kupungua kwa deni hilo kulitokana na kukua kwa uchumi wetu kwa kipindi husika pamoja na misamaha mbalimbali ya madeni kutoka nchi ya wahisani na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa chini ya utaratibu wa *HIPC* na *MDR*. Aidha, uwiano wa deni la Serikali kwa pato la Taifa uliongezeka hadi kufikia asilimia 49.3 katika mwaka 2011/2012. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa limetokana na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola za Kimarekani kulikoathiri deni la nje ambalo ni asilimia 75.1 ya deni lote.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuongezeka kwa mikopo mipya ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na malimbikizo ya riba kutoka kwa nchi ambazo zinatakiwa kutufutia madeni kwa mujibu wa makubaliano ya *Paris Club*. Lakini bado hazijatufutia madeni pia lilichangia kuongezeka kwa deni letu. Fedha zilitumika katika miradi mikubwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hapa kwa kifupi kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi sana walipenda angalau wapate picha, deni hili ni kubwa, kiufupi fedha hizi ziliwekwa wapi au ziko wapi au ziko katika nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu, niseme kiufupi aina ya miradi ambayo kwa miaka michache iliyopita tumewekeza na deni likawa linakua. Nitaje maeneo machache; upande wa barabara, tumekuwa na barabara ya Mtukula kwenda Kigoma, tumekuwa na barabara kutoka Dar es Salaam kwenda Somanga, tumekuwa na barabara kutoka Shelui kwenda Nzega, tumejenga barabara kutoka Singida-Babati-Minjingu. Huo ni mfano peke yake na tumetumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umeme nitasema miradi michache. Tumekuwa na mradi wa *Songosongo Gas Development* na *Power Generation Project*. Tumekuwa na mradi wa Iringa Shinyanga *transmission line project,* tumekuwa na mradi wa Kihansi *Hydroelectric Power*, tumekuwa na mradi wa megawati 100 wa *Gas Turbine* P*ower plant* wa Dar es

Salaam, tumekuwa na mradi wa megawati pale Nyakato mwanza ambao vilevile ni mradi wa umeme. Kwa upande wa maji katika miradi mikubwa tumekuwa na miradi ya *Rural Water Supply and Sanitation*, tumekuwa na mradi wa Dar es Salaam *Water Supply and Sanitation*. Tumekuwa na mradi wa *Water Sector Development Program.* Hiyo ni miradi mikubwa. Halafu tumekuwa na mradi mkubwa wa kutoka Lake Victoria unakuja Shinyanga na kuelekea Tabora.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumekuwa na upanuzi wa viwanja vyetu vya ndege ambako nako tumetumia hela nyingi. Kwa mfano, Kiwanja cha Songwe *Airport Project*. Tumekuwa na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Upande wa Afya tumekuwa na Muhimbili *Hospital Rehabilitation Project.* Tumekuwa na *MUHAS Medical Centre Construction Project* upande wa mawasiliano tumekuwa na mradi mkubwa wa mkongo wa Taifa. Lakini vilevile tuna miradi Zanzibar, *Zanzibar Water and Sanitation Project*, mradi wa *Zanzibar Roads Upgrading Project,* tumekuwa na *Zanzibar Basic Education Improvements Project* na tumekuwa na mradi wa Mkongo wa Taifa na vilevile kule *Zanzibar International Airport Terminal Two Project* na mradi wa *Zanzibar Health Development Requirement Study*.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu naigusia tu miradi mikubwa. Tumekuwa *na Primary Education Development Program,* ambao ni mradi mkubwa sana halafu tumekuwa na *Secondary Education Development Program.* Kwa kilimo natoa mfano,

tumekuwa na *Agriculture Sector Development Project, National Agriculture Extension Project, phase two*. Nimetaja kiufupi aina ya miradi iliyochukua pesa nyingi bila kuweka mradi huu ulichukua shilingi ngapi. Kwa sababu miradi mingine bado inaendelea. Naelewa Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakasema ungeweka na fedha lakini fedha mkihitaji tunaweza tukazitayarisha. Lakini hiyo ndiyo miradi mikubwa ukiacha mtandao mkubwa wa barabara ambao upo nchini uliochukua pesa nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini wa kuangalia uhimilivu wa Deni la Taifa yaani *debt sustainability analysis* iliyofanyika mwezi Februari mwaka huu unapimwa kwa viashiria ambavyo ni vya Kimataifa. Hoja hapa ilikuwa kwamba Waheshimiwa Wabunge wangependa kujua kisayansi kwa namna gani wanaweza kuwa na amani na hali ya Deni la Taifa tulilonalo dakika hii. Tathmini inaonesha kuwa viashiria vyote vya deni vipo katika viwango vinavyokubalika Kimataifa. Viashiria hivyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huwa tunatumia viashiria vikubwa vitano kupima uwezo wa Kitaifa kuhimili madeni na hali ilivyo kama nchi inahimili madeni. Kipimo cha kwanza ni kipimo cha deni kama asilimia ngapi ya pato la Taifa, *debt as percentage of GDP*. Kiwango kikubwa ambacho ukivuka pale unaonekana wewe huwezi tena kuitwa unahimili deni kisivuke asilimia hamsini yaani deni lako lisizidi asilimia hamsini ya pato la Taifa. Sisi Watanzania mpaka mwaka huu tulikuwa asilimia 18.9, kwa hiyo, utaona hapo bado tuna *long way to go*.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha pili, tunapima kiwango cha Deni la Taifa ni asilimia ngapi ya mauzo yetu ya nje, kwa sababu yale mauzo ya nje ndiyo yanayo-*service* lile deni. Kwa hiyo, ni lazima tupime deni lililopo ni asilimia ngapi ya mapato yetu yanayotuwezesha kulilipa. Kipimo ambacho tunatakiwa tusivuke, deni lile lisivuke asilimia 200 lakini mwaka huu tupo asilimia 56.2, kwa hiyo, utaona kwamba kipimo hiki tunakidhi.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha tatu, tunapima deni lile ni asilimia ngapi ya kipato cha ndani kwa sababu na kipato cha ndani kinatumika kulipia deni, kwa hiyo kipimo kilichopo ambacho ni cha uhimilivu usivuke asilimia 300 lakini sisi tupo asilimia 111.3. Kwa hiyo, utaona bado tuna-*gap* kubwa.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha nne, tunajipima uwezo wa ulipaji wetu wa deni na ni asilimia ngapi ya mauzo yetu ya nje ya nchi, kwa hivi kile kipimo kingine kilikuwa kipato cha ndani sasa tunatazama lile deni ni asilimia ngapi ya mauzo yetu ya nchi za nje, kinatakiwa kisizidi asilimia 25, lakini sisi deni lile ni asilimia 2.5. Utaona kwamba bado tupo mbali. Vipimo hivi hatuweki sisi, tunapimwa Kimataifa na hizi ndiyo *average indexes* za Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipimo kikubwa kingine cha mwisho ni ule ulipaji tuliokuwa tukilipa au ulipaji huo ambao huwa tunalipa, ni asilimia ngapi ya mapato yetu ya ndani, kipimo hicho kinatakiwa kisizidi asilimia 35, sisi ni asilimia tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu, utaona kwamba, katika kutazama vipimo hivi vikubwa ambavyo vinapima uhimilivu wa Taifa, bado Taifa letu lina nguvu na lina uwezo wa kuhimili madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja kwamba, ni lazima tukope kwa ajili ya kuwekeza maeneo ambayo yatatupa ufanisi wa kutuwezesha kuboresha uchumi wetu, kujenga miundombinu, kuimarisha uchumi, lakini tusikope kwa sababu tunataka kula. Mkopo wowote unaokopwa ukuwezeshe wewe kuzalisha na kujenga uchumi, huo ni mkopo ulio na ufanisi na hivyo ndivyo tunavyokopa, tunakopa ili tuwekeze, na hivyo ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hilo, naomba sasa nieleze kifupi juu ya madeni ya ndani. Serikali inaelewa kwamba inakabiliana na madeni mbalimbali kutokana na huduma inazozitoa kutoka kwa Wakandarasi na watoa huduma na wananchi wetu. Vile vile ili kurekebisha hali hii Serikali inaandaa mkakati wa kulipa madeni yaliyopo na kuyapangia utaratibu wa kuyalipa kwa kadri tunavyokuwa na fedha za kutosha. Kuhusu madai ya malimbikizo ya mishahara, Serikali inaendelea kuyalipa kwa kutumia utaratibu wa kuyaingiza kwenye malipo ya mishahara kila mwezi baada ya Watumishi kukamilisha taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika na Wabunge kuna hoja nyingine ilitolewa na Wabunge wakipenda kuelezwa ni namna gani tumejitayarisha kwa ajili ya kukabiliana na

rasilimali gesi, Mwenyezi Mungu ametujalia tuna gesi ya kutosha, lakini tuna mkakati gani gesi hiyo inaweza ikatumika kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi mmeongelea kuhusu upatikanaji wa gesi asili nchini, pamoja na kukamilika kwa taratibu za kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kama alivyosema Profesa Sospeter Muhongo, juzi tulisaini mkataba wa kukamilisha mkopo huu wa kujenga bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam litakalotugharimu dola 1.225 bilioni na sisi tumeshatenga pesa dola za kutosha milioni 60 sawa na hela za Tanzania bilioni 93 ambazo tayari tumeshatenga kwenye bajeti. Tumeshatia sahihi na pesa ya ndani ambayo ni *counterpart fund* tumeshaitenga, tuko tayari kuanza mradi huu tuingize gesi ya kutosha inayozidi *megawatt* elfu mbili Dar es Salaam tuingize kwenye viwanda, kwenye nyumba za watu binafsi, tuone namna itakavyochangamsha uchumi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, huu ni wakati wa wote kuungana pamoja kuona kwamba, baraka hii ya *energy to energize our country* na kuhakikisha kwamba inatumika kujenga uchumi wa nchi yetu. Tuhakikishe kwamba deni hili wote tunaolisimamia na ninyi Wabunge mnakuwa jirani na sisi tuliopewa mamlaka ya kuchunga huu mradi ili kwa niaba ya wananchi baadaye waje waone *value for money*.

Mheshimiwa Spika, aidha, upatikanaji wa gesi hii utaongeza msukumo kwa sekta mbalimbali za uzalishaji na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa kada mbalimbali na kupunguza gharama za uzalishaji kupitia unafuu katika gharama za umeme. Waziri Wassira alieleza namna chanzo cha umeme unaotumia gesi ulivyo rahisi kuliko vyanzo vingine, huu ndiyo wakati wa kuhakikisha kwamba tukishaingiza umeme *cost of doing business in* Tanzania itakuwa imekwenda chini. Kama nilivyosema huu ndiyo wakati wa kuhakikisha kwamba uchumi wetu unajengeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzisha kitengo kipya kitakachoshughulikia utozaji kodi kwenye makampuni yenye hadhi ya Kimataifa yakiwemo madini na gesi. Aidha, mamlaka imekuwa ikiwajengea uwezo watumishi wake katika fani ya ukaguzi na usimamiaji wa sekta ya madini na hivyo itatumia uzoefu huo katika kutoza kodi kwenye makampuni ya gesi asili. Vile vile, Serikali kupitia ofisi ya Mwanasheria itatoa mafunzo ili kuwaongezea uwezo watalaam wetu ili kuhakikisha mikataba inayoandaliwa inakuwa na tija kwa Taifa hili kama walivyoshauri Wabunge. Maelezo ya kina yatatolewa na Waziri mwenye dhamana ya sekta hii ya *energy*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya Wabunge ni kwamba, wangependa kufahamu hali halisi ya uwiano wa bajeti yetu na matumizi ya maendeleo. Wote tumeona kwamba eneo lingine ambalo limeongelewa sana na Wabunge wengi ni kuhusu uwiano wa matumizi ya kawaida ya maendeleo katika bajeti ulivyooneshwa na kwamba wangependa iwe asilimia

65 kwa upande wa matumizi ya kawaida na asilimia 35 kwa upande wa miradi ya maendeleo, kitu ambacho wote, Serikali pamoja na Wabunge ndiko tunakopenda twende na iwe hivyo kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Stephen Wassira asubuhi hii alifafanua ni namna gani hali halisi ilivyo na kwamba kwa kusema ukweli ukichukua ile *human capital investment* kulingana na *strategic plan* yetu basi *investment* yetu inakua kwa asilimia 35.5, ingawaje kimahesabu hapa tulikuwa kwanza tumetenga tukaiacha ile pembeni, lakini uwekezaji katika taaluma, uwekezaji katika elimu, ni namna ya kujenga nguvu, ni namna ya kujenga uwezo kinchi ili ikabiliane na mahitaji, ni sawa unavyowekeza katika vitu vilivyo *fiscal*, unapowekeza katika elimu, unapowekeza katika afya kwa kweli unawekeza kama unavyowekeza maeneo mengine kwa sababu unajenga uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo Wabunge waliiweka mbele yetu au Serikalini ni juu ya *Skills Development Levy*. Hili ni eneo ambalo limezungumzwa sana na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa ufasaha mkubwa na Wabunge wamependekeza kwamba kiwango kinachotozwa sasa cha *Skills Development Levy* ambacho ni asilimia sita kipunguzwe. Pendekezo la pili ni kwamba, tuongeze wigo wa wale wanaolipa *Skills Development Levy*. Kwanza, kipunguzwe kutoka asilimia sita kiteremshwe kwenye asilimia ndogo na kusema kweli wengine wamependekeza kwamba *Skills Development*

*Levy* iwe asilimia mbili pia waongezeke wanaolipia *levy* hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na hoja hizi nzuri na kwamba Serikali inalifanyia kazi ili utaratibu mzuri wa kulipa kodi hii kwa Mashirika yote ya Umma yanayofanya biashara kuanzia Januari mwaka huu unaokuja utaratibu huu uwe umekamilika na unafanya kazi na kweli tuwe tumepanua wigo wa walipaji wawe wengi, tunakubaliana na hoja ya Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba nguo zinazozalishwa na viwanda vya ndani kwa kutumia mali ghafi za hapa nchini kama vile pamba ziondolewe Kodi ya Ongezeko la Thamani, Wabunge wamekuwa na hoja nzuri kwamba kwa kupunguza au kwa kuondoa *VAT* kunafanya mambo mawili makubwa. La kwanza, ni kuvifanya viwanda vyetu vinavyotumia mazao ya pamba inayolimwa hapa nchini viweze kuongeza ajira. Pili, kwa kufanya hivyo mapato ya wananchi wetu watakaokuwa wameajiriwa na viwanda hivyo yataboreka na hali ya wananchi wetu itakuwa nzuri kwa sababu wote tunataka kuboresha maisha ya watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia hoja na mapendekezo yenu Wabunge na kwamba tunauona umuhimu huo wa kusaidia viwanda ambavyo vinatengeneza nguo zinazotokana na pamba inayozalishwa nchini mwetu. Serikali inaunga mkono hoja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, kwa hoja nzuri ya Waheshimiwa Wabunge ya kuomba Serikali iondoe *VAT* ili kuvipa nafasi viwanda vyetu vya nguo vinavyotumia pamba iliyozalishwa hapa nchini, ambayo itawezesha viwanda vyetu vinapozalisha hizo nguo zinazotumia pamba tuliyolima wenyewe iongeze ajira na wananchi wetu wapate mapato mazuri ili kuboresha maisha yao ya kiuchumi. Tumeipokea hiyo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa utaratibu wa utendaji wa Serikali tunaifanyia uchambuzi…

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**WAZIRI WA FEDHA:** Subirini, tunaifanyia uchambuzi na matokeo yake tutawapeni katika *Finance Bill* kabla hatujafunga Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekubali, tunalifanyia uchambuzi tuone, siyo kuona mantiki, ni kuona namna gani tunaweza tukafidiana katika yale mahesabu yetu, lakini hoja si ya ubishani, tumekubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapoileta *Finance Bill* tutawapa picha halisi ya uchambuzi wetu. Serikali imezingatia maoni hayo ya Wabunge wanaowakilisha wananchi milioni kumi na sita kutoka maeneo hayo ya pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iwezeshe upatikanaji wa ajira kwa vijana hasa kupitia mipango ya uwezeshaji ikiambatana na elimu ya

ujasiriamali na kuboresha huduma za fedha. Haya mliyauliza Wabunge wenyewe na kutaka kujua Serikali inasema nini juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwani ushauri huu unakwenda sambamba kabisa na azma ya Serikali ya kutanua fursa za ajira kwa vijana kwa kutekeleza mipango mbalimbali. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti, Serikali itachukua hatua mbalimbali za kisera na kisheria kuwezesha sekta binafsi kukua hususan sekta ya viwanda, sekta ya huduma na kupanua fursa za upatikanaji wa mikopo sambamba na kuwekeza kwenye elimu ya ujasiriamali. Katika kuboresha huduma ya fedha, Serikali imeendelea kufanya mageuzi ya sekta ya fedha, hivyo kuongeza idadi ya mabenki kutoka benki 43 zilizokuwepo mwezi Aprili mwaka jana hadi kufikia benki 49 mwaka huu mwezi Aprili.

Mheshimiwa Spika, huduma ya fedha kupitia kadi za simu za mikononi iliruhusiwa nayo imeongezeka na kuenea maeneo takriban yote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya mageuzi ya ushirika nchini ili kuimarisha Vyama Vikuu vya Ushirika na kuiwezesha kutoa huduma za fedha. Hivi sasa Vyama vya Kuweka na Kukopa vimeongezeka na kufikia 5,346 kutoka vilivyokuwa 5,314 mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii ni azma ya Serikali kuendelea kupanua huduma za fedha kama

nyenzo muhimu ya upatikanaji wa mikopo nafuu kwa miradi ya uwekezaji mdogo na ule uwekezaji mkubwa. Serikali iko hatua za mwisho za kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kuongeza mtaji kwa benki zilizopo. Kiasi cha shilingi bilioni 72.6 zitaelekezwa kwa ajili ya kuimarisha mitaji ya Benki za Umma, *Program* ya *SELF* inayotoa mafunzo na mikopo kwa wajasiriamali wadogo nchini kote, Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji; Mfuko wa Taifa wa Vijana na Wanawake, *SIDO, VETA*, ambavyo ni vyombo muhimu katika kuwekeza vijana wetu kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo. Tutawapa mafunzo. Mwaka ujao wa fedha unaoanza Julai, 1 Serikali itapeleka shilingi bilioni 40 *Tanzania Investment Bank* na shilingi bilioni 70 Benki ya Maendeleo ya Kilimo *TADB* ambayo zitaongeza fursa za kukopesha vijana wetu na wananchi kwa ujumla. Fedha hizo tumeshazitenga katika bajeti inayoanza mwezi Julai, siyo hela za kutafuta, tumeshazitenga makusudi hizo benki, *Tanzania Investment Bank* ipanue ukopeshaji mpaka kule vijijini na vile vile *Tanzania Agricultural Development Bank* ikopeshe wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo niliyosema bomba la gesi litakapomalizika litaongeza fursa za ajira kwani shughuli nyingi za uzalishaji kwa umeme zitajitokeza. Lingine ni kilimo cha umwagiliaji tumetenga mabonde ya Mto Wami, Kilombero, Malagarasi na Ruvu tunajua haya mabonde yataongeza ajira kwa vijana wetu. Vile vile tumetenga bilioni 4.5 kwa ajili ya sekta ya ujasiriamali tukiwekeza kwenye *SIDO* tuna uhakika 4.4 zitasaidia vijana wetu katika shughuli za ujasiriamali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa tuseme kwa nini Serikali inaruhusu uagizaji kutoka nje kwa vilainishi (*lubricants*) wakati kuna viwanda vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa suala la kulinda bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa kutoka nje linawezekana tu pale ambapo uwezo wa uzalishaji unakidhi mahitaji ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo uzalishaji wa vilainishi haukidhi mahitaji ya soko. Hata hivyo, kulingana na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, vilainishi vinavyoagizwa kutoka nje hutozwa ushuru wa forodha kwa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiwango cha juu cha ushuru wa forodha ambacho kimewekwa kwa bidhaa timilifu *(Maximum Tariff).* Aidha, viwanda vya ndani vinahimizwa kuzalisha bidhaa zenye ubora na kwa wingi ili viweze kukidhi mahitaji ya kiushindani.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kubwa ilikuwa kodi kwa wajasiriamali wa kipato cha shilingi milioni tatu ziondolewe. Sheria ya Kodi ya Mapato hailengi kutoza kodi kwa mapato yatokanayo na kifaa au chombo fulani. Sheria hii inatoza kodi kwenye faida kutokana na taarifa za kibiashara zinazotengenezwa na kuwasilishwa na mlipa kodi kwenye mamlaka ya mapato Tanzania au kwenye mapato ghafi kwa wale wasiotengeneza mahesabu. Taarifa hizo kuhusu faida au mapato ghafi hutokana na vyanzo mbalimbali

kulingana na shughuli za kibiashara zinazofanywa na mlipa kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, walio wengi kuhusu suala la utozaji kodi vijana na wananchi wa kipato cha chini kwa ujumla wakiwemo vijana wa bodaboda, Serikali inapendekeza kuwa tabaka la kwanza libadilishwe kutoka mapato yasiyozidi shilingi milioni tatu kuwa mapato yasiyozidi milioni nne. Tukipandisha hilo tabaka la kwanza kutoka milioni tatu mpaka milioni nne kama mapato ghafi ya chini ya kiwango cha kutoza kodi, kiwango hiki cha chini kisichotozwa kodi kinapendekezwa kupandishwa ili kuwafanya vijana wetu wafanyabiashara walio wengi wadogo wadogo kutotozwa kodi ya mapato ya Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo tunavyoamini kwamba vijana wetu wa bodaboda na wengine wenye vipato hivyo vya chini watakidhi. Kwa hiyo, tumesikia kilio cha vijana wetu, tumesikiliza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Tunawashukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya mwisho, Waheshimiwa Wabunge walitaka Serikali iseme neno na kwamba inaonaje iongeze ushuru wa mafuta ya kula kutoka nje ili kukidhi kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hoja zote zilizowekwa mbele yetu na Waheshimiwa Wabunge, sababu zao nzuri za kulinda viwanda vyetu, Serikali imeunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwango hivi tunachosubiri ni kupeleka hoja kwenye Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki ili tupate muafaka kwa sababu ya *East Africa Protocol,* lakini Serikali imekubali mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge, wote mliopo naomba muidhinishe bajeti hii ifanye kazi kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Wanauliza simu? Muda hautoshi. Waheshimiwa Wabunge haya mtayafanyia kazi kwenye *Finance Bill* kwa sababu ndio maana tuliona *Finance Bill* iende mwisho kwa sababu kuna mambo ambayo mnaweza kuyafanya kule na yatakuja hapa na hili ni suala la *Finance Bill*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba kengele igongwe kwa muda wa dakika moja ijayo.

*(Hapa kengele ililia ili Wabunge waweze kuingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Tutakapoanza kupiga kura naomba utulivu uwepo kusudi tuwe tunasikia maneno ya ndio na hapana au vinginevyo. Hiyo, kengele ni ya kuwaita walioko nje siyo waliko ndani, ndio maana imeshagongwa. Naomba mtulie mahali penu, tunaanza kazi.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH:** Mheshimiwa Spika, Orodha ya Wabunge kwa madhumuni ya kupiga kura ili kupitisha bajeti ya Serikali.

**SPIKA:** Tutakachofanya utasema Ndiyo au Hapana kwa sababu ukisema ndiyo au siyo mara nyingine tunachanganya, endelea Katibu.

Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Samuel John Sitta... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli... ... Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe... Ndiyo
Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa... ... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Sophia Mattayo Simba... ... ... ... ... ... ... .. Ndio

Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe... ... ... ... .. Hakuwepo

Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa George Huruma Mkuchika... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Balozi Khamis Juma Suedi Kagasheki... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa William Augustao Mgimwa... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo... ... Ndiyo

Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Job Yustino Ndugai... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Adam Kighoma Malima... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Gregory George Teu... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Pereira Ame Silima ... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim... ... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Saadalla... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa George Boniface Simbachawene... Hakuwepo

Mheshimiwa Stephen Julius Masele... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa January Yusuf Makamba... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla... ... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Janet Zebadayo Mbene... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Saada Mkuya Salum... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa John Momose Cheyo... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema... ... Hapana

Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa James Daudi Lembeli... ... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Pindi Hazara Chana... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Hassan Athumani Ngwilizi... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Andrew John Chenge... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto... ... ... ... ... ... ... Hapana

Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu... ... ..
Hapana
Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis... ... ... ... ... ... .
Hapana
Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Said Amour Arfi... ... ... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse... ...
Hapana
Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Joseph Roman Selasini... ... ... ... .
Hakuwepo
Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi... ...
Hakuwepo
Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi...
Hapana
Mheshimiwa Halima James Mdee... ... ... ... ... ..
Hapana
Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa John John Mnyika... ... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli... ...
Hapana

Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya... ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Antony Gervase Mbassa... ... ... . Hakuwepo
Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula... ... Hapana
Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi... ... ... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay... ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa... ... .. Hapana
Mheshimiwa Highness Samson Kiwia... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa David Ernest Silinde... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Christina Lissu Mughwa... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah... ... ... ... ... ... ... .. Hapana

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah... ... ... ...
... ...Ndiyo
Mheshimiwa Bahati Ali Abeid... ... ... ... ... ... ...
... . Ndiyo
Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Chiku Aflah Abwao... ... ... ... ... ...
.. Hapana
Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed... ... ... ... ... ...
. Hapana
Mheshimiwa Lameck Okambo Airo... ... ... ... ..
Hakuwepo
Mheshimiwa Abdalla Haji Ali ... ... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Juma Othman Ali... ... ... ... ... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali ... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Sara Msafiri Ally... ... ... ... ... ... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Hussein Nassor Amar... ... ... ... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir... ... ... ... ... ... ...
.. Ndiyo
Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir... ... ... ... .
Hakuwepo
Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer... ... ...
.. Ndiyo
Mheshimiwa Amina Abdallah Amour... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub... ... ... ... ... ...
... .. Ndiyo

Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar... ... ... ... . Hakuwepo
Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Ester Amos Bulaya... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Selemani Said Bungara ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Felister Aloyce Bura... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Cyril August Chami... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Mary Pius Chatanda... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Kapt. John Zefania Chiligati... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Amina Andrew Clement... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Ali Juma Haji... ... ... ... ... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Khatib Said Haji... ... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Zahra Ali Hamad... ... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Hamad Ali Hamad... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Azza Hillal Hamad... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Asaa Othman Hamad... ... ... ... ... .. Hakuwepo

Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Agness Elias Hokororo... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd... ... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Christina Gabriel Ishengoma... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Yahya Kassim Issa... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Waride Bakari Jabu... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Juma Sururu Juma... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Riziki Omar Juma... ... ... ... ... ... ... .. Hapana

Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa David Zacharia Kafulila... ... ... ... ... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Haji Khatib Kai... ... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Vick Paschal Kamata... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya... Hakuwepo
Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Eustace Osler Katagira... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Kheir Ali Khamis... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Salim Hemed Khamis... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Susan L. Aloyce Kiwanga... ... ... .
Hakuwepo
Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Silvestry Francis Koka ... ... ... ... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba...
Hakuwepo
Mheshimiwa Mussa Haji Kombo... ... ... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo... ... ... ... ...
Hapana
Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu... ...
Hapana
Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir... ... ...
Hakuwepo
Mheshimiwa Michael Lekule Laizer... ... ... ... ... ...
... . Ndiyo
Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola... ... ... ...
... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu... ... ... ...
Hakuwepo
Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola... ...
Hakuwepo
Mheshimiwa Riziki Said Lulida... ... ... ... ... ... ... ...
.. Ndiyo
Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde... ... ... ...
... . Ndiyo
Mheshimiwa John Paul Lwanji ... ... ... ... ... ... ...
... Ndiyo
Mheshimiwa Moses Joseph Machali... ... ... ... ...
Hapana

Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Madelu... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa John Shibuda Magalle... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Catherine Valentine Magige... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Faki Haji Makame... ... ... ... ... ... ... . Hakuwepo

Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac... ... ... Hapana

Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Dkt. David Mkiwa Mallole... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Donald Kelvin Max... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka... ... Hakuwepo
Mheshimiwa James Francis Mbatia... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli... ... .. Hapana
Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba... ... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita... ... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi... ... ... ... ... . Ndiyo
Mheshimiwa Desderius John Mipata... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali... ... ... ... ... ... ...Hapana

Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Rita Louise Mlaki... ... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Martha Moses Mlata... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo ... ... ... ... Hapana

Mheshimiwa Herbert James Mntangi... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa... ... Hapana

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed... ... ... ... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed... ... ... Hapana

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina... ... ... ... ... .. Hakuwepo

Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha... ... ... ... ... ... Hapana

Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, acheni kuongea kusudi msikie majina yenu.

**NDG. DOKTA THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea.

Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu... ... ... ... ... ... ... . Ndiyo

Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Joyce John Mukya... ... ... ... ... ... ... .. Hapana

Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu... Hakuwepo

Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa... ... ... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Mch. Luckson Ndaga Mwanjale... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa... ... .. Ndiyo
Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau... ... ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari... ... ... ... ... ... ...Hapana
Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo... ... .. Hakuwepo

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi na walishangilia sana)*

**SPIKA:** Jamani, hebu acheni, mnapoteza muda. Waheshimiwa, mnapoteza muda, sijui mtindo huu umeanza wapi? *(Kicheko)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea.

Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile... ... Ndiyo
Mheshimiwa William Mganga Ngeleja... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, upo wapi? Hatukusikii.

Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani... ... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye... ... ... ... ... ... ... ...Ndyio
Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Said Juma Nkumba... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya... ... ... ... .. Hakuwepo
Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina... ... ... ...Ndio

Mheshimiwa Omari Rashid Nundu... ... ... ... ... ... ... ... Ndio

Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo... ... ... ... .. Ndiyo

Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Rashid Ali Omar... ... ... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Asha Mohamed Omari... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba... ... ... ... ... ... Hakuwepo

Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso... ... ... ... ... ... ... Hapana

Mheshimiwa Ismail Aden Rage... ... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert... ... ... ... ...Hapana

Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare... .. Ndiyo

Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza... ... .. Hakuwepo

Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Said Suleiman Said ... ... ... ... ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Moza Abedi Saidy... ... ... ... ... ... ... .. Hapana
Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh... ... ... ... ... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim... ... ... ... ... ... ...Hapana
Mheshimiwa Ahmed Ali Salum... ... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga... ... ... ... ... Hakuwepo
Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Ali Khamis Seif... ... ... ... ... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Haji Juma Sereweji ... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah... ... ... ...Ndiyo
Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis... ... ... ... ... Hapana
Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu... ... ... ... ... ... ... ... Ndiyo
Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni... ... ... ... ... ... ... .. Hakuwepo

Mheshimiwa Rose Kamili Sukum... ... ... ... ... ... ... Hapana

Mheshimiwa Suleiman Masoud Suleiman... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar... ... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura... ... ... ... ... .. Hapana

Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Salim Hassan Abdullah Turky... ... ... Hakuweo

Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Anastazia James Wambura... ... ... ... ... ...Ndiyo

Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi... ... ... ... ... ... ... Ndiyo

Mheshimiwa Said Mussa Zubeir... ... ... ... ... ... ... .. ... Ndiyo

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, mwisho wa majina.

**SPIKA:** Wale waliorudi? Kuna majina mawili. Yupo Mheshimiwa Mbilinyi, nimetoa jina, nimewapeni jina, Mheshimiwa Mbilinyi, ndio huyo. Mheshimiwa Mbilinyi na Mheshimiwa Kawambwa.

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, jina sijalisikia, jina langu mie sijaitwa.

**SPIKA:** Nani?

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naitwa Kheir Ali Khamis, nasema Ndiyo.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Ali Juma Haji. Pia nasema Ndiyo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kupiga kura yangu ya Hapana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Yuko Mheshimiwa Kawambwa. Umeshindwa kupiga kura?

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa!

**SPIKA:** Ngoja kwanza, wale wote ambao hawakupiga kura sasa hivi, wasimame kwanza. Halafu mtumie muda kidogo kwa sababu inabidi wafungue *page.*

**WABUNGE:** Aaah!

**SPIKA:** Aah, mnasema nini? Mheshimiwa Kawambwa, pia asimame. Tuanze na Mheshimiwa Mbilinyi pale, mmepata jina lake. Taja jina lako.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, Hapana.

**SPIKA:** Taja jina lako, taja jina lako.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mbunge taja jina lako na useme kura unayopiga.

**SPIKA:** Taja jina lako. *Ooh, My Lord.*

*(Hapa Wabunge walishangilia sana)*

**SPIKA:** Haya jamani, utaratibu. Waheshimiwa, ngojeni tufanye utaratibu. Haya, Mheshimiwa Mbilinyi, ameonekana jina lake?

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mbilinyi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, taja kura yako. Mbilinyi, nini?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, Joseph Mbilinyi, Hapana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kawambwa, pale. Taja jina lako na useme kura yako.

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naitwa Juma Ali Khamis, Ndiyo.

**SPIKA:** Aah haa, tunakuja huku kwanza.

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Kheir Ali Khamis.

**SPIKA:** Aah haa, huku kwanza. Subiri kwanza Mheshimiwa Khamis. Mheshimiwa hapo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Ndiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif, sema jina lako?

**MHE. KHEIR ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naitwa Kheir Ali Khamis, Ndiyo. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, jina langu ni Ali Juma Haji, Ndiyo.

**SPIKA:** Ngoja kwanza wapate hii nyingine ya kwanza, subiri kidogo.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Ali Juma Haji!

**SPIKA:** Unapigaje kura?

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, Ndiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, naomba utulivu kidogo, wafanye hesabu. Naomba mtulie tu kwanza, halafu tufanye hesabu. Mkitulia itakuwa vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa Mamlaka niliyonayo kwa kufuatana na Kifungu cha 28, nitaongeza nusu saa, baada ya saa ya kawaida ya kuahirisha.

Katibu, nadhani shughuli imekwisha. Kuna haja ya ku-*computerise,* bado kidogo, tutafanya hiyo kazi. Kuna haja ya ku-*computerise* baadaye. *(Makofi)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge wote Kikatiba ni 357. Idadi ya Wabunge waliopo ni 252. Lakini waliotakiwa kupiga kura ni 351 kwa sababu, Spika, hapigi kura.

Mheshimiwa Spika, Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni 54. Idadi ya Wabunge wote waliopo na kupiga kura leo ni 297. Kura za Hapana ni 72. Kura za Ndiyo ni 225. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, maana ya kupiga kura za kuitwa tena, hauna haja ya kuwahoji maana tayari zimejitoa zenyewe. Lakini ni wazi kuwa, inabidi tujaribu kuwa kisasa kidogo namna ya kupiga kura, kuliko hii kazi ya Ndiyo na Hapana, kwa mdomo, kidogo kuna matatizo ya mitambo ya umeme.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu napenda kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu

wake wote, kwa kazi nzuri sana waliyofanya kwa shabby toka wamepata hiyo kazi mpaka wanawasilisha hii bajeti yao, muda ulikuwa mfupi sana. *(Makofi)*

Naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge, kama walivyosema wao, kwa sababu, tumetoa muda mrefu wa *Finance Bill,* nadhani Kamati yetu itaendelea kufanya kazi na Waziri wa Fedha na Wabunge wengine wenye mawazo, watafanya. Hata sisi wenyewe tutajiweka katika Kikosi kile kidogo cha kujaribu kupendekeza *other sources of revenue* kwa sababu, mapendekezo yetu sio maana yake uamuzi. Kwa sababu, sisi tunaweza kupendekeza, lakini utaalam halisi wanao wenyewe. Kwa hiyo, hiyo kazi pia tutaifanya.

Kwa hiyo, niwashukuru na nyie Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, mmeshiriki kikamilifu, mmeshiriki vizuri, ndio maana hata Waziri, amekuwa na maelezo ya kueleza ni nini kimekuwa wapi na kiwe nini kwa sababu, mlikuwa mnajenga hoja. Kasoro ndogondogo zilizotokea, nadhani katika kujifunza, si vizuri sana kama nilivyosema; tunaangaliwa Waheshimiwa, watu wote wanatutaka tutoe mawazo. Kutofautiana kifikra sio vibaya katika Ukumbi kama huu, ni vizuri sana kwa sababu ndio mnavyozidi kuboreshana ama tunazidi kuboresha msimamo wetu wa namna ya kupitisha bajeti.

Kwa hiyo na kama tulivyosema, naamini Serikali na wenyewe watakuwa tayari, sisi tungependa ku-*revise* utaratibu huu. Tuanze na Sekta hizo, halafu tumalizie na

Wizara ya Fedha. Nadhani tukishirikiana, tutapata mfumo mzuri zaidi kuliko huu tunaofanya sasa hivi. Kwa sababu, leo tutajadiliana sisi mpaka karibu mwezi wa Agosti wote, wakati ndiyo muda mzuri wa Serikali kufanya kazi, lakini kila siku tunakaa hapa. Kwa hiyo, tunajaribu kuona kwamba, ni namna gani tunaweza ku-*revise* utaratibu, inapofika tarehe 30 Juni, kila kitu kiwe kimemalizika na watu wanakwenda kufanya kazi. Mwisho, nawapongeza sana Waziri, Manaibu wako na Wataalam wenu waliofanya kazi *tirelessly,* mpaka kupata kitu kizuri kama tulichokuwanacho. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, hatuna matangazo yoyote. Isipokuwa kesho asubuhi saa tatu, Wenyeviti, *Presiding Officers* wote, tutakutana pale Ofisini kwangu; ina maana Naibu Spika na Wenyeviti wale watatu, tutakutana saa tatu kusudi tuweze kufanya kazi pamoja, maana hatujakaa toka tumechaguana.

**WABUNGE:** Mheshimiwa Spika, hatusikii.

**SPIKA:** Haisikiki? Hamnisikii kabisa?

**WABUNGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Nimesema hivi, kesho saa tatu tutakuwa na Kikao cha *Presiding Officers,* maana yake ni Wenyeviti, Wabunge, pamoja na Naibu Spika na Spika, saa tatu kule Ofisini kwangu. Lakini sina matangazo mengine yoyote, nawatakieni *weekend* njema, muweze kutafakari namna ya kumsaidia Waziri katika *Finance*

*Bill*. Halafu Jumatatu, tutakuwa na Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu huo.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Kikao cha Bunge, mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.53 Usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Terehe 25 Juni, 2012 Saa 3.00 Asubuhi)*